## BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 4 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia katika Shughuli za asubuhi hii. Kabla ya yote, leo ni siku ya kumbukumbu ya aliyekuwa Makamu wetu wa Rais mpendwa wetu Dr. Omari Ali Juma. Nimeshauriwa hapa na nimeona inafaa tusimame kwa dakika moja kumkumbuka shujaa wetu aliyefariki dunia tukikwa hapa hapa Dodoma tarehe 4 Julai, 2001.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka Marehemu Dr. Omari Ali Juma, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwenye *Gallery* kuna mgeni wa Mheshimiwa Juma Killimbah, ambaye ni Katibu mwenezi wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Iramba. Naomba asimame pale alipo. Karibu sana. *(Makofi)*

Leo tuna wageni pia hapo hapo kwenye *Gallery* mkono wa kulia ni wanafunzi 14 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Kiluvya Dar es Salaam naomba msimame. Ahsante sana. Karibuni sana. Tunawapongeza walimu kwa kuwaleta vijana kuweza kuona namna demokrasia ya nchi yao inavyoendeshwa. Karibuni sana. Shughuli inayofuata Katibu endelea na *Order Paper.*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 137

**Hospitali ya Mkoa wa Manyara**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma za Madaktari Bingwa *(Specialists)* na zile za ziada zinaanza kwenye ngazi ya Hospitali za Mikoa; na kwa kuwa, Sera ya Afya inatamka wazi kuwa kila Mkoa utakuwa na Hospitali ya Mkoa:-

(a) Je, ujenzi wa Hospitali mpya ya Mkoa wa Manyara utaanza lini na ujenzi unatazamiwa kukamilika baada ya muda gani?

(b) Kwa kuwa, hospitali nyingi za Mikoa zimejengwa zamani sana na hivyo hazitoshelezi mahitaji ya sasa. Je, hospitali mpya ya Mkoa wa Manyara itakayojengwa Mjini Babati itazingatia kiwango cha majengo ya kisasa yatakayomudu *Specialization* kwa ajili ya huduma maalum?

(c) Je, Hospitali hiyo itakuwa na wastani wa uwezo gani wa vitanda na wataalam wa fani zipi maalum?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, taratibu za ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara zimekwishaanza tangu mwaka wa fedha 2004/2005 baada ya Mkoa kuidhinisha shilingi milioni 100,000,000/= katika Bajeti ya Maendeleo. Hatua za awali za ujenzi wa hospitali hii zimefanyika na kiwanja kimeshapatikana ambacho ni cha hekta 6.7. sawa na ekari 18.63 . Kiwanja hicho kipo Mtaa wa Miyomboni mkabala na jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kando ya barabara iendayo Singida.

Mheshimiwa Spika, kiwanja kimekwishapimwa kwa gharama ya shilingi milioni 2,500,000 na malipo ya fidia ya Shs.30,230,000 zimekwishakabidhiwa kwa Halmashauri ya Mji wa Babati. Ujenzi wa Hospitali hii unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2006/2007. Na jumla shilingi milioni 100 zimetengwa kwa ajili ya kuanzia. Gharama za kujenga hospitali yote zimekadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 3.5.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu za Wizara ya Afya, Hospitali za Mikoa za Rufaa Daraja la II zinatakiwa kuwa na fani za taaluma zifuatazo:-% Idara ya Tiba (*Medical Department*);% Idara ya Upasuaji *(Surgical Department*);% Idara ya Magonjwa ya akinamama (*Obstetrics and Gynaecology Department);* % Idara ya Magonjwa ya watoto (*Paediatric Department*);% Idara ya Mionzi (*Radiology Department*).

Aidha, ili kukidhi utoaji huduma katika taaluma hizi, Hospitali ya Mkoa wa Manyara itakuwa na majengo ya kisasa yatakayomudu na kuwezesha utoaji wa huduma maalum kama zilivyoainishwa katika Sera ya Afya.

(c) Mheshimiwa Spika, hospitali hii inatarajiwa kuwa na vitanda kati ya 250 mpaka 300. Aidha, hospitali itakuwa na wataalam (Madaktari Bingwa) wa fani maalum za Tiba, Upasuaji, Magonjwa ya Akinamama, Magonjwa ya watoto na Mionzi kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Afya.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Omar Kwaangw' ile kutafakari sana inaleta matatizo. Haya nakuruhusu kwa sasa.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa eneo la Halmashauri ya Mji wa Babati kuna zahanati moja tu na Kituo cha Afya kimoja tu cha Bonga na zahanati ya Kiongozi. Je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba zahanati ya Kiongozi inapandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya ili kumudu ongezeko kubwa la wananchi au la watu katika eneo la Halmashauri ya Mji wa Babati?

(b) Kwa kuwa hospitali ya sasa ya Babati ya Wilaya imekuwa na watu wengi kutokana na kuanzishwa kwa Mkoa wa Manyara. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuimarisha hospitali hiyo wakati tukisubiri hospitali ya Mkoa kujengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu tatizo la huduma za Afya katika Mkoa wa Manyara kwa kuwa ni Mkoa mpya. Kwa hiyo, Serikali inaangalia zaidi tatizo hili hasa katika Mikoa mipya na Wilaya mpya.

Kwa hiyo, Serikali itahakikisha kwamba inaimarisha vile Vituo vya Afya na zanahati zilizopo katika Mkoa wa Manyara ili kuhakikisha kwamba zinakidhi mahitaji ya wananchi wa Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Na. 138

**Gari la Kituo cha Afya Kitunda**

**MHE. LUCAS L. SELELII (K.n.y. MHE. SAID J. NKUMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tarafa ya Kiwele ina Kituo cha Afya cha Kitunda kinachotegemewa na wakazi wa Tarafa hiyo kwa huduma za afya; na kwa kuwa, gari lililopo ni bovu na mara nyingi Kituo kimekuwa kikikaa bila usafiri wa uhakika:-

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo cha Afya cha Kitunda gari jipya ili kuondoa tatizo la usafiri?

(b) Je, Waziri atakuwa tayari kufika hapo Kituoni Kitunda ili aone umbali uliopo kati ya Kituo cha Makao Makuu ya Wilaya na kuthibitisha umuhimu wa usafiri wa uhakika kwenye Kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Serikali ilifanya zoezi la kujua mahitaji halisi ya magari ya kubeba wagonjwa katika Vituo vya Afya vyote nchini. Zoezi hilo lilibainisha kuwa jumla ya magari mpya 300 yanahitajika katika Vituo mbalimbali vya Afya.

Baada ya utafiti huo, Serikali ilianza kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa magari hayo. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua magari hayo ambazo zimetosha kununua magari 30 tu. Magari hayo yamesambazwa katika Vituo vya Afya, kwa kuangalia baadhi ya vigezo kama vile Halmashauri zinazoanzishwa hivi karibuni na ambazo hazina kabisa magari ya kubebea wagonjwa. Hospitali na Vituo vipya vya Afya ambavyo kulingana na takwimu za tangu awali zina uhitaji mkubwa wa magari hayo kutokana na ukubwa wa eneo na wingi wa watu katika sehemu husika.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuendelea kununua magari hayo.

Serikali haina uwezo wa kununua magari katika Vituo vya Afya vyote Nchini kwa mara moja. Hivyo, Vituo vya Afya ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya Kitunda vitapatiwa usafiri wa gari hatua kwa hatua kadri fedha zitakavyopatikana na jinsi vigezo vitakavyofikiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba Kituo cha Afya cha Kitunda kipo katika Tarafa ya Kiwele yenye jumla ya wakazi 28,152 na kipo umbali wa kilomita 185 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kunikaribisha kutembelea Kitunda. Hata hivyo, nitahakikisha kwamba katika ratiba zangu za kazi natembelea Wilaya ya Sikonge hasa katika Kituo cha Afya cha Kitunda. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali ya kukatisha tamaa hasa kwa wananchi wa Kitunda ambao wanaishi kilomita 185 kutoka Makao Makuu ya Wilaya.

(a) Kama anajua kuna umbali wa namna hiyo kutoka Makao Makuu ya Wilaya na Kituo cha Afya kipo kimoja tu pamoja na zahanati moja. Kwa nini wasingepewa upendeleo maalum wananchi ambao wako mbali na Makao Makuu ya Wilaya katika Tarafa ya Kitunda?

(b) Kwa kuwa ameeleza katika jibu lake kwamba Serikali imeweka Bajeti ya kununua baadhi ya magari kwa nini asitangaze ili tukaelewa ni magari mangapi na yanaenda wapi ili hata mgao wa pili wananchi wa maeneo hayo tukawaambia wasubiri. Kwa sababu kukaa tu kwamba watanunua magari bila kueleza wapi wanayapeleka magari ni jambo ambalo linawapa wasiwasi wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba Kituo cha Afya cha Kitunda kipo kilomita 185 na ni mbali kutoka hospitali ya Wilaya. Siyo rahisi sasa hivi kukumbuka kwamba hayo magari 30 yamegawiwa katika Vituo vya Afya gani. Naomba Mheshimiwa Mbunge tukitoka nikamwonyeshe orodha ya Vituo vya Afya ambavyo vimepatiwa usafiri huo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.. Kwa kuwa tatizo hilo la Kituo cha Afya cha Kitunda linafanana sana na tatizo linalowapata wananchi wa Kata ya Ifinga ambapo ni mwenendo wa masaa 12 kutoka waliko mpaka katika Hospitali Kuu ya Wilaya na kwa kuwa kwa muda mrefu wananchi hao kupitia Waheshimiwa Wabunge wao wamekuwa wakiiomba sana Serikali iwasaidie gari kwa ajili ya kuwahisha wagonjwa katika matibabu yao.

Je, Serikali iko tayari kuwangalia wananchi hao wa Kata ya Ifinga katika mgao huo unaokuja? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu alizotoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI mtaona mahitaji ni mengi na ushauri kwa jumla ni kwamba kusema kweli Serikali haiwezi ikatimiza hiyo katika muda mfupi na tunashauri kwamba Halmashauri ziweze kutenga fedha katika Bajeti zao ili waweze kununua hayo magari. Kuna Halmashauri ambazo zimefanya hivyo. Kwa hiyo, pale ambapo kuna matatizo makubwa tujaribu na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa kuangalia ni vigezo gani na tuanze wapi. Kusema kweli nchi yetu ni kubwa na kuna maeneo mengi sana ambayo yako mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya.

Na. 139

**Uboreshaji wa Mishahara na Maslahi ya Walimu**

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI** aliuliza:-

Kwa kuwa, walimu wanafanya kazi yao katika mazingira magumu ingawa matunda ya kazi yao yanaonekana hususan katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mishahara yao ili waweze kumudu maisha?

(b) Kwa kuwa, katika miaka ya 1980 walimu walikuwa wanapewa posho ya asilimia 50 ya mishahara yao kama (*Teaching Allowance*) kila mwezi. Je, ni sababu zipi zilizosababisha Serikali kuifuta posho hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa iliwasaidia walimu kumudu maisha yao ya kila siku?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Malipo ya mishahara kwa Watumishi wa Umma yanategemea mambo yafuatayo:-

(i) Uzito wa majukumu ya kila mtumishi.

(ii) Uwezo uliopo kutokana na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kuboresha maslahi ya watumishi wake, wakiwemo walimu, Serikali ilipitisha Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mshahara kwa Watumishi wa Umma mnamo mwaka 1999. Kama sehemu ya utekelezaji wa Sera hii, Serikali iliamua kujumuisha posho mbalimbali katika mishahara ya watumishi wa umma.

Kwa kujumuisha posho hizo katika mishahara, Serikali ilikuwa na lengo la kuwawezesha watumishi wake kupata malipo mazuri ya pensheni, kwa vile posho hazihusiki katika kukadiria malipo ya pensheni. Aidha, pamoja na hatua hiyo, Serikalil iliendesha zoezi la kutathmini kazi katika Utumishi wa Umma kati ya mwaka 1999 hadi 2002. Katika zoezi hili uzito wa kila kazi pamoja na ya ualimu ulibainishwa. Utekelezaji wa mapendekezo ya zoezi hilo ulianza mwaka 2003. Hivyo msingi wa malipo ya mshahara ya walimu ni tathmini ya kazi au *Job Evaluations*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bafadhili, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali itaendelea kuboresha mishahara ya walimu na watumishi wengine kulingana na misingi ya Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma na kadri pato la Taifa litakavyoongezeka.

(b) Mheshimiwa Spika, posho ya kufundishia asilimia 50 ya mshahara waliyokuwa wanapewa walimu ilifutwa kama posho nyingine zilizokuwa zinatolewa kwa watumishi wa umma na kuongezwa katika mshahara kutokana na maelekezo ya Sera ya Malipo ya Mshashara ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa jambo la msingi ni kwa watumishi wote kufanyaka kazi kwa bidii ili kuiwezesha Serikali kuongeza mapato yake na hivyo hatimaye kuwa na uwezo wa kulipa mshahara inayokidhi mahitaji. Faida za kulipa kiwango kizuri cha mshashara ni kuwa mbali ya kumudu maisha yao wakiwa kazini, pia ni kuwawezesha kupata malipo mazuri ya pensheni baada ya kustaafu.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa wanafunzi wengi wanatoka katika familia zenye kipato duni na kwa kwa wanafunzi hao asubuhi hawapati chakula kiasi kinachosababisha wanafunzi wale waziwezi kuhudhuria vizuri masomo yao. Kwa sababu wanafunzi wasiposhiba hawawezi kumsikiliza vizuri mwalimu anachofundisha. Je, Serikali ina mpango gani angalau kuwapatia mlo mmoja kwa siku wanafunzi katika shule?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hilo ni swali jipya kwa hiyo, hakuna majibu. Kwa sababu linahoji sasa namna ya kuwahudumia watoto kupata lishe. Swali la msingi hapa linahusu Maslahi kwa Walimu. Endelea na swali la pili.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** La pili, kwa kuwa walimu wengi wanaishi katika maeneo ya Mjini na wengi wanadhalilishwa katika nyumba za kupanga.

Je, walimu hao Serikali haioni ni wakati muafaka kuwapatia viwanja ili waweze kujenga nyumba zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango mzuri wa kuwasaidia walimu ili kuweza kupata nyumba. Kwa wale wanaoishi Mjini wanapaswa kulipa pango la nyumba kutokana na mishahara yao. Kwa wale wanaoishi Vijijini upo mpango maalum wa kuwasaidia walimu kupata nyumba kutokana na nguvu za wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya pamoja na Serikali Kuu. Hata hivyo, juhudi kubwa zimewekwa katika kuhakikisha kwamba kero ya nyumba kwa walimu inamalizwa. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nina swali moja la nyongeza.

Kwanza, napenda nitambue nia nzuri ya Serikali ya kuunganisha posho zote kwenye mshahara kwa maana ya kwamba pengine kuwawezesha watumishi kuwa na pensheni kubwa pale wanapostaafu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni lazima tukubali kwamba mazingira katika nchi hii yanatofautiana. Kuna walimu ambao wanafundisha katika mazingira magumu sana. Lakini pia ni ukweli kwamba zile posho nyingine zilikuwa zinawawezesha walimu waweze kuvumilia hayo mazingira magumu. Je, Serikali haioni kwamba muda sasa umefika wa kuweka posho ya mazingira magumu ili kuwapa motisha wafanyakazi hasa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inatambua kwamba wapo walimu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu na kwa kuona hivyo Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilimwajiri mshauri ambaye alifanya utafiti wa kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kuwapatia vivutio watumishi wakiwemo na walimu wanaoishi katika mazingira magumu. Mshauri huyo ameishatuletea taarifa ya kwanza ambayo tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya kuangalia maslahi ya watumishi kwa ujumla wakiwemo na walimu. Mara Tume hiyo itakapomaliza kazi yake ni imani yangu kabisa kwamba walimu hao wanaoishi katika mazingira magumu Serikali itakuwa imeshajua ni nini cha kuwafanyia ili kuwafanya waishi katika mazingira mazuri zaidi. *(Makofi)*

Na. 140

**Huduma kwa Askari wa Jeshi la Ulinzi**

**MHE. ISSA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutoa huduma kwa Askari wa Jeshi la Ulinzi kwa njia ya kuponi, utaratibu ambao ni mzuri kwani huwapunguzia mzigo mkubwa wa madeni kwa watoa huduma hizo yaani wazabuni:-

(a) Je, ni kiasi gani cha deni kimebakia?

(b) Je, ni lini Wazabuni hao watalipwa madeni yao yote?

(c) Je, Serikali haioni fedha zinazotolewa kwa ajili ya huduma ya kuponi hazitoshi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Jimbo la Mpendae, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, aya nambari 28.35, Juzuu ya kwanza (Utawala) Kanuni za Majeshi ya Ulinzi (*Forces Routine Order*) ndiyo iliyotoa uwezo wa Askari/Afisa wa Jeshi kulishwa na Jeshi mbali na mshahara wake wa kila mwezi. Utaratibu uliokuwa unatumika awali ni wa kununua chakula kibichi kupitia kwa Wazabuni na Wanajeshi wenyewe kujipikia vikosini.

Kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha, utaratibu huo ulishindwa kulipa madeni ya Wazabuni walitoa huduma vikosini kwa ukamilifu, hivyo kupelekea kuwepo kwa malimbikizo ya madeni yaliyofikia Tsh.23,503,742,286. Malimbikizo hayo ni tokea mwaka 1990 hadi 2000.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2001, Jeshi la Ulinzi lililazimika kubadilisha utaratibu huo na kuanzisha utaratibu wa kuponi. Utaratibu huo mpya umelifanya Jeshi la Ulinzi kuandaa makadirio kwa kila mwaka ya kumwezessha Askari/Afisa wa Jeshi kuweza kula milo mitatu kwa siku. Makadirio ya sasa ni T.Shs.60,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim, Mbunge wa Mpendae, lenye sehemu (a), (b) na (c)) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya deni hilo la Shilingi 23,503,742,286/= lililokuwepo awali, deni lillilosalia ni Shilingi 2,280,861,187/=. Kanda ya Zanzibar inadai T.Sh.185,468,112 na zilizobaki zinadaiwa na Wazabuni wa Tanzania Bara.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikizifanyia uhakiki nyaraka mbalimbali za Wazabuni na deni lililosalia litalipwa baada ya kukamilika kwa kazi ya uhakiki na kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, nawaomba Wazabuni wavute subira.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kiwango cha fedha kinchotolewa kwa sasa kwa ajili ya chakula kwa Askari/Afisa hakitoshi. Utaratibu uliopo ni kuwa kila baada ya miaka 2 hadi 3 kiwango cha posho na chakula hufanyiwa mapitio na kuongezwa kulingana na hali halisi ya bei za vyakula na kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi wa Serikali.

Napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa Makao Makuu ya Jeshi imeanza kazi ya kufanya mapitio ya bei za vyakula na hali ya fedha itakapoturuhusu tutaongeza.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Napenda kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Jeshi au Serikali ina nia njema ya kuweza kuwapa huduma Wanajeshi ikawafungulia maduka katika *Barracks* zao wakapewa wafanyabiashara na kupunguziwa ushuru. Kwa nini vifaa hivyo wanaviuza ghali sawasawa na bei ya huko ng'ambo?

(b) Wizara ina makubaliano gani na wafanyabiashara hawa hata ikawa wana kiburi cha kuwatolea wale wa huduma wanaowahudumia? Naomba jawabu.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, tatizo alilolieleza Mheshimiwa Mbunge nasi tumeliona na Jeshi tayari tumeshaunda Kamati ya kuchunguza hali hiyo na tunasubiri ripoti ya Kamati ili tuweze kuchukua hatua.

Na. 141

**Wanafunzi Wanaojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBERI (K.n.y. YAHYA KASSIM ISSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, maelezo ya Serikali juu ya Swali Na. 56 lililojibiwa hapo tarehe 31 Februari, 2006 ni kwamba, taaluma itolewayo Chuo Kikuu haizingatii ni wapi mwanafunzi anakotoka licha ya kuwa na sifa kutoka sehemu hizo mbili za Muungano yaani Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar:-

(a) Je, ni nini tafsiri ya Muungano wa Elimu ya Juu kwa sehemu hizi mbili juu ya matumizi ya chuo husika?

(b) Je, kuna ushirikishi gani wa Muungano ikiwa haizingatii uingizaji wa wanafunzi chuoni kwa kuangalia ushiriki wa pande zote mbili za Muungano?

(c) Kwa nini chuo kisiwe na kumbukumbu za takwimu za wanafunzi wanaoingia na kumaliza chuoni kwa pande zote mbili za Muungano kama kielelezo cha ushiriki kwa pande zote?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tafsiri ya Elimu ya Juu kama kipengele cha Muungano ni kwamba sehemu zote za Muungano zina fursa sawa katika ushindani wa nafasi katika Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu Nchini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kama Serikali itaamua kutoa Elimu ya Juu kwa utaratibu wa *Quota System* iwe baina ya Tanzania Bara na Visiwani au baina ya mikoa yetu nchini, ni dhahiri kuwa hali hii itaathiri ubora wa elimu nchii, ambao ndiyo kigezo muhimu katika ushindani wa ajira.

(b) Mheshimiwa Spika, ushirikishi wa Muungano baina ya Tanzania Bara na Visiwani upo katika Idara/Mabaraza/Bodi zote zinazoshughulikia masuala ya Elimu ya Juu nchini. Idara/Mabaraza/Bodi hizo zina Wajumbe kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambazo ni pamoja na:-

- Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA)* ina wajumbe wawili (2) kutoka Zanzibar.

- Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wqa Elimu ya Juu *(HESLB)* ina wajumbe watatu (3 kutoka Zanzibar.

- Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)* wawili (2) kutoka Zanzibar.

- Kamati Ndogo ya Ushauri katika masuala ya Elimu ya Juu *(Sub Advisory Committee on Higher Education and Training* - *(SACHET)* ina wajumbe watatu (3) kutoka Zanzibar.

- Idara ya Elimu ya Juu Makao Makuu ya Wizara wapo mfanyakazi kutoka Zanzibar wawili.

- Tume ya Taifa ya *UNESCO* inao wajumbe 4 kati ya 9 kutoka Zanzibar.

(c) Mheshimiwa Spika, naomba kumthibitishia Mheshimwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Vyuo vyote vya Elimu ya Juu Nchini vinaweka kumbukumbu za wanafunzi wote wanaosajiliwa na wanaohitimu kila mwaka. Hata hivyo kumbukumbu zinazowekwa ni zile tu zinazoonyesha ni Watanzania wangapi wamedahiliwa na kumaliza katika chuo husika bila kutofautisha ni sehemu ipi ya Muungano anayotoka mhitimu.

Aidha, wanafunzi husajiliwa kwa kutumia kifupisho cha aina moja kwa wote wanaotoka nchi moja. Mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wao hutumia kifupisho T kwa kuwatambulisha wanafunzi wote wanaotoka Tanzania wanaosajiliwa chuoni hapo bila kutofautisha wanaotoka Bara au Visiwani. Hivyo siyo rahisi kufahamu wangapi

wanaotoka Tanzania Bara na wangapi wanaotoka Tanzania Visiwani. Hata hivyo kwa kuzingatia umuhimu wa kufahamu wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu wanatoka sehemu ipi ya Muungano, Vyuo vya Elimu ya Juu vitaagizwa kuanzia sasa kuweka kipengele hicho katika udahili.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza suala dogo tu la nyongeza. Aidha nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika jibu alilolitoa katika Swali Namba 56 kama alivyouliza muulizaji alisema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Zanzibar tukazane sana katika elimu na tunafanya hivyo. Katika elimu tunakazana sana.

Lakini kuna nafasi ambazo wanafunzi wa Zanzibar wanazikosa katika Elimu ya Juu na wanakosa nafasi katika Vyuo Vikuu vya Tanzania Bara. Je, utaratibu huu uko wa kutoa nafasi maalum kwa Wazanzibar ambao wame-*qualify* lakini bado wanaachwa?

**SPIKA:** Kabla ya Mheshimiwa Waziri hajajibu. Kwa kuwa neno hili kukazana lina maana isiyopendeza ndani ya jamii. Ni matumizi tu ya Kiswahili, ningeomba tusilitumie. Ahsanteni.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba wanafunzi kutoka Zanzibar hawapatiwi nafasi katika Vyuo Vikuu au Taasisi nyingine za Elimu ya Juu zilizoko huku Tanzania Bara.

Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina wanafunzi wengi sana kutoka Zanzibar tatizo ni kwamba hatuwezi kuwafahamu kutokana na utaratibu wa kudahili. Tumejaribu kuulizia Vyuo vingine kwa mfano Sokoine tumeambiwa kuna wanafunzi 9 kutoka Zanzibar, Chuo Kikuu cha Mzumbe kinao wanafunzi 7. Hata hivyo inavyoonekana wanafunzi wanapenda kusomea maeneo ambayo ni karibu na nyumbani.

Chuo Kikuu cha Zanzibar yaani *State University of Zanzibar* ambacho ni cha Serikali kinao wanafunzi karibu 400 wakati kutoka Tanzania Bara ni wanafunzi wanne (4) tu. Kwa hiyo, wanafunzi wanapenda zaidi kusomea maeneo ambayo wanatoka jirani. Sio suala la kutowachukua kutoka huku wala kule. Tunachozungumzia hapa ni kwamba elimu yetu lazima tuitoe kwa vigezo vya ushindani wa sifa. Anayekuwa na sifa awe Mtanzania Bara au awe Mtanzania wa Zanzibar anachukuliwa. Aidha wanafunzi wanapenda zaidi kwenda kwenye vyuo kulingana na taaluma, fani wanazozipenda ambazo zinapatikana kwenye vyuo hivyo.

Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia sasa tumesema tutaagiza Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu nchini ziweke hizi kumbukumbu kwa manufaa ya Muungano wetu. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimwa

Naibu Waziri. Kwa kuwa suala la taaluma sio suala la upendeleo kama watu wengine wanavyofikiria na kama Serikali ambavyo imejibu na Serikali nyingi zinafuata akili ya mtu katika kufaulu. Je kama malalamiko yapo kwamba wenzetu wa upande wa Zanzibar wanashindwa kwenda kwenye vyuo labda vya Tanzania Bara na kadhalika.

Serikali itasaidia vipi kwa upande wa wenzetu wa Zanzibar kuinua kiwango cha elimu kama ilivyo Tanzania Bara ili kusudi na wao waweze kuhimili katika ushindani wa kufaulu na kuingia kwenye vyuo hivyo? Serikali itasaidia vipi ili kuhakikisha kwamba wanaleta uwiano kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri nimekwishaeleza maana ya ushindani huu wa elimu ni kwamba bila ya ushindani katika taaaluma hatutaweza kuwa na ushindani hata katika soko huru la ajira. Kwa sababu uwe umetoka Tanzania Bara au Visiwani kama kuna *interview* lazima u-*meet* zile *demands* za *interview*.

Sasa kama kuna haja ya kuhakikisha kwamba Wazanzibar wangapi au Watanzania Bara wangapi wanaingia katika Vyuo vya Elimu ya Juu nafikiri kuna mazungumzo yanaendelea kuhusiana na Muungano. Lakini inapokuja kwenye taaluma nina wasi wasi kama tutaweza kubadilisha vigezo vya ushindani wa sifa za kujiunga na Chuo Kikuu.

Na. 142

**Uhitaji wa Kituo cha Polisi Kiwangwa**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kila msimu wa mavuno ya zao la Mananasi kwa wakulima wa Kiwangwa katika Jimbo la Chalinze, wakulima hao huvamiwa na majambazi wakati wa kuuza mazao yao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea kituo kidogo cha Polisi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kila msimu wa mavuno ya zao la mananasi eneo la Kiwangwa, Jimbo la Chalinze, matukio ya uhalifu huongezeka kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, kituo kidogo cha Kiwangwa kufuatana na daraja lake hakimo katika mpango wa kujengwa hivi karibuni. Vituo vya namna hii kwa nchi nzima,

vimekuwa vikijengwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, wananchi wa eneo la Kiwangwa kupitia Ofisi ya Mtendaji wa Kata yao walikabidhiwa mchoro wa kituo hicho tarehe 10 Aprili, 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa kituo hicho, namwomba Mheshimiwa Mbunge ahamasishe wananchi wa maeneo hayo na kwingineko ili waweze kujipanga na kuanza ujenzi wa Vituo vya Polisi kikiwemo cha Kiwangwa na Serikali itakuwa tayari kuunga mkono jitihada hizo za wananchi. Aidha, kwa wakati huu Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani litaendelea kuimarisha doria katika maeneo hayo.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ujambazi ni kero na wananchi wa Kiwangwa wameshaanza kuchanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapeleka wataalamu wa ushauri kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba sasa hivi vituo vya daraja hili Serikali haijaweka fungu kwa ajili ya kuvijenga. Lakini pale ambapo nguvu za wananchi zimeanzishwa na kuonesha mfano mzuri Serikali itaunga mkono.

Kuhusiana na kutafuta wataalamu tayari ramani tumeshaipeleka kwa Afisa Mtendaji wa Kata. Huu ndio utaalamu tosha kwa kupata ramani ile nafikiri ingetosheleza kabisa kwa wananchi kufanya shughuli zao na sisi tuko tayari kuunga mkono jitihada hizo. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa wananchi wa Kiwangwa tayari wameshachanga shilingi milioni nane (8). Na kwa kuwa Afisa Mtendaji anajua hiyo, lakini mpaka sasa kituo hicho hakijajengwa. Je, Wizara itatusaidia ili kituo hicho kijengwe kwa sababu mpaka sasa hata madawa ya kulevya yanauzwa sehemu hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kiwangwa kwa jitihada zao za kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana na yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi wake

tutazame ni kwa nini ucheleweshaji huo umetokea ili kazi hiyo ianze mara moja, kituo kipatikane na Jeshi la Polisi lifanye kazi ya kupambana na uhalifu katika eneo hilo.

Na. 143

**Barabara ya Kibiti – Mkongo, Utete na Pantonti – Utete**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya kutoka Kibiti kupitia kijiji cha Mkongo – Utete yenye urefu wa km. 40 ni mbovu sana na haipitiki kwa sababu ni ya matope lakini pia ina madaraja mabovu kama, Daraja la Ruhoi na Rambo na hakuna kivuko cha Utete, na kwa kuwa, kutokana na matatizo hayo kumeifanya safari ya kutoka Kibiti – Utete Bomani, kupitia Daraja la Mkapa, umbali wa km. 84 kuwa ndefu mno; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliwaahidi wananchi wa Utete kuwa barabara ya Kibiti – Mkongo – Utete, itatengenezwa na kivuko cha Utete kitapatikana mara moja:-

(a) Je, Serikali italihakikishia Bunge kwamba, itatekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ya kuijenga barabara hiyo, pamoja na madaraja na kuhakikisha upatikanaji wa kivuko cha Utete;

(b) Je, Serikali itaanza lini kujenga barabara ya Ndundu – Somanga ambayo inawapa adha kubwa sana wananchi wanaokwenda Mikoa ya Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu Swali la Mhe. Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibiti – Utete kupitia kijiji cha Mkongo ina urefu wa kilometa 45. Barabara hii ni kati ya barabara za Mkoa zilizopo chini yangu zinazofanyiwa matengenezo na Wakala wa Barabara *(TANROAD)* Mkoa wa Pwani. Barabara hii kwa sehemu kubwa ni ya kiwango cha udongo na imekuwa ikipata matengenezo ya kawaida ili kuiwezesha kupitika. *(Makofi)*

Katika mwaka wa fedha 2005/2006 jumla ya kilometa 13 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi 19.14 milioni. Aidha, madaraja ya Ruhoi na Rambo yamefanyiwa matengenezo ya kinga (*Preventive Maintenance*) hivyo kuiwezesha kupitika.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 barabara hii itakarabatiwa. Madaraja ya Ruhoi na Rambo yataendelea kupata matengenezo ya kinga (*Preventive Maintenance*) ili kuhakikisha kwamba barabara hiyo inapitika.

Aidha, katika mpango wa Serikali wa kununua vivuko vipya, Serikali itaanza kutenga fedha katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008 kununua kivuko kipya cha Utete. Kivuko hiki kitakachokuwa kinajiendesha chenyewe kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 50.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Ndundu – Somanga yenye urefu wa kilometa 60 itaanza kujengwa katika mwaka huu wa fedha (2006/2007) kwa mkopo kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait. Mchujo wa Makandarasi umefanyika tayari na kutumwa Kuwait mwezi Juni 2006 kwa kibali cha mwisho ambapo mkataba wa ujenzi unategemewa kusainiwa mwezi Novemba, 2006.

Nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia hali ya utekelezaji wa barabara hii muhimu kwa Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara na kumhakikishia kuwa Wizara yangu nayo haitasita kutimiza wajibu wake katika mradi huu. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza ni lile lile la awali kivuko cha Utete hakipitiki kabisa. Na hiyo ilimfanya Mheshimiwa Rais kutoa ahadi kwamba hiki kivuko kitengenezwe na barabara ipitike. Nauliza haya matengenezo yataanza lini? Swali la kwanza.

Swali la pili ni kwamba sisi Madaktari kama kuna mgonjwa mahututi huwa hatumpeleki *Assistant Nurse,* tunampeleka *Consultant* amtazame mgonjwa na aamue huyu *alhamdullilah* au atapona. Sasa namwomba katika suala la Kivuko cha Utete ni mahututi hakuna barabara pale je Mheshimiwa Waziri atakwenda mwenyewe na wakubwa wa Wizara wahakikishe kama barabara hiyo itapitika? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Serikali imedhamiria kutekeleza ahadi hiyo ya Rais ya barabara na kivuko. Nimesema kwamba kutokana na ufinyu wa bajeti mwaka huu tunaanza na barabara. Tutaijenga kwa kiwango kinachohitajika na mwaka unaofuata tutanunua kivuko. Kama kuna tatizo tu la kivuko cha sasa kupitika wataalamu watakwenda kuangalia namna gani wanaweza kufanya angalau kiendelee kufanya kazi wakati tukisubiri hiyo Bajeti ya mwaka kesho kwa ajili ya kununulia kivuko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka wataalamu waliobobea kuangalia hali ya kivuko hicho tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Na. 144

### Kuendeleza Bonde la Kilimo la Ruiche

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kigoma ni kati ya Mikoa michache hapa Tanzania inayopata mvua za kutosha na kuna mabonde ya kilimo mazuri ambayo hayaendelezwi vizuri, na kwa kuwa Bonde la Ruiche lina hekta 8000 za kilimo:-

Je, Serikali ina mipango gani kwa sasa ya kuendeleza bonde hilo kwa kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, naomba nimpongeze Mheshimiwa Serukamba, Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wa Kigoma kwa jithada wanazofanya kujitahidi kujitosheleza kwa chakula hata wakati wa ukame na kuiondolea Serikali au kuipunguzia mzigo wa chakula cha msaada. Wanachohitaji sasa ni kupanua kilimo chao, kutumia pembejeo na zana za kilimo. Baada ya pongezi hizo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bonde la Ruiche ni kati ya mabonde makubwa yaliyoko Mkoani Kigoma. Bonde hili kwa kiwango kikubwa linawanufaisha wakazi wa maeneo ya Kigoma, Ujiji na Stesheni ya Ruiche na maeneo mengi kupitia Reli ya Kati. Kwa kutambua umuhimu huo, Bonde la Ruiche limo katika mpango wa Serikali ambao utaendeleza sekta ya kilimo. Mpango huu ambao utaanza kutekelezwa mwaka 2006/2007 unatarajia kuongeza eneo linalomwagiliwa kufikia Hekta 1,000,000.

Mheshimiwa Spika, tathmini za awali zilionyesha kuwa, tatizo kubwa katika bonde hili ni kuwepo kwa mafuriko ya Mto Ruiche. Jitihada nyingi za kitaalamu zimekuwa zikifanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuunyosha mto ili uelekee ziwani na kuchimba mifereji ya kutoa maji ndani ya bonde *(river draining and drainage canals*). Hata hivyo, baada ya kufanya uchunguzi kwa kutumia wataalamu waelekezi, mapendekezo yaliyotolewa yanaelekeza kwamba, lijengwe bwawa kubwa kwenye sehemu iitwayo Nyangova.

Mheshimiwa Spika, mipango ya Serikali ni kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kufanya upembuzi yakinifu na hatimaye kupata gharama za ujenzi wa bwawa hilo. Katika mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu imepanga kuanza na kazi ya usanifu (*Design)* wa bwawa na baada ya usanifu, gharama halisi za ujenzi wa bwawa zitajulikana.

Bwawa la Nyangova likijengwa litasaidia kuzuia mafuriko na kuhifadhi maji yatakayotumika kumwagilia mashamba wakati wa kiangazi na katika vipindi vya ukame. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amekubali umuhimu wa bonde hilo. Katika mazingira ambayo nchi hii mwaka huu ilikuwa na njaa na tunalo bonde kama la Ruiche ambalo lingeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana katika kutatua tatizo la njaa katika nchi hii. Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni suala la dharura kuliendeleza bonde hili sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tayari tumeshatambua na tumetambua kwa muda mrefu kwamba bonde la Ruiche ni muhimu sana. Sio tu linalisha maeneo niliyoyataja. Linalisha karibu ukanda wote kwa kutumia Reli ya Kati na kwa hivyo jitihada zinazofanywa sasa hivi pamoja na kuiweka katika mpango ambao ni wa muda mrefu lakini bado tunaendelea kutoa fedha za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika ngazi ndogo ndogo au kwa wakulima wadogo waliopo pale. Pale ambapo tutakuwa tayari kuendeleza kwa *scale* kubwa baada ya kupata fedha katika mpango bonde la Ruiche nataka nimhakikishie kwamba litapanuliwa litaendelezwa na kufikia kiwango ambacho anakihitaji Mheshimiwa Mbunge.

Na. 145

**Mpango wa MEMKWA**

**MHE. DR. LUCY S. NKYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mojawapo ya malengo ya Taifa ya kuboresha elimu ni kuhakikisha kwamba, watoto wote wenye umri wa kwenda Shule wanaanza shule; na kwa kuwa, Serikali imenzisha mpango wa MEMKWA ili kuwapatia watoto wenye umri mkubwa fursa ya kupata elimu:-

(a) Je, kuna vituo vingapi vya MEMKWA hapa nchini; na vinahudumia watoto wangapi?

(b) Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kuendeleza mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kabla ya kujibu swali la Dr. Lucy Sawere Nkya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, MEMKWA ni Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa ulioanzishwa mwaka 1997 kwa majaribio katika Wilaya za Masasi na Kisarawe. Mwaka 2001 Mpango huu ulienezwa hadi kufikia Wilaya tano zikiwemo Songea Vijijini, Musoma Vijijini na Ngara. Mwaka 2005 mpango ulienezwa katika Wilaya zote nchini chini ya Mkakati wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kugharamiwa na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM).

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba kujibu maswali (a) na (b) ya Mheshimiwa Nkya, kama ifuatavyo:-

(a) Sasa hivi vituo 7,751 nchini kote vinavyohudumia watoto 532,419.

(b) Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kuendeleza MEMKWA.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kwa kuwa vituo vya MEMKWA vipo kama sehemu ya Shule ya Msingi mahali pengi hapa nchini. Na kwa kuwa Walimu wanaotumika katika Mfumo Rasmi wa Shule za Msingi wanaambiwa waendeleze hivyo vituo inaelekea kwamba hawa Walimu wanatoa umuhimu zaidi kwa wale watoto wa Shule ya Msingi ambayo ni rasmi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Shule Maalum za MEMKWA ziwe na uongozi maalum hapa nchini ili kuboresha elimu ya hawa watoto?

(b) Kwa kuwa watoto wa MEMKWA wanasoma miaka miwili na baada ya hapo wanafanya mtihani wa darasa la 4 ili waweze kuingia kwenye Mfumo Rasmi wa Shule. Na kwa kuwa wengi wao wanashindwa huo mtihani na hawaendelei.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga pia vituo vya mafunzo ya Ufundi vya MEMKWA ili hao watoto wapate stadi za maisha na stadi za kuweza kufanya kazi waweze kujitegemea?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli madarasa ya MEMKWA mengi yamekuwepo katika shule za msingi kwa sababu walimu hawa wanaofundisha katika madarasa ya MEMKWA wanafundishwa katika vyuo vyetu vya kawaida na madarasa haya yanatolewa katika mazingira hayo ya shule. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hawa wanafunzi wa MEMKWA madarasa yao yanaweza pia yakatengenezwa nje ya madarasa haya ya shule za msingi ili waweze kufundishwa vizuri.

Suala la pili kuhusu wanafunzi wa MEMKWA wafundishwe ufundi ili waweze kujipatia ujuzi wa kuweza kujiajiri. Hili ni wazo zuri na kwa sababu Wizara yetu ya

Elimu bado iko katika mchakato wa kuweza kuunganisha Idara ya *VETA* na Wizara ya Elimu, suala hili tutalizingatia kwa makini ili hata hawa wanafunzi wa MEMKWA waweze kufundishwa stadi mbalimbali za maisha ili waweze kufanya vizuri katika maisha yao.

**SPIKA:** Ingawa muda wa kawaida wa maswali umekwisha lakini kwa madhumuni ya kufidia muda tuliotumia katika shughuli nyingine leo asubuhi basi naomba nimwite Mheshimiwa atakayeuliza swali la mwisho kwa asubuhi hii kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika.

Na. 146

**Ofisi ya Ubalozi wa Msumbiji Nchini**

**MHE. JUMA A. NJWAYO ( K.n.y. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, raia wetu wengi hutembelea Msumbiji mara kwa mara na raia wa Msumbiji hutembelea nchini mwetu Tanzania mara kwa mara, na kwa kuwa, raia wa pande zote mbili hupata taabu sana kupata hati za kusafiria kama *visa* na hati nyinginezo:-

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika sasa waweze kuongea na Serikali ya Msumbiji ili waweze kufungua Ofisi ya Ubalozi Mdogo wa Msumbiji Mjini Mtwara hasa ukizingatia kwamba, tangu enzi za ukoloni kimetengwa kiwanja kwa ajili ya Ofisi za Ubalozi Mdogo wa Msumbiji Mjini Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. (Mstaafu) George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Jimbo la Newala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba raia wetu wengi hutembelea nchi jirani ya Msumbiji mara kwa mara na vivyo hivyo raia wengi wa Msumbiji huitembelea Tanzania mara nyingi , hivyo kuhitaji huduma kama vile *visa* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuimarisha zaidi mahusiano kati ya Tanzania na Msumbiji, ikiwa ni pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma kama *visa* kama Mheshimiwa Mbunge alivyosisitiza, Serikali imekwisha anza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Msumbiji zilitia saini Mkataba wa kufutiana *visa* (*Visa Abolition Agreement*) mnamo tarehe 25 Oktoba 2005 wakati wa ziara nchini mwetu ya Mheshimiwa Armando Guebuza, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliweka saini Mkataba huo kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na kwa upande wa Msumbiji Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hiyo aliweka saini kwa niaba ya Serikali ya Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Msumbiji imeshaijulisha Serikali ya Tanzania kuhusu kuridhiwa kwa Mkataba huo na Bunge la Msumbiji. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hivi sasa inakamilisha taratibu za kuwasilisha Muswada wa Mkataba huo kwenye Bunge lako Tukufu ili nalo liweze kuuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali zetu mbili kufutia na utaratibu wa *visa,* wazo la Mheshimiwa Mbunge kuhusu Serikali ya Msumbiji kufungua Ofisi Ndogo ya Ubalozi huko Mtwara ni zuri sana. Hili ni suala la Serikali ya Msumbiji yenyewe kulifanyia uamuzi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaufurahia uamuzi kama huo na iko tayari kusaidia kurahisisha mchakato wa kufungua ofisi hiyo mjini Mtwara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wakati huu hatuna kumbukumbu zenye kuthibitisha kwamba kuna kiwanja kilichotengwa mahsusi kwa ajili ya Ubalozi Mdogo wa Msumbiji mjini Mtwara, tuna imani kwamba kwa ushirikiano na mamlaka zinazohusika kiwanja hicho kitaweza kupatikana hapo Msumbiji itakapoamua kufungua Ofisi hiyo mjini humo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa umeonyesha nia ya kushirikiana na Serikali ya Msumbiji ili kuwepo na ofisi ndogo Mtwara. Je, Wizara inataka kuliambia nini Bunge hili na kwa kuwa Bunge hili ni la Ari Mpya, Kasi Mpya na Ngvu mpya, kwamba kwa muda gani itakuwa tayari imeshaanza kufanya jitihada za kuwepo na ofisi ndogo pale Mtwara?

Pili kwa kuwa maingiliano haya ya wananchi wa Msumbiji na Tanzania yamekuwa yakiendana pia na biashara iliyo holela ya bidhaa mbalimbali za Tanzania na Msumbiji. Je Serikali inaweza kuliahidi Bunge hili kwamba itaanza *Trade Agreement* kati ya nchi hizi mbili ili Serikali iweze kupata mapato na hivyo kujenga uchumi wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyeleza katika jibu langu la msingi ni juu ya Serikali ya Msumbiji kuamua kufungua ubalozi wake Mtwara. Hilo sio suala la Tanzania, Tanzania itatoa ushirikiano na kila msaada unaowezekana kuwezesha Serikali ya Msumbiji kufungua ubalozi wake Mtwara. Pili, Serikali itafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba ushirikiano wa kibiashara kati ya Msumbiji na Tanzania unaendelezwa na kukua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamekwisha. Sasa ni Matangazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala Mheshimiwa George M. Lubeleje, anatangaza kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wakutane leo tarehe 4 Julai 2006 katika Ukumbi Namba 231, Jengo la Utawala ghorofa ya pili saa tano asubuhi hii.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, wakutane leo katika ukumbi huo huo namba 231 ila ni saa saba mchana.

Mheshimiwa Balozi wa *Amani Forum,* Mheshimiwa Paul Kimiti anapenda akutane na wanachama wa Taasisi hiyo ya kimataifa ya *International Federation for World Peace* leo kwa muda mfupi katika chumba cha *CPA*, *Common Wealth Parliamentary Association* mara baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania anaomba Kamati ya Utendaji ya *UPNAC* itakuwa na mkutano mfupi kwa ajili ya maandalizi ya mkutano wa *GOPAC* na ujio wa Mwenyekiti wa *GOPAC* Kimataifa ambaye anatarajiwa kuwasili wiki ijao, ikutane leo mara baada ya kipindi cha maswali na majibu katika jengo la utawala ghorofa ya kwanza chumba namba 133 mara baada ya kipindi hiki.

Waheshimiwa Wabunge ninao wachangiaji, 13 ambao nadhani tutaweza kutosheleza kwa kufika saa kumi na moja na nusu ambapo Mheshimiwa mtoa Hoja na Naibu Mawaziri wataanza kujibu hoja. Kwa hiyo, niwataje kwa sababu wengine wanakuwa hawapo, kwa hiyo nimeweka orodha fupi mbadala ili hawa waliotajwa kama hawapo basi hawa wengine watachukua nafasi yao.

Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Idi Azzan, Mhesimiwa Siraji Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Manju Salum Msambya.

Waheshimiwa Wabunge, sasa wale ambao wamekaa kama *stand by* hivi ni Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Damas Nakei. Kwa sasa nitamwita Mheshimiwa Richard Nyaulawa atafuatiwa na Mussa Azan Zungu na wakati huo huo Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, ajiandae. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Miundombinu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika hotuba ya Miundombinu. Awali ya yote ningetaka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Manaibu Mawaziri wote wawili na wafanyakazi wale wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya kwa kuitayarisha Bajeti hii kwa kipindi kifupi. Kwa hakika ninaimani kwamba Bajeti hii au hotuba hii ni nzuri ukizingatia ukubwa wa nchi ya Tanzania na matakwa ya matarajio ya Watanzania katika kupata huduma ya miundombinu. Imetayarishwa kwa kuzingatia sera za nchi na hasa kwenye upande wa usafirishaji lakini vilevile imechukulia hali halisi ya Ilani na ahadi ambazo Mheshimiwa Rais alikuwa amezitoa. Mambo hayo yamejitokeza katika Bajeti hii. Kwa hiyo, nawapa hongera sana. (*Makofi*)

Katika Bajeti hii sikuwa nategemea kwamba naweza kuona dira ya miaka mitatu, minne, mitano kwa sababu ni Bajeti ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, kitu ambacho kilikuwa kinaonyeshwa hapa ni vitu mbalimbali ambavyo vinaweza kufanywa ili kuweza kuwaridhisha wananchi waTanzania katika kuongeza ufanisi katika shughuli za miundombinu. Miundombinu ni Wizara kubwa na ina mambo mengi na inawezekana kwamba mahitaji na malalamiko na ya Wabunge yanaweza kuwa ni makubwa sana, lakini vilevile inawezekana kwamba kutokana na ukubwa wake kulikuwa na matatizo makubwa ya huko nyuma katika utekelezaji wa mambo mbalimbali ambayo yako chini ya miundombinu.

Kuna vitu mbalimbali ambavyo vimeweza kuleta matatizo kama *ATCL* ukichukua *TTCL*, *ATCO*, labda na matatizo ya reli, yote haya yanaweza kuwa ni matatizo lakini nina imani kwamba wenzetu ambao wako katika nafasi mbambali katika Wizara ya Miundombinu sasa hivi wanafanya kazi kubwa ya kuweza kurekebisha matatizo haya ambayo yalikuwepo huko nyuma. Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri kama tutawapa ushirikiano tufanye kazi kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba mipango iliyopo mbele yetu inaweza kufanyika kwa urahisi.(*Makofi*)

Lakini cha msingi cha kuweza kuchukua hapa ni kwamba hii mikataba ya huko nyuma imetupa matatizo makubwa sana. Mikataba mibovu ni gharama kwa Serikali, na wananchi kwa ujumla. Fedha ambazo Serikali inachangia *ATCL* kwa leo, fedha ambazo zinachangiwa na Serikali kwa upande wa *IPTL* na fedha ambazo inachangia kwa upande wa *TANESCO* zote hizo ni fedha nyingi sana ambazo zisingekuwa zinatumika endapo mikataba ya huko nyuma ingekuwa ni mizuri.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata tunapozungumzia kuhusu ufinyu wa Bajeti yetu tunajua kabisa kwamba kuna fedha zingine ambazo zinapotea kwa sababu hazikutumika sawa sawa kutokana na mikataba ambayo ilikuwa ni mibovu. Changamoto kwa wenzetu kutokana na miundombinu kuwa ni Wizara kubwa ni kuhakikisha kwamba mikataba ambayo itakayokuwa inaingiwa inakuwa ni mizuri na ambayo inaweza kutekelezwa sawasawa. Kwa hiyo, awamu ya nne tuipe nafasi ya kuweza kuanza kwa kuwapa changamoto kwa kuwaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika ukarabati wa barabara ni muhumi hasa katika Jimbo langu la Mbeya Vijijini pamoja na sehemu nyingine kama Wabunge wengine walivyosema. Lakini Mbeya Vijiji tunazalisha mahindi kwa wingi sana na sisi kwa njia moja au nyingine tunailisha Dar es Salaam. Viazi vingi vinatoka mbeya, mchele unatoka Mbeya, kawaha inatoka Mbeya, pareto, inatoka Mbeya. Yote haya hayazailishwi mjini yanazalishwa vijijini ambako kunahitaji miundombunu ya barabara safi ili tuweze kusafirisha mazao hayo kwa urahisi zaidi na kuweza kufika sokoni kwa ghrama nafuu.

Mheshimiwa Spika, huwa tunapata matatizo sana wakati wa mvua kuweza kusafirisha mazao kwa sababu barabara zetu ni mbaya. Barabara ya kutoka Mbalizi kwenda Ilembo ambako kuna mazao mengi sana ni mbaya sana, wakati wa mvua haipitiki kabisa. Barabara ya kutoka Mbalizi kwenda Lushewe mpaka Chunya ni barabara mbaya sana. *(Makofi)*

Lakini vilevile barabara ya kwenda Igoma ambako kuna Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ambayo kwa wakati huu haitumiki sawa sawa kwa sababu barabara huwa haipitiki kwa urahisi. Ningeomba rai kwa wenzangu nimeona kwamba safari hii labda katika Bajeti haijaonyeshwa sawasawa lakini angalau kwa siku zijazo ningeomba barabara hizo ambazo ni muhimu katika kuzalisha mawazo na kuweza kuhakikisha kwamba yanasafirishwa katika masoko yanafanyiwa kazi kubwa.(*Makofi*)

Hata kama tunasema tungekuwa tunasema tungekuwa tunahitaji lami lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti basi ziwe ni barabara ambazo zimetengenezwa kwa changarawe lakini zimejengwa kwa ufanisi wa hali ya juu. Sasa hivi ujenzi wa barabara za vijijini sio nzuri ufanisi wake sio mzuri. Kwa hiyo, tutawaomba wenzagu waweze kuangalia jinsi ambavyo wanaweza kutusaidia ili tuhakikishe mazao hayo yanaweza kuzalishwa vizuri na kuyafikisha kwa wateja kwenye masoko yao kwa gharama nafuu.

Mawasiliano ni kitu cha muhimu na kwa kweli mawasiliano ya mkononi kwa wakati huu yana wateja wengi na natumaini wameshafika zaidi ya milioni tatu. Mawasiliano hayo ni muhimu kwa sababu yanasaidia sana watu vijijini kuweza kufanyabiashara zao bila matatizo yoyote. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana watu wa *Celtel* kwa kuwa mara baada ya kuwaomba kuweka minara katika sehemu fulani ambako kulikuwa na matatizo makubwa ya mawasiliano. Sehemu za Ilembo wameweza kufanya kazi hiyo kwa muda mfupi sana. Nawapa hongera sana. Lakini vilevile najua kwamba sasa hivi wameanza kufanya kazi hiyo sehemu ya Igoma, ambako ninauhakika kutakuwa na mawasiliano mazuri sana vilevile. Lakini bado hawajaanza kufanyakazi hiyo sehemu ya Isuto ambako vilevile kuna matatizo ya usafiri na kule kuna kahawa nyingi sana ambayo ingeweza kusafirishwa na tunahitaji mawasiliano ambayo ni mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ambalo nataka kueleza hapa ni kwamba wenzetu ambao wako kwenye mawasiliano wakiweza kuwa wanachukua majitaji kwa urahisi na kuyafanyia kazi tutakuwa tumeongeza ufanisi sana katika kuhakikisha biashara za Watanzania zinainuka na zinafanyika kwa uzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi wa kijiografia unategemea sana mambo ya bandari. Bandari ya Dar es Salaam ni ya muhimu, kwa wakati huu Wachina wanawekeza kwa kiwango kikubwa sana katika bandari ya Mombasa, na wanategemea kwamba bandari ya Mombasa wangetaka iwe ni bandari kubwa na bora ambayo inaweza kutoa huduma nzuri kwa nchi ya Uganda, Rwanda, Burundi pamoja na Kongo na sisi ndiyo nchi hizo hizo ambazo tunataka kuzifanyia kazi kwa upande wa magharibi. Lakini bado hatujaanza sawasawa katika kujitayarisha kwenye suala la kuboresha vizuri zaidi bandari zetu. Natumaini tunastahili kukarabati bandari ya Tanga. Tunahitaji pia kukarabati bandari ya Kasanga, Kigoma na kuzifanya ziweze kuhudumia nchi za jirani kwa ufanisi mkubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bila kuzitengeneza hizi bandari hata kama tunataka kwenda kwenye ushindani wa kibiashara wa kimataifa itakuwa ni vigumu. Ni pale tu ambapo kunaweza kuwa na ufanisi mkubwa katika hizi bandari na watu wakafanyakazi kwa ari mpya, nguvu mpya na kwa kasi mpya. Hapo ndipo tunapoweza kuhakikisha kwamba ushindani ambao wenzetu wa nchi jirani wanajaribu kuleta basi tunaweza kuukabili sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nina uhakika kabisa kwamba hata kama tungekuwa tumekarabati bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Kasanga, ili kuhakikisha mizigo kutoka sehemu za Mbeya inaweza kupitia kwenda Congo, bandari ya Kigoma kwa kwenda Rwanda na a Burundi na bandari ya Mtwara. Lakini bila kuwa na reli ambazo zimetengenezwa vizuri hatuwezi kusafirisha mizigo yetu. Itakuwa ni kazi bure kujaribu kutengeneza bandari bila kukamilisha ujenzi wa reli. Kwa sababu ni vitu ambavyo vinategemeana. Reli yetu ya kati inahitaji kukarabatiwa kwa kiasi kikubwa sana. Ili kuhakikisha kwamba mizigo mingi inaweza kusafirishwa kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma na kwenda nchi za jirani.(*Makofi*)

Reli ya *TAZARA* katika Bajeti wametenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa reli ya *TAZARA*. Natumaini hiki ni kiasi kidogo cha kuweza kutumika katika ukukarabati wa reli. Lakini ninauhakika kwamba kuna mizigo mingi sana kutoka Zambia, Malawi ambayo yote inahitaji kupita kwenye reli ya *TAZARA* ili kuweza kufika kwenye bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi za nje. Lakini kuna mizigo mingi ambayo inatoka nchini za nje inapita katika reli hii kwenda katika nchi jirani itakuwa ni vizuri pamoja na sisi kama upande wa Mbeya kama tukiweza kuiga mfano wa kuwa na bandari ya nchi kavu kama ya Isaka ambayo inafanya kazi vizuri sana, na natumaini bandari ya Isaka inastahili kupanuliwa ili iweze kutoa huduma kubwa zaidi kwa nchi za jirani za Rwanda na Burundi. Lakini kwa upande wa Mbeya tulikuwa tunahitaji kuwa na bandari ya nchi kavu ambayo ingeweza kuwa pale Mbeya ili tuweze kuwahudumia jirani zetu wa Malawi, Zambia na Congo kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kwamba haya yakiweza kutekelezwa inaweza kusaidia sana katika kuongeza kukua uchumi wetu katika suala la usafirishaji. Utengenezaji wa reli gharama za kutengeneza kilomita moja ya reli ni sawa na gharama za kutengeza kilomita moja ya barabara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tusiwe tumekazania tu kwa upande wa barabara lakini tunajua kabisa kwamba usafirishaji wa mizigo ambao ni wa mwendo mrefu unahitaji reli hauhitaji barabara. Kwa hiyo, tuangalie kwamba tunaziangalia hizi reli zetu na kuweza kujenga nyingine kwa sababu gharama ya kujenga ni ile ile sawa na zile za barabara. Lakini uzuri ambao unaweza kutokea ni kwamba kama tukiweza kujenga reli basi reli hizo zinaweza kukodishwa zile *wagons* zikawa zinatolewa na watu binafsi lakini miundombinu ya reli ikawa mali ya Serikali na wakalipa kiasi cha kutosha kama mapato kwa Serikali kwa kuweza kutumia reli hizo, mpango ambao natumaini ambao kwa sasa hivi ambao unataka kutumika kwenye reli ya kati.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeshauri wenzetu waweze kutusaidi katika kuhakikisha kwamba siku zijazo tunaweza kujenga reli hasa kutoka Tanga kwenda Musoma na vilevile kutoka Mtwara kwenda sehemu za Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nilitaka kuunga mkono hoja ya kujenga barabara ya kutoka Tarakea kwenda Marangu kwa sababu ni barabara inayotumika kwa mambo ya utalii. Mwenzetu Mheshimiwa Mwanri jana alitueleza kwa kiwango kikubwa kidogo kuhusu umuhimu wa kuweza kujenga barabara mahali ambapo panakuwa na utalii.

Barabara hiyo mwaka jana iliweza kusafirisha watalii 32,000 ambayo ni takriban dola za kimarekani milioni 17 ziliweza kupatikana kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, ni barabara muhimu na natumaini kwa kufanya hivyo bila shaka tutakuwa tumekwenda kwenye ushindani kamili na Kenya ambayo wamejaribu kutengeneza barabara yao mpaka Rongai kwa kiwango kikubwa sana ili watalii wengi kutoka Kenya waweze kwenda kuangalia Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tusipojiandaa kuwa na barabara nzuri ambayo inakwenda Mlima Kilimanjaro basi inawezekana kwamba ushindani wetu utakuwa dhaifu sana. Kwa hiyo, katika msingi huo naunga mkono ujenzi wa barabara hiyo tukielewa kwamba lengo hapa ni kuhakikisha kwamba tunashinda katika ushindani kibiashara ya Utalii wa watu kutoka Kenya wa kuweza kuleta watalii kuja Tanzania. Mlima wetu ni mkubwa na tunaimi kwamba tunaweza kupata kiasi kikubwa sana cha fedha kutokana na Utalii wa mlima huo wa Kilimanjaro.(*Makofi*)

Nilitaka kumalizia kwa kuishukuru sana Serikali kwa kuweka bilioni 4.35 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa Songwe. Uwanja wa Songwe utaleta manufaa makubwa sana na utafumua uchumi wa Mikoa ya Mbeya na wa Mikoa ya Kusini kwa ujumla. Kwa hiyo, tuna uhakika tukiweza kujipanga sawa sawa, tukashirikiana kwenye ngazi ya kitaifa na kwenye ngazi ya Mikoa, tunaweza kufanya kazi nzuri sana ya kuweza kuhakikisha kwamba uwanja huo tukijitayarisha tutaupokea na utaweza kuleta changamoto kubwa sana katika kukuza uchumi wa sehemu ya kusini mwa Tanzania kikamilifu. Nina uhakika kwamba dakika zangu ndiyo kwanza zinaisha nilitaka kuwapongeza wenzangu kwa kuweza kutayarisha Bajeti hii ambayo ni kwa muda mfupi ni Bajeti makini na imeweza kukidhi mahitaji ya wengi na hasa kwa kuweza kuchukulia

kwamba kulikuwa na ahadi nyingi ambazo zilitolewa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge, na nyingi zimeonyeshwa katika Bajeti ya safari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MUSSA AZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti mpya wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na viongozi wenzake wote waliochaguliwa kukiongoza Chama cha Mapinduzi katika Taifa letu.

Pili nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa jitihada kubwa aliyoifanya kujenga na kuhakikisha asilimia 70 ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Mkoa wa Dar es Salaam wanapata shule na wanasoma. Inaweza kuwa hapa si pake lakini nitamtumia ujumbe wa haraka haraka najua anasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mpango wa kuhujumu mpango wote huu leo wa wakaguzi wa shule wa Serikali wanaanza kuzifunga shule hizi na wanaanza kuzuia wanafunzi wasiingie kwa sababu hazijakidhi *standards* wanazozitaka. Tunakubali kabisa kila shule lazima iwe na *standards* zake. Lakini shule hizi zimejengwa kwa *operation* maalum ya kusaidia na kuokoa watoto ambao sasa hivi walikuwa wameshaanza kuzagaa mitaani wamehifadhiwa kusoma ili waje kuwa viongozi wa Taifa hili. Tunaomba watendaji na wakaguzi hawa wasitishe mpango huu wakielewa shule hizi zimejengwa kwa *operation* maalum iliyofanywa na Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mzee Yusuf Rajab Makamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza hotuba ya Waziri wa Miundombinu, lakini vile vile niseme kitu kimoja, ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne, ilikuwa ni kuheshimu na kuendeleza miradi iliyoachwa na Awamu ya Tatu. Sasa, Utawala Bora ni kuheshimu uongozi unaochukua na uongozi ambao unakupisha. Kuna miradi ambayo haikukamilika mwaka 2005 na bajeti hii sasa ya Mheshimiwa Basil Mramba ya Wizara ya Miiundombinu, inagusia maeneo ambayo hayakukamilika mwaka 2005. Ni wajibu wa Mheshimiwa Basil Mramba, kuendeleza mipango hiyo ili iweze kumalizika na ahadi zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka 2005 ziweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Zakia Meghji, itatoka mwaka huu itaanza mwezi wa Tisa. Waheshimiwa Wabunge, kuanzia mwezi wa tisa, ni wajibu wetu sasa kufuatilia mipango yetu yote, ambayo tunataka ianze kufanyiwa kuanzia mwaka ujao na kuendelea mpaka 2010.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kuwapongezaWabunge wote waliochangia. Kwa kweli hasa Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi, alinifurahisha sana jana kwa michango yake na ku-*quote* wazee wa zamani, akina Carl Max, pamoja na Lenin, kwa kuonyesha kweli sasa hivi chama chetu kimepata viongozi ambao wataisaidia Serikali katika kutekeleza mipango yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi *by profession* ni *Engineer* wa Ndege. Huwa napata masikitiko makubwa sana, kuona Shirika la Ndege Tanzania linazidi kufa na linakufa. Mimi, ningeishauri Serikali kama inataka utaalam mwingine, sisi tupo hapa kuwasaidia, ili na sisi tutoe michango yetu, Shirika hili lifufuliwe upya na liweze kuwabeba Watanzania. Kuna nchi jirani sasa hivi ndogo sana, matangazo yao yanaonekana kwenye mpaka *CNN* na *BBC*. Leo sisi tumekaa lakini bado Shirika hili linakufa, tunaingia Mikataba mibovu. *Service* ndogo tu ya kawaida ya ndege, inaenda kufanywa Afrika Kusini, gharama ya mafuta *up and down* zinagharimiwa na nchi yetu, pamoja na kuzidi kulitia hasara Shirika hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sasa, Wizara hii inayohusika ianze sasa kutafuta njia ya kuliokoa Shirika hili, ili tuwe na *National Flag* ya kuwa na sifa ya nchi yetu kuwa na Ndege zetu. Si vizuri kuwa na Timu ya Taifa, inakwenda kucheza nchi nyingine ikienda na ndege za kukodi. Ni vizuri tukishuka na ndege yetu, tunaonyesha ile hamasa na kutisha wapinzani katika nchi tunazokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la barabara limezungumziwa na Wabunge wengi sana na mimi naliunga mkono. Ni bora sasa hivi kuwe na mpango maalum, *operation* maalum ya kufufua na kutengeneza barabara zetu. Mimi siyo niliyepanga Mawaziri, lakini laiti ningeweza kutoa wazo, hili suala la barabara lingepata Waziri wa peke yake, ambaye ndiye atakayekuwa anawajibika na barabara na masula ambayo yanahusiana na suala la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakosa mapato mengi sana sasa hivi kwa kutokuwa na barabara nzuri. Leo, mizigo ya Malawi inashughulikiwa na Bandari ya Mombasa, kutokana na barabara zetu kuwa ni mbovu.

*Transit Trade,* chombo ambacho kingeweza kutusaidia kutupatia mapato mengi sana kwenye Taifa letu, sasa hivi tunaachia nchi za jirani kuchukua mpango huu. Hivi kweli watendaji wa Serikali yetu, wanashindwa kuwa na *Vision* au kuweka *writeup* ya kupata wawekezaji kuboresha bandari zetu ili tuweze kupokea mizigo hii na kuitoa ili kuipeleka nchi za jirani. Napata wasi wasi, mara nyingi huwa tunalaumu Wakurugenzi na Madiwani, lakini kuna utendaji mbovu wa baadhi ya watendaji kwenye Serikali Kuu. Uzalendo wao ni mdogo na wengi wao hata suala la neno uzalendo, hawalijui. Kuna umuhimu mkubwa sana baadhi ya watendaji wa Serikali, wakapewa mafunzo maalum ya kuweka maslahi ya Taifa kwanza kabla ya maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makampuni ya simu nchini mwetu, wengi wao wanatengeneza faida nje ya utaratibu wa faida. Tunapotangaziwa na Shirika la Simu kuwa dakika moja ni dola moja, basi utakuta ile dakika ya saa na dakika ya simu, zinapishana. Dakika ya simu ni sekunde 30, lakini dakika ya saa ni dakika moja, kwa maana ya sekunde 60. Kwa hiyo, huwa tunapoteza pesa nyingi sana kwa kuambiwa kuwa tunalipia dakika moja, kumbe tunalipia sekunde 30 tu.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye suala la barabara, yamezungumzwa mengi sana na Wabunge wenzetu kutoka maeneo mbalimbali. Wana haki kabisa ya kusema. Wana haki na wanastahili wapongezwe na wapatiwe hizi barabara. Lakini *end of the day*, mazao yote na vifaa vyote hivi vinaishia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Barabara za Dar es salaam zina hali mbaya sana. Sasa, tumeambia kuwa Waziri amepewa kazi maalum ya kuwa na programu ya kutengeza barabara za Dar es Salaam, kwa maana ya kutafuta pesa ili barabara za Dar es Salaam ziweze kuwa na thamani kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tukitengeneza barabara zetu, nyumba za wanachi wetu zinapanda thamani. Nyumba zikipanda thamani, kodi za majengo zinapanda, Halmashauri zitafaidika sana. Kwa hiyo, ninaomba, mpango huu wa kutaka kuboresha barabara za Dar es Salaam ufanywe kwa uadilifu na uangalifu, sababu isije ikawa kama hadithi nyingine, pesa zinapatikana kwa Dar es Salaam lakini badala yake zinapelekwa sehemu nyingine kwa maslahi ya mtu binafsi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna barabara ya Uhuru. Barabara hii ina historia kubwa sana katika Mkoa wa Dar es Salaam, ndiyo inayopitisha Viongozi wa Kitaifa na viongozi wa nchi za nje. Barabara ina hali mbaya sana. Tunaomba Waziri na tunamwomba Waziri Mkuu, kwa umuhimu wa barabara hii, angalau atafute pesa za ziada za kuikarabati, kupunguza msongamano na kurudisha heshima ya jina la Barabara hii ya Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Dar es Salaam hatuna madini ya dhahabu wala almasi. Lakini, wenzetu sasa wanaanza kulipwa fidia na makampuni ya madini katika Wilaya zao. Sisi, tuna bahari. Hii bahari lini sasa Serikali itaanzisha *Port Authorities,* ianze kuwalipa Halmashauri angalau *token* ya kuwa sisi tuko katika Mkoa ule na bahari ndiyo mali asili ya Mkoa wetu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, niipongeze Serikali kwa kuweka Kivuko kipya katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, kwa wakazi wa Kigamboni. Hii ni hatua moja, ambayo inaonyesha namna ambavyo Serikali inavyowajali watu wake. Lakini nataka kupendekeza, Kivuko hiki kikija ni kikubwa sana, naomba Serikali sasa iwafikirie wale waendao kwa miguu, wasilipe nauli katika kivuko hiki. Magari na Pikipiki, tukitumia Kivuko hiki, inatosha kabisa kugharimu na kukiendesha Kivuko bila kuwagusa waendao kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, sasa hivi utendaji katika Pantoni hizi unatia mashaka. Inapotokea dharura na mimi nime-*experience* wakati nakwenda Kigamboni, *boat* hii ikizimika, watendaji kwenye *boat* hii hawafahamiki kwa sababu hawavai *uniform*. Kwa hiyo, yule mtu wa kuongoza au kuwasaidia watu ambao wako kwenye *boat* ili wasiweze kupata matatizo au kuwa na wasi wasi, hafahamiki anayeongoza ni mtu wa kawaida au mhudumu ndai ya pantoni hizi. Kwa hiyo, ninaomba hao wahudumu wawe na *uniform* maalum na wakivaa *uniform* maalum watakuwa na *authority* ya kuonyesha kuwa sasa, huyu akitoa agizo anatoa agizo la kitaalam na kunusuru ili watu wetu wasiweze kupata ajali au kuweza kupata *accident* ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali peke yake, haiwezi kujenga miundombinu. Lazima sasa tuwe na *Vision* ya kukaribisha wawekezaji, kuwa na *writeup* nzuri za kuweza kusaidia. Katika Mkoa wa Dar es Salaam, tukipewa sisi kibali na Serikali, kwa mapato tunayoyapata Dar es Salaam na kuandaa nafasi ambazo tunazo za Halmashauri zetu za Dar es Salaam, tuna uwezo wa kukopa *World Bank* na tukalipa mikopo hii ya *World Bank,* kwa kodi za majengo ambazo tunapata katika Mkoa wa Dar es Salaam. Dar es Salaam peke yake, kwa mwaka tunapata kodi za majengo takriban labda ni shilingi bilioni tatu. Sasa, tukipewa kibali na Serikali, tunaweza kuisaidia Serikali tukajenga barabara zetu kwa vyanzo vya kodi zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba, huu ni ujumbe wakaufanyie kazi, kama wanaweza, sababu tukiwa na barabara nzuri, majengo yatapanda thamani na yakipanda thamani, tutaongeza kodi za majengo. Kwa hiyo, mkopo huu utakuwa–*serviced* na kodi za majengo. Tunaomba, Waziri alichukue hili na akalifanyie kazi, halafu atatuambia kama itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini, vile vile naishukuru tu Serikali, kwa kuwa sasa wanaandaa mpango vile vile mzuri wa barabara za Dar es Salaam. Tunaomba mpango huu uanze mapema ili wakaazi wetu wa Dar es Salaam wawe na imani kweli wameambiwa kitu ambacho kitatekelezeka. Ukienda Upanga, Kinondoni, Shariff Shamba, Bungoni, Temeke, Gerezani, Keko, barabara zinatia aibu sana. Sura ya nchi yetu, Makao Makuu yetu ni Dar es Salaam, Watalii kabla hawajakwenda Mikoa mingine huanzia Dar es Salaam. Wanapoona Dar es Salaam inapendeza, watakuwa na uhakika na huko vile vile wanakokwenda kutakuwa kuna mapendekezo makubwa watakayoona na kufurahia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya machache na kabla ya kengele ya pili kupigwa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu, kwa hoja hii ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze na shukrani kwa Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia wote tulioko hapa, kupata baraka zake kuja kuwawakilisha wananchi wa Tanzania katika Bunge lako Tukufu. Bila kibali chake, nafikiri tusingeweza kuja hapa. Nawapongeza wote waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali ndani ya Serikali na ndani ya Chama, kwani Mungu amependa iwe hivyo, vinginevyo isingekuwa hivyo. Kwa hiyo, namshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, pia kwa kuniwezesha mimi binafsi kuingia tena katika Bunge hili, kwa kipindi kingine na pia niwapongeze sana wananchi wa Jimbo langu la Magu, kwa kunipa imani ili niwawakilishe tena. Nasema ahsanteni sana na ninaahidi nitawatumikia kwa nguvu zangu zote, akili zangu zote na kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Ninaamini wananisikiliza. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Magu, wamenituma niishukuru sana Serikali, kwa chakula cha njaa, ambacho kama kisingekwenda hali ingekuwa mbaya sana. Wameshukuru sana na wanaomba wasiwasahau kwa sababu hali haijawa nzuri sana. Kwa sababu baadhi waliuza mifugo yao mingi na mifugo yao mingi ilikufa kwa ukame na waliuza mifugo kwa ajili ya kujihami na sasa hali ya mvua haikuwa nzuri na kwa hiyo, hawakulima pamba ya kutosha. Kwa hiyo, ina maana kwamba, chakula kiasi kidogo kilichopatikana, itabidi wakiuze kwa ajili ya kujipatia matumizi mengine kama ada za shule na kadhalika. Kwa hiyo, bado hali ya chakula siyo nzuri sana, wanaomba Serikali iendelee kuwatazama.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze sana Wizara ya Miundombinu; Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa bajeti nzuri waliyosoma jana. Naamini kwamba, imekidhi mahitaji mengi ya barabara kulingana na uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kuwa makini kwa maana ya kwamba, wameweza kutafsiri Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 katika mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa kwanza huu tulionao na kwa miaka mitano ijayo. Ni kitu ambacho kwa kweli siyo cha kawaida kwamba, Serikali inapanga na inajua kuanzia mwaka wa kwanza kwamba, itafanya nini katika kipindi cha miaka mitano. Naipongeza sana Serikali kwa hilo. Hii inaonyesha kwamba, ni Serikali makini, Serikali mahiri na kwamba, ita *deliver* kile ambacho iliahidi kwa wananchi hadi wakakipa kura Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niingie katika baadhi ya maeneo ambayo nataka nitoe mchango wangu. Kitu cha kwanza, ni kile ambacho kwa kizungu nitakiita, *Intergration of Road Network* ama *Inter-connectivity,* sijapata neno sahihi la kiswahili labda muunganisho wa barabara katika maeneo husika. Najua tatizo hili liko sehemu zote, kama siyo sehemu zote nchini. Nitatolea mfano wa eneo ambalo natoka. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 katika Ukurasa 53, inasema kwamba, Serikali ina azma ya kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya kwa barabara zinazopitika mwaka wote. Sasa ukiangalia Makao Makuu ya Wilaya ya Bariadi, Magu, Maswa na Ngudu, ili utoke Bariadi ufike Magu, ukitoka Bariadi unakuja Nguliati, ukifika Kasoli, njia inakosekana, inakufa. Huwezi kutoka Kasoli kuja Magu. Lakini, Barabara ya Kasoli kuja Magu haiko kwenye bajeti na haijatengenezwa miaka karibu 20 sasa. *Inter-connectivity* au muunganisho baina ya Bariadi na Magu haupo. Kwa hiyo, ninaomba kwamba, barabara inayounganisha Kasoli na Magu, iingizwe iwe barabara ya Mkoa ili hili linalosemwa kwenye Ilani ya Uchaguzi, liweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwenye bajeti kuna barabara ya kutoka Bariadi mpaka Mwamlapa, hilo ni zuri. Lakini kutoka Kasoli – Mwamlapa – Kasoli kuja Magu, barabara haipo. Ukitoka Maswa kuja Magu, unatoka Maswa unakuja mpaka Sishiyu katikati hapo kabla hujafika Kijiji cha Bilishi, barabara inakufa. Ukitoka Maswa kabla hujafika Bilishi, njia ni nzuri kabisa, unaweza ukaenda *speed* mpaka 120, lakini ukikaribia Bilishi kuja Miligisu, njia inakosekana. Kwa hiyo, huwezi kuendeleza eneo

hili, kama hujatengeneza hiyo barabara ikafika mpaka Miligisu, ikafika mpaka Kabila, ikaenda mpaka Magu ama ikapita Kadashi ikaenda Nyambiti na hatimaye kuja Magu. Watu wa Maswa, watapataje samaki kutoka Magu kama barabara inaishia Bilishi, inaanzia katikati ya Shishiyu na Bilishi?

Nashukuru kwa bajeti hii kutenga fedha kwa ajili ya barabara ya Bukwimba kwenda Kabila, kwa sababu hii barabara ilikuwa ni kero kubwa. Nasema sasa itakapotengenezwa, kutoka Bukwimba kwenda Kabila na ile ya kutoka Magu kwenda Bukwimba ikitengezenezwa, utakuwa na tatizo unapotaka kwenda Maswa na unapotaka kutoka Bariadi kuja Magu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara ifanye uratibu wa kuhakikisha kwamba, muda wote hizi barabara zinaingizwa kwenye bajeti na Mikoa pamoja na Wilaya husika ili kwenda na *inter-connectivity*.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye hoja ya pili ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Mheshimiwa Rais, alipokuwa anaashukuru wananchi wa Mwanza, kwa kumpa kura nyingi Kitaifa, aliahidi na kusema kwamba, Serikali ina mpango wa kuufanya Mji wa Mwanza uwe *Hub* ya Nchi za Maziwa Makuu. Sasa utafanyaje Mwanza iwe *Hub* ya Nchi za Maziwa Makuu, kama Uwanja wa Ndege wa Mwanza, haujapata hadhi ile na uwekezaji kama hauanzi sasa. Ni lini huo Mji wa Mwanza utakuwa *Hub* ya Nchi za Maziwa Makuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ombi letu Wanamwanza, ni ombi la Kitaifa pia, kwa sababu *Mwanza Airport* ikitengenezwa, haitakuwa tu kwa maslahi ya Wanamwanza, bali ni kwa maslahi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mpango, niliambiwa hapo nyuma kwamba, *NSSF* walikubali kugharamia ujenzi wa *Terminal* ile *(*ku-*finance)*. Hili limeishia wapi? Ningependa kujua mpango huu uliishia wapi na kama uliishia mahali, utaendelea vipi na kama hauendelei, basi kuna mpango gani mbadala wa kuifanya *Mwanza Airport* iwe ni *Terminal* nzuri na isipunguze mapato ya Serikali, siyo ya Mkoa wa Mwanza, mapato ya Serikali ambapo sasa Ndege zinatua *Jomo Kenyatta International Airport?*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ilizingatie hili, kama haiwezekani Serikali kupata hela zake, basi itafute watu watakaojenga kwa *Build Operate and Transfer (BOT)*, kama hilo haliwezekani. Lakini, naamini Serikali ama Wizara, haija-*exhaust* na kwa maoni yangu, kwa kweli haijafanya juhudi za kutosha kuiendeleza *Airport* ya Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo ningeomba nichangie, ni kuhusu hizi Mamlaka zilizoko chini ya Wizara ya Miundombinu. Mamlaka ya Usafiri wa Anga, wana mpango wa kujenga *Aviation House* kwa shilingi bilioni nane katika kipindi cha miaka mitatu. Mamlaka ya Hali ya Hewa wamepanga jengo, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nao wanatafuta ofisi *TANROADS* nao wametenga shilingi bilioni nne kujenga ofisi. Sasa, mimi hainingii sana akilini kwangu kwamba, kila Mamlaka ijenge ofisi yao. Mamlaka ya Usafiri wa Anga, wajenge *Aviation House*, Mamlaka ya Hali ya Hewa, wajenge *Hewa*

*House* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wajenge *Ndege House!* Kwa nini wasingejenga jengo moja kwa ujumla wao na wakaita *Mawasiliano House*? Wajenge jengo moja kubwa, litakalo-*suit* mahitaji ya kila mamlaka na waliite *Mawasiliano House,* kama walivyofanya wenzetu wa nchi za Ulaya, walipojenga *Umoja House,* ambako kuna ofisi kadhaa humo. Kwa nini tunataka kila mtu ajitegemee na awe Jogoo kwenye sehemu yake? Watafute eneo moja, wajenge na waite *Mawasiliano House*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ni kwa maoni yangu. *Advantage* ya kufanya hivyo ni pamoja na kupunguza gharama za *transaction*. Pili, itaokoa ardhi ambayo ingewezwa kujengwa kwa sababu sasa inabidi tupanuke *vertically*. Dar es Salaam ipanuke *Vertically*, siyo *horizontally*. Uwezekano wa kuendelea kupanuka *horizontally* unapungua kwa Dar es Salaam. Sasa kila mtu kama atajenga banda lake, *Aviation House*, *Hewa House*, *Ndege House*. Kwa nini wasiwe na jengo moja kama walivyofanya wenzetu wakawa na *Umoja House,* Mabalozi wa nchi za nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii pia itaokoa fedha, kwa sababu msingi utakaojengwa kwa hiyo shilingi bilioni nane, wengine watajenga juu yake. Hutahitaji tena kujenga misingi mizito kwa kila Mamlaka. Ukijenga msingi mmoja mzuri, waka-*design* vizuri, Mamlaka ya Hali ya Hewa Mitambo yake wataifunga na hao wa Usafiri wa Anga watafunga na kadhalika. Nafikiri hiyo itaokoa fedha za walipa kodi na pia itafanya mawasiliano watu wanaotaka kwenda kwenye Mamlaka moja, wataishia kwenye jengo moja, itakuwa ni *Clearing House, so to say!*

Mheshimiwa Spika, naomba niende sasa kwenye *Road Fund*. Kila Mbunge anapozungumza, anazungumzia kwanza Jimbo lake, barabara zilizopo pale kama na mimi nilivyoyasema ya kwenye Jimbo langu. Lakini, pia kuna barabara za Kimkoa na barabara za Kitaifa. Nina matatizo kidogo na takwimu ambazo zimetolewa. Bajeti ya *Fuel Levy* ya mwaka wa fedha unaoisha (2005/2006), ilikuwa shilingi bilioni 76. Bajeti ya Mwaka huu tunaojadili, kwa mwaka huu tulioanza, bajeti ya *Fuel Levy* ni shilingi bilioni 77, kama walivyoandika kwenye kitabu.

Lakini nafikiri ni makosa ya uchapaji, ni shilingi bilioni 85. Kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri wa Miundombinu, wameandika bajeti ni shilingi bilioni 77, lakini kwa kweli hilo nafikiri ni kosa la kiuchapaji. Haiwezi kuwa shilingi bilioni 77, nafikiri ni shilingi bilioni 85. Nitasahihishwa kama nitakuwa nimekosea.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha uliopita, kila lita moja ilikuwa inatozwa shilingi 90 kwa lita na zikapatikana hizo hizo shilingi bilioni 76. Maana yake nini? Hiyo maana yake ni kwamba, kiasi cha mafuta kilichotozwa shilingi 90 na kikaenda kwenye *Road Fund* ni lita milioni 840. Kwa mwaka huu kwa ongezeko la shilingi 10 kwamba, sasa ni shilingi 100 badala ya 90, bajeti ya *Fuel Levy* ya shilingi bilioni 85, ambayo ni sawa na lita milioni 850. Sasa hapo kuna ongezeko la lita milioni 10. Kutoka lita milioni 840 mpaka milioni 850, ni ongezeko la lita milioni 10. Hii ni sawa sawa na *growth rate* ya 1.19%.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi sijajua kwambam kigezo cha kubajeti kiasi hiki kwa ajili ya *Road Fund, basis* yake ni nini? Kama uchumi unakua kwa asilimia sita na

kuendelea, uchumi unapokua, matumizi ya *Petrol* hayakui na kama yanakua, je, yanakua kwa asilimia 1.1?

Mheshimiwa Spika, ukichukua hizi lita 850 milioni Kitaifa kwa mwaka, maana yake ni kwamba, ni lita milioni 70 kwa mwezi, maana yake ni kwamba ni lita milioni 3.3 kwa Mkoa kwa mwezi. Kwa sababu tunajua Dar es Salaam ndiyo inayochangia asilimia kubwa kwenye kodi ambayo ni zaidi ya silimia 60 ya *Total National Revenue*, kwa hiyo, Dar es Salaam peke yake kwa hesabu hizi inaweza ikawa inakula lita milioni 42 kati ya hizo milioni 70. Sasa inabaki lita milioni 28 kwa mikoa mingine, ambazo ni sawa sawa na lita milioni 1.4 kwa kila mkoa kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, hizi hesabu nina mashaka kama ziko sahihi. Matumizi ya *Petrol* imekadiriwa, kuna watu walifanya tathimini wakagundua kwamba, matumizi ya *Petrol* ukiondoa haya kwenye migodi na viwandani ni kama lita milioni 2,150 kwa mwaka. Ambayo ukitoza shilingi 100 kwa lita, maana yake ni shilingi bilioni 215 na bajeti ya *Road Fund* wao wanakadiria milioni 200. Wakipata shilingi milioni 200, barabara zote zitajengwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tulipotembelea Kamati ya Mahesabu ya Serikali, walitueleza na walisema kwamba, fedha za barabara ziko. Kuna maoni kuwa lita zinazotozwa kodi ni milioni 840, lakini *TRA* ukizungumza nao wanasema *estimate* ya *consumption* ya *fuel* ni lita milioni 700. Kuna takwimu tatu tofauti: *TRA*/Serikali lita 700 - 840 milioni na utafiti unasema ni lita 2,150 milioni. Ukweli ni upi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa na mimi nichukue nafasi hii, kumpongeza kiongozi wetu, Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Pia niwapongeze wale wote ambao wameteuliwa kushika nyadhifa katika Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, niliwashukuru wananchi wa Jimbo la Kinondoni, kwa kunichagua kwenye Jengo lile la zamani. Sasa niko kwenye Jengo Jipya, basi nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kinondoni, kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Miundombinu, yeye pamoja na Manaibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini zaidi kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa tu nizungumzie suala la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Bahati nzuri hata yeye mwenyewe katika hotuba yake, amelizungumzia na analifahamu na nafikiri kuna hatua zinazochukuliwa kupambana na msongamano ule, lakini na mimi nimeona nilizungumzie kidogo.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari Dar es Salaam kwa kweli ni kero kubwa sana na si suala ambalo labda limejitokeza juzi na jana. Ni suala ambalo takriban miaka 10 iliyopita, limekuwa likiendelea kukua hadi hivi sasa kuwa linatisha zaidi. Unapotoka Mwenge kwenda mjini asubuhi, mahali ambapo labda ungetumia dakika 10, hivi sasa unatumia takriban saa mbili. Hali kadhalika unapotoka Mwembechai kwenda mjini asubuhi unatumia saa mbili badala ya kutumia dakika tano ama kumi. Kadhalika pia unaporudi kutoka mjini kuja katika maeneo hayo wakati wa jioni, msongamano ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeishauri Wizara, pamoja na mpango wake mzuri ambao imeuandaa, lakini ingejaribu kuangalia barabara ambazo zingeweza kusaidia zile barabara zetu kuu. Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, ambayo inakwenda Mwenge, zipo barabara ambazo zimetengenezwa zinazopita Makumbusho, Kijitonyama hadi Mwenge. Kama barabara zile zingeweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami, nina hakika msongamano katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi, ungepungua ama ungekwisha kabisa. Lakini, hata katika barabara ya Morogoro, maeneo ya Magomeni Mikumi, ama barabara ya Zamani ya Kigogo kuja Magomeni, ambayo inapita Mzimuni, inapita kwa Sheikh Yahaya, Mburahati mpaka Ubungo, barabara ile nayo ikipewa kipaumbele, nina hakika suala la msongamano litakuwa limepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la Soko la Tandale. Wote ni mashahidi, Wabunge wenzangu katika maeneo yao wanao wakulima, lakini wanategemea sana kuuza bidhaa zao katika soko la Tandale. Unapokuja pale Sokoni Tandale, mbali ya kukuta mabanda ya Soko lile hayaridhishi, lakini barabara inayokupeleka pale nayo

inatisha zaidi na inawezekana hata usifike kule Sokoni, kwa kipande kidogo tu cha hiyo barabara.

Najua suala lile liko kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, lakini uwezo wa Halmashauri yetu hivi sasa kuweza kupata pesa kutengeneza barabara ile kwa kiwango cha lami, kwa kweli ni mdogo sana. Tunaweza tukakaa na kero hiyo hata miaka 10 inayokuja, Halmashauri isiitengeneze. Kwa hiyo, niwaombe Wizara hii katika mpango wao huo, basi waliangalie hili nalo kwa sababu soko hilo ni muhimu sana katika nchi yetu.

Ni soko ambalo tunaweza tukasema hivi sasa ni soko la Kimataifa, kwa sababu wapo wananchi kutoka nchi za jirani wanakuja kununua vyakula pale. Lakini wa Dar es Salaam wote tunategemea kupata chakula kutoka kwenye soko lile. Wakulima wa mikoa mingi ambayo wanalima, wanategemea kuleta bidhaa zao kwenye soko lile kuja kuuza, lakini kipande cha barabara ile ambacho hakizidi kilomita tatu kwa kweli kinasikitisha. Kwa hiyo, niiombe Wizara wajaribu kulifanyia kazi na hilo najua hivi sasa halikupangwa, lakini nina hakika zitatafutwa angalau kuweza kutengeneza kuondoa hiyo kero ambayo iko pale.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam tumepata fedha za kusaidia ujenzi wa barabara, lakini bahati mbaya Kinondoni hazikufika. Nimpongeze mwenzangu, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, kwa sababu kwake hizo fedha zimefika. Wizara iangalie na huku Kinondoni nako, basi angalau hizo fedha zifike, wananchi angalau nao waone kwamba, Serikali yao ya Awamu ya Nne, inawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la ajali. Nchi yetu imekumbwa na misukosuko mikubwa sana ya ajali nyingi, tunasema ni kwa sababu ya uzembe wa madreva na ubovu wa magari. Lakini nina hakika vyombo vinavyohusika, vinachukua hatua kupambana na hilo. Liko suala pia la barabara, pamoja na kwamba, labda magari ni mabovu, madreva ni wazembe, lakini suala la barabara nalo ni muhimu sana. Yapo maeneo mengi, barabara siyo nzuri, lakini hata pale ambapo kuna barabara nzuri, kuna vitu vinakosekana kwenye barabara, ambavyo vinasababisha magari kupata ajali. Barabara hii ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, kuna matuta ambayo kama hujui, unaweza ukakutana nayo, hakuna alama inayokuonyesha na kama kuna alama basi ni alama ambayo iko mita tano kabla ya kukuta hilo tuta na wewe uko kwenye *speed,* kwa hiyo, matokea yake unaweza ukalivaa lile tuta na unaweza ukapata ajali. *(Makofi)*

Lakini suala la alama, michoro ambayo inachorwa kwenye barabara tuchukulie mfano barabara ya Chalinze kuja Morogoro, kwa kweli hii barabara inaridhisha na inafurahisha, ni barabara ambayo kwa kweli iko kwenye *standard* inayotakiwa. Basi tutumie barabara ile, kuiga ili barabara nyingine zote, angalau zifanane na ile kwa sababu alama zake zote zinaonekana. Michoro inayoonyesha kingo za barabara inaonekana na mchoro wa katikati unaonekana vizuri sana. Kwa hiyo, niombe tuangalie ujenzi wa hizi barabara kuhakikisha kwamba, tunaweka alama.

Lingine ni suala la barabara, ziko barabara ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa sana, lakini ubora wake hauridhishi. Barabara imejengwa mwaka jana au miaka miwili iliyopita, hivi sasa haifai. Sitaki kuzitolea mfano, lakini wote ni mashahidi na mnazifahamu. Tuangalie hawa makandarasi ambao wanatengeneza barabara zetu, kweli wanazitengeneza kwa kiwango ambacho kinatakiwa ama wanalipua tu ilimradi imepigwa lami pale, baada ya siku mbili, tatu, mwaka, barabara imekuwa haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ningeomba Wizara itusaidie ni la usafiri kwa wanafunzi, hasa pale Dar es Salaam. Mzee wetu Yusuf Makamba, amekuwa akipiga kelele sana na tumekuwa tukimsaidia. Lakini basi na Wizara ione kupitia vyombo vyake, ni jinsi gani watafanya ili kuwasaidia wanafunzi wa Dar es Salaam, waweze kupata usafiri wa uhakika. Waweze kupata usafiri ambao hauna matatizo, utakaowapeleka shuleni na kuwarudisha majumbani mwao vizuri sana. Nakumbuka ilikuweko *UDA* na najua hivi sasa ipo ingawa inasuasua, Wizara iangalie uwezekano wa kuiwezesha ili iweze kutoa huduma kwa hawa wanafunzi wetu. Kwa kweli ni adha kubwa sana kwa wanafunzi, ni adha kubwa sana kwa watoto wetu. Kwa hiyo, Wizara ijaribu kuliangalia hilo, kama kuna uwezekano, basi tuweze kutumia shirika hilo kuwasaidia wanafunzi ili waondokane na adha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, imeniridhisha, kwa sababu ameeleza msongamano wa magari ya Dar es Salaam, naona niishie hapo. Nampongeza na ninatamka tu kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ipite. Nina hakika mara hii kama sikupata, bajeti ijayo na sisi wa Kinondoni tutakumbukwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nami kwa mara nyingine tena, niweze kuchangia moja ya hotuba muhimu za Serikali au Waziri wa Serikali ya Awamu ya Nne. Awali ya yote, napenda niungane na wenzangu, kumpa pongezi nyingi za dhati Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana, kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Aidha, vile vile napenda niwapongeze Waheshimiwa Watendaji wote, waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali za sektretarieti ya Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa napenda nichangie Hotuba ya Waziri wa Miundombinu kama ifuatavyo: Miundombinu nailinganisha na mishipa ya damu katika kiwiliwili cha mwanadamu. Kwa maana kwamba, mishipa ambayo imejaa *cholesterol,* inaweza kumletea matatizo mwanadamu na kwa mantiki hiyo hiyo, barabara mbovu zinaweza kukwamisha maendeleo ya uchumi wa nchi. Ni kwa kuzingatia umuhimu huo, ndiyo maana tunalitilia uzito sana, suala hili la miundombinu na ujenzi na uimarishaji wa miundombinu katika nchi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora, kwa nini ni muhimu? Ujenzi wa barabara hii una sababu nyingi, lakini miongoni mwake ni kama ifuatavyo: Kwanza, barabara hii ni fupi kwa takriban kilomita 200 ukilinganisha na ile inayotoka Manyoni – Singida – Nzega – Tabora. Kwa kuwa na ufupi wa kilomita 200, unapunguza matumizi ya mafuta, unapunguza muda wa kusafiri kutoka Manyoni kwenda

Tabora na vile vile unapunguza uchakavu wa vifaa vinavyosafiri baina ya Manyoni na Tabora. Kwa maana hiyo, ndiyo maana tunahimiza sana ujenzi wa barabara hii, pamoja na kwamba, kama Serikali ingeweza kuisaidia Tabora kwa sasa hivi, kwa kuiunganisha Tabora na Nzega, umbali wa takriban maili 75 tu kwa kiwango cha lami, basi Tabora inaweza ikawa katika mtandao kwa kuanzia, ambao utamfanya msafiri kutoka Tabora mpaka Dar es Salaam au mpaka Mwanza, aweze kutumia barabara ya lami. Lakini anapokuja kutoka Dar es Salaam akipita njia hiyo niliyoisema, hasara zake ni kwamba, ni safari ndefu kwa takriban kilomita 200.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Itigi – Tabora, ilikwishasanifiwa toka mwaka 1998, kilichobaki ni ujenzi, kwa nini haijengwi? Ujenzi wa barabara hii ya Nzega – Tabora – Itigi – Tabora, Tabora – Sikonge – Mbeya, pamoja na Tabora – Kigoma, ni muhimu ukizijumlisha na uimarishaji wa huduma ya reli ya kati. Ni muhimu sana kwa kuleta maendeleo na changamoto ya maendeleo katika sehemu hii ya Tabora na Mikoa inayozunguka. Haya yakifanyika, maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Mkoa wa Tabora, yatapiga hatua kubwa sana. Tabora itakuwa ni moja ya kitovu au vitovu, ambavyo vitakuwa ndiyo vinakuza ajira na mambo mengi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, badala ya watu wetu wengi wote kukimbilia Dar es Salaam. Tunaweza tukaifanya Tabora ikawa ni moja ya vitovu vingi, ambavyo vitaendeleza maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wengi waliotangulia kuzungumza, wamelizungumzia suala hii la huduma ya reli ya kati, kwa ufanisi wa hali ya juu. Nitumie fursa hii tu kuongezea hapo walipofikia wenzangu kwamba, kwa kuwa Serikali inafahamu umuhimu wa uchumi wa kijiografia na inafahamu kwamba, Tanzania imezungukwa na nchi ambazo hazina *direct access* kwenye Bahari ya Hindi, njia ya pekee ya nchi hizi kuweza kupitisha bidhaa zinazotoka na kuingia katika nchi yao ni kupitia Tanzania.

Kwa ufahamu huo, Serikali imekuwa inafanya juhudi kubwa za kuzitengeneza bandari zetu ikiwemo ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na sasa Bagamoyo. Lakini kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, shughuli zote za kutengeneza bandari zetu zitakuwa hazitazaa matunda yanayostahili, ikiwa reli ya kati na barabara ziendazo Magharibi, hazitakuwa nzuri na za kuweza kupitisha mizigo, pamoja na abiria wakati wote wa mwaka. Kwa hiyo, nazidi kusisitiza tu kwamba, ili azma ya Serikali ya kuziboresha bandari zetu iweze kuwa na maana inayostahili kiuchumi, hatuna budi kuzitengeneza barabara zetu ziendazo katika nchi jirani, pamoja na reli ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa reli ya kati vile vile kwa upande wa Tabora Mjini, utaamsha ari ya kuweza kutengeneza nafasi za ajira ambazo mpaka sasa zimefubaa. Kihistoria baadhi ya wazee au wenye rika kama langu, wanaweza kukumbuka kwamba, katika historia ya shirika la reli huko nyuma ilijulikana kama *East African Railways* na kabla ya hapo ilikuwa ni *East African Railways and Harbours*. Kulikuwa na vyuo viwili tu katika Afrika Mashariki, vinavyofundisha watendaji wa Shirika la Reli. Chuo kimoja kilikuwa Nairobi na kingine kilikuwa Tabora, chuo hiki sasa kimefubaa kwa sababu ya uzorotaji wa shirika lenyewe la reli.

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu ni kwamba, Shirika la Reli likiboreka, kutokana na mambo ambayo Serikali sasa hivi inafanya, ama kubinafsisha baadhi ya shughuli za reli, matarajio yangu ni kwamba, Chuo cha Reli cha Tabora, nacho kitaimarika. Sambamba na kuimarika Chuo cha Reli cha Tabora, pale Tabora kuna karakana. Ziko karakana moja ni kubwa ilitumika katika siku za nyuma, kutengeneza reli ambayo sasa hivi ndiyo inayokwenda Mwanza. Reli inayokwenda Mwanza kwa baadhi yetu, ambao hatufahamu, iliunganishwa Tabora kwenye karakana kubwa ya *railway*. Karakana ile sasa ime-*lay fallow,* kwa sababu hakuna kinachofanyika. Tabora ni kituo kikubwa cha reli katika reli ya kati. Kwa sababu ya umashuhuri wake huo, siku za nyuma kulikuwa na karakana kubwa ya *engine* za reli. Sasa haifanyi kazi tena na kama ipo ni ndogo sana. Kuamka kwa shughuli za reli ya kati, kutaamsha shughuli za karakana ya *engine,* pamoja na mabehewa pale Tabora. Hii ni njia moja ya kutengeneza ajira, ambazo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumezizungumzia kwamba, tunataka kutengeneza nafasi za ajira zisizopungua milioni moja katika kipindi cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua uamuzi wa kuuza nyumba zake kwa baadhi ya wafanyakazi wa Serikali wanaostahili. Zoezi hilo limefanywa na sasa limesitishwa. Lakini lilipofanywa, tulipewa ahadi kwamba, sambamba na kuuza nyumba hizo, zitajengwa nyingine kwa ajili ya wafanyakazi wa Serikali. Inasikitisha kwamba, mpaka sasa hivi kasi ya ujenzi wa nyumba mpya kwa wafanyakazi wa Serikali ni ndogo sana. Matokeo yake ni nini? Pale Tabora tuna Hospitali, kubwa ya Mkoa Kitete, Madaktari Bingwa na watalaamu wengine wakija wakiwa *assigned* Tabora, wanauliza kwanza tutakaa wapi? Nyumba za kukaa hamna, mpaka leo zimejengwa nyumba mbili tu za Serikali ya *RCO* pamoja na *RPC*. Naiomba Serikali, itie mkazo na iongeze kasi katika ujenzi wa nyumba za Serikali kwa watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ameelekezea kwamba, kutakuwa na ujenzi katika viwanja vya ndege vya Kigoma, Mwanza, Shinyanga na Tabora. Lakini katika kitabu cha *estimate* za maendeleo, hakuna tarakimu inayoonyeshwa kwamba, Uwanja ya Ndege wa Tabora, umepangiwa kiasi fulani cha fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo yaliyokusudiwa. Kiwanja cha Ndege cha Tabora, kitakuwa ni *gate way* katika Mikoa ya Tabora na Rukwa. Ikishakuwa hivyo, Mikoa ya Tabora na Rukwa, ina mbuga nzuri za wanyama, ambazo zinastahili kuvutia watalii wetu, badala ya kwenda Kaskazini, wanaweza kuja Mikoa ya Magharibi na hivyo kuchangia katika suala zima la kutengeneza ajira na kuongeza Pato la Taifa. Watalii hawa hawawezi kuja kama hali ya Kiwanja cha Ndege cha Tabora, itaendelea kuwa kama ilivyo. Wale wachache wanaokuja mara nyingi wanapata adha ya kutokupata hata maji kwa sababu ya matatizo ya maji katika Kiwanja cha Tabora. Kwa hiyo, fedha ambazo ninaziomba, zionekane kwa maendeleo ya Kiwanja cha Tabora. Inawezekana nyingine zikaenda hata kusaidia kuchimba kisima, kupata ufumbuzi wa matatizo ya maji katika Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *mobilization of internal resources* ni tatizo kubwa, tunazungumza hapa kwamba, hatuna fedha, sawa hatuna za kutosha. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kutumia *government bonds,* kuuza *government bonds* ili ku-*mobilize long term resources* kutokana na fedha nyingi zilizoko ndani ya nchi yetu.

Mifuko ya *Pension* ina fedha, Serikali inaweza kuzi-*tape* hizi kwa kuuza *government bonds,* lakini ni vizuri basi *government bonds* zikiuzwa za muda mrefu na wa kati, ziwe tayari zimekusudiwa zinapelekwa kwenye miradi gani. Kwa bahati *government bonds* sasa hivi ziko *listed* katika *Dar es Salaam Stock of Exchange*. Atakayezinunua siyo lazima akae nazo miaka kumi au miaka mitano, katikati hapo akijiona anahitaji fedha nyingine atakwenda *Dar es Salaam Stock of Exchange* na kuziuza. Kwa maana hiyo, Serikali ifanye utaratibu wa kuwa *market maker, when it comes to a situation* kwamba, aliyeshika *government bonds* ya miaka kumi anataka kuiuza, asije akakwama nayo. *Dar es Salaam Stock of Exchange* itafanya kazi hiyo. Lakini kwa kutumia *resources* zetu za nchini, tunaweza kuziba pengo la upungufu wa fedha ambazo tunazungumza kuwa hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la simu, Serikali imefanya vizuri sana kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kampuni mbalimbali za simu za mkononi, kutoa huduma nzuri na kwa kweli wanatoa huduma nzuri. Lakini bei ya simu kwa maana ya gharama za simu, ziko juu. Serikali iangalie kwa kutumia *regulator* wake, bei za simu zipungue. Lakini vile vile zile zilizopo, huduma hii haitoshi katika baadhi ya miji, Tabora ikiwa ni mojawapo ya miji hiyo. Watu walioko nje ya mji, katika kata, inabidi wapande mlimani, wapande mitini, ili kuweza kuzungumza na kupata huduma nzuri za simu.

Mheshimiwa Spika, nayaomba makampuni ya simu, ambayo mpaka sasa yamefanya kazi nzuri, yaendelee kuboresha huduma zao ili wananchi wasipate adha ya kupanda mitini, kwa ajili ya kupata huduma hii muhimu ya simu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzugumza na kuchangia katika Bajeti ya Miundombinu. Mwisho ni kwamba, nikipata maelezo mazuri kuhusu upungufu wa fedha za ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora, sina matatizo na bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kushukuru kwa kunipa nafasi hii. Aidha, naomba niungane na Wabunge wenzangu walionitangulia, kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupata kura nyingi, zilizotosha yeye kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile naomba niwapongeze Wabunge wote, waliopata bahati ya kuteuliwa na kuwa Wajumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, hongereni sana. Vile vile naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza mzee wangu, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa kuwasilisha vizuri bajeti ya Wizara yake ya Miundombinu. Kabla ya yote nataka niseme, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Lakini nikiwa naunga mkono hoja, nataka nichangie yafuatayo: Kwanza, barabara ya Kibiti – Lindi, inapigiwa kelele tangu nilipokuwa na umri mdogo sana,

nilikuwa nasikia. Kila siku, Kibiti – Lindi, hivi ukiwa na watoto wawili, mmoja anakwenda kufanya *masters,* mwingine anakwenda kuanza kidato cha kwanza, nani unampa *priority* katika hali ya kawaida? Nadhani kwa akili ya kawaida, huyu anayeanza kwanza ndiyo utampa kipaumbele. Sasa maajabu ninayoyaona kwenye bajeti hii, Tarekea – Malangu, shilingi bilioni 17, lakini Kibiti – Lindi hata shilingi bilioni 10 haifiki kwa ujumla wake, kuna tatizo gani hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuna nia mbaya, lakini Kilimanjaro kuna barabara mbadala. Lakini matatizo ya Mtwara na Lindi kila siku kelele, watu hawaendi kufanya kazi kule kwa sababu ya barabara. Kule hatuna Hospitali ya Rufaa, hivi unafikaje Dar es Salaam kwenye Hospitali ya Rufaa, ambako inaonekana karibu na kule? Jamani mtufikirie, tufike mahali tuangalie kule. Mimi nasema, ningekuwa Waziri Mkuu leo, bahati nzuri anaingia, afadhali atanisikia. Ningekuwa Waziri Mkuu na namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa, atumie mamlaka aliyonayo kusitisha bajeti ya shilingi bilioni 17. Kama sungura yule ni mdogo, si uangalie wale wenye matatizo zaidi? Sasa Mtwara hakuna barabara, Singida – Sherui tatizo barabara *and still we are concentrating on Tarakea – Marangu, what is this*? *(Makofi)*

Jamani inauma, tumewasikia akina Nabahani, mimi nikiwa mdogo. Mimi nina miaka 43, walionitangulia nimekuwa nawasikia nikiwa mdogo mpaka leo hapa mimi nakuja kusema haya haya, hatuoni aibu? Serikali kwani kuna tatizo gani na kule au ndiyo *segregation* hiyo? Maana Watanzania tunasifika kwa umoja, lakini umoja wa kuleta maendeleo ya kutukuka, yanayounganisha nchi nzima, tunakuwa wagumu, kuna tatizo gani? *(Makofi)*

La pili, katika *administrative law,* kuna dhana ya *audit alterum partem,* kwa Kiingereza *hear other part,* dhana ya kusikia upande mwingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokwenda kutembelea Mkoa wa Lindi, alimwita Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, atoe maelezo kidogo kwa wananchi wale, kwa nini barabara ile ina matatizo chungu mbovu? Kaka yangu, Mheshimiwa Mudhihir alisema sana jana. Lakini Waziri alisema barabara ile mkandarasi ana matatizo, kiburi hasikii la mpiga kengele Kanisani wala mwadhini Msitikini.

Mimi kwa dhana hii, nikapata wasiwasi kidogo, nikasema hivi kweli! Basi nikaona nitafute upande mwingine wa kusikia, maana nilikuwa najua mkandarasi yule, hana nafasi ya kuongea, basi nikapita. Unajua ninavyopita kule kwanza, huwa siweki bendera ile, maana naona kelele kwa barabara hiyo, maana tunasemwa vibaya. Ukiweka tu bendera tayari, ukikuta watu wamekwama kama una maji mle, *biscuits,* vyote, wanachukua kwamba, nyie ndiyo mnaochelewesha barabara.

Basi nikaenda *very simple,* nikawapata wale makandarasi, nikawauliza, hebu nielezeni upande wa pili, si mmesikia Waziri wa Miundombinu alivyosema hapa? Walichoniambia ni kwamba, bwana sisi wadogo na hatuna mahali pa kusemea. Lakini sasa hivi madaraja tuliyoyatengeneza haya, asilimia 90 ya madaraja hayo, Serikali imeyakubali, iko asilimia kumi, kidogo ina matatizo na tumeshauriwa kuyarekebisha, lakini licha ya kupata *certificate* kwamba, tumefanya vizuri, tunaidai Serikali shilingi bilioni 34, haijatulipa.

Lakini kingine, wale makandarasi wanasema kwamba, watendaji akienda huyu anaambiwa kokoto hizi endelea nazo. Baada ya mwezi anakuja mratibu mwingine, anasema kokoto hizi mbaya sana hazifai msiendelee. Sasa hali hiyo ndiyo imetufikisha kwenye migogoro hii na mimi nilikuwa kwa kweli kwa upande mmoja, nasadiki kwa sababu hii *dispute* kama ingekuwa *controlled* mapema, ingefikia mahali pa kutuambia kwamba, barabara imechelewa miaka miwili. Mimi sidhani kama kweli kuna wasimamizi wazuri, kusingekuwa na sababu ya barabara hii kuambiwa kwamba, imechelewa kwa miaka miwili. Nadhani kuna uzembe fulani, ningeomba Waziri wa Miundombinu na Waziri Mkuu, maana ndiyo viranja wa Serikali, waangalie watendaji wetu hawa, kwa namna moja au nyingine, wamekuwa wakijenga matatizo kweli. Kwanza, wanapokwenda tu kwa makandarasi wenyewe, tayari wanakuwa na *negative attitude* vichwani mwao, sasa mnakwenda na *negative attitude* vichwani; hivi kweli mnaweza ku-*compromise* jambo? Si rahisi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuangalia kwenye *TV* siku moja, najaribu tu kulisema hili ili nikuonyeshe uozo ulioko kwa watendaji wetu na kwamba, *you have to be serious from now onwards, more serious.* Nilikuona unambana mtu fulani, akakuambia unajua mtu mzima ukikuta anaguna, basi ujue amekosea. Nikakuona Chang'ombe pale kwenye *TV* ukawa unasema naondoka *but I am not satisfied.* Sasa ujue hali hiyo, ndiyo barabara ya kule kwetu, watendaji wote hao, kwa sababu *most of them,* hawajui matatizo tunayopata, basi wanaiacha hivyo hivyo. Kwanza, hawatembelei kwa wakati na hii nataka nikupe mfano wa dhahiri kabisa, niliouona hapa majuzi, tulipomwita Waziri wa Nishati na Madini. Kule Mtwara kwenye mradi ule wa *Mnazi Ba,* tulimkuta Kamishna wa Nishati na Madini hajawahi kutembelea kwenye ule mradi, lakini ndiye Mwenyekiti wa timu ya *Negotiation Team;* hivi ana-*negotiate* nini? Namshukuru Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, amechukua angalau hatua kidogo, hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina utaratibu wa kutoa vipaumbele, kwa maeneo ambayo labda kwa sababu hayapo kwenye bajeti, lakini inachukua kipaumbele makusudi kuhakikisha mambo hayo yanakwenda vizuri na hasa kwenye sehemu ya utalii, kwenye sehemu yenye mazao ya biashara, uchumi na madini. Kwetu kule zao letu kubwa ni korosho, korosho mwaka 2004 ilikuwa ya kwanza kwa kuleta fedha nyingi za kigeni hapa nchini na mwaka 2005 ilikuwa ya pili, lakini barabara inazopita korosho hizo inachekesha sana huwezi kuamini.

Barabara hiyo ni ya kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba - Newala – Masasi. Mapato ya mwaka 2005 ya korosho tani 90,000, karibu asilimia 52 ya korosho hizo zimetoka kwenye barabara hiyo. Sasa niiombe Wizara ya Miundombinu na Serikali kwa ujumla, tunajua barabara hiyo iko *TANROAD,* lakini si chachu ya maendeleo, si chachu ya uchumi wa nchi hii. Kwa nini angalau lami nyepesi, isiwekwe kwenye barabara ile? Kama inawezekana jambo hili likafanyika sehemu yenye dhahabu, sehemu yenye watalii, kwa nini pale tusifanye ili tusukume uchumi wa pale?

Jamani Mtwara na Lindi, kuna kura nyingi kweli za CCM. Tusifike mwaka 2010, wale watu wakageuka tukawapa ujiko *CUF,* tena Mwenyezi Mungu aepushie mbali hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko suala la Bandari ya Mtwara. Nimeangalia kwenye bajeti hii hapa, yaani inatajwa kwa mbali tu, tena pale palipoandikwa Ukanda wa Mtwara, ndiyo inatajwa tajwa kidogo, lakini vinginevyo, hakuna hapa jambo la maana linaloelezewa kuhusu bandari ile.

Lakini ijulikane wazi kwamba, kwanza ni *natural,* ina kina kikubwa, bandari ile tukiitumia tunaweza tukaongeza uchumi wa Tanzania maradufu. Hivi sasa mtu anatoka Songea anakwenda karibu kilometa 1,100 mpaka Dar es Salaam, kutafuta mafuta tu.

Kwenda kutafuta bidhaa tu mbalimbali, kwa nini asitumie pale Mtwara kilometa 600 kutoka Mtwara kwenda Songea? Watu wa Mbeya wangenufaika pale, hata wa Iringa. Lakini pameachwa achwa tu, kuna tatizo gani au kwa sababu bandari ile iko Mtwara? Nia siyo mbaya, lakini jamani, jamani, uchumi tunauacha makusudi. Uchumi wetu unaweza ukatukuka kama, vyanzo tulivyonavyo vya uchumi, tutaviendeleza kwa nia nzuri.

Mheshimiwa Spika, liko suala lingine la Bohari Kuu, liko chini ya Wizara ya Miundombinu. Lakini nimepita pale, wale bado wako dunia ya zamani kabisa, wapo kama kuku asiyekuwa na mwenyewe. Wameachwa vyovyote tu. Mimi naomba Waziri wa Miundombinu, uiangilie Bohari Kuu, uitengenezee mazingira yanayoendana na wakati huu wa sasa. Bohari Kuu pale kunaweza kukasaidia mambo mengi ya manufaa kwa ajili ya uchumi wetu. Nilikuwa naomba hilo nisisitize kwa sababu nia ni nzuri, ya kukuza uchumi wetu na nia ya kuhakikisha wafanyakazi wale wanafanya kazi tarajiwa, vizuri na kwa manufaa ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lingine humu ndani, kama nilivyotangulia kusema, hizi barabara zilizotajwa Singida - Shelui, Kibiti - Lindi, pamoja na kuchelewa kwake, hatujaambiwa sasa zitatengemaa lini, zitaisha lini na wananchi wetu wangetaka wajue lini zitaisha? Maana haya matatizo yanatakiwa yatatuliwe na Serikali, wananchi wangetaka wasikie zinakwisha lini. Kwa hiyo, utakapokuwa unafanya majumuisho, mambo mawili hayo, uyape kipaumbele tafadhali; barabara hizo zilizochelewa mwaka mmoja na nusu zitaisha lini na lile la kwanza nililowaambia kwamba, tumekuwa tukisikia upande wa Serikali peke yake, lakini upande ule wa pili hatusikii. Kwa namna yangu, nimepita pale wameniambia hayo. Tafadhali maana hawa Watendaji hawa ndio wanatulostisha, Kiswahili cha mtaani kule.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nakushukuru sana na nasema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Ningependa nianze kwa kutoa pongezi, kwa Mheshimiwa Rais, Jakaya

Mrisho Kikwete, kwa ushindi alioupata wa kumfanya awe Mwenyekiti wa Chama chetu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile nawapongeza Wabunge wenzetu, ambao wamepata nafasi za juu katika Chama chetu Chama cha Mapinduzi. Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Manaibu wake. Nimepitia hotuba yake kwa kina, kwa kweli kuna mikakati mingi ambayo imewekwa, pamoja na michango mingi ambayo Waheshimiwa Wabunge, wametoa kwamba, kunahitajika maboresho katika maeneo fulani fulani. Lakini kwa ujumla, Bajeti ile imeandaliwa kwa ustadi mkubwa sana. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu hiyo, ninaunga mkono Bajeti hiyo, kabla hata sijafika mwisho wa mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza, kukumbushia tu ahadi za Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi, ambazo zimeainishwa kwenye hiki kitabu cha Mwelekeo wa Utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005 na ahadi za Mgombea Urais. Kwa bahati mbaya nafikiri katika ahadi alizozitoa katika Mkoa wa Shinyanga, kuna ahadi mbili muhimu, ambazo nafikiri zilisahaulika. Kwanza, alipokuwa akiongea na wananchi kwenye Jimbo langu, sehemu inayoitwa Kagongwa, aliahidi kwamba, barabara ya kutoka Nzega kuja Kahama kupitia Itobo na Kagongwa, itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Naamini bado tuna muda, pamoja na kwamba, haijaonekana sehemu yoyote katika bajeti ya mwaka huu. Naamini bado tuna miaka minne katika miaka ya Ilani yetu, nina matumaini lakini niliona ni vizuri nilikumbushie hili.

Mheshimiwa Spika, lingine katika ahadi za Mheshimiwa Rais, pia alizungumzia kwa uchungu sana, kuwepo kwa mchwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na hili alilisema kuwa mchwa wale wanakula noti za wananchi na kwamba, atatusaidia dawa ya kupulizia mchwa wale. Nimefurahishwa sana na hotuba ya hitimisho la Bajeti ya Wizara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliposema maneno mazito kabisa kwamba, itabidi nyakati nyingine, tufumbe macho kwa hatua kali ambazo zitachukuliwa. Mimi tayari nimeshafumba macho, kwa kujua kabisa kwamba, tatizo hili la mchwa linataka mtu wa kuweza kukabiliana nalo. Nina matumaini makubwa, ila ningependa tu nikumbushie hapa kwamba, matatizo yapo, pamoja na kujipanga kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuchangia kuhusu bajeti yenyewe ya Miundombinu. Kwa ujumla bajeti ni nzuri kama nilivyosema, lakini nilifikiri inakosa vitu vitatu muhimu. Kwanza, inakosa kuangalia maeneo ambayo ni ya kipaumbele katika sura ya nchi yetu kwa sasa. Kwa kurejea katika hotuba ya Waziri Mkuu, wakati wa kuhitimisha Bajeti inayohusu Bajeti zilizo chini yake, alisema kwamba, sasa hivi mkakati au kipaumbele ni kilimo na elimu. Sasa ili kufanikisha elimu na kilimo, ni lazima tuweke mikakati ya kuboresha miundombinu. Msingi mkubwa wa kuboresha miundombinu, uwe unalenga zaidi kwenye barabara zinazoenda kwenye maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa unaozalisha zao la pamba na katika uzalishaji wa pamba kwa takwimu za mwaka jana Mkoa wa Shinyanga ulizalishaji asilimia 60 ya pamba yote inayozalishwa hapa nchini. Mkoa huu ni mkubwa una zaidi ya kilomita za mraba 50,000 na barabara zenye jumla ya kilomita 11,043. Katika barabara

hizi kilomita 9,174 ni barabara zinazohudumiwa na Halmashauri. Kwa hiyo, kuna kilomita chini ya 3,000 ambazo zinahudumiwa na Serikali Kuu.

Sasa katika mazingira haya, ninaona kutakuwepo matatizo makubwa hapo baadaye. Nikizungumzia uzalishaji wa pamba na matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza kwa zao hili. Moja ya matatizo ambayo yamekuwepo ni pamoja na bei kuwa ndogo sana na bei inakuwa ndogo kutokana na matatizo mbalimbali, mojawapo ni uchafu wa pamba. Pamba inakuwa chafu kutokana na *process* nzima, kuanzia uzalishaji wenyewe, utunzaji, usafirishaji kutoka mashambani, hadi kufikia kwenye *ginnaries.* Katika sura au hali ya barabara tulizonazo sasa hivi, pamba yetu tunasafirisha kwa kutumia mikokoteni inayokokotwa na ng'ombe.

*Handling* ya pamba hii inakuwa siyo nzuri, matokeo yake kwa takwimu za mauzo ya pamba za mwaka 2005, wakulima wa pamba walipata hasara zaidi ya dola milioni 32, ambazo ni zaidi ya shilingi bilioni 40 za Tanzania, kutokana na pamba yao kuwa chafu. Sasa katika sura nzima ya kupunguza umaskini, nilifikiri ni vizuri Serikali ikaweka Mkakati Maalum wa kuangalia barabara za vijijini. Kuziachia Halmashauri kuzikarabati barabara hizi, naona wazo hili lina matatizo na Waheshimiwa Wabunge wengi, wamechangia. Wasema kwamba, Halmashauri nyingi hazina uwezo. Ni kweli, ukiangalia kwa wastani wa mgao wa fedha ambao Halmashauri zetu zimepatiwa, Mkoa wetu wa Shinyanga pesa ambazo zimetolewa ni wastani wa shilingi 134,600, kwa kilomita moja kwa mwaka. Sasa shilingi 134,600 zinatosha tu *trip* mbili za malori ya kokoto.

Sasa *trip* mbili za malori ya kokoto kwa mwaka, hazitoshi chochote katika kukarabati barabara hizi. Kwa hiyo, ombi hapa ni kwamba, Serikali Kuu kupitia *TANROADS,* tu-*up grade,* tukubali maombi yanatolewa na wananchi wa sehemu mbalimbali, kuzi-*up grade* barabara za vijijini ili ziingie katika mfumo wa kukarabatiwa na kutunzwa na Serikali Kuu. Hii itasaidia sana kuboresha mawasiliano vijijini na pia itaweza kupunguza matatizo ambayo tayari tunayo. Ikumbukwe pia kwa mfano, katika mkakati wa kuongeza uzalishaji wa pamba, tumesema kwamba, tunataka ifikapo mwaka 2010, tuongeze uzalishaji wa pamba kutoka kilo 300 kwa eka hadi kilo 1,000, ambayo maana yake ni *production* zaidi ya mara tatu.

Maana yake ni kwamba, mwaka 2007/2008, wakulima wa Mkoa wa Shinyanga, kwa jinsi ambavyo wameitikia wito huu wa Serikali, watakuwa na uwezo wa kufikia kilo labda 500 au 700 na mwaka 2010 lengo hilo tutafikia. Maana yake ni kwamba, *production* ya pamba itaongezeka mara tatu. Lakini *infrastructure* ya kuweza kusomba pamba hii kutoka vijijini, kama haijaangaliwa, maana yake ni kwamba, tutakuwa na kikwazo hapa ambacho kinaweza kikaathiri thamani ya pamba yetu na tukawavunja moyo wakulima wetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, Serikali iliangalie jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, labda nisionekane kwamba, naipa mzigo mno Serikali, nilifikiri ni vizuri nikatoa mapendekezo tu ya namna ya kukabiliana na matatizo ya fedha za kugharamia ukarabati wa barabara zetu za vijijini. Kwanza, katika mkoa wetu wa Shinyanga, kama nilivyosema, ni mkoa unaozalisha zao la pamba, lakini kwa bahati

mbaya hatuna mpango maalum au mradi wowote unaozungumzia uboreshaji wa barabara za mikoa, inayozalisha zao la pamba. Kama ilivyo kwa mfano, kwenye mikoa inayozalisha zao la kahawa, tumeona kwa mfano, Mradi wa *STABEX*, ambao unajikita katika kuboresha barabara zinazohusu mikoa hiyo. Lakini katika zao la pamba, kwa bahati mbaya inavyoonekana, Serikali haijatupia macho eneo hilo. Nilikuwa naomba kwa makusudi kabisa, ili kuinua uzalishaji wa zao hili, tujaribu kuangalia mkakati wa namna hii, ambao tutawashirikisha wafadhili waweze kushirikiana na sisi katika kuboresaha barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusisha wawekezaji katika kutunza barabara. Mimi natoka Jimbo la Msalala, ndiyo ambalo lina mgodi mkubwa kabisa wa dhahabu hapa Tanzania, Mgodi wa Bulyanhulu. Kwenye eneo hili, nimekuwa na matatizo mengi sana, kuhusu barabara inayotoka Mjini Kahama kwenda Kakola, ambayo inaunganisha barabara kati ya Kahama na Geita. Kwa bahati mbaya sana, barabara hii watumiaji wake wakulibwa ni *Kahama Mining,* wanapitisha malori yanayosomba mchanga, wastani wa malori yanayopita katika barabara hiyo yenye zaidi ya tani 40 kwa lori, ni malori kumi kwa siku. Kwa hiyo, kila siku zinapita tani 400 za mchanga, katika barabara inayokarabatiwa na Halmashauri. Kwa wastani wa *trip* mbili za kokoto au za kifusi kwa mwaka na malori mazito ya namna hii yanayopita, haiwezekani barabara hiyo ikawa katika ubora. Sasa hiyo barabara haipitiki kabisa.

Kwa kawaida barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 56 na kwa barabara ambayo ni nzuri kama ilivyokuwa imekarabatiwa kule nyuma, mtu unaweza ukatembea kwenye barabara kwa chini ya nusu saa. Sasa hivi tunatumia zaidi ya saa tatu na inakuwa ni aibu na kila mtu anakuwa anasema kwamba, eneo hili linahitaji kuangaliwa. Sasa katika majadiliano na hawa wawekezaji, kumejitokeza suala kwamba, mazungumzo yanakwenda vizuri, wameanza kutoa dola laki mbili kwa mwaka, kama kodi kwa Halmashauri.

Nilipenda kutoa kama tahadhari kwamba, dola hizo laki mbili zinazokuwa zimetolewa, si kwamba zinatolewa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii pekee, bali zinatolewa kwa ajili ya *community development activities,* ambazo zinafanyika kwenye Halmashauri kama wanavyofanya kwenye Halmashauri nyingine. Hawatoi tu kwa Halmashauri ya Kahama peke yake, bali wanatoa kwenye Halmashauri nyingine ambazo hazina utaratibu huu wa kusomba mchanga. Tatizo linalokuwepo hapa na ombi hapa ninalotaka kulitoa kwa Serikali ni kwamba, Serikali ifanye mazungumzo mahsusi na wawekezaji hawa, ili washiriki katika ukarabati wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ni kwamba, kwa bahati mbaya tu, Mikataba hii ya uwekezaji imekuwa ni ya siri sana. Matokeo yake tunalazimika kuegemea kwenye fununu. Fununu zilizopo ni kwamba, *Sutton Resources,* ambao walikuwa wanamiliki mgodi huu kabla ya kuuza kwa *Barrick*, walikuwa wameji-*commit* kuwa wataikarabati barabara hii. Mwaka 1999 mgodi huu ukanunuliwa na *Barrick* kwa dola milioni 280, wakaanza kuuendesha. Toka wakati huo, ukarabati wa barabara hii ukafifia na kwa kuwa kipengele hiki kilikuwa kinaonekana kwamba, kilikuwemo kwenye Mkataba au *commitments* za *Sutton Resources.* Inavyoonekana ni kwamba, kuna kitu kilichotokea

katika uhamishaji wa umiliki kutoka yule mmiliki wa awali hadi mmiliki wa sasa, kilichowafanya *Barrick* waache kuikarabati. Naomba kiangaliwe.

Ukimwuliza mmiliki wa sasa, anavyoonekana kudai ni kwamba, mazungumzo tu hayajakamilika kikamilifu, yeye ana nia kabisa ya kuweza kuikarabati barabara hii. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba pamoja na kwamba, tumekuwa tukiomba kila wakati Mikataba hii ingekuwa wazi, ili na sisi wananchi tujue haki zetu kwamba, hiki kitu ni haki yetu, kwa hiyo, tudai kutokana na Mkataba au la. Pia ningeomba tu kwamba, kwa sababu Wizara ya Nishati na Madini, imeonyesha mwenendo mzuri sana wa mazungumzo kati yao na wawekezaji. Hadi sasa tumefanikiwa kuondoka kwenye hili tatizo la kutopata hizi dola laki mbili. Nilikuwa naiomba Wizara hii iendelee na *spirit* hiyo hiyo ya kufanya mazungumzo na hawa watu, ili waweze kukarabati barabara ambazo zinatoka kwenye maeneo yao na hasa hii barabara ya Kahama – Kakola, ambayo kwa kweli mimi ninavyoiona, zaidi ya asilimia 80, mtumiaji mkuu ni *Kahama Mining Corporation Limited (KMCL)* na Halmashauri yetu haiwezi kuikarabati.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Wizara ijaribu kuwasiliana na hawa. Baada ya kusema hayo, nilikuwa naomba tu nishukuru na vile vile nimalizie kwa kuomba kwamba, fedha zinazowekwa kwenye Mfuko wa Barabara ziongezwe, kwani hata barabara zinazo karabatiwa na *Road Fund,* bado pesa ni kidogo na wachangiaji wengine wametoa namna mbalimbali za kuongezea fedha kwenye Mfuko na kwa sababu muda umekwenda nisingependa kurejea hilo. Lakini nilikuwa naomba tu kwamba, fedha ziongezwe kwenye *Road Fund* ili tuweze kukarabati barabara za vijijini. Tukiwashirikishe wawekezaji waliokuwa kwenye maeneo yetu, barabara zetu zitaboreka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kuwasilisha hoja hii vizuri na naamini kabisa yeye ni mahiri, akiwa ni Waziri mzoefu wa miaka mingi na pia kapewa Wizara nzito namna hii, kwa sababu ya uwezo alionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwanza, kwa upande wa barabara, umuhimu wa barabara unaeleweka. Lakini shukrani zangu nazitoa kwa jinsi ambavyo unavyoweza kuziangalia barabara, walau barabara kuu ya Mkoa wa Kagera. Ukiangalia sasa kwa upande wa barabara yetu ya kutoka Mutukula mpaka Muhutwe, Muhutwe mpaka Kagoma, ambayo ndiyo mwisho wa lami mpaka hivi sasa katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Natoa shukrani kubwa sana na nimesoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Serikali imekusudia kuwa itaitengeneza barabara inayotoka Kagoma kwenda mpaka Rusahunga. Kwa kuwa Rusahunga kuna lami, basi itakuwa tumeunganishwa kutoka Mutukula kufika mpaka Rusahunga. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba marekebisho madogo madogo, ambayo yalijitokeza katika barabara ya Muhutwe - Kagoma na nilikuwa sijaiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika. Ningelipenda uiangalie, kwa sababu imesababisha malalamiko makubwa na inakuwa ni kero kwa wananchi, ikiwemo maeneo ambayo maji

yanapita kwa kasi na maeneo mengine ambayo yalitakiwa kuwekewa makalvati, hayakuwekwa inakuwa kidogo ni kero. Nilipowasilisha ilionekana inaweza ikarekebishwa lakini haijarekebishwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ombi tu, tunaomba tupewe matuta. Mimi ninashangaa nilipowahi kuomba tutapate matuta katika barabara hiyo wakati haijakamilika vizuri, niliambiwa kwamba, barabara kuu haiwezi kuwekwa matuta. Kinachonishangaza ni kwamba, unapotoka Morogoro kuelekea Dodoma, kuna matuta mengi tena mengine ni ya ajabu kabisa, kwa sababu hata alama za barabarani, unawekewa alama, kutoka pale ni hatua kumi tu kuna tuta na hata sijui ni utaalam gani wa kuonyesha kwamba, alama ya barabara inawekwa hatua kumi kabla ya kuifikia. Kwa sababu tuchukulie ile ni *high way,* ni lazima tu *speed* ya dreva inakuwa ni kubwa. Kwa hiyo, inatakiwa atoe taarifa walau hatua hata 100 kabla ya kufikia ile alama kwamba, hapo ni mahali ambapo inatakiwa kupunguza mwendo, kwa sababu inaweza kusababisha ajali kutokana na hali halisi. *(Makofi)*

Inashangaza ni katika barabara ile ile ambayo imekatazwa matuta yasiwekwe katika barabara ya kwetu. Naomba maeneo yanayostahili matuta yapo, yawekwe matuta kama ni sera ya nchi. Kama ni Sera ya nchi kutokuweka matuta, yaondolewe katika barabara zote za Tanzania. Ziwekwe alama ya *zebra,* ambazo zitaweza kutumika sawasawa katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa tusaidiwe sisi wananchi tunaotoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa mpaka Kanda ya Kati, bado hali ya usafiri siyo nzuri. Tunashangazwa kwa pamoja, ni kwa kiwango gani ambavyo ujenzi wa barabara unakwenda pole pole sana. Barabara inayotoka Dodoma kuelekea Manyoni, Shelui mpaka Ilula, haieleweki ni kwa nini haijakamilika mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama utaratibu uliokuwa umeanza kutumika siku za zamani utakuwa unatumika kwamba, kama Mkandarasi atacheleweshwa kujenga, basi atailipa Serikali, mimi nitakuwa nashukuru. Kwa sababu pamoja na kuchelewesha kukamilika kwa barabara, basi awe anailipa Serikali yetu, kwa kuchelewesha kuijenga barabara hiyo. Lakini kama ataendelea kuchelewesha na Serikali bado inaendelea kumlipa, nafikiri lipo tatizo na hilo tatizo lirekebishwe haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba barabara ya Usagala - Bwanga – Kyanyolwa, ikamilike. Sisi wananchi wa Mkoa wa Kagera na Mara, tunatumia sana sisi Mji wa Mwanza, kwa sababu ni mji ambao kwa namna nyingine, ndiyo mji mkubwa katika yale maeneo. *(Makofi)*

Inapokuwa kuna barabara zinazoelekea Mwanza zimekaa vizuri, ni rahisi sana kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa, kutumia makao makuu ya Mwanza kama eneo la kupatia mahitaji yao muhimu. Lakini vile vile ni mji ambao ni mkubwa, ukiangalia katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kwa hali hiyo, naishauri Serikali jambo hilo iliangalie na lisiendelee kuchelewa kama ambavyo inaelekea hali ambayo iko sasa.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la barabara, naishukuru Serikali kwa sababu katika pesa za *STABEX* imetenga kwamba, barabara yangu ya Ruhanga - Nyakahama inatengenezwa na nimeacha iko katika hatua nzuri imekwishaanza. Naishukuru Serikali pia kwa Daraja la Kamwana, ambalo lilikuwa limekwama kwa sababu ya kukosa barabara. Nashukuru pia Serikali kwa kukubali kuitengeneza barabara ya Kanyambogo – Rubya - Ibuga, ambayo ilikuwa imekwama kwa pesa za *STABEX.*

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba ni usimamizi, barabara hizi mara nyingi zinaachwa chini ya Wahandisi wa Halmashauri za Wilaya na mara nyingi si wafuatiliaji wazuri. Ukizingatia kitengo pia cha Uhandisi cha Halmashauri hakina gari. Kwa hiyo, ili iweze kutembelea miradi hiyo, inategemea mpaka Mkurugenzi awe amekubali kutoa usafiri.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, ninaomba uwanja wetu wa ndege wa Bukoba pia uangaliwe katika ahadi ambayo tulipewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipotutembelea ni kwamba, uwanja wetu wa Bukoba utatengenezwa. Uwanja wetu ni miongoni mwa viwanja vidogo, lakini ni muhimu. Nawashukuru walioweza kufanya uwanja huu ukaendelea kuwa muhimu, waendeshaji wa ndege za *Precision,* wamefanya uwanja huu umeendelea kuonekana ni muhimu sana, kwa sababu ndiyo wanaorusha ndege zao kila siku katika ule uwanja. Lakini bado ni uwanja mdogo, ambao hautoshelezi kwa ndege ambazo ni kubwa.

Wananchi wengi wangependa kutumia usafiri wa ndege, lakini ndege inayokwenda pale ni ndogo, mara nyingi abiria wanabaki. Kwa hiyo, tunaomba uwanja wetu utengenezwe na ninaamini itakuwa ni kichocheo kizuri cha uchumi kwa Mkoa wa Kagera, kwa sababu Mkoa wa Kagera sasa hivi una samaki wa kutosha na kuna madini ya bati ambayo yaliachwa achwa tu kwa sababu hayakufuatiliwa. Lakini pia kuna maeneo mengine mazuri ya Ngara na kadhalika, uwanja ule unaweza ukasaidia kuharakishwa kwenda kutembelea kuona hayo maeneo.

Nomba nizungumzie kuhusu barabara za Halmashauri. Kamati ilipendekeza kwamba, ingelifaa barabara hizi zingelijengwa *TANROADS.* Kwa kuwa mimi nafikiria kwamba, majukumu mengi yameelekezwa katika Halmashauri za Wilaya, pengine nikaona sababu ya pendekezo hili, ilizingatia uwezo mdogo walionao Wahandisi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba wataalam wawe ni makini katika suala zima, mathalani la ujenzi wa barabara. Suala la uhandisi katika Halmashauri za Wilaya ni suala ambalo ni la kitaalam. Naomba suala zima la kuwateua hawa wataalam ambao ni Wahandisi, basi lizingatiwe. Izingatiwe sifa ya mwombaji, kazi, uwezo wa kazi anayokusudiwa kwenda kuifanya au inayokusudiwa kuwa imefanyika. Lakini vile vile uaminifu na uadilifu, hasa katika uteuaji wa Makandarasi. Yamekuwepo matatizo makubwa sana ambayo Wahandisi wengi wamekuwa wakiyachangia katika uteuaji wa Makandarasi. Hili nina mfano, mwaka 2004, TAMISEMI ilinipatia shilingi milioni 30 kwenda kujenga Daraja la Kishala. Hizo pesa zingeweza kutosha kama zingetumika mwaka ule.

Ilichukua mwaka mzima kumteua Mkandarasi, alipoteuliwa akateuliwa mkandarasi ambaye mimi naweza nikamwita, Mkandarasi feki. Kwa sababu alishindwa kujenga daraja na mpaka sasa hajajenga daraja. Kwa hiyo, ilifahamika kuwa, Mkandarasi huyo aliteuliwa kwa makosa na hata Mhandisi mwenyewe hana sifa za Uhandisi, ambapo sasa hivi ameachishwa kazi. Lakini wakati Mhandisi akiachishwa kazi, wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini, wamebaki hawana daraja. Hakuna pesa zile na hatujui mpango gani unaofuata wa kuhakikisha kwamba daraja lile linaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima la uaminifu na uadilifu na uwezo wa kukwepa vishawishi vya rushwa, litakuwa ni la msingi kwa Wahandisi wa Halmashauri za Wilaya, ili waweze kuendelea na kazi hii ambayo ni muhimu sana. Tunavyozungumza suala zima linazohusu barabara, hakika barabara ni muhimu na huwezi ukasema utakuwa na maendeleo mazuri, kama hauna barabara nzuri. Mawasiliano mengine yatafuata, simu utapata na mambo mengine muhimu, *internet* na kadhalika, lakini barabara kwa kila mmoja. Hata ambaye hatumii gari, angependelea kuwa na barabara nzuri, aweze kutembea bila kujikwaa miguu yake.

Kwa hiyo, nashauri kwamba, Halmashauri ziendelee kufanya kazi za barabara, lakini wakati huo huo ule Mkataba wa kazi, ambao Serikali inakusudia kuuanzisha, uwabane kweli kweli ili wanapokuwa wamepewa kazi, wahakikishe kwamba, wanaitekeleza kwa jinsi ambavyo imekusudiwa. Lakini pia naiomba Sheria ya *Road Toll* irekebishwe, kiwango wanachopewa cha asilimia 30 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na asilimia 70 zikabaki Serikali Kuu, mimi naona ni kidogo. Sasa hivi Serikali Kuu, imeshapungukiwa barabara nyingi, ukichukulia kwamba, barabara nyingi sasa hivi ni za lami kwa hiyo, matengenezo yake ni madogo madogo. Barabara nyingi sasa zimebaki katika Halmashauri na barabara hizo nyingi ni za udongo na katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, ambako kuna mvua nyingi kama Mkoa wa Kagera, barabara hizi zinaharibika mara kwa mara. Kwa hiyo, pesa inayotengwa inakuwa haitoshi.

Kwa hali hiyo, ni vema sheria hii ikarekebishwa ili kiasi hiki cha asilimia kiweze kuonekana, ni kwa namna gani kitakavyoweza kusaidia kupunguza matatizo ya Halmashauri, lakini kisiendelee kuwa asilimia 30. Ikiwezekana iwe ni *vice versa* iwe asilimia 70 kwa asilimia 30. Halmashauri ichukue asilimia 70, Serikali Kuu ibaki na asilimia 30, bado naona inaweza Serikali Kuu ikapata wahisani kutoka maeneo mengine. Vile vile kuwe na posho zinazoangalia mazingira. Sisi tunaotoka katika Mikoa na Wilaya za pembeni mwa nchi, hakika ni za mipakani mwa nchi, mazingira yetu bado ni magumu. Tunaomba watu wanaofanya kazi katika maeneo hayo, waangaliwe kwa jicho la kuwasaidia na kuwapa moyo wa kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nachangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilizungumzia suala zima la bei ya mafuta. Baada ya tarehe 1 Julai, 2006 ni vituo vichache sana, ambavyo vilikuwa vimeweza kurekebisha kidogo hiyo bei ya mafuta. Mimi nawapongeza sana kwa walioweza kufanya hivyo. Lakini kilichonikera na

kunisikitisha, ni wale waliokuwa wametoa mawazo yao kwamba, hawawezi kubadilisha bei kwa sababu walikuwa na *stock* ya zamani.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wetu, tunapokaa katika vikao kama tunaongeza bei, kama bajeti inakuwa ni ya kuongeza bei, wengine wanafikia hata kubana ile bidhaa kusudi ifike ile tarehe wapandishe bei, bila kusahau kuwa *stock* ile ni ya zamani kusudi wapate faida. Katika hili, hili ni azimio la nchi. Nchi kama imeazimia kwamba, sasa tunakwenda kupunguza, tunaondoa *VAT* katika mafuta kusudi bei iteremke, usafiri uwe ni rahisi, uzalishaji katika viwanda uwe ni rahisi, jambo hili ni lazima lifanyike bila kuangalia habari ya *stock* ya zamani. *(Makofi)*

Niendelee kuishauri Serikali kwamba, katika hili iliangalie kwa umakini sana na ihakikishe kuwa, kama siku za zamani haisimamii bei sasa baada ya kuhakikisha kwamba, imeondoa *VAT*, ni lazima ijulikane hii *VAT* imeondolewa, ni asilimia ngapi ambazo wanatakiwa kushusha.

Kwa sasa aliyeshusha kwa hela kidogo tu, mathalani mimi nilinunua mafuta tarehe 28 Juni, 2006, ilikuwa ni petroli ilikuwa lita moja shilingi 1,480, leo wanauza shilingi 1,420. Wamepunguza shilingi 60 tu. Sina hakika kama shilingi 60 ndiyo *twenty percent* ya *VAT,* ambayo inauzwa kwa kila lita. Nilikuwa naomba suala hili litazamwe ili ile haki iliyokusudiwa kwa mtumiaji, iweze kuonekana kweli imeweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali, ione uwezekano wa kuanzisha wakaguzi binafsi wa magari. Sasa hivi magari ni mengi na hakika Serikali peke yake, kwa hiki kiasi inachosema itatoa mafunzo, bado ni wachache. Katika Mataifa mengine, kunakuwa na wakaguzi binafsi, wanakuwa sambamba na Serikali, wanasaidiana katika ukaguzi na hawako juu ya sheria kwamba, watakuwa wao ndio wakaguzi wenye mamlaka ya mwisho.

Kauli zote zinatoka katika Serikali, lakini watahakikisha kwamba, wanaisaidia Serikali kuwa waaminifu kukagua katika viwango na wakati mwingine kufanya utafiti na kuishauri Serikali jambo la kufanya. Hakika tukiendelea na wakaguzi wetu wa humu nchini, tutaendelea kuwa na matatizo mengi tuliyokuwa nayo.

Watanzania wamekuwa na tabia fulani, ambayo hawapendi *challenge*, inapotokea jambo jipya, tunakuwa ni wachelewaji kupenda kubadilika. Nina hakika hata huu ukaguzi, bado utaendelea kuonekana ni ule ule wa kizamani, wakitoka chuoni ni wale wale. Sasa kama kungekuwa na wakaguzi binafsi, wanaoanzishwa kwa sheria ya nchi yetu na ambao hakika watakuwa wanakagua bila kwenda nje ya utaratibu, mimi naamini wanaweza wakaisaidia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kuboresha usafiri, kushukuru kwa barabara zetu za Mkoa wa Kagera, kiwanja chetu cha ndege cha Bukoba, kuangalia habari ya *VAT* tena na bei halisi ya mafuta baada ya *VAT* kutolewa, pamoja na kuomba

wakaguzi wa magari binafsi wawepo wanaojitegemea. Basi naomba niseme, ninakushukuru tena na ninarudia kusema ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii aliyoiwasilisha Mheshimiwa Basil Mramba. Kabla ya kufanya hivyo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na wana-CCM, kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Vilevile niwapongeze viongozi wa sekretarieti wakiongozwa na Mheshimiwa Yusuf Makamba, kuwa katika sekretarieti ya chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wategemee uongozi bora chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kama ambavyo wamekuwa wakiupata kuanzia Mwalimu Nyerere, Mzee Mwinyi na Mzee Mkapa.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza, ndugu zangu wa jimbo la Mlalo, kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi na wateule wa Chama cha Mapinduzi, kwa upande wa Rais na Mbunge na Madiwani wote. Sisi kule kwetu, wananchi wa jimbo la Mlalo, hawana wasiwasi na Chama cha Mapinduzi, ndio maana Rais wamempa kura zaidi ya asilimia 90, Mbunge wamempa kura zaidi ya asilimia 90 na Madiwani wote ni wa CCM. Kwa hiyo, Chama cha Mapinduzi pale kipo katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nikupongeze wewe mwenyewe, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu hili. Tunashukuru kwa kazi nzuri unayoifanya na tunaamini kwamba, utaendelea kuwatumikia Waheshimiwa Wabunge, ili tuweze kufikia malengo ya Bunge letu kuwepo na vilevile niwapongeze Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Katika enzi hizi za utandawazi, ili uendelee unahitaji vitu vifuatavyo: Unahitaji maji, kwa maana ya kwamba, kila kiumbe, iwe binadamu, wanyama na mimea, kinahitaji nishati, iwe ni *hydro, thermo, petroleum* ama inatokana na gesi. Ili uendelee, unahitaji chuma ambacho tunacho cha kutosha kule Liganga na Mchuchuma na makaa ya mawe. Unahitaji mawasiliano katika ujumla wake, iwe ni kwa maana ya *technohama,* iwe ni kwa maana ya usafiri wa anga, usafiri wa ardhi na kwenye maji. Leo hii tunazungumzia Wizara hii ya Miundombinu, sina matatizo na hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mramba, ni nzuri, inakidhi malengo ya bajeti na kwa vyovyote vile, bajeti tumekwisha ipitisha. Hiyo ndio mipango iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, labda kitu cha kuzungumzia hapa ni mwelekeo wa huko tunakokwenda. Kwa sababu Wizara hii ni muhimu mno katika uhai wa Taifa letu. Ni muhimu kwa sababu ni Wizara mtambuka, kama vile ilivyo TAMISEMI. Inamgusa kila mwananchi. Mimi nataka kujikita zaidi kwenye sera ya mawasiliano, hususan barabara. Nikizungumzia barabara, nataka kuzungumzia barabara zile ambazo zimetajwa katika Ilani ya Uchaguzi. Lakini vilevile na barabara za vijijini, ambazo kwa bahati mbaya

hazihesabiwi kama ni muhimu kwa *level* ya Wizara hii, ila zile ziko chini ya Halmashauri zetu. Lakini Wizara hii inahusika, kwa sababu fedha zinazogawiwa katika Halmashauri zetu, zinatoka kwenye Mfuko wa *TANROADS.* Kwa hiyo, ufanisi wa matengenezo na uimarishaji wa barabara za vijijini, unategemea tunapata fedha kiasi gani kutoka Serikali Kuu. Hapo ndio napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine, waliotoa rai kwamba, gawiwo linalotolewa kwenye Serikali za Mitaa, lazima liongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, suala hili limezungumzwa kwa takriban zaidi ya miaka minne sasa. Katika kila kipindi cha bajeti, Wabunge wanasimama, wanazungumza jinsi gani ambavyo fedha hazitoshi. Mgao ule unaotolewa wa asilimia 30, unaokwenda TAMISEMI na asilimia 70 kubaki Wizara ya Mawasiliano, kwa kweli ni kugeuza mtazamo mzima. Wazungu wangesema una-*put the cart before the horse.* Fedha ingekuwa vizuri uwiano uwe ni asilimia 70 ziende kwenye Halmashauri na asilimia 30 zibaki Serikali Kuu. Sababu ni ndogo tu. Serikali Kuu inazo *sources* nyingine, inapata wafadhili, inapata misaada kutoka nje. Serikali za Mitaa hazina mahali pengine zinapopata. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima tutafute njia ya kuongeza fungu hili, kwa sababu hata hizo barabara tunazojenga, kama haziwezi kuunganishwa na barabara za vijijini, hazina maana yoyote kwa Mtanzania. Lazima tuweke mkazo katika kuziwezesha Halmashauri zetu, ziweze kuhudumia barabara hizi za vijijini. Nimekuwa nikiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hapa, wanazungumzia juu ya mikoa ya pembezoni na sisi ni wilaya ya pembezoni, tumepakana na Kenya. Zipo wilaya za kati sisi tuko pembeni kule. Lakini kwa bahati nzuri, wananchi wa Wilaya ya Lushoto ni watu ambao wanajituma, wanachimba, wanajenga barabara zao wenyewe. Tunachokihitaji sana sana katika kuwasaidia, ni basi kama *road fund* ile itaongezwa, itawezekana kuwasaidia kuwawekea makalvati ama madaraja pale ambapo panahitaji au kulipua miamba.

Mheshimiwa Spika, nawashauri ndugu zangu wa Wizara ya Mawasiliano wafike Wilaya ya Lushoto na vilevile hata jirani zangu Wilaya ya Same pale na Mwanga, waone juhudi za wananchi katika kujiletea maendeleo yao kwa kuchimba barabara zao ili angalau wahamasike kuona jinsi gani watawasaidia wananchi hawa. Kuna barabara zinachimbwa. Utakuta linalowasumbua wananchi ni mwamba tu, unahitaji kulipuliwa, lakini mwananchi atapata wapi vifaa vya kulipulia miamba ile. Anachohitaji ni makalvati tu, sasa inahitajika nguvu kutoka nje ya uwezo wa kijiji ama daraja. Kwa hiyo, ni vitu kama hivi, ndio maana tunahitaji Mfuko wa Barabara uongezwe. Sisi wenyewe tuna uwezo wa kuchimba barabara zetu, wakati maeneo mengine wenzetu wanakazania barabara za lami, sisi tunataka kuanzia kwanza na kuwezeshwa ili tujiwezeshe sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nizungumzie sera kwa ujumla, nizungumzie suala la *transport corridors*, kwa sababu inaelekea wakati tunazungumzia mawasiliano, mara nyingi tunakimbilia tu kwamba, unajua hapo upo utalii, hapa kuna faida hii na hapa kuna faida hii, hatuangalii *network* au mfumo wa barabara wa mawasiliano katika nchi yetu unakwenda vipi. Wakoloni waliotutawala waliliona hilo, ndio maana Mjerumani akaona kitu cha kwanza katika kuitawala Tanganyika, lazima

watandike reli kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, lakini yeye aliona umuhimu huo sisi hatujaliona hilo. Nadhani juhudi tunazofanya hazitoshi, kwa sababu mwelekeo wetu tunavyozungumzia inaelekea kana kwamba, tunachotaka ni kuiendeleza reli hii hii. Kwanza, reli ile iko *below standard*, ni *narrow gauge*, inatakiwa sasa twende kwenye *international gauge.* Nafurahi Waziri amezungumzia kwamba, upo uwezekano, lakini hata usipokuwepo uwezekano, ni lazima twende kwenye *international gauge*, kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, kutoka Tabora kwenda Mwanza na Mpanda, na mahali popote ambapo tuna reli.

Pili, hiyo haitoshi, nilitazamia *planners* wetu sasa hivi wangekuwa wanazungumzia jinsi gani tutatandika *a second rail line*. Hii habari ya kungojea treni inatoka Da es Salaam mpaka ikifika Kidugalo ipishane na nyingine, ikifika Morogoro ipishane na nyingine, ndio tunaongezea muda wa safari na mwishowe tunaongeza gharama. Nchi zote ambazo zinathamini reli, sasa hivi wanaweka *second rail line*, kwa nini sisi hatufikirii hilo? Lakini hilo halitoshi, hatuna mafuta sisi na reli zetu hizi zinategemea mafuta, hivi kwa nini tusifikirie ku-*electrify.* Silioni mahali popote katika mipango yetu ile?

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani ni lazima suala la kufungua mawasiliano kwenda Magharibi, yawe ni ya reli, yawe ni ya barabara, lazima liwe mbele yetu kama vile sala ya bwana. Haiwezekani kila siku tusimame hapa, tuombane kana kwamba, tunaomba fadhila kufikisha mawasiliano bora kule Kigoma, kana kwamba, tunaomba fadhila kuweka mawasiliano kati ya Mtwara na *Mbamba Bay* au kutoka Tanga kwenda Musoma. Haya ni lazima tuyafanye. Wakati tunapanga, lazima tufikirie na maslahi na usalama wa Taifa. Hata wakati tunazungumzia viwanja vya ndege tunazungumzia tu Kilimanjaro, Dar es Salaam, sijui na Mbeya, hivi hatuoni kwamba, Mtwara lazima kuwe na kiwanja cha ndege cha Kimataifa, Songea lazima iwe na kiwanja cha ndege cha Kimataifa, sio kwa sababu ya biashara tu lakini vilevile kwa usalama. Sasa kama ungekuwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, tungejadili kwa undani zaidi, lakini *certainly* hata Mkoa wa Rukwa, lazima kuwe na uwanja. Nchi hii na dunia hii sio kila mtu ni ndugu yetu. Kuna wengine wanatuangalia kwa jicho la husuda kama kila siku tunavyoomba hapa. Kwa hiyo, lazima tuweke viwanja vya ndege Mkoa wa Rukwa, Kagera, lazima tuweke *International Airport.* Hayo matatizo yatakwisha, kama hao wanaotuzunguka tutaungana, lakini kama hatujaungana, lazima tujihami hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano ya simu, nimeona tunazungumzia ikifika mwaka 2018 zitakuwepo simu sita kwa kila watu 100, hatuendi na wakati. Kinachotakiwa sasa ni kuhamasisha kampuni hizi za simu za mkononi, wahakikishe kila kijiji kinafikika, hivyo tutakuwa tumeifanyia *short cut* mara moja. Kwa nini tungojee mpaka mwaka 2018. Maendeleo ya mwananchi anayataka leo sio kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba *planners* wetu wanapofikiria mikakati ya kuweka mipango yetu, lazima wafikirie sio tu suala la uchumi, vilevile suala la maslahi na usalama wa nchi hii. Lazima tufikirie kwamba, katika kuwekeza upande wa Kusini, tusitafute *quick buck,* kwa

sababu sasa inaelekea tunataka kuzungumzia utalii, *that is perishable commodity,* unachohitaji ni Osama Bin Laden mmoja, hakuna utalii, kwani hatukuona wakati Ubalozi wa Marekani unalipuliwa, tuwekeze kwenye *basic infrastructure* yetu na hiyo kama hatukuifanya sisi, basi wengine hawatatufanyia. Barabara zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi, nashauri tuhakikishe tunazijenga kwa sababu maendeleo yetu hayawezi kungojea. Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kazungumza kwamba, planners wetu wawe wanzalendo, kwanza, wasitumie tu *economic basis for their planning.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa kutangaza kwamba, Wabunge wote wanaotokana na Chama cha Mapinduzi, wanatakiwa kwenye kikao kifupi cha dharura, kwenye Ukumbi wetu wa Zamani. Mara baada ya Bunge kusitishwa kwa asubuhi hii, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, wanaombwa kukutana katika Ukumbi wetu wa Zamani saa saba na dakika kumi na tano, ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi nichukue nafasi hii, kumpongeza Rais wetu, ambaye juzi juzi hapa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi, kwa kura zote, isipokuwa kamoja. Lakini pia nichukue nafasi hii kuipongeza sekretarieti mpya ya Halmashauri Kuu ya Taifa na uongozi wa Mheshimiwa Luteni Yusuf Makamba na wenzake. Tunahakika sasa hiyo Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, ndio itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Lakini pia niwapongeze wale waliokuwepo huko nyuma, ambao wameachia ngazi juzi juzi, huku wakiwa wamefanya kazi nzuri na wametufikisha hapa tulipofika. Nimpongeze pia Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye *speed* yake tunaiona na uwezo wake mkubwa tunauona, hatuna shaka miaka mitano inayokuja, mambo yatakuwa tofauti kabisa. Nikupongeze pia wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, kwa *standard* na *speed* ya hali ya juu na nina hakika hata tutakavyokutana, kule kwenye jengo letu kule ni katika hali hiyo hiyo ya *speed* na *standard*, baada ya hapa. *(Makofi)*

Sasa niingie moja kwa moja kwenye mchango wangu, nimesikia mazungumzo mengi sana Wabunge wenzangu, katika suala la mawasiliano na hasa barabara. Mimi nina hakika kama Wabunge wawili au watatu, nikiwachukua nikawapeleka kwenye jimbo ambalo mimi naliwakilisha, wataona huruma na uchungu jinsi maisha yalivyo mabovu, duni, uchumi ulivyokuwa nyuma ya watu wale wa kando kando ya Ziwa Nyasa. Ziwa Nyasa lile ni ziwa la pili kwa ukubwa katika Afrika yetu hii, lakini ziwa chafu hasa wakati wa mawimbi, la kwanza katika Afrika yetu hii. Lakini ziwa lile linahudumia mikoa mitatu; Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Ruvuma, hasa hasa wilaya tatu; Wilaya ya Kyela, Wilaya ya Ludewa na Wilaya ya Mbinga. *(Makofi)*

Watu wale wanaoishi eneo hilo kuanzia Matema, mpaka Chiwanda, kuanzia hapo panapoitwa *Matema Beach* mpaka Chiwanda, hawajawahi kuliona basi. Maisha yao yote tangu Adam na Eva, hawajawahi kuliona basi likipita na kuna kiti watu wanakaa wanasema, simama kituo, kituo hawajakiona tangu wamezaliwa. Serikali inakuja, inakwenda, kwa hiyo, wao wameona ni wa hivi hivi na wale wenyewe wanasema sisi si

Watanzania na wala si Watanganyika, wanasema sisi ni wa *Nnyasa land,* maana hata Wanyasa wenyewe wa Malawi waliashaamua kuacha jina hilo wanaita Malawi. Lakini wale wa *Nnyasa land* na wakiyaona yale maji, ndio Mungu wao, ndio mkombozi wao, maana hawaoni kama kuna kitu kingine kitakachokuja kuwakomboa. *(Makofi)*

Mimi nilipokuja kugombea Ubunge kule, wale watu wakasema tumezoea mnakuja mnakwenda na wewe mtoto wetu umeimbaimba sana huko, njoo na wewe ufanye hapa, ndio walivyoniambaia sasa wameshazoea. Wanasema Mbunge wao alishakufa zamani sana na wanaomba afufuke, dunia hii ifike tena, atakuwa Mbunge wao tena. Nikawauliza Mbunge wenu nani? Wakasema ni Dr. Hastin Kamuzu Banda, maana Banda wakati wa miaka 64 ile alitangaza sehemu kutoka Kyela kule Ludewa, Ruvuma, *Mbamba Bay* mpaka Chiwanda ni eneo la Malawi. Kwa hiyo, alipotangaza hivyo, Serikali ikashtuka ndio ikaanza kutengeneza angalau madaraja ama barabara, ndipo watu wakaanza kuona magari kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, huyu akitangaza vile, huku tunaanza kuona magari, alipokufa hakuna kutangaza, kwa hiyo, Mbunge wao kafa. *(Makofi)*

Wanasema hivi kwa ukweli kwa uchungu, ziwa lile ni kubwa, lakini miaka ya 1970 kulikuwa na boti tatu; *MV Iringa, MV Songea* na *MV Mbeya*. *MV Mbeya* iligonga ikakazama mwaka 1978, watu walikufa, mizigo ikapotea, hakuna fidia, wakajua ni hivyo hivyo kwa sababu Mbunge alikufa, angekuwepo Mbunge wao angewatetea. *MV Iringa* hiyo boti imeharibika, imebaki boti moja inaitwa *MV Songea,* ambayo ndiyo inabeba mizigo, ndiyo inafanya kazi za kubeba watu. Saa nyingine mimi naomba Mungu tu, isitokee kama ilivyotokea kule Mwanza. Lakini wakati wowote, tutegemee kuzama kwa meli ile na watu ndani. Kwa sababu Ziwa linachafuka sana, ikifika mchana saa 8.00 huwezi kuvuka, lakini lazima ile boti ipite.

Sasa watu wanakwenda kutokana na mawimbi, mawimbi yakija anayakwepa anakwenda lakini ni hatari sana na kule watu wanakufa mara mbili, si mara moja, watu hufa mara mbili kwa nini? Kama mtu amekufa katika kijiji hiki, anataka akazikwe kwenye kijiji kingine cha kwake, lazima apande kwenye mtumbwi na likija wimbi kubwa maiti ile inapinduka inazama, kwa hiyo, inakufa tena mara ya pili. Maiti inazama, alikufa jana na anakufa tena leo. Kwa hiyo, utakuta watu wameweka makaburi kule lakini mtu amezama kwenye Ziwa. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, naomba sana Mawaziri wanaohusika na Wizara hii, watembelee si Tanzania hii, Tanzania si mpaka Ziwa Nyasa, kwa hiyo, watembee waende wakaone. Mimi nampongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, nilimwambia kuhusu hali hii na akaniambia twende, tukaenda. Tulipofika Mjini Songea, *Regional Engineer,* akasema siwezi kumpeleka mimi Waziri wangu huko akaumwe na mbu, nikamwuliza kwani huko hamna nyumba ya kukaa Waziri, nikamwambia atakwenda atalala nyumbani kwangu, ataangalia barabara. *(Makofi)*

Nikamwangalia Waziri usoni, unakwenda huendi, bwana mkubwa huyu uliyemweka hapa anasema usiende utaumwa mbu, mimi nasema twende, utakwenda

huendi? Mheshimiwa Makongoro akasema, Komba nimekuja kufanya kazi twende tukalale hata kwenye mchanga. Hhuyo nampongeza kweli kweli, amelala ameumwa, lakini ametuangalia jinsi tulivyo duni kule na nina hakika alivyorudi, miundombinu itaboreka. *(Makofi)*

La pili, kuna kivuko kule Mto Ruhuhu, mimi nimeona vivuko vingi sana kule, vingi sio kule tu sehemu zote nimeona. Vivuko vingi vina *engine, engine* inapigwa inakwenda mpaka ng'ambo watu wanavuka. Kivuko chetu sisi ni *engine* mgongo, inafungwa kamba huku watu wanavuta ile kamba, ndio waende ng'ambo, hicho ndicho kivuko tulichopewa sisi. Cha kwanza tulipewa hivyo, kikaanguka watu wakapotea, kiko pale pale hakijaondolewa, hiki cha pili sasa, nacho kitakata kamba.

Naomba sana Wizara hii, iangalie maisha ya watu wale kule nao ni Watanzania kama walivyo Warombo, kama walivyo Waarusha, kama walivyo Wadodoma na wengine, ni Watanzania wale. Redio hazifiki, habari hazifiki, magazeti hayafiki, kwa hiyo, wanaona ni kitu cha kawaida, wanasikia Redio Malawi kwamba, ngoma zikiwa Malawi ndio redio yao, basi wamezoea. Tunamshukuru pia Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, tulivyomwambia tu akawaambia *Celtel* waende kule, wamekwenda kule na sasa Mheshimiwa Maua wanatengeneza ile minara.

Kwa hiyo, naomba mwende kule, Waziri Mramba ufike kule, uone mambo ya kule, maana Serikali unaijua, umekaa muda mrefu tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, lakini kakanyage hii ya leo. Walivyokuwa mwaka 1961, wako vile vile, maisha yao vile vile. Kwa hiyo, ukatusaidie watu wale wanatia uchungu, wana uchumi mzuri, wana mahindi, wana samaki, wana mihogo, hawawezi kusafirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninyi nyote Wabunge mliopo humu ndani, wilaya yangu mimi moja kutoka sehemu moja mpaka sehemu nyingine, nauli shilingi 30,000, umeona wapi, wilayani kutoka Mbinga mpaka Dapori shilingi 30,000, kwa nini? Hakuna gari, kwa nauli mbili ya ghorofani na ya ndani, nikauliza ghorofani maana yake nini? Juu ya *carrier, landlover* juu ya *carrier* iko na nauli yake na ndani iko nauli yake. Unaambiwa unatafuta ipi, ya ghorofani au ya chini? Wilaya gani iko hivyo, jimbo gani liko hivyo? Lakini unakuta shilingi milioni 17 Rombo! *(Makofi)*

Ooh! Rais alisema huko kwa hiyo, ni sawasawa huku Rais hasemi? Rais anasema upande mmoja tu, kwa kweli si vizuri, hiyo keki tugawane vizuri, sisi hatujaonja keki hiyo inanoga vipi, ina harufu gani, ina maziwa au ina sukari. *(Makofi)*

Tunaomba katika nchi yetu wenyewe, mtufikirie kule, hatuna barabara, kiwanja cha ndege Songea ni lami, ndege haziendi ni kama Mwanza tu, kiwanja kizuri tu lami tu pyeeee! Lakini hakuna ndege inayokwenda kule na hakuna mtu anasema habari ya Songea. Sijui tunakaa watu gani, wanyama sijui, *actually* tuna majina ya wanyama, Komba, Kasunde, nani haya ni majina tu, lakini sisi ni watu.

Hebu tufikirieni na sisi, kaeni kule kuna kiwanja cha lami tuleteeni ndege hizo tunataka, hela tunazo si tunalima mahindi, si tunalima kahawa sisi, si tunavua, kwa nini, unang'ang'ania tu *Arusha International* ndege, Arusha mjini ndege na Siha na Moshi Mjini nako ndege. Nyie kina nani na sisi kina nani, ninyi mpate mna nini na sisi tukose tuna nini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niligombea Ubunge. Kwa hili, mimi sikuwa na shida. Mimi ni Msanii Mkuu katika nchi hii. Hela napata duniani kote, lakini maisha ya watu wale yalinifanya nirudi kule Kijijini nikawatetee. Ninaomba sana Waziri wa Miundombinu ukitoka hapa, ziara yako ya kwanza tembea na lile boti kuanzia Kyela mpaka Mtwara kama utakuwa hujalowa jasho. Ni maisha ya hatari! Maisha duni! Uone magari ya ghorofa ambayo hayako Dar es Salaam, yako Mbinga! Uone Shilingi elfu thelathini ndani ya Wilaya kwa kilomita 70! Sisi ni watu gani? Sisi Watanzania gani? Sisi lini?

Mheshimiwa Spika, Bandari ya *Mambabay*, mimi nimeziona Bandari na nazijua. Naijua Bandari ya Tanga, Dar es Salaam na Mtwara.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Sawa, hiyo kengele, sawa tu. Lakini pia naijua Bandari ya *Nkata Bay* ambayo itaunganisha *Mbamba Bay* na *Nkata Bay*.

**WABUNGE FULANI:** Kengele ya pili.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Kengele ya pili! Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hata Spika ameguswa sana na mchango huo. Natumaini Serikali imesikia. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Juma Killimbah, naona mwisho tunaweza kupata nafasi kwa Mheshimiwa Manju Salum Msambya na wazungumzaji wawili jioni. Tutakuwa na Mheshimiwa John Cheyo *(UDP)* - Mbunge wa Bariadi Mashariki na tutamalizia na Mheshimiwa Ngombale-Mwiru - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kupata wakati huu nikiwa mtu wa mwisho kuchangia mjadala huu mchana wa leo.

**WABUNGE FULANI:** Sio wa mwisho!

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Nikiwa wa mwisho kwa maana ya mchana wa leo, bado mjadala utaendelea jioni, watakuwepo wachangiaji wengine.

**WABUNGE FULANI:** Sio wa mwisho!

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichangie mjadala huu ambao kwa kiwango kikubwa Wabunge wamekuwa wakiongea kwa uchungu sana kwa minajili ya kuwawakilisha wananchi. Mimi naamini kabisa Wabunge wameonja joto ya jiwe kwa jinsi walivyopita huko wakiwa katika kampeni na wamejionea hali ya miundombinu ya nchi yetu jinsi inavyokwenda ikisuasua hasa hii ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilichangia katika mjadala wa Wizara ya Fedha. Moja ya jambo nililochangia, nilizungumza sana kuhusiana na barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida hadi Shelui. Nashukuru sana kwamba, baada ya kusema hapa, mwishoni mwa wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Miundombinu waliambatana na wakatembelea Singida kwenda kuona hali hiyo. Mimi nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu japo uliishia njiani hukufika katika safari yako kama ilivyokusudiwa. Lakini ile tu inatupa moyo na tunaamini kwamba Serikali ilisikia kilio chetu. Lakini kwenda kwa Waziri Mkuu bado haitoshi kwa sababu tumezoea viongozi wamekuwa wakifika na wanaondoka, matokeo yake hali ile inaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Waziri wa Miundombinu alituita baadhi ya Wabunge wa Mikoa ya Singida, Mtwara, Lindi na Dodoma tukawa na Kikao naye. Siku ile ndio nikagundua kwamba hatuna barabara hata moja ambayo inaweza kwisha kwa kipindi cha mwaka 2007. Ndio nikasikia pale katika Kikao kile barabara zote ambazo zinazungumzwa zitaisha mwaka 2008. Nikauliza, kwa nini? Nikaambiwa barabara ya Dodoma – Manyoni ilikuwa ipo kwenye mpango wa *Design and Build,* lakini ilicheleweshwa na mpaka sasa hivi kazi iliyotendeka ni asilimia 56.

Sasa tukaambiwa lazima kutakuwa na ucheleweshо katika barabara hiyo, hali kadhalika kwa barabara inayotoka Manyoni – Singida. Lakini hatukupewa ufumbuzi wa dhati kwa sababu hata yule mjenzi wa barabara ya kutoka Singida – Manyoni, baada ya kutokea kutoelewana na Serikali wakaambiwa waende wajenge barabara hiyo iishie eneo la Isuna. Sasa hatuelewi hiki kipande kilichobakia kitamaliziwa na nani na wakati gani. Hilo bado linatukwaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana, Waziri Mkuu ameniambia atakwenda tena Singida na safari hii namwomba badala ya kwenda na helikopta, sasa twende na barabara ili aone adha tunayopata sisi watu wa Singida, adha tunayopata sisi watu wa barabara ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ngoja niliache, ngoja niingie barabara hizi zinazoitwa za *TANROADS* (Barabara za Mikoa). Tunapokaa katika vikao vya namna hii, tunakuja kufanya mijadala muhimu inayohusu wananchi na Waheshimiwa Mawaziri wanapojibu majibu yanayowahusu wananchi naomba kwa kweli tuwe tunazingatia ni majibu gani tunayoyatoa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali juzi kuhusiana na barabara moja inayotoka Kizaga – Ndago – Sepuka. Barabara hii ina urefu wa kilomita 69 na barabara hii ilijengwa kwa kipindi cha mwaka 2004/2005. Barabara hii ilijengwa kwa kiasi cha fedha za Kitanzania zisizopungua Shilingi milioni 873. Leo ile barabara ni kiini macho na ni aibu kwa Watanzania kuonyesha barabara ile kama imejengwa. Barabara ile imedumu kwa kipindi cha miezi sita tu. Sasa leo tunasema tunafanya kazi, *value for money,* ndio hiyo kweli? Kazi inayofanyika ndio hiyo? Miezi sita barabara haipitiki, barabara imekwenda! Haipo! Pesa za walipa kodi nazo zimekwenda! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ule niliuliza, hivi sisi watu wa Singida tumewakosea nini? Singida hatuna kosa tulilofanya na Singida ni CCM yote na hii tunafuata Ilani ya CCM. Kwa hiyo, jamani waangalieni hao wananchi. Eneo ninalolisema barabara hiyo ina watu wasiopungua 55,000 magari yanaingia na kutoka. Sababu nilizopewa, naambiwa kwamba ile barabara baada ya kukamilika ilipitisha magari mengi sana, ilipitisha 140 kinyume na kiwango kilichotarajiwa cha magari 35.

Mheshimiwa Spika, sasa haya ni majibu gani? Barabara tunatengeneza, kumbe hata magari hatutaangalia kwamba yatapita kwa idadi gani! Naomba sasa mtuangalie sisi watu wa Singida kwamba tunapata adha na hasa wananchi wanapata adha kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara inayotoka Misigiri na kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya Kiomboi. Hii ina urefu wa kilomita 21. Tuliahidiwa barabara ile tukaambiwa tutaweka ile lami nyepesi na wakasema tutaweka katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha sijui, nimepekuapekua humu sijaona hizo milioni 500 ziko wapi na wananchi wanakumbuka yale mliyosema. Naomba tuwawekee wananchi wale ile lami nyepesi nao watakapofika kwenye kiunganishi cha Misigiri ili basi iwe karibu na Makao Makuu ya Wilaya yao. Hili ni suala muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hizi barabara za Halmashauri. Nitazungumzia barabara muhimu, hasa katika hali ya sasa ya kupambana na umaskini. Barabara hii ni muhimu sana na Halmashauri haina uwezo wa kuitengeneza. Lakini kwa kipindi kadhaa kupitia vikao vya *TANROADS*, Vikao vya Halmashauri tumeshawahi kusema barabara hii, basi iwe ya Mkoa. Barabara yenyewe ni ya Shelui – Konkilangi – Ntwike – Mingela – Tulya – Kidaru na baadaye kupandia Kisiriri ili uende Makao Makuu ya Wilaya Kiomboi.

Mheshimiwa Spika, katika barabara hii kuna sehemu inaitwa Tulya. ambapo kuna Ziwa Kitangiri na kuna vijana walioajiriwa wasiopungua 1,500 wanafanya kazi ya uvuvi. Lakini wavuvi wale wakishavua samaki ina maana samaki pale basi kwa hali yoyote ile zinaoza na sizipooza watakuja watu kuzilangua kwa bei ya chini na haiwezi kutosheleza kumwendeleza kijana wa pale Tulya. Kwa hiyo, ni muhimu kuangalia barabara hii ili tuweze kuinua hali ya maisha na hasa tukipambana na hali hii ya umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Barabara ya Kaselya – Kibaya – Mirungu – Urughu – Mtekente, nayo tunaomba iangaliwe badala ya kupiga kelele kwenye Halmashauri. Hii ni barabara muhimu sana na kule kuna watu wasiopungua 30,000 lakini hali ni ya matatizo sana na ndio maana hata leo hii utakuta kule kuna upungufu wa Walimu. Haiwezekani Mwalimu akaenda kule! Hata ukimpa milioni mbili atakwenda, lakini atarudi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikwenda Mheshimiwa Naibu Waziri, hayupo hapa, Mheshimiwa Mahiza amejionea, gari lake mwenyewe lilipata pancha karibu matairi yote. Tunasema hatuna Walimu, lakini Walimu tunawapeleka kule wanasema hapana, kama ni huku na kazi yenyewe ya Ualimu basi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie matumizi ya barabara. Hotuba imezunguzia suala la kuweka mizani barabarani ili kupima magari. Lakini hadi hivi sasa tunaona magari yanapita yakiwa na ujazo zaidi ya hizo tani yanayobeba. Gari ya tani tano linakwenda kubeba mpaka tani 12! Hizi *Fuso* hamzioni?! Mheshimiwa Waziri unataka kusema hamzioni hizi?! Zinapita na ukienda unaambiwa katozwa faini Sh.20,000/=. Sh.20,000/= ndio itafidia kujenga barabara zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu angalieni barabara. Nyie Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi, barabara ya kutoka Dar es Salaam ilijengwa juzi na Bunge hili limeanza, eneo la Magubike. Barabara ile haifai sasa hivi. Barabara ile imeshaweka tuta katikati, kisa ujazo wa magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana hawa watu wa mizani wafanye kazi ya kweli kweli ya kulinda barabara zetu sio kila mwaka tuje tupige kelele barabara ya Gairo, tunapojenga basi na hizi barabara tuzilinde kwa kuamini kwamba hawa watu wa kufanya kazi katika kitengo hicho wanafanya kazi kwa usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia Shirika la Posta. Upo umuhimu sasa Shirika la Posta liendane na hali ya sasa ya utandawazi, liingie katika mashindano. Shirika la Posta sasa hivi ni kweli linakwenda, lakini uendeshaji wake mimi siamini kama linakwenda na linashindana na hali ya sasa jinsi linavyokwenda. Ndio maana sasa unaweza ukakuta pamoja na kwamba tunaruhusu fursa nyingi kwa ajili ya kufanya biashara, lakini bado Shirika hili kwa sababu ni la kizalendo, tunaweza tukalihimiza sana na tukahakikisha kwamba linafanya kazi zaidi na hasa kuweza kutoa huduma kwa sababu lilikuwa linaaminika sana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hapa wamesema kwamba wamefungua Posta ndogo katika sehemu hizo walizozitaja za Kicheba, Bereko na baadaye wakasema kwamba Posta kamili Nyakato na Namanga. Lakini hata Iramba tuna maeneo makubwa. Sehemu kama ya Shelui, Ndago tunahitaji Posta ndogo hapo! Tunaomba sana ili kuweza kuendana na ushindani na hali ya kibiashara, shirika hili liongeze juhudi.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa simu upo, lakini naomba mashirika kama ya *Tigo, Celtel, Zantel* na *Vodacom* yaje yawekeze zaid. Mimi bado nina upungufu katika Kata zangu zile kumi na tano. Ni Kata tisa tu ambazo tayari zina minara, hizo nyingine sita bado hazina minara. Nawaomba sana tuje kuwekeza ili wale watu waweze kupata mawasiliano ya kutosha.

Mwisho nizungumzie kuhusiana na suala la Uwanja wa Ndege Singida. Kwa mwaka huu sijaona kama Waziri amezungumza juu ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Singida huko mnakojenga Viwanja vya Ndege sawa na sisi pia tunahitaji Kiwanja cha Ndege. Muda umefika, Singida Kiwanja cha Ndege tunakihitaji kwa sababu ya kuweza kuvutia watu mbalimbali na ushindani wa mambo mbalimbali. Tunaomba sana Uwanja wa Ndege Singida nao sasa ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwisho mchana huu.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nasikiliza kwa makini nikawa najiuliza, nianzie wapi niishie wapi? Lakini kwanza nimpe pole ndugu yangu Capt. John Komba kwa yale yote aliyoyazungumza, lakini asidhani yuko pake yake, tunafanana fanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuzungumzia Shirika la Reli. Anayetoka Kanda ya Magharibi Kigoma, Tabora akisimama hapa kama hakuzungumzia reli atakuwa yeye mwenyewe ana upungufu. Tumeelezwa kwamba hii reli inakodishwa na katika kukodishwa itatoa huduma nzuri. Naomba nitoe tahadhari, tusifanye kama ilivyofanyika kwa *TANESCO*. Imekuja Kampuni inayoitwa *Net Group Solution,* lakini Mitaani kuna kauli inayokwenda na *Net Group Solution,* imegeuzwa, wanasema, *They grouped them, they netted them and there was no solution*. Ndio imesababisha matatizo mengi ya hali ya umeme yaliyoko nchini sasa hivi.

Sasa naomba nitoe tahadhari kwa Shirika la Reli. Tunategemea Shirika la Reli kwa kukodishwa litoe huduma nzuri ya kisasa ili wananchi waone kwamba kweli kwa kipindi hiki ambacho ilikuwa haijakodishwa lilikuwepo tatizo na aliyekodishwa amekuja kuondoa tatizo.

Mheshimiwa Ngwilizi amezungumza vizuri kabisa kuhusu suala la reli na akatoa ushauri ambao naamini Wizara ikizingatia huyu anayekodishwa, tukiingia Mikataba vizuri tunaweza kupata na *second track,* treni zikapishana kama magari kuliko ilivyo sasa ambapo mnaweza kugandishwa kwenye stesheni moja hata masaa matatu mnangojea treni nyingine ifike ama ni ya mizigo au ya abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, reli hii imechakaa na reli tulinayo mbali ya matengenezo ya kuondoa taruma moja hapa na pale, ni reli ambayo tumeipata tangu wakati wa Mkoloni.

**MBUNGE FULANI:** Kabla!

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Nakumbushwa hapa, naambiwa ni kabla. Lakini kabla sijui alijenga nani kama sio Mkoloni.

**MBUNGE FULANI:** Mjerumani.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mjerumani alikuwa Mkoloni vile vile au mnafikiri Mkoloni ni Mwingereza tu?

Mheshimiwa Spika, huduma za reli ni duni na nauli zinapanda kila siku. Watu kwenye reli hii hawapati kile kinachosemwa *they don't enjoy their money worth*, wanalipishwa nauli kubwa, haduma zile za *catering* mle ndani ni hafifu. Hii ndio hali tunayokwenda nayo sisi watu tunaotoka Kanda ya Magharibi na watu tunaotumia Shirika la Reli kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, leo nilipokwenda kwenye chai asubuhi, sitaki kumtaja Mheshimiwa Mbunge huyo kwa jina, lakini ananiambia mbona mnaanza kulinganisha Kaskazini, Magharibi na Kusini? Hii inanikumbusha kauli niliyoitoa humu Bungeni mwaka 1992, sitaki kuirudia kauli ile. Niliambiwa kwamba nataka kuigawa nchi kwa sababu wale niliokuwa nawaonyeshea kidole, kwao tayari mambo yamewanyookea. Sasa sisi ambao mambo hayajatunyookea, tukisema jambo, tunaambiwa tunataka kuigawa nchi, hapana. Nchi hii ni yetu wote na sisi sote tu-*enjoy* matunda yanayotokana na uhuru wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la barabara na kwa bahati mbaya wewe mwenyewe huna kauli ya kuzungumza hapa, tutakuzungumzia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wabunge wenzangu waliokwishazungumzia barabara ya Kigoma – Itigi. Nawakumbuka wawili kwa haraka haraka, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, wamezungumza vizuri. Naeleza kwa masikitiko, pengine ndio *style* ambayo Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu amekuja nayo. Alitualika Wabunge wa kutoka Mkoa wa Kigoma Ofisini kwake na tukaona tumezungumza mambo mazito sana pale Ofisini, lakini kwenye hotuba yale mambo tuliyoyazungumza hayamo. Sasa pengine ile ilikuwa danganya toto. Alituambia, baada ya kuongea na ninyi hapa, nina safari ya kwenda Marekani, nitakuja na mambo mazito. Pengine bado ameyafungia ni siri yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigoma – Tabora – Itigi ina umuhimu kwa nchi hii kama ilivyo barabara ya Dar es Salaam – Arusha. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mwelewe iko Mikoa ndio inayotengeneza Wamachinga katika nchi. Tunao Wamachinga wa kutoka Bukoba kwa sasa hivi, labda pengine baadaye litaondoka, Mwanza, Kigoma, Mbinga kwa Capt. John Komba kwa sababu hawa wakishaondoka wakifika Dar es Salaam ndio wanatembea na maduka mabegani.

Lakini kule ambako barabara zimenyooka, zinafanya kazi vizuri, hawa watu wamebadilisha *style* ya umachinga. Anatoka na nyanya Mbeya anazipeleka Dar es

Salaam, ananunua bidhaa anamwachia bidhaa mdogo wake anauza Mbeya, anapeleka nyingine. Lakini anayetoka Kigoma, bado ile hali ya umanamba ipo. Akishafika Dar es Salaam ametua, anaendelea kuwa Machinga wa kudumu anayetoka Tabora hali kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unawaeleza nini Wabunge? Unaueleza nini Umma wa Watanzania? Zinatengwa fedha Tarakea – Rombo na tunapewa *warning* tusizungumzie Tarakea – Rombo, tunataka kuigawa nchi, kwa nini? Inanikumbusha kauli aliyowahi kuitoa aliyekuwa Rais wa Zaire, alisema, ukifanya kazi hotelini, utakula hotelini. Sasa pengine Waziri wa Miundombinu kwa sababu yuko hotelini ndio maana anapeleka Tarakea – Rombo. Tunatakiwa tuelewe na narudia, nchi hii ni yetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara ya Ilagala – Kalya kwenye Jimbo langu. Mbunge mmoja jana alikuwa anachangia akaeleza kwamba yaliyoko kwenye makisio haya ni ahadi zilizotolewa na Serikali iliyopita, nashukuru. Ni vizuri tuheshimu ahadi za nyuma. Katika kuheshimu, tunaheshimu na utendaji na mchango wa Viongozi waliopita kwenye Serikali ile.

Kama hivyo ndiyo, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu wakati huo, mimi Wapigakura wangu wamenipumzisha nikiwa *DC* Handeni, nimesikiliza, amekwenda tena kwa bahati nzuri ndio Tarafa ninayotoka pale Ilagala ndio Makao Makuu ya Tarafa ya kwetu. Kaenda kuzindua kivuko na namshukuru sana Mheshimiwa Magufuli kwa kazi nzuri aliyotufanyia kule, lakini kazi nzuri hiyo ikiwa imeanzishwa na Mheshimiwa Nalaila Kiula alipokuwa Waziri wa Ujenzi. Mbunge mmoja amesema wanayo pantoni ya kukanyaga kwa kamba, ndio tuliyokuwanayo wakati huo, lakini Mheshimiwa Magufuli kajitahidi tumeletewa pantoni yenye *engine* japokuwa inaweza kufanya kazi siku tatu kwa miezi minne. Ndio hali halisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu alipokwenda kuzindua kivuko kile alitoa ahadi akaeleza nataka nije nimtangaze Mgombea atakeyeteuliwa na Chama cha Mapinduzi, mwisho wa barabara hii na mwisho wa eneo lile katika Jimbo langu ni sehemu inayoitwa Kalya. Ni sehemu ambayo wananchi wanayo ardhi ambayo haijaguswa kwa lugha rahisi na Kiswahili safi na wala sio tusi, ni ardhi bikira. Tangu Adamu na Hawa ardhi hiyo haijaguswa. Lakini ardhi hiyo haiwezi kuendelezwa kwa sababu hakuna barabara. Nashukuru uko mchango kidogo umetolewa na *TANROADS*.

Nimemsikiliza sana Mheshimiwa Ngwilizi alipokuwa anazungumza utaratibu wa kwao wa kutengeneza barabara na sisi tunao ule na kule kwetu, ulikuja ukatiwa chachu na Mheshimiwa Ukiwaona Ditopile Mzururi alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. Tumeweza kutengeneza barabara kutoka pale Ilagala mpaka Sunuka ninapotoka mimi. Mheshimiwa Komba ameeleza kwa masikitiko!

Pale kwetu ninapotoka kabla ya mwaka 1995 ilikuwa ukitamka neno gari wanakuuliza: Je, hilo ndio jina la pili la Mheshimiwa Obasanjo, Rais wa Nigeria? Maana walikuwa hawajawahi kuona gari na gari ya kwanza kufika pale ni ya Msambya akiwa Mbunge. Sasa tunapoyazungumza haya, watu wanasema mnataka kuigawa nchi, hapana.

Nchi hii ni yetu wote. Hii keki ya Taifa lazima ifike kila mahali, sio wengine wasikie harufu na wengine wale nyama, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao usafiri wa meli Ziwa Tanganyika. Ni usafiri duni. Tunatakiwa tupate matishari, yajengwe magati ili wasafiri wakipanda na kushuka kwenye meli wawe katika hali ya usalama. Nimekuwa natazama kwenye *gallery,* nimemwona Afisa mmoja, ni Kiongozi wa Idara ya Hali ya Hewa, Mheshimiwa Mohammed Mhita. Afisa wake alikwenda kwenye Jimbo langu kukusanya takwimu za hali ya hewa kutoka ndani ya meli pale Kalya ili aingie ndani ya boti limpeleke ufukweni, ametumbukia ndani ya maji na *briefcase* yake. Bahati nzuri vijana wazamiaji wakatumbukia ndani ya maji wakamwokoa, wakamweka ndani ya mtumbwi. Iliwapata kazi wananchi kumshawishi meli ilipokuwa inatoka Zambia kumwingiza ndani ya boti ili akapande meli aje Kigoma, apande ndege arudi Dar es Salaam. Hakuna usafiri mwingine, ni meli. Hii ndio hali tunayoishi nayo kule. Sasa tungeomba ama matishari yawekwe au magati ya uhakika yajengwe, sio Tarakea – Rombo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie habari ya simu za mkononi. Tunaomba kuwe na mtawanyo wa simu hizi kwa nchi nzima. Wizara iwashawishi wawekezaji wapeleke simu hizi kila sehemu ili wananchi waweze kuwasiliana na wenzao sehemu zote katika nchi na nje ya nchi na katika mawasiliano haya yatasaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanguka Ubunge mwaka 2000, Meneja wa *TTCL* pale Kigoma, aliniambia, baada ya miezi sita Kalya na kwenye Jimbo langu lote watapeleka simu za *TTCL wireless* sijui kama ndio zinaanzishwa sasa hivi! Inaonekana nilipoanguka uchaguzi na simu zile nikaanguka nazo. Sasa tunaomba watu wa *TTCL* Makampuni haya ya simu za mkononi yaangalie na upande ule ili watu waweze kwenda na dunia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii ambayo imeniwezesha kutoa mchango wangu. Namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake waangalie wanapoandaa Bajeti za Wizara yao wajue. Nchi hii ni yetu wote, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi umetimia. Kuna matangazo mafupi tu.

Kwanza, kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mbinga, huko huko kwenye matatizo mengi, lakini wakulima wa Mbinga wameleta kahawa katika eneo letu lile kuelekea kwenye uwanja tunapokutana kwa ajili ya burudani na kadhalika. Wapo vijana kutoka Mbinga, wageni wa Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki na Mheshimiwa Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi. Hawa wana *sample* ya kahawa ya Mbinga. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kwanza mfike pale, kuionja ni bure. Lakini ukitaka kununua kopo moja ni Sh.1,000/=. Ni kahawa nzuri, inasifika na wakipata soko tutakuwa tunawaimarisha wakulima wa Mbinga. *(Makofi)*

Tangazo la pili ni kwamba, jioni ni uamuzi wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Kama kawaida yetu, Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa tuwepo kwa sababu hoja ya kupitisha Makadirio ni hoja ambayo imetambuliwa hata Kikatiba. Kwa hiyo, wote tuliopo hapa Dodoma tunaombwa kuhudhuria ili tusaidiane kupitisha hoja hii.

Kama nilivyosema, ataongea Mheshimiwa John Cheyo saa 11.00 halafu Mheshimiwa Ngombale Mwiru - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii, ataongea saa 11.15 na baada ya hapo, saa 11.30 nitamwita Naibu Waziri wa kwanza. Sina maana ya kuwapangia vyeo kwa maana ya kusema, halafu Naibu Waziri wa pili atafuatia na baada ya hapo Mtoa Hoja kwa musa wa nusu saa. Halafu saa 12.30 tutaingia katika Kamati ya Matumizi.

Nakumbusha, Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi (CCM), mnaombwa kukutana mara baada ya kumaliza shughuli za hapa, katika Ukumbi wa zamani kwa Kikao kifupi. Ni muhimu sana.

Baada ya matangazo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni. *(Makofi)*

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tulipokuwa tunamalizia hadi nasitisha Kikao kwa leo asubuhi, nilighafilika na nikatoa orodha ya wachangiaji inayomhusisha Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru ambaye yeye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais. Baada ya kutafakari na kuziangalia upya kanuni, hilo lisingewezekana kwa sababu yeye hatazamiwi amhoji Waziri Mwenzie.

Kwa hiyo, hata mchango wake nadhani atajaribu pengine kusaidia kujibu. Kwa maana hiyo, namchanganya kwenye ile ile saa moja na kwa hiyo, kwa mpangilio wa saa 12:30 kwa Manaibu Waziri halafu tutamfikia yeye kama mchangiajiwa tatu ili Mheshimiwa Waziri aweze kumalizia kwa nusu saa. Ahsante sana.

**MHE: JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, natoa shukrani kwa kupata nafasi hii na zaidi ni kwamba ni mchangiaji wa karibu na mwisho wa mjadala huu muhimu wa Miundombinu.

La pili, nataka kuungana na wananchi wote waliompongeza Rais Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM na sisi katika *UDP,* nami nikiwa Mwenyekiti wa *UDP,* namkaribisha sana ili tuchangie mawazo pamoja katika ushirika wetu wa *Tanzania Centre for Democracy* ili kuhakikisha kwamba nchi hii inadumisha amani na tunakuwa tunaweza kupingana bila kupigana. *(Makofi)*

Pia, nawapongeza wote waliochaguliwa kwenye utendaji wa CCM pamoja na rafiki yangu Bwana Yusuf Makamba. Lakini hapa kabla sijaanza kuchangia hoja niliyonayo, nataka kurejea tu jibu la Mwanasheria Mkuu ambalo alilitoa kwa wasiwasi wangu niliokuwanao wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alimalizia ufafanuzi wake kwa kusema na ninanukuu: "Mwisho nimalizie kwa kueleza kwamba, Rais anapomteua Mkuu wa Mkoa kuwa Mbunge, uteuzi huo ni wa kisiasa, hivyo, haukiuki masharti ya Ibara ya 67(2)(g) ya Katiba ya Nchi kwani Ukuu wa Mkoa ni Ofisi ya Kisiasa na siyo utumishi wa Serikali." Akaishia na: "Ahsante sana."

Sasa juzi baada ya kusikia hilo, nilifanya utafiti kidogo na hapa nimemletea Mwanasheria Mkuu *Judgement* ya Mheshimiwa Mrema, Jaji wa Mahakama Kuu aliyoitoa mwaka 1998 na pia ningemshauri ajielekeze katika *page 43* ambayo inasema wazi kabisa, ninukuu kwa haraka: "*As already observed about Public Officers extend to and include every person holding Public Office invested with the performing duties of a Public nature and is immaterial whether or not they are under the immediate control of the President that it is settled that other sees and this is a note exclude from the list of Public Officers.*" Mwisho wa kunukuu.

Pia alimalizia kwa kumwondoa Mheshimiwa wakati ule Mheshimiwa Dr. William Shija kuwa Mbunge baada ya kusema maneno yafuatayo: "*In the upshot am satisfied from both direct and resistable circumstantial evidence that the first respondent Dr. William Shija did not qualified to contest for the post of Member of Parliament for Sengerema Constituency because he did not sees to be in the service of the Government of the United Republic of Tanzania contrary to section number 36 of the Election Act. Act number one of 1995 as amended and read together with Article 67(2)(g) also Article 67(2)(f), 68(8), (72(a), (b) ) and the Constituency of the United Republic of Tanzania.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, maneno haya yanadhihirisha kwamba *RCs* na *DCs* ni Watumishi wa Umma. Sasa kwa kuwa hili jambo halijaweza kutenguliwa na Mahakama ya Rufaa, ningependa basi Mwanasheria Mkuu alieleze Bunge hili usahihi wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa ushahidi kitabu hiki, nitakabidhi kwenye Meza yako ili Mheshimiwa Waziri achukue kama *reference*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka kujielekeza sasa kwenye hoja tuliyonayo. Baada ya kuwasikia Waheshimiwa Wabunge wengine kabisa wakilalamika na karibu kulia, mimi nilishangaa. Sijui nianzie wapi katika hotuba hii! Ninashukuru kwamba umenipa angalau nianze kuzungumza mchana huu, nimetafakari na nimeona nianzie katika ubora wa maamuzi ya Serikali, mimi naona hilo ndiyo tatizo.

Ukiangalia ubora wa maamuzi ya Serikali zaidi kibajeti, unashangaa. Kwa mfano utaona tumejikita sana katika kutoa fedha ya matumizi ya kawaida na kweli matumizi ya

kawaida ya Serikali yameongezeka, ukiangalia matumizi ya Serikali yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 1.5 mpaka Shilingi bilioni 2.3. Siyo hivyo tu, ukiangalia mtazamo wetu juu ya fedha za maendeleo, unaona kwamba Serikali haiipi fedha upande huu ambao ndiyo tunaokutana nao kwa mambo kama ya barabara.

Nichukuemfano, jambo ambalo tunazungumizia sasa, Waziri ametuambia atatumia Shilingi bilioni 280 kwa ajili ya maendeleo kwa Wizara yake kwa ujumla, lakini ni Shilingi bilioni 90 tu ndiyo zinakwenda kwenye barabara na hizo Shilingi bilioni 90 ni Shilingi bilioni 53 tunategemea jinsi mafuta yanavyonunuliwa na Shilingi bilioni 33 tunagemea wafadhili na ni Shilingi milioni 870 tu ndiyo zinazotoka kwenye kodi. Hii ni wazi kabisa kwamba, Serikali haijatoa kipaumbele kwa barabara na tutalia wote, tutalaumiana hapa, lakini ukweli ni kwamba hii inaonyesha kuna udhaifu juu ya uamuzi wa Bajeti zaidi kwa upande wa maendeleo.

Pia, naweza kutoa ushahidi mwingine. Ukiangalia vitabu vyote vya Mkaguzi wa Serikali, utaona upande wa maendeleo ni kama asilimia 68 tu, ndiyo ambayo inatumika pamoja na hiyo Bajeti inayowekwa hapo. Lakini siyo hivyo tu, ukiangalia hizi fedha ambazo ni Shilingi milioni 53 za *TANROAD* unaona kwamba hela zote hizi Shilingi bilioni 34 zinakwenda kwenye *maintenance* na nyingine zinaishia kwenye mambo ya *administration*, *performance*, *evaluation* na kadhalika, hazijengi barabara mpya kwa misingi hiyo utapata wapi barabara?

Kama tunaendelea kwa namna hiyo, tutakuja hapa tunalia. Mimi nimeangalia hili eneo, nimesikiliza hapa na huwezi ukachoka kusikiliza, nilikuwa namsikiliza rafiki yangu wa Mbinga kule, kweli na mimi nilitaka kutoa machozi. Hakuna barabara na siyo kilio chake tu! Hivyo hivyo na sisi watu wa Bariadi tunalia, hatuna barabara! Sisi tulifikiri kuwa angalau kila Kata inaweza ikawa na barabara ya kuiunganisha kwenda kwenye Wilaya. Gambosi hakuna barabara, Mahembe hakuna barabara, Mkoma hakuna barabara. Naweza nikaendelea kila mahali. Bariadi ina watu 605,000, yaani 6,003 kwa sensa ya mwaka 2002. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kwamba hata sisi, nikianza kuwaambia yanayotutokea kule kwa kukosa barabara, sisi wote tutalia.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza juu ya kupeleka Shule. Shule bila barabara ni bure. Mwalimu akiugua atafanya nini? Tunazungumzia juu ya Zahanati, tunazungumzia juu ya akina mama kutibiwa, barabara hakuna, Serikali haijaweka ubora, haijatuonyesha umahimi au ubora wa maamuzi juu ya jambo hili la barabara. Naweza nikaonyesha sehemu nyingine juu ya ubora wa maamuzi ya Serikali. Angalia juzi hapa tu kila mmoja amelalamika juu ya nyumba za Serikali kuuzwa. Mtu anauza nyumba 8,000 kwa Shilingi bilioni 60 kwa kukopesha, *average price* ya milioni 18. Hata kiwanja Dar es Salaam ni karibu Shilingi milioni 200 katika sehemu ambazo nyumba nyingi zimeuzwa na wala hazikuuzwa kwa watumishi tu, nyingine zimeuzwa kwa watu ambao sio Watumishi wa Serikali. Ubora wa maamuzi yetu ni mbovu.

Siyo hivyo tu. Sasa hivi nawasikia Wabunge na kweli nawasifu jinsi mnavyotoa *debating* safi kabisa. Mimi naona Bunge hili kwa pande zote mbili na zaidi mlio wengi mnatoa maneno sawasawa kabisa ya kuweza kusimamia Bunge hili, lakini mwisho wa

kilio chote hiki mnasema mnaunga mkono hoja. Sasa hii pia inanipa wasiwasi kuhusiana na ubora hata wa maamuzi yetu Bungeni. Tutakaa hapa tutaamua, lakini kiasi gani Bunge hili linaweka *stamp* tu baada ya kulalamika au kweli Bunge hili lina uwezo wa kusema kwamba hatupendi, leo mmemlalamikia Mheshimiwa Basil Mramba sana, kila mmoja amelalamika, lakini ukweli mimi nauliza; hivi Mheshimiwa Basil Mramba aliamua peke yake? Mimi nazungumza juu ya Shilingi bilioni 17, *actually* katika miaka mitatu ni Shilingi bilioni 33. Je, ameamua peke yake au ameamua katika Baraza la Mawaziri? *(Makofi)*

Sasa mimi nawapa changamoto tu. Walio wengi mnapoona kuna jambo ambalo hamlipendi, *say no*! Mseme hivyo! Mimi nasema, katika Mabunge mengine *the say resign!* Mwambie Waziri Mkuu ajiuzuru kwamba yeye ameweza kusimamia Kikao ambacho kimetoa maamuzi kama hayo.

Kwa hiyo, mimi nasema kwamba maamuzi yetu, ubora wetu, lazima tuangalie. Mimi ningependa kushauri Bunge hili, labda tuangalie upya namna tunavyofanya Bajeti yetu, *may be* njia ya kufanya Bajeti ni kuhakikisha kwamba vipaumbele hivi viletwe kwenye Bunge hili Januari tuzungumzie vipaumbele kwanza. Tukizungumzia vipaumbele, basi tunawaambia mkatengeneze Bajeti. Lakini hii kuletewa Bajeti imetengenezwa halafu tunakuja huku tunafanya vilio, haileti hadhi ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho mimi nataka kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa niaba ya watu wa Bariadi kwa kuhakikisha kwamba Rais ametuahidi kujenga daraja la Simiu. Daraja hili watu wanaweza kusema siyo daraja tu. Daraja hili likijengwa ndio kusema tutakuwa tumefungua njia mpya kabisa ya kuweza kuhakikisha kwamba mtu anaweza kutoka Singida akipita Meatu, Bariadi badala ya kuzunguka njia yote ile akaenda moja kwa moja mpaka Mwanza. Kwa hiyo, daraja hili ni la maana sana na nashukuru kwamba kuna Shilingi milioni 100 ambayo iko tayari, basi liongezewe hapo.

Lakini daraja peke yake haitoshi. Tukijenga daraja lile bila kujenga kutoka kwenye mto mpaka Lagangabilili, hatuwezi tukafika mahali popote. Mimi naona, kutoka kwenye daraja pale na barabara kutoka Meatu mpaka kwenye daraja mpaka Lagangabilili na kwenda Rugulu, liwe daraja ambalo ni la Mkoa. Siyo hivyo tu, kwa upande wa Bariadi, Mji wenyewe hauna barabara kwa kuwa sasa ni Mji mdogo. Tungependa tunapoweka makadirio angalau Shilingi milioni 70 iwekwe kwa ajili ya Mji tu pekee wa Bariadi, lakini tunahitaji njia kutoka Bumera kwenda Njolelezi kwenda Longalombogo, kutoka Lagangabilili kwenda Migato.

Mheshimiwa Spika, sehemu zote hizi ni sehemu za uchumi. Tunashukuru sana watu wa Bariadi, bila *Father Paul* wa *Merino Fathers,* Bariadi tungekuwa labda na barabara moja tu ya katikati ya kujivunia basi. Tunamshukuru sana, amejenga barabara kutoka *Old Maswa* Mpaka *Nkololo* na ningemshauri Waziri atembelee huko aone jinsi mtu mmoja na Shirika dogo linavyoweza kufanya kazi kubwa zaidi kuliko Serikali.

La mwisho, ninashauri kwamba kama tulivyoonyesha mfano wa kushirikiana kwa pamoja kujenga Shule wakati wa mradi wa *MMEM,* mimi naona Serikali sasa itupie

macho yake kwa barabara za Vijijini. Maana ya maendeleo ni barabara. Bila ya barabara hakuna maendeleo na bila barabara hakuna MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii, mimi sijaridhika. Kwa hiyo, siungi mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge naona baadhi ya wageni wetu waliokaa kwenye *Gallery* ya mkono wangu wa kulia wamekosa viti na wamekaa chini tu kwenye ngazi. Ningependa kuwafahamisha Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge msaidie wasikae hivi kwa unyonge, kuna nafasi upande wa pili mnaweza kuwasaidia kwa sasa hivi ili waweze kukaa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nilipata ombi la muda mrefu la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi. Kwa hiyo, atakuwa ndiye mchangiaji wa mwisho kwa jioni hii.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:-** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ambayo ninaichukulia kama ni zawadi kubwa kutoka kwako. Bila kupoteza muda, nitoe niliyotaka kusema kutoka rohoni mwangu ambayo Wabunge wengi kwa kweli tumekuwa tukiilalamikia hotuba hii ya Waziri wetu, ambaye kwa kweli tumemuweka wenyewe Ndugu yetu Basil Mramba. Kwa kweli tunaposema haya, nia yetu ni kutaka atuelewe kwamba Wabunge tunawakilisha wananchi wanaotutuma. Tunayoyasema ni yale ambayo wananchi wanayasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili nisipoteze muda, niseme kuhusu eneo ambalo watu wengi najua watategemea nitalizungumzia la Miundombinu katika maeneo ambayo tumezungumzia kwamba tuelekeze maeneo ambayo yataongeza uchumi wa Taifa letu yatakayoweza kuzalisha zaidi, tupate fedha ili tuwekeze kwenye barabara nyingine na kwenye maeneo mengine ya maendeleo.

Nataka nitumie muda kidogo kuzungumzia habari za miundombinu katika Wilaya ya Ludewa na hususan katika maeneo tunayotaka wenyewe ku-*develop* katika kuchimba madini kwa ajili ya Mkaa wa Mchuchuma na Liganga kule Ludewa. Nataka nianze kwa kusema kwamba ilani inazungumzia kwamba madini haya yataanza kuchimbwa, lakini vilevile nataka niseme na nilisema wakati nikichangia kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango kwamba Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha ambaye ni Waziri wa Nishati na Madini alisema kule Ludewa kwamba madini yale yataanza kuchimbwa sasa.

Lakini vilevile Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa alipokuwa anajibu, alisema kwamba, kwa kweli wana nia hiyo ya kuchimba yale madini ila tu katika kipindi cha mwaka huu hawakuweka fedha. Lakini vilevile niseme kwamba Wilaya ya Ludewa ikiwa ni sehemu ya Iringa, ni sehemu iliyo pembezoni, lakini sijui kwa nini Mkoa wa Iringa unachukuliwa kwamba, nadhani uko *central,* lakini uko pembezoni. Wilaya ya Ludewa na Wilaya za Makete kwa mfano ziko pembezoni na zilitakiwa zipewe huduma kama Wilaya na Mikoa ambayo iko pembezoni. Kwa nini Wilaya kama Ludewa ambayo haina

*infrastructure,* haina miundombinu, kwa nini haipewi kipaumbele kama Mikoa mingine na Wilaya nyingine ambazo ziko pembezoni?

Kwa hiyo, utaniuliza: Je, Wilaya ya Ludewa inastahili kupewa kipaumbele katika mambo ya Miundombinu? Ndiyo! Kwa sababu hizo nilizozitaja. Lakini vilevile ina raslimali kubwa hapa nchini kote, hata nadhani tungepiga kura, tungekubali kwamba madini yale au chuma kile na makaa yale ni raslimali ya nchi hii na wote tungependa kuona kwamba yanasaidia Taifa na sio watu wa Ludewa tu. Kwa hiyo, ninapopiga kelele, sio kwa faida ya watu wa Ludewa tu, ni kwa faida ya Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spiia, nilichotaka mimi kujua ambacho nilitegemea kwenye suala la miundombinu, angalau basi wangetupa ratiba kwamba kwa vile tunataka sasa kuanza kuchimba madini yale, ratiba yetu ya kujenga miundombinu ambayo haipo katika miaka hii mitano, kipindi hiki hatukuweka hela, pengine hata mwaka kesho tutaweka hela kadhaa kwa ajili ya shughuli hii, mwaka unaofuata fedha kadhaa kwa shughuli ile na pengine ifikapo kabla ya mwaka 2010 pengine tutakuwa tumeshaanza kuchimba madini kwa sababu *infrastructure* itakuwa imewekwa *in place*.

Lakini kama ilivyokuwa kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango, halizungumzwi, suala la miundombinu katika Wilaya ile ambayo tunategemea kwenda kuchimba madini na tunasema tutaanza sasa. Halizungumzwi! Hii inanipa wasiwasi sana. Hata kama tukitoa ahadi kwenye ilani, Rais akienda akitoa ahadi, wananchi wale hawawezi kuamini hata siku moja! Kama walivyosema Wabunge wenzangu, watadhania hii ni danganya toto. Kwamba leo tukikubaliana hapa, mradi Bajeti imepita, basi hatutaangalia mbele. Mwaka kesho tutatafuta namna nyingine ya kuzungumza ili Wabunge hao wakubali na wananchi wale wadanganyike kama tunavyowadanganya sasa.

Kwa hiyo, Ludewa tunalima mazao kama Kahawa, lakini hata kwenye ule utaratibu, naambiwa kuna kitu kinaitwa *STABECS.* Ukisoma ukurasa wa 47 kuna ule Mradi wa *STABECS.* Nimesema Wilaya ya Ludewa iko pembezoni, lakini vilevile Wilaya ya Ludewa inalima Kahawa. Waziri wa Kilimo sijui kama yuko hapa, anajua hivyo! Mwaka huu tumeingizwa kwenye utaratibu wa kilimo cha Kahawa hii mpya ambayo tunasema kwamba inavumilia magonjwa, inazaa zaidi na inazaa haraka. Hivyo basi, Ludewa imeingizwa kwenye mpango huo, kwa hiyo tunalima Kahawa. Lakini ukiangalia Mikoa inayolima Kahawa, Iringa inalima Kahawa Wilaya ya Ludewa, *in particular* inalima Kahawa, lakini haimo humu. Kwa nini sisi tunaachwa nje wakati kuna fedha za Wahisani ambazo zimetengwa kwa ajili ya kusaidia barabara kwenye maeneo ambayo tunalima Kahawa? Kwa nini sisi hatumo?

Mheshimiwa Spika, nilitaka Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha, aniambie na hilo. Kwa nini Wilaya ya Ludewa au Mkoa wa Iringa umetolewa katika utaratibu? Pengine tungepata vibarabara, kidogo na sisi tukaona angalau tuko Tanzania kama alivyosema Ndugu yangu Mheshimiwa Capt. John Komba kwamba tunaonekana ni watu wa Malawi sisi. Lakini sisi tunajivunia Utanzania, ni Watanzania sisi! Sisi sio watu wa Malawi hata siku moja! Lakini Serikali yetu ionekane inatujali kwamba hawa ni wenzetu, ni wananchi wa Tanzania na wapewe haki kama maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nilizungumzie ambalo na mwenzangu alilisema, lakini sio vibaya kuongeza uzito au kuongezea uzito, Mwenzangu Capt. John Komba alizungumzia habari ya Meli zile kwa kweli ni boti zile, siyo meli! Ni boti tu mbili, moja imekufa na nyingine ilizama mwaka 1977, hatuambiwi kama hii boti itakuwa *replaced,* hakuna mawazo yoyote ya ku-*replace* ile meli. Imekwisha moja, moja, imebaki kama moja ndiyo hiyo inafika katikati ya Ziwa Nyasa *engine* zinazima na gharika ipo. Ndiyo maana mwenzangu na ninakubaliana naye Waheshimiwa ninyi na pengine na Mheshimiwa Waziri Mkuu wangu mimi namheshimu sana, aende na yeye akatembee kule pengine na akaingie kwenye maji upate uchungu wanaoupata wananchi wa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwomba Waziri Mkuu aende na amesema atakwenda na ninadhani Mheshimiwa Waziri Basil Mramba naye atakwenda pengine kabla ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hajakwenda tukaangalie hali ilivyo. Wananchi wale tutakuja kuzika baadhi! Lakini mwenzangu alisema watu kule wanazikwa mara mbili. Hatutaki kuzika watu mara mbili, tunazika watu mara moja. Tuwasaidie wananchi wale wapate usafiri ili tuondokane na uwezekano wa kupata ajali za ajabu sana na za kujitakia kwa sababu tunatoa tahadhari, lakini isiwe vitu vinaingilia sikio hili vinatokea huku.

Mheshimiwa Spika, lingine nililotaka kuongezea, kwa sababu nilipata muda, nilitaka kuzungumzia habari ya hii minara ya simu. Minara ya simu kwa sisi wengine watu wa mazingira, inaleta kero sana. Kila utakapopita ni minara mitupu, sisi tunasema inaathiri sana mazingira. Mtu wa mazingira ukiangalia unakerwa! Kila mwekezaji, iwe *Celtel, Mobitel* na kadhalika kila mtu anaweka minara, sehemu nyingine minara mitatu hadi minne sehemu hiyo hiyo kwenye kamlima kamoja, kwa nini? Kwa nini watu hawa wasipewe utaratibu mnara mmoja washirikiane kujenga mnara mmoja wote waweke mitambo yao kwenye mnara mmoja? Hiyo kwanza inawasaidia kupunguza gharama, wata-*serve* sana, lakini inatupunguzia athari kwenye mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, nilidhani kwa vile Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulika na Mazingira yupo hapa, nadhani anakubaliana na mimi kwamba hakuna sababu ya watu hawa kila mmoja kuweka minara yake kwa sababu hata hii njia ya umeme ni basi tu, sisi tuko nyuma sana, lakini zilitakiwa zipite *under ground* kupunguza kile tunachokiona machoni, athari zile tuone vitu vizuri tu, nguzo zile siyovitu vizuri, vinaathiri mazingira. Kwa hiyo, nilidhani na hilo pengine tungeliangalia.

Mwisho, labda nipate fursa vilevile ya kusema kwamba kwa sababu tunazungumzia mambo haya ya Miundombinu na Uchukuzi, najua tulikubaliana kule nyuma, Naibu Waziri wa Fedha alinieleza kwamba utakapokuwa unakwenda *Celtel* wanapeleka mitambo yao kule Mbinga Songea watachepusha pale Madaba ili huduma za *celtel* vilevile ziende Ludewa. Nategemea kwamba hiyo nia bado ipo na bila shaka Waheshimiwa hawa wa *Celtel,* taarifa wanayo na bila shaka watakapokuwa wanapeleka *Celtel* kule Mbinga, Songea na Ludewa. Kadhalika tutaweza kupata huduma hiyo. Mimi ni Profesa, najua *time* maana yake nini? Ni kwamba unapofundisha *time* ikifika, unaacha. Sitaki kupigiwa kengele.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupewa fursa ya kuzungumza kidogo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri wa Wizara hii kwa hotuba ya Bajeti yenye kuleta mafanikio kwa Watanzania. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ninayo maoni yafuatayo: Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida. Ujenzi wa barabara ya lami toka Dodoma hadi Manyoni kilometa 127 na sasa imefikia eneo la Boha kilometa 56, lipo nyuma kwa takribani mwaka mmoja.

Inaelekea katika hili eneo kuna mzozo baina ya mkandarasi na wasimamizi wa ujenzi (*TANROADS*). Mizozo hii inasemekana inadhoofisha ujenzi. Wizara ina mpango gani kuondoa sababu zinazochelewesha kukamilika kwa mradi huu? Wananchi wana hamu ya kuona mradi huu unakamilika mapema iwezekanavyo. Wizara inaombwa kutoa msimamo ili kuleta kasi katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Manyoni yenye urefu wa kilometa 119 unaofanywa na Kampuni ya *SEATCO* upo katika hatua inayotia mashaka kabisa. Mkandarasi huyo japo alipewa atengeneze barabara ya urefu wote kilomita 119, hivi sasa amesema ana mpango kazi *(action plan)* na fedha za kutengeneza kilomita 1.5 tu, yaani Singida hadi Itigi. Je, hizo kilomita 50 zilizobaki nani atatengeneza? Kama ataendelea kutekeleza, kutekeleza mkandarasi huyu huyu atasaidiwaje ili atekeleze kazi hii kwa kasi mpya?

Barabara hii ya Rungwe – Itigi – Mkiwa ni sehemu ya barabara kutoka Mbeya Mjini, kupitia Chunya hadi Makongolosi. Kwa upande wa Mkoa wa Mbeya, barabara hii imefanyiwa upembuzi yakinifu na ujenzi kwa kiwango cha lami umeiva. Barabara hiyo kwa upande wa Wilaya ya Manyoni, yaani kutoka Rungwe – Itigi – hadi Mkiwa bado haijafanyiwa upembuzi yakinifu. Je, upembuzi yakinifu umepangwa kuanza kufanyika lini? Ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza?

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru jitihada za Wizara hii kwa kuboresha mawasiliano ya simu katika Makao Makuu ya Wilaya ya Manyoni Mjini, lakini mtandao huu haujafika Vijijini ambako tayari wananchi wanazitumia ila wanakosa *network* hadi waende Manyoni Mjini, ndiyo wanapiga simu zao. Tunakumbusha Makampuni ya simu yaweke minara maeneo ya Sanza, Ntinho na Kintikhu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha tena leo nikiwa bado niko hai. Vile vile, niizingatie

itifaki kwa kuwapongeza wote walioteuliwa katika nafasi mbalimbali. Pia, niwape pole wale wote waliopatwa na misiba mbalimbali. Natoa pongezi kwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imebeba iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Ujenzi. Bila shaka hii ni kazi kubwa.

Suala la barabara litaguswa karibu na kila atayezungumza na kuchangia kwa maandishi. Hii ni kwa sababu ya umuhimu wake. Ile nia ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi ya kuziunganisha barabara zote Tanzania ifikapo mwaka 2008, naomba mbio za Wizara hii zielekezwe huko kama itawezekana. Kauli hii, iliwapa moyo sana wananchi na bila shaka hili limechangia kwa kiasi kikubwa CCM kushinda kwa kishindo tulioshuhudia mwaka huu.

Barabara za Mikoa ya Kusini – Lindi, Mtwara na Ruvuma, Barabara za Kanda ya Magharibi, Mikoa ya Rukwa, Kigoma, Kanda ya Kati Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Singida na kwingineko, hii ni kazi kubwa ambayo tunaomba Wizara, kila itakapotoa kauli, basi kauli iwe ya uhakika, kwani katika mambo yanayowatia moyo sana wananchi ni pamoja na suala la ujenzi wa barabara.

Jambo jingine ninalotaka kuchangia, ni suala la nyumba za Kisasa, Dodoma, *Area D*, *(flats)* na nyumba nyinginezo zinazomilikiwa na Serikali na kuzipangisha/kuzikodisha. Serikali iliangalie vizuri suala la kodi inayotoza katika nyumba hizi. Kodi ni kubwa sana kwa Mtanzania yeyote wa kipato cha kawaida, seuze cha chini! Nyumba hizi, Serikali ilikusudia waje wapangishe akina nani? Tena Dodoma!

Kama kweli wamejengewa Watanzania, basi bei iko juu mno. Tena ni aibu kwa Serikali ya CCM. Kama itawezekana, basi kodi inayotoza Serikali katika nyumba iangaliwe tena na ikibidi ipunguzwe. Haiwezekani Serikali ipandishe kodi kiasi kile wakati wakiitwa kufanya matengenezo wahusika hukimbia. Kodi ishushwe kwa vile Serikali haifanyi biashara au Serikali iweke bayana kwamba inakusudia kufanya biashara kwenye nyumba hizi.

Mwisho, napenda nichangie kwenye suala la usalama wa usafiri wa bahari. Kutokana na misiba inayoanza kutokea kwenye maziwa, bahari, zetu, Serikali ichukue hatua za makusudi kufanya ukaguzi katika vyombo vinavyosafiri majini ili kujiridhisha kwamba hawatokei watu wachache wakataka kupata faida ya haraka haraka kwa kupakia watu katika vyombo vya baharini kupita uwezo wa chombo ulioruhusiwa kisheria. Wanaofanya hivi wakigundua kuwa Serikali inalifuatilia hili, basi wataambizana na wataacha kuchukua watu kupindukia idadi walioruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri Basil Mramba na Wasaidizi wake kwa kazi nzuri ya kuandaa Bajeti hii kufuatana na Ilani ya uchaguzi ya CCM na ahadi za Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Ni kweli kwa mwaka huu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Nne, tusingetegemea maajabu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara, ni nyeti na tungependa wana Rukwa tuharakishiwe kuwa fedha za kujenga barabara kwa kiwango cha lami toka Tunduma – Sumbawanga zipo na zimetengwa. Ikiwezekana Mheshimiwa Waziri awapatie kwa ufupi ratiba ya ujenzi huo awamu kwa awamu ili wana Rukwa safari hii wajue kuwa barabara hii siyo kitendawili tena.

Mheshimiwa Spika, ningemwomba Waziri ashirikiane na *SUMATRA* ili kuhakikisha kuwa makubalinao tuliyofanya katika Kamati yetu kuwa badala ya kusambaza shilingi 150 milioni katika kukarabati gari nyingi, basi fedha hizo zitolewe kwa ajili ya gari ya kasanga. Ninaamini kuwa uamuzi huo ulitolewa ili kuimarisha biashara na nchi jirani za Kongo, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya miaka 30 tangu Mkoa wa Rukwa uanzishwe, Ofisi ya Posta imeendelea kuwa chini na ndani ya jengo dogo sana ambalo halina hadhi ya Mji ambao sasa ni Manispaa.

Mheshimiwa Spika, nashauri mpango kabambe uandaliwe ili jengo lijengwe kubwa na lifanye kazi ya kibiashara kwa kukodisha vyumba vingine kwa wafanyabiashara wengi ambao hawana mahali pa kuendeshea shughuli zao vizuri. Sumbawanga ikifunguka kwa barabara ya lami – biashara itashamiri vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, tungependa kushauri Wizara itafute utaratibu wa kuwatafutia makandarasi wadogo vifaa vya ujenzi ili waweze kuzifanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi mkubwa.

Maombi yaliyowasilishwa rasmi miaka mingi Bungeni na mimi mwenyewe kuhusu ukarabati wa Uwanja wa Ndege Sumbawanga, Uwanja huu tusipoushughulikia utakuja kutuletea madhara kwa viongozi wetu ambao mara nyingi ndio wanaotumia Uwanja huu, kutokana na umbali wa eneo la Sumbawanga toka Dar es Salaam. Nashauri eneo la *approach* na *take off* hasa wakati wa kutua (*landing*) liwekwe lami angalau mita 300.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na madhara ya malumbano na maandamano ya wafanyakazi wakati wa ukodishaji wa Shirika la Reli *(TRC)*. Tusingependa shirika hili lianze kwa matatizo yasiyo ya lazima. Tuepuke sana hali hii isitokee. Tufanye jitihada ya kuwalipa haki zao mapema.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuanza mpango wa kutandaza nyaya za mawasiliano ya simu (*optic fibre*) kupitia chini ya ardhi kati ya baadhi ya Miji Mikuu kupitia mtandao wa *TANESCO, TAZAMA* na *TRC*. Kila jitihada ifanyike ili kufanikisha azma hii kwa nia ya kuwapunguzia wananchi gharama za simu za mikononi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Mchango wangu ni kusikitika na kushangaa sana,

kwamba, Tabora ina matatizo gani katika nchi hii? Nadhani tukubali kuwa Uwanja wa Ndege ni mbovu, barabara ni mbovu treni ndio kama hivyo. Wananchi wasemeje? Kuhusu kuwajali katika suala la usafiri, matokeo yake mnasema Mkoa usio endelea! Mnategemea nini? Utaendeleaje bila hata njia ambayo Tabora kuna kampuni moja tu ya ndege inayokuja hapo na hata hizo ndege zenyewe sio nzima. Inatokea hata siku tatu ndege haijafika Tabora. Bado tujiulize: Je, wananchi wetu wanaweza kupanda ndege wote?

Barabara ya Manyoni, Itigi, Tabora, nadhani kwa barabara hiyo sio ndefu sana ila ukiritimba, uchoyo ni njia mojawapo ya kurudisha nyuma maendeleo ya Mkoa wetu. Je, haya mambo yote yanayoandaliwa kama MKUKUTA, sisi Tabora yanatufikia kweli au MKUKUTA utakuwa wa maneno ya msamiati na maneno magumu katika makatarasi! Sidhani kama tuko pamoja na haya yanayopangwa na Serikali ili kuleta maendeleo ya kila mtu na maisha bora. Ubora wa miundombinu uko wapi Tabora? Tunalima tumbaku na asilimia 5.2, imeongezeka na kodi inapanda kwenye sigara. Ina maana haya yote hamyaoni kama nao wanachangia mapato ya nchi hii?

**MHE TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Naomba niende moja kwa moja kwenye hoja kama ifuatavyo: Moja, naomba nizungumzie barabara inayotokea Tabora Mjini ambayo inajulikana kama *Old Mwanza Road* ambayo inakuja mpaka Maambali – Jimbo la Bukene, Toka Maambali inakwenda Semembele. Barabara hii ni ya tangu Wakoloni kama sikosei enzi za Wajerumani, Toka Semembele, inapitia Nhabala *Center*, Kata ya Kahama ya Nhalanga, Mwamakumbi, Nkinga, Malolo, Mwamala, Lububu, Kasela *Center*, Mwangoye *Center*, inatokea Nata *Center*, Tinde *Center*, kuendelea Shinyanga hadi Mwanza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunga Mikoa mitatu, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Pia, inapitia sehemu za wakulima sana, hivyo mengine yatasafirisha Mwanza hivyo kuwawezesha na wananchi hao kujikwamua kiuchumi na hivyo kuondokana na umaskini uliokidhiri.

Mheshimiwa Spika, magari/malori ya mizigo yanayotoka Dar es Salaam kwenda Burundi, Rwanda, huwa yakifika Nzega, mengi yao yanapita Mwangoye kama njia fupi *(short cut)* kwenda Isaka *Dry Port.* Barabara hii ni ile inayotoka Nzega Mjini, inakwenda hadi Kijiji cha Isunga – Ngwanda, ikifika hapo, inachepuka kwenda Mwangoye *centre*, inaendelea Kijiji cha Ilagaja, inavuka mto Igung'homa, Mwamasumbi – inaendelea Isaka *Dry Port* na hivyo kufika Kahama – Burundi/Rwanda barabara hii inapita Kata ya Mwangoya ambapo ndio sehemu kubwa ya walimaji wa mpunga ambao ni zao la biashara.

Kama nilivyosema pale awali, naomba barabara hii, kwa kuwa inaunganisha Mikoa miwili, pia inatoa mizigo Dar es Salaam kupeleka nchi jirani ambayo ni Burundi, naomba iangaliwe ipasavyo ili la kuvuka mto Igulung'homa lijenge na ikiwezekana iwekewe lami na hivyo isaidie wakulima wa sehemu inapopita katika kuuza na hata kusafirisha mazao yao hadi Burundi/Rwanda.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuwa anapita katika *campaign* mwaka 2005, aliahidi zile ahadi za papo kwa hapo, kwamba barabara ambayo alipita toka Tabora hadi Kahama itatengenezwa kwa kiwango cha changarawe, yaani. Tabora/Maambai, Bukene Centre, Itobo/Nzega na Itoba Mwamala/Igusule, Jimbo la Bukene wa kuendelea Kagongwa hadi Kahama.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inasikitisha! Au ahadi hii imesahaulika? Kwani siioni, naomba basi iwekwe katika ahadi za Rais wa Awamu ya Pili. Hata yeye akikumbushwa atakumbuka. Naomba barabara hii iwe katika kiwango cha lami, maana inakwenda kuungana na barabara za Rwanda/Burundi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inisaidie kupata simu ya *Celtel, Voda* na *Tigo*. Kweli ni kazi watu kwenda kuzungumza kwenye kichuguu, mpaka lini? Au wenye uwezo kwenda Nzega kwa *bus* ili kwenda kupiga simu. Naomba tuwahurumie ili wafanye biashara kwa mtandao.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara toka nzega mpaka Bukene iwe ya lami ili kuunga barabara toka Igunga/Nzega/Bukene yote iwe ya lami, ili kuwezesha stesheni ya Bukene ifanye kazi ipasavyo, yaani mizigo, mazao, ng'ombe ipakiwe na kupakua Bukene. Hivyo, ni ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Korogwe na mimi mwenyewe kuipongeza Wizara hii ya Miundombinu kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba Wizara hii imeboresha sana, ina miundombinu katika maeneo mengi nchini pote.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaipongeza hotuba na pia ninampongeza Waziri Mramba, Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Mahanga, Mheshimiwa Dr. Maua, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Watalaam wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri wanayofanya katika Wizara yao. Ninawatakia kila la kheri katika kuondoa kero sugu hasa ya barabara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ipo kero sugu ya muda mrefu ya barabara ya kutoka Korogwe Mjini, Magoma, Mashewa, Dalumi, Muramba hadi Mabonkweni – Tanga. Barabara hii haipitiki kabisa wakati wa mvua. Hivi sasa ninavyoandika hotuba yangu, barabara hiyo haipitiki.

Kwa muda mrefu Serikali ilitoa ahadi hapa Bungeni kwamba, barabara hiyo imepangwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa nia ya kuondoa umaskini na moja ya barabara zilizopangwa kwenye mpango wa kuondoa umaskini. Lakini cha kushangaza hadi leo hii hakuna dalili zozote.

Ninaomba kuelekezwa ni kwa nini barabara hiyo haijashughulikiwa hadi sasa na wala hata dalili hazipo? Je, lini sasa barabara hiyo itaanza kutengenezwa? Kwa kuwa barabara hiyo sasa ni kero; Je, Wizara haioni ni muhimu sasa hivi kuishughulikia barabara hiyo hata kwa kiwango cha changarawe? Suala hili ni nyeti sana na linahitaji ufumbuzi wa haraka.

Barabara ya kutoka *Old Korogwe*, Mnyuzi hadi Magunzoni, ndiyo barabara ya zamani ya kwenda Tanga. Hali ya barabara hiyo ni mbaya na ni nyembamba sana. Je, Wizara haioni busara barabara hiyo sasa ikaimarishwa hasa ukizingatia kwamba barabara hiyo ndio pekee inayoweza kutumika kwenda Tanga iwapo kutatokea tatizo katika barabara ya Segera – Korogwe, Hale, Tanga?

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la Halmashauri zetu kuwapatia tenda makandarasi wabovu, matokeo yake ni barabara nyingi kutengenezwa chini ya viwango. Kwa sababu fedha nyingi zinapotea bure na *impact* haipatikani: Je, Wizara ina mkakati gani wa kulikomesha tatizo hili lililokubuhu?

Mheshimiwa Spika, kutengeneza maeneo sugu badala ya kuchonga barabara kila siku, matokeo yake ni barabara nyingi za Wilaya ya Korogwe kushindwa kupitika. Mimi ninashauri sana barabara zitengenezwe kwanza kwenye maeneo korofi kuliko kila wakati kuchonga barabara yote.

Sasa Korogwe Mjini umepata hadhi ya mji *(Town Council),* lakini barabara zake ni mbovu sana, hazipitiki kabisa na hata hizo chache zinazopitika, hazina mifereji ya kupitisha matokeo yake ni barabara hizo kuharibika haraka kama vile vya kutoka *bank* ya *NMB* kwenda Magunga Hospital. Je, Serikali haioni ni busara Mji huo sasa barabara zake zikatengenezewa mifereji kabla hata kujenga barabara kwa kiwango cha lami au changarawe? Je, ni lini Wizara itasaidia ujenzi wa mifereji hiyo?

Mheshimiwa Spika, Mji wa *Old Korogwe* ni siku nyingi na Mji wa Korogwe *Vodacom* inasikika Mji wa Manundu tu. Lakini *Old Korogwe* kilomita mbili tu *Vodacom* haipatikani. Je, sababu ni nini? Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kulitatua tatizo hilo linalokera wananchi?

Katika zoezi la kuuza nyumba za Serikali, Wilaya ya Korogwe, imekuwa kubwa na tatizo kubwa la Viongozi Wakuu wa Wilaya kukosa mahali pa kuishi na matokeo yake kulazimika kupanga Mitaani jambo ambalo ni hatari kulingana na hadhi ya vyeo vyao. Viongozi hao ni *OCD*, Hakimu wa Wilaya, Afisa Usalama Wilaya, Afisa Mgambo wa Wilaya na kadhalika.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa haraka wa kuwajengea Viongozi hao nyumba mpya na kama jibu ndio utaanza lini?

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo nami kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba

ya Wizara hii ya Miundombinu. Pia, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Fuoni kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze tena Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa CCM.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa kifupi sana hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nizungumzie Usimamizi wa Bandari Tanzania. Kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake, niipongeze Serikali kwa kupata mafanikio makubwa katika kuziendeleza Bandari za Mwambao kwa kuzifanya kuwa za kisasa na ziweze kuhimili ushindani wa kibiashara Kikanda.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wakati tumekusudia kushindana, naishauri Serikali iiongezee fedha Wizara hii ili itengeneze hiyo miundombinu iliyochakaa ili matangenezo yaende sambamba na maazimio yaliyokusudiwa pamoja na ajira kwa vijana na wananchi wa sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, pia lazima tukubali kuwa wizi katika Bandari zetu upo na ni kero kwa wanaotumia Bandari hizo. Kwa hiyo, kwa kuwa suala hili ni dhahiri linafanywa na wafanyakazi wenyewe, naishauri Serikali suala hili linapotokea, basi Viongozi wa sehemu husika wawajibishwe kwa kulipa gharama ya upotevu uliotokea. Hiyo ndio dawa pekee, kuliko kuwaachia hivi hivi bila ya adhabu yoyote. Bila kufanya hivyo, Serikali itakuwa imeyakubali yanayotokea.

Mheshimwa Spika, baada ya mchango wangu huu mdogo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Ndugu John Kijazi, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, *CE* wote *(TAMESA, TANROADS, TBA)* na watumishi wote wa Wizara ya Miundombinu kwa maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, ninawatakia kazi njema na Mungu awajalie Bajeti yao ipite. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *All the best*.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa asilimia mia moja na kumpongeza yeye binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wa Watendaji wote wa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi ni kati ya Majimbo nchini ambayo miundombinu yake ni mibaya kuliko yoyote ile, japo kutokana na kuwa Mkoani Mbeya, matatizo yake hayajapewa kipaumbele hata kidogo. Namshukuru Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki ambaye kwa kuona shida tuliyonayo, jirani zake wa Mbozi Magharibi kila akisimama kutoa hoja hakosi kutaja matatizo yetu.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi limegawanyika katika sehemu mbili kijiografia. Moja, Ukanda wa Bonde la Ufa la Rukwa na pili, Ukanda wa Juu ambao ni mwendelezo wa *Plateau* ya Ufipa. Sehemu hizi mbili hazina *direct communication*.

Kutoka Kamsamba au Ivuna kwenye ufukwe wa Ziwa Rukwa lazima upitie Jimbo la Mbozi Mashariki kwa kilomita zaidi ya 120 ndiyo ufike Chitete au Msangano kwenye Bonde hilo hilo la Ufa na ili ufike Ndalambo au Kapele au Myunga au Mkutano lazima upitie Jimbo hilo hilo la Mbozi Mashariki kwa umbali wa zaidi ya kilomita 300 japo Tarafa za Kamsamba, Msangano, Ndalambo na Kata ya Myunga ni *adjacent* na kwa hakika kungekuwa na barabara sehemu hizi, Vijiji vyake umbali wake hauzidi kilomita 60 kati yao.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi kwa sehemu kubwa, kati ya Novemba na Juni wananchi wake wanatengwa na hata Makao Makuu ya Wilaya yaliyopo Vwawa na hivyo kuishi maisha ya ajabu kiasi cha kukatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, Mbozi Magharibi kuna madaraja ya kubembea, ya waya tu, hasa kwenye Bonde la Ufa kwa Vijiji vifuatavyo ambavyo ni Makao Makuu ya Kata kama ifuatavyo:-

1. Kwenye Mto Nkana ambao ni mto mkubwa unaoanzia Vwawa na *Mbozi Mission* hadi kuungana na mto Mko na Mpemba kwenye Kata ya Msangano, kuna Daraja Msangano, Ntinga na Nkala.
2. Mto Mambo ambao ni mkubwa sana kutokana na Mto Nkana, Mko, Mpemba, Halungu na Mtembwa (Nyinaluzi) kuungana na kupeleka maji yake Ziwa Rukwa. Hapa kuna madaraja ya bembea Kijiji cha Chuo na Kamsamba.

Madaraja haya ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya Jimbo hili. Wananchi ni wakulima wakubwa wa mazao ya mpunga, alizeti, ufuta, mtama na mahindi. Pia, ni wafugaji wazuri wa ng'ombe kwa utaratibu unaokubalika na wavuvi wazuri, lakini nguvu zao zinaishia ardhini, kwani baada ya kazi kubwa ya kilimo na mavuno, hawawezi kusafirisha mazao yao na pia hawawezi kupata soko la mazao hayo, kwani ukosefu huo wa barabara na madaraja ni kikwazo kikubwa.

Mheshimiwa Spika, barabara chache zilizopo ni vinjia ambavyo kutokana na wembamba wake na zimejengwa kwenye kingo za Bonde la Ufa, hata wenye magari,

wenye roho ngumu, wanasita kupeleka magari yao, kwani hayawezi hata kupishana licha ya kwamba kwa kumbukumbu zangu nyingi zililimwa kwa *grader* mwaka 1962 nikiwa niko Darasa la Tano.

Mheshimiwa Spika, ni kwenye sehemu hii hii ya Bonde la Ufa kwa umbali wa kilomita 200, hakuna hata mtandao wa simu za mkononi, hali inayofanya mawasiliano kuwa magumu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa, kutokana na hali hii, majambazi wamejikita kwenye barabara hizi na kufanya uhalifu kila leo, kwani hata inapotokea hali hiyo, taarifa huwafikia Polisi Makao Makuu ya Wilaya baada ya siku mbili au tatu baada ya tukio.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Miundombinu itoe kipaumbele kwa barabara zifuatazo ambazo zinaitwa za Mkoa lakini hazishughulikiwi: Mlowo – Igamba – Kamsamba na Daraja kati ya Kamsamba (Mbozi Magharibi) na Chilyamatundu (Kwela), Igamba – Isalalo – Msangano na Daraja kati ya Msangano na Mnyuzi (Kata ya Msangano), Kakozi – Chiwezi – Msamba II – Chindi – Msangano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Miundombinu kwanza ieleweke ni Wizara mama katika Wizara zote. Inawajibika kikamilifu kufanya kazi yake vizuri zaidi na kitaalam na kwa uaminifu mkubwa sana. Nasema uaminifu mkubwa sana kwa sababu utekelezaji wake katika mikataba haieleweki kwa sababu makandarasi wanakuwa mbogo, tofauti kabla ya kupewa kazi, hatimaye Wizara inakuwa kama tela, kwani huburuzwa mno.

Mheshimiwa Spika, nchi zetu za Kiafrika zinakuwa hodari sana kutafuta fedha za ujenzi wa barabara, lakini tatizo linakuja katika utunzaji kwani hufa mara moja, hivyo Serikali inaonekana sio makini. Mfano leo hii nenda kaangalie barabara ya Morogoro mbele ya Ubungo Plaza, yameanza mashimo madogo madogo. Bila kuwahi kurekebisha hali hiyo, tutakuwa tunasubiri kujenga ukuta badala ya kuziba ufa.

Mheshimiwa Spika, zaidi, mitaro ambayo Serikali imejenga kwa fedha nyingi na vizuri, lakini imeziba na imejaa uchafu, inakuwaje na Serikali imejipangia kuwajibika ipasavyo? Naishauri Serikali, hivi sasa tumeshakuwa na nchi yetu yenye sifa zote, hivyo tuwajibike kama nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu pia wawajibike kuangalia uchakavu wa majengo na kuyafanyia usafi kwa kupaka rangi na kuufanya Mji wetu kuwa angavu muda wote.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Miundombinu ni Wizara ambayo inatakiwa itoe ufafanuzi, kwani kuna tetesi kwamba inaanza vibaya shughuli zake. Hivi karibuni zipo habari kwambaWizara hii kupitia Viongozi wake wameomba fedha *World Bank* za ujenzi wa Daraja la Kigamboni huku wakijua *NSSF* tayari imeshapata fedha kutoka Uholanzi, hivyo, kupelekea Serikali yetu kupata fedheha isiyo na sababu kupitia Bunge lako Tukufu. Naomba Waziri atakapotoa majumuisho atoe kauli ili Watanzania wajue nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la ndani linalotusumbua ni ufuatiliaji wa vyombo vyetu vya usafirishaji. Wizara hii sasa lazima ijikite katika hili kwani Watanzania tumeshachochwa na vifo vya kizembe. Hivi sasa lazima Wizara ifuatilie vizuri vivuko, *boat*, meli na kadhalika, badala ya kusubiri ajali, hatimaye uombolezaji wa mamia ya watu pasipo sababu. kwa mfano, hivi sasa kabla ya kufika katika mizani ya Kibaha, tayari pana msongamano wa malori makubwa katika barabara kuu (*high way*). Mimi sifahamu kwa nini? Kama pana ulazima, kwa nini wasiweke *alternative parking* kwa ajili ya kutekeleza kazi zao? Naongea hivi, sio muda mrefu patatokea kitu. Nasema hivi kwa sababu naelewa *driving* ya madereva wetu na zaidi sio kitu cha kawaida kinachofanyika pale. Naomba sana suala hili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namalizia kwa kuomba Serikali kuwa makini aidha, katika ubinafsishaji na ukodishaji katika sekta zote za miundombinu muhimu katika jamii, hasa kwa kuigiza vigezo vya wenzetu waliotangulia katika zoezi hilo badala ya kuingia kinadharia.

Mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kushika kalamu na kuandika haya maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake ambayo imenipa taaluma ndani ya Ukumbi wako wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Msemaji wa Upinzani kwa hotuba yake iliyotoa dira ya maslahi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako Spika, pia kuwa mtaalam mzuri katika Ukumbi wa Bunge lako. Mwenyezi Mungu akupe imani.

Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Lowassa kwa umahiri wake katika kazi zake. Natoa pongezi kwa dhati kwa Rais Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa CCM.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu niandike yangu machache kuhusiana na Wizara hii ya Miundombinu. Kwa kuanzia, Wizara inazungumzia vipi juu ya Viwanja vya Ndege? Tanzania Viwanja vya Ndege sio vichache, ila uangalifu sio mzuri. Nasema

hivi nikiwa na maana viwanja vimo sehemu nyingi, lakini ni jambo la kushangaza kuona vina viwango tofauti. Kwa mfano kiwanja cha ndege cha Dodoma pamoja na Serikali kuifanya Dodoma ni Makao Makuu, udhaifu wa Kiwanja kile ni taa zilizokipelekea kiwanja kisite kufanya kazi zake nyakati za usiku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu simu za mkononi; hivi nchi yetu inataka twende kama wanavyokwenda jirani zetu Kenya na Uganda? Kama ni hivyo, basi Watanzania tuangaliwe kwa kipato, elimu na kadhalika. Sio leo kumlazimisha Mtanzania aishi kama Mkenya ama Mganda. Naiomba Wizara ya Miundombinu itujulishe, ni Watanzania wangapi wanaotumia simu za mkononi, Wakenya wangapi wanaotumia simu za mkononi na Waganda wangapi wanaotumia simu za mkononi. Kama kiwango kikubwa ni Watanzania, kwa nini jirani zetu hawawalazimishi watu wao ili wafikie idadi yetu? Tanzania tunapandisha kodi ili tuwe sawa na jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya majini: Je, Wizara inaweza kutujibu kwa nini vifo vingi vinasababishwa na vyombo vya majini? Watanzania wanakufa kwa mamia katika meli. Ni kwa nini? Naomba jibu kuhusu usafiri wa magari. Pamoja na mahesabu ya Wizara juu ya magari. Iko hoja kuwa na uangalizi wa kina juu ya magari yetu kwani mara nyingi hutokea ajali barabarani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Kwanza, napenda kuwapongeza Wapigakura wangu wa Wilaya ya Micheweni kwa kunipa kura nyingi na leo nikawa Mbunge. Pia, nakishukuru Chama changu cha *CUF* kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano na nampongeza Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama chake. Vile vile, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake yenye kulenga kuwakomboa maskini.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe kwa kuongoza Bunge hili kwa hekima na busara na kwa *speed.* Mwisho, nawapongeza Wabunge wenzangu wote kwa kuchaguliwa kwenye Majimbo yao.

Sasa napenda kuchangia hoja. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa nchi kavu na Majini *(SUMATRA),* kwa sababu vyombo vingi vya majini hupakia abiria zaidi ya uwezo wake na hivyo kuhatarisha maisha ya abiria na mali zao. Vyombo hivyo vingi huwa ni vichakavu na hubeba mizigo chini ya uwezo wake na husabisha ajali na vyombo kuzama. Vile vile, vyombo vya nchi kavu hupakia abiria mara tatu zaidi ya kiwango kinachotakiwa. Serikali haioni hilo ni kosa kubwa!

Kwa hiyo, Serikali iwe na udhibiti mkubwa kuzuia tatizo hilo na wahusika washikiliwe kwa kupelekwa kwenye vyombo vya Sheria na tunataka Serikali iwalipe fidia waliopata hasara kwa mali zao na wale waliopoteza maisha yao. Naomba Waziri anipe ufafanuzi kwa masuala haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ongezeko la simu za mkononi, naona ni vyema Watanzania waondokane na bei zao na kuelekea kwa wenzetu kama vile Kenya na Uganda kutoka asilimia tano hadi asimilia saba. Kusema hivi, ilipaswa tupime mambo mengi katika nchi tatu hizi Kenya, Uganda na Tanzania, kwanza kwa elimu, elimu, mishahara, uchumi (kipato kwa mtu). Kama haya yatakua sawa, tungejua wapi tupo. Tungependa kujua ni nchi gani inayoongoza kwa watumiaji wa simu za mkononi!

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, naiomba Serikali iziangalie barabara zilizotolewa ahadi, nazo zitengenezwe ili tuondoe umaskini nchini na ahadi zitekelezwe.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri wa Miundombinu pamoja na wataalam walioandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa kukumbusha ahadi ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alizotoa wakati wa kampeni mwaka 2005 katika Wilaya ya Liwale. Ahadi hizo ni kuboresha barabara ya Nangurukulu – Liwale, Liwale – Nachingwea hasa eneo la mchanga kilometa 30 kutoka Liwale. Pia, ahadi ya ujenzi wa Daraja ya mto Ruhuu barabara iendayo Lilombe hadi Tunduru.

Pia, nimewahi kuandika barua ya kukumbusha kwa Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Miundombinu na nimechangia kwa kusema Bungeni wakati wa hoja ya Bajeti ya Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakhia Meghji. Kwa vile kuboreshwa kwa barabara hizo ni changamoto kubwa kwa maendeleo ya wananchi wa Liwale, ninashauri ahadi hizo zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana Awamu ya Tatu wananchi wa Liwale walielezwa kwamba *OPEC* imetoa Shilingi milioni 800 ($800,000) kuboresha kilometa 30 za barabara ya mchanga kutokea Liwale kwenda Nachingwea. Hakuna kilichofanyika hadi hivi leo. Katika kikao cha *RCC* kilichofanyika Nachingwea, Lindi – *TANROAD* walieleza fedha hizo sasa hazitatosha kukarabati kilometa 30 kama ilivyokusudiwa hapo awali na kwamba badala yake fedha hizo zitakarabati kilometa 13 tu na kwamba kazi hiyo ingeanza mara tu. Kwa nini kazi hiyo haijaanza? Tatizo ni nini na fedha hizo ziko wapi sasa?

Mheshimiwa Spika, mbali na barabara nilizotaja hapo juu, barabara zifuatazo ni muhimu sana kujengwa kwa manufaa ya wananchi. Ipo barabara inayounganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Lindi. Barabara hiyo inatoka Ndapata Wilaya ya Liwale na kwenda Ilonga – Ulanga Mahenge. Kikwazo kikubwa kwa kufufua barabara hii ni Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo inadai kwamba barabara hiyo itahatarisha hifadhi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, sababu hiyo imepitwa na wakati, kwani kuna barabara inayopita Mbuga za Wanyama Mikumi, pia ipo ile inayopita *Lake Manyara*, Serengeti hadi Lobo. Iweje barabara ya Ndapata (Liwale) – Ilonga (Ulanga – Mahenge) isijengwe

kwa kigezo cha wanyamapori? Wananchi wa Liwale na Ulanga/Mahenge ni ndugu na barabara hiyo ni fupi sana. Nashauri ijengwe ili wananchi hawa weweze kutembeleana. Wakati wa uchaguzi wa mwaka 2005 wananchi hawa almanusura wapigie kura Vyama vya Upinzani kwa madai ya barabara hiyo. Naomba Serikali ilione hilo na kuamua kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni kutoka Mirui Liwale kwenda Ruangwa. Kikwazo cha barabara hiyo ni daraja la Mto Mbwenkuru. Ninashauri zile daraja za zamani zinazotolewa kwenye ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Lindi, mojawapo nzuri, naomba itumike kwenye mto wa Mbwenkuru barabara inayounganisha Wilaya ya Liwale kupitia Mirui hadi kufikia Wilaya jirani ya Ruangwa ili wananchi wa pande zote mbili waweze kuwasiliana kwa njia hiyo fupi.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana Mawaziri wa Mawasiliano Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya na Dr. Maua Daftari walionisaidia sana kuleta mtandao ya simu *Buzz* na *Celtel* ambazo zinaendelea kusambaza mawasiliano hayo katika Wilaya ya Liwale. Ninashukuru sana. Tatizo kubwa sasa ni *TTCL* hakuna. Hivyo hakuna mawasiliano ya *Fax*. Hili sio tatizo la Liwale tu, bali hata Ruangwa na Nachingwea. Kwa karne hii, kutokuwa na *Fax* sio kitu cha kawaida, naomba tatizo hilo liondolewe mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamishwa, Tume ya Mawasiliano imekwishaanza kujenga Ofisi zake kwenye barabara ya Sam Nujoma? Kama bado, nini kinakwamisha na hali ikoje kuhusu ujenzi huo?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, Wilaya ya Ludewa katika Mkoa wa Iringa iko pembezoni mwa nchi. Kwa hiyo, katika upendeleo wa kujenga/kutengeneza barabara katika maeneo ya pembezoni mwa nchi Wilaya ya Ludewa ifikiriwe.

Pili, Wilaya ya Ludewa tunalima na kuzalisha sana kahawa na Waziri wa Kilimo anajua hilo, kwani Wilaya hii ni mojawapo ya maeneo yaliyoko kwenye mpango mpya wa kilimo cha kahawa nchini. Kwa nini Mkoa wa Iringa na hasa Wilaya ya Ludewa haiko kwenye mradi wa *STABEX* unaohusisha Mikoa minane inayolima zao la kahawa?

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Miundombinu, napenda nichangie moja kwa moja kwa baadhi ya maeneo muhimu ambayo naona hayajagusiwa sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na bahati tarehe 02 Julai, 2006 kuhudhuria Mkutano wa Wadau muhimu. Kikao ambacho kilijibu maswali yangu mengi kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Dar es Salaam Kibiti - Lindi - Mingoyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Miundombinu ajibu maswali yafuatayo ambayo ni sawa na upande wa pili wa Shilingi kutokana na Mkutano wake wa Jumapili.

Moja, nimepata taarifa kuwa mjenzi wa barabara ya Minyogo -Lindi - Nangurukuru, yaani M.A. Kharafi hajalipwa toka Desemba, 2005 kiasi cha Shilingi bilioni 34. Fedha hizi ni kutokana na kazi ambayo wameifanya mpaka sasa. Kutokulipwa kwao kunaathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kazi yao. Haieleweki kwa nini hawalipwi kwa kazi ambayo imekwishathibitishwa na *Certificate* imetolewa. Nitashukuru endapo Waziri atafafanua. Suala hili limeathiri utendaji.

Pili, Wizara imeteua wasimamizi wawili, (*Project Coordination/Supervisor*) kuangalia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu. Badala ya kuwa ni neema, jambo hili linazua balaa, kwani kila mmoja anatoa maagizo yake, yakitekelezwa, mwingine anapokuja baadaye anabadili maagizo ya yule wa kwanza. Matokeo yake ni kumbabaisha mkandarasi kiasi kwamba anafanya mabadiliko ya mara kwa mara ambayo yanachelewesha kazi na kuongeza gharama. Naomba Waziri achunguze suala hili ili kupata ufumbuzi muafaka.

Tatu, Wizara sasa ijikite zaidi katika utendaji ili yale yanayotoka Wizarani yawe na ukweli wa ufanisi wa kazi inayofanywa, kusitokee Waziri ama Rais kutoa taarifa kuwa barabara fulani itakamilika mwezi Desemba wakati wataalam wanaona dhahiri kuwa haitawezekana. Wataalamu wajipange vizuri kutekeleza wajibu wao na kufanya kazi kitaalamu. Waiheshimu *professional* yao na kutuletea mambo ya ukweli tupu.

Mwisho, Waziri atueleze, barabara ya Mingoyo - Lindi - Dar es Salaam itakamilika lini. Watoe tarehe ambayo wana uhakika kazi hii itakamilika ili wananchi wa Mikoa ya Kusini waweze kuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Miundombinu.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake, lakini natangulia kusema kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimeona safari hii nisiongee, nijaribu kuchangia kwa maandishi. Kuongea juu ya gati na *Airport* Mafia iwe imetosha. Wakati mwingine nafikiriwa kuwa labda mimi ndiyo Mbunge wa Jimbo hilo.

Pamoja na kuongelea nchi nzima, Mkoa mzima wa Pwani na Tanga, nalazimika kuvutika kuongelea Mafia, kwani zaidi ya nusu ya maisha yangu nimeishi Mafia.

Mheshimiwa Spika, kufika kwangu Bungeni kumechangiwa na wanawake wa Mafia na baadaye wanawake wa Pwani kuniunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kufikiria kwa karibu zaidi barabara ya Bagamoyo - Msata, Bagamoyo Saadani –Pangani -Tanga. Lakini pia naomba sana isiishe hatua hiyo ya awali tu, bali tuone basi mwakani barabara hizo zikitengewa fedha za ujenzi. Mheshimiwa Waziri, najua unafahamu juu ya Saadani -

Mkwaja kuwa sasa kuna Hifadhi. Lakini isitoshe Pwani yote ya Pangani imekuwa kivutio kikubwa cha utalii. Hivyo basi, ni wazi kuwa barabara hii ni muhimu sana.

Pili, suala la mawasiliano ya simu. Kwa sasa baadhi ya maeneo ya Kanda hii, bado simu hazijafika. Mkwaja ni moja ya Kijiji ambacho kipo ndani ya Hifadhi.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa kuhakikisha nao wapata mawasiliano haya ya simu? Tunashukuru sana kwa kuona umuhimu wa Tanga – Horohoro. Hii ni barabara muhimu sana hasa kwa wakati huu ambapo tunafufua *East African Community.* Mimi sina tatizo na hata ile barabara iendayo Tarakea, Ng'ambo ya pili Kenya, lami safi, majengo safi, huku kwetu vumbi, majengo ovyo ovyo. Sasa mtatutoa aibu.

Mheshimiwa Spika, nasema kazi kubwa na nzito bado iko mbele yetu. Jitihada na ushirikiano mkubwa unatakiwa kati ya Mheshimiwa Waziri na Watendaji na wataalam wote kwenye shughuli za barabara. Pesa zilizopangwa zifanye kazi kweli, yaani zitumike kama ilivyokusudiwa kwa kuleta matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kiwanja cha Mafia na gati, jamani hatujui tutaongea lugha gani! Nawatakia kila la kheri.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kuchangia katika hoja ya Waziri wa Miundombinu.

Kwanza napenda Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Miundombinu afahamu, kama alivyosema Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kuwa hakuna lami kati ya Tabora - Kaliua - Malagarasi hadi Kigoma wala haionyeshi umakini unapolieleza Bunge kuwa Wizara yako inapanga kufanya ukarabati wa lami katika barabara za Dodoma - Manyoni, Manyoni - Singida na Singida hadi Shelui. Maeneo hayo hayana lami. Sasa iweje ukarabati wa lami pale ambapo haijawahi kuwepo? Hapa kuna umakini kweli!

Mheshimiwa Spika, pili Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Mashariki ameshangaa kusikia Reli ya Kati ya Dar es Salaam -Mwanza. Nani alibadili mwelekeo wa Reli ya Kati isiwe Dar es Salaam -Kigoma? Hivi tunamdanganya nani katika kubadili historia ya nchi hii bila kuheshimu yale yanayostahili kubadilishwa? Relil ya Kati inatakiwa iwe Dar es Salaam - Kigoma na sio vinginevyo. Kubadili historia kwa utashi wa wachache waliopewa dhana ili kukidhi matakwa ya ubinafsi wao kuna lengo la kuigawa nchi.

Tatu, barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora - Urambo - Kigoma inaelekea haionekani umuhimu wake kwa upande wa Wizara. Lakini nimshukuru sana Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara yake pale alipowaalika Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma kwenye chakula cha mchana na akatuahidi kuwa barabara ya Kigoma hadi Dodoma kupitia Uvinza - Nguruka - Kaliua - Urambo - Itigi na Manyoni ana hakika ndio mkombozi wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia ahadi ya Serikali ya Korea Kusini ya kujenga Daraja la Malagarasi itatupa uchumi na hivyo kutuwezesha kupambana na umaskini na kuleta maisha bora kwa Watanzania.

Nne, hali ya usafiri ndani ya Ziwa Tanganyika siyo nzuri. Tumelalamika kuhusu usalama wa usafiri wa meli ya Mwongozo na Liemba ni ya mashaka. Nimesoma katika kitabu kuwa yapo magati nane yatakayojengwa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, niombe kuwa katika mgao wa magati, maeneo yafuatayo yakumbukwe, maeneo hayo ni Kalya, Subwasa, Buhinga (Mgambo) Sigunga na Kirando (Suruha) katika Jimbo la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Spika, usafiri duni wa meli husababisha wananchi wengi kupoteza maisha na mali zao na pia kuumia. Msafiri anapopanda na kushuka ndani ya meli kwa kutumia mitumbwi wakati wa tufani, msafiri ana mashaka na maisha yake. Kwa hali hiyo, naomba magati hayo yajengwe kwa kuangalia maeneo niliyoyataja hapo juu.

Tano, barabara ya Ilagala hadi Kalya hivi sasa inatengenezwa kwa kupitia *TANROAD*. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ametenga Shilingi milioni 95.70. Hivi nimesoma vizuri au kuna kosa la uchapaji? Hivi sasa wananchi wanachangia nguvu zao kwa kung'oa visiki kwa kulipwa Sh. 2,700,000/= kwa kila kilomita saba. Napenda nifahamu pesa ambazo zimetajwa ndani ya hotuba hii zitafanya kazi gani?

Aidha, napenda ieleweke kuwa, wananchi wanahoji malipo hayo sio sahihi. Kadhalika wanalalamika kucheleweshwa malipo kwa barabara hii. Tunashauri kwamba pale Ilagala pawekwe daraja badala ya kivuko ambacho kimeletwa mwaka 2005, lakini tayari kimeanza kusimama kwa siku kadhaa.

Mwisho, tunahitaji simu za simu za mikononi. Simu hizi ni kwa ajili ya uchumi na usalama wa Taifa. Ahsante.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, mchango wa nyongeza baada ya kuchangia kwa kuzungumza.

Moja, barabara ambazo sasa zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe sasa tunaomba zihudumiwe na *TANROADS* (Mkoa).

- Barabara ya Kayanga - Rwambaizi - Kigarama - Businde - Murongo kilometa 124, ni ndefu mno. Hivyo, gharama ni kubwa. Inaunganisha Tanzania na Uganda inapita katika maeneo ya uzalishaji mkubwa.

- Barabara ya Kigarama - Mabira - Kyerwa (Rwenkorongo) kilometa 51.8. Ni ndefu na yenye *terrain* ngumu ya vilima vilima.

- Barabara ya Mabira - Nkwenda kilomita 32, ni ndefu na yenye *terrain* ngumu ya vilima vilima.

Pili, barabara ya Kyaka – Kayanga (Karagwe Mjini). Tunaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami.

- *Traffic Density* ni kubwa.

- Kuna uchumi mkubwa.

Lakini zaidi ya yote naungana na Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Gosbert Blandes Mbunge wa Karagwe kukumbushia kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Wana-karagwe wote wanalikumbuka hili, wanalikumbushia na wana imani na ahadi hiyo. Tafadhali.

Tatu, Uwanja wa Ndege wa Bukoba. Tafadhali tuwezeshe ndege kutua na kuondoka. Ku-*Tarmac runway*.

Nne, Ukarabati wa barabara za Mkoa wa Kagera. Barabara ya Bugene - Kaisho - Murongo, tunaomba umakini mkubwa uwekwe pale.

- Kati ya Nkwenda na Lukulaujo penye dimbwi la maji.

- Kwenye Mlima Rwabumuka kuongeza kokoto na kuzuia barabara kuliwa na maji ya mvua.

**MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, reli na simu za mikononi. Kata ya Lumuma na Kidete katika Jimbo la Kilosa, Wilaya ya Kilosa, zina matatizo makubwa ya mawasiliano. Naomba Wizara ya Miundombinu iangalie uwekezano wa kusaidia maeneo yafuatayo:-

Moja, barabara, sehemu kubwa ya barabara kutoka Kilosa Mjini kupitia Lumuma hadi Kidete ni mbaya na haipitiki wakati wa mvua. Maeneo haya ni tajiri sana kwa kilimo cha vitunguu, mahindi na maharage. Wanunuzi wengi inabidi wazunguke kupitia Mpwapwa na Gairo. Tatizo hili linasababisha wakulima kupata bei ndogo na wanunuzi kulipa gharama kubwa za usafirishaji.

Pili, Reli ya Kati *(TRC)*. Wakazi wa Kata ya Kidete na Mzaganza na Vijiji vyake wanategemea usafiri wa Reli ya kati. Baada ya reli hiyo kufungwa kati ya Dar es Salaam na Dodoma, wakazi hawa sasa hawana usafiri wa kuaminika. Naomba Wizara iangalie aina ya usafiri wa viberenge kati ya Kidete na Kilosa Mjini ili kuwanusuru wananchi hawa hadi hapo reli itakapokuwa imerejeshwa katika hali yake ya kawaida.

Tatu, Tarafa yote ya Kidete haina mtandao wowote wa simu za mkononi. Tarafa ina mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji uliyofadhiliwa na *DANIDA*. Kuna wakulima wengi wa vitunguu, mahindi na maharage. Mwezi Septemba, 2005, kulikuwa

na wafanyabiashara zaidi ya 650 wenye simu za mkononi ambao zilikuwa hazitumiki kwa sababu hakuna mtandao.

Kwa vile barabara ni mbaya, reli haifanyi kazi, watu hawa hawana mawasiliano yoyote na wenzao katika Jimbo langu na Wizara nzima. Naomba *Celtel, VODACOM* au *TIGO* wapeleke mtandao huko.

Nne, Mheshimiwa Spika, namkaribisha Mheshimiwa Waziri au Naibu wake kutembelea Tarafa hii ili ajionee mwenyewe matatizo yanayowasibu wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mindombinu, kwanza kwa kumpongeza kwa hotuba nzuri Mheshimiwa Basil Mramba na Wasaidizi, Manaibu wake Mheshimiwa Dr. Mahanga na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu wakandarasi wamesemwa sana kuwa ni chanzo cha kazi mbaya katika Ujenzi, ukarabati au matengenezo ya barabara. Mimi nadhani hii siyo sahihi, kwa sababu Mikataba kati ya *Client/Employer* na *Contractor* ni makubaliano yanayozingatia usawa. Hakuna *boss* wa mwingine. Lakini kwa sasa katika sehemu kubwa, *Clients* wanaonekana ndiyo mabosi wa *Contractors. Clients* wakati mwingine wamehusika katika ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi, hivyo kuathiri sana *cash flow* ya mkandarasi na hiyo lazima iathiri ufanisi wa kazi.

Tumeona kuna mpango wa kuboresha shughuli za ukandarasi kwa Makandarasi wadogo na wa ndani. Inaweza kuwa ni nia ya kuwawezesha baadhi. Bila shaka ni vigumu kupata vigezo vya kuchagua miongoni mwao. Nashauri wapewe nafasi sawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu simu za mikononi, naipongeza Serikali kwa jitihada zake. Lakini sehemu za Dongobesh na Bashanet, bado hatujapata huduma za simu pamoja na kulia kwetu kwa muda mrefu. Naomba sasa kwa mara nyingine niombe Wizara kuhamasisha Makampuni ya simu hususan *Celtel* ambao tayari wapo ukanda ule.

Kwa maoni yangu, mtambo wa simu ukiboreshwa, itasaidia sana, lakini muhimu ni kuboresha/kufikisha mawasiliano Dongobesh (Mbulu) na Bashnet (Babati) umbali wa kilomita 15 kati yao maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TANROADS*, nawapongeza sana kwa kazi nzuri, lakini nashangaa, siku hizi *culverts* zinavyojengwa. Mtindo wa kuweka nundu au *hump* juu ya *culvert* unakera sana kwenye barabara nzuri. Mara nyingi tumejikuta tukirushwa ghafla au kutupwa nje ya barabara, wakati uko kwenye *speed* nzuri na kwenye barabara nzuri. Hili lirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu tumefika wapi kuhusu Uwanja wa Ndege Mkoani Manyara. Nakumbuka walikuja wataalam kufanya *reconnaisance* kutafuta *location* nzuri, nini matokeo yake?

Mimi ningeshauri Serikali kuwa, ili huduma ya ndege hata za dharura zipatikane, ni vyema kufikiria kuboresha kwa muda Kiwanja cha Ndege cha Dareda, kwani ndiyo kiwanja pekee cha karibu katika *Vicinity* ya Babati. Kiwanja hiki kinasaidia sana kutoa huduma ya *Flying Doctors* kwa Hospitali ya Dareda ambayo mpaka sasa ni kubwa Wilayani Babati kwenye Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara. Je, Serikali itazingatia ushauri huu wa kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Dareda?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya watumishi, hususan kwenye Makala *(Agencies),* inaonekana hakuna mpango wa kuwaendeleza kwa mafunzo. Nionavyo mimi, ni muhimu kuwa na mkakati wa kuwaendeleza watumishi wa ngazi zote hata wahudumu. Kwa upande wa maslahi/mishahara yao inaonekana kuna *gap* kubwa mno kati ya ngazi ya juu na ya chini, hata Mkoani tu. Mfano mtumishi wa ngazi ya chini anakuwa na Sh.90,000/= na ngazi ya juu Mkoani Sh.1,200,000/= lakini wote hawa wanashinda Ofisini toka asubuhi hadi jioni. Siyo *fair!* Nashauri wa chini wafikie angalau Sh.200,000/= ili kujali pia mchango wao kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake wawili na wataalam wote wa Wizara ya Miundombinu kwa kutayarisha hotuba nzuri. Aidha, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kutamka bayana kwamba itajenga daraja la Mto Kilombero. Wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro wanasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanza mchakato wa ujenzi wa Daraja la Mto Kilombero, ninaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuiboresha barabara ya Mkamba - Ifakara - Mahenge na Lupilo - Malinyi -Songea kwa sababu sasa Daraja la Mto Mwakisi linakamilishwa. Uboreshaji wa barabara hii kwa kiwango cha lami utachochea maendeleo ya kilimo katika bonde la Kilombero ambalo linao uwezo mkubwa wa Kilimo cha Mpunga na Pamba.

Aidha, ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapunguzia wananchi wa maeneo husika mzigo wa gharama za usafiri katika Jiji la Dar es Salaam kwa kufanya yafuatayo:-

(1) Kutengeneza mtandao wa usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Dsm – Pugu;
Ubungo – Kiluvya;
Ubungo – Mwenge – Mbweni; na
Temeke – Mbagala Mwisho.

Utekelezaji wa ushauri huu utapunguza msongamano, uchafuzi wa mazingira na kupunguza gharama za usafiri pamoja na kuwasaidia sana wanafunzi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

(2) Usafiri wa treni kwa abiria kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma. Usafishaji wa treni ya abiria unawaathiri sana wasafiri katika eneo hili hususan katika Mkoa wa Morogoro kati ya Kilosa na Msangara.

Ninamwomba kumjulisha Mheshimiwa Waziri kwamba wakulima wa vitunguu na mboga mboga eneo la Ulaya sasa inabidi wasitishe kama usafiri wa treni ya abiria hautarudishwa. Aidha, usafiri wa barabara kutoka Dar es Salaam - Dodoma - Dar es Salaam ni gharama kubwa na ya ziada kwa wananchi.

(3) Kiwanja kidogo cha Ndege cha Morogoro. Hiki kiwanja ni cha nani?

(4) Vituo vya mizani, ni vyema utawala na uendeshaji wa hivi Vituo ukaangaliwa upya kama kweli Serikali imepania kuzitunza barabara zetu pamoja na kupunguza ajali za barabarani. Aidha, *positioning of these places* pia iangaliwe upya kwani kwenye maeneo mengine Vituo vya Mizani vinasababisha msongamano wa magari na kuongeza uwezekano wa kutokea ajali. Kituo cha Kibaha ni kero kubwa sana nyakati za jioni kwa magari yatokayo Dar es Salaam kuelekea Bara.

(5) Serikali iangalie tena (upya) usajili wa wakandarasi ili kuboresha kiwango cha barabara na madaraja. Sasa hivi kuna wakandarasi ambao hawana ujuzi *(skills)* wa ujenzi. Wao ni wafanya biashara hivyo matokeo ya kazi zao siyo mazuri.

Mheshimiwa Spika, ninapenda sasa kuunga mkono hoja na kumtakia Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake na Watendaji wake wote kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kuboresha miundombinu kwa maendeleo ya nchi yetu.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Kwanza, kuna ujanja unaotumiwa na wenye mabasi kutoka Dar es Salaam - Dodoma kukwepa kunaswa kwenye mizani kwa kuzidisha uzito wanapokaribia kwenye mizani (Kibaha). Kwa hiyo, hulazimisha abiria kuteremka na kuingizwa kwenye gari ndogo hadi wanapopita kwenye mizani, ili ionekane kwamba hawajazidisha uzito.

Hii huleta usumbufu kwa abiria na pia kuharibu barabara na kujaza zaidi ya uwezo wa basi. Haya nimeyaona mimi mwenyewe jana tarehe 3 Julai, 2006 wakati nikitoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Naomba Serikali ifuatilie suala hili kuepusha usumbufu kwa abiria.

Pili, alama muhimu za barabarani kutoka Dar - Dodoma, nyingi zimefutika na hazionekani. Ni vyema kwa Wizara husika kuziweka kwa uwazi ili zionekane kwa uwazi.

Tatu, pamoja na kutengenezwa, lakini barabara kutoka Dumila hadi Gairo imeharibika na haifai kutumika kutokana na matuta na kupondeka. Ni vyema mkandarasi aipitie upya kabla Serikali hawajakabidhiwa.

**MHE. ABASI Z. MTEMVU:** Wakati wa kampeni katika Viwanja vya Mwembe Yanga Temeke, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete alitoa ahadi kwa wananchi wa Manispaa ya Temeke kwamba Serikali itatengeneza barabara kwa kiwango cha lami katika Manispaa ya Temeke.

(a) Je, ni barabara ngapi na zipi katika Manispaa ya Temeke zipo katika ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete?

(b) Lini matengenezo hayo yataanza katika Manispaa ya Temeke?

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niwapongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM. Naomba pia niwapongeze Wabunge wenzangu wa CCM Mheshimiwa Mzee Yusufu Makamba, Mheshimiwa Kidawa, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Rostam Aziz kwa kuteuliwa kuongoza Idara za Sekretariati ya CCM, kazi ambazo naamini moja kwa moja zitaongeza ufanisi wa usimamizi wa Chama Serikalini na Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Mramba Waziri wa Miundombinu na Watendaji wote wa Wizara hii kubwa na yenye majukumu mazito yenye umuhimu wa kipekee, kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Naomba niseme kwamba, ari mpya, nguvu mpya, kasi mpya ni lazima ieleweke kwa Watendaji wa Idara hii nyeti kwani Watanzania wengi wanatarajia kuona mafanikio makubwa yatokanayo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM. Katika hili, naomba nihimize kwamba uongozi wa Wizara ya Miundombinu na Watendaji, wapitie kwa umakini na waielewe Ilani ya Uchaguzi ya CCM ili uwe ndio mwongozi wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, watu waliokuwa wanamtafutia sababu Nabii Mussa, walifanya mpango wa kuja na Msahafu wa kwao, hali ya kwamba Msahafu wa Mussa ulikuwepo na ulikuwa unakidhi! Waumini wa kweli wakauliza, tunataka Msahafu mwingine wa nini, hali ya kuwa tuna Msahafu wa Mussa?

Mheshimiwa Spika, nami nataka niwaambie ndugu zangu wa Miundombinu kwamba, katika ugawaji wa vipaumbele, vigezo vinavyotumika, matumizi ya pesa na kadhalika, waongezwe na mfano wa Msahafu wa Mussa, yaani Ilani ya Uchaguzi na

wasitafute kutunga ya kwao. Tutawachukulia kuwa ni maadui wa mikakati yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu ina mambo mengi:-

1. Barabara Kuu na za Mikoa na kadhalika;
2. Bandari na Viwanja vya Ndege;
3. Nyumba za Serikali na majengo mengine;
4. Mawasiliano, Uchukuzi na Usafirishaji; na
5. Mamlaka ya Hali ya Hewa na kadhalika.

Majukumu yote haya yanafanya upana wa hoja hii kuwa kubwa na hivyo ni kweli lazima tuwe wenye kuuma na kupuliza wakati wa kuchangia hoja hii. Kazi zao ni nzito sana! Nawapa pole kwa majukumu, hongera kwa imani na Rais Kikwete juu ya uongozi wa Wizara na ninawaahidi ushirikiano wangu wote ili tufikie matarajio ya Watanzania kwenu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe malalamiko yangu kwa Wizara kwamba inashindwa kutambua umuhimuy wa kukamilisha barabara ya Dar es Salaam - Pwani - Lindi mpaka Mtwara. Wabunge wengi wamelalakia kiwango kidogo cha fedha zilizotengwa kwa mradi huu, hali ya kwamba mradi wa Marangu – Tarakea imetengewa kwa mwaka huu Shilingi bilioni 17. Hivi kweli umuhimu wa Marangu - Tarakea kiuchumi, kisiasa na kijamii ni zaidi kuliko umuhimu wa Dar es Salaam – Lindi kupitia Mkuranga Kibiti na Somanga? Ni vigezo gani vilivyotumika kufikia uamuzi huu?

Mheshimiwa Spika, ninaomba maelezo ya kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Miundombinu inipatie *assessment,* tathmini ama *economic evaluation* ya Shilingi ngapi ambazo tunaweza kupata kama Taifa kwa kusafirisha mizigo kwa reli zetu yaani:-

(a) Kupeleka mizigo Zambia, Zimbabwe, Malawi, Kongo kwa *TAZARA*; na

(b) Kwa kupeleka mizigo Kongo ya Mashariki, Burundi, Rwanda na Uganda.

Ni mamilioni mangapi tunayokosa kwa kushindwa kufanya uwekezaji stahili na usimamizi wenye ufanisi kwenye reli zetu? Hivi jamani tunashindwa kusimamia reli mpya yenye umri wa miaka 30 tu! Hata hilo mpaka tupate Wachina waje watufundishe namna ya kuwa na mabehewa masafi na kusafisha vyoo na kuboresha huduma za Vituo!

Mheshimiwa Spika, ni lini tutafungua njia ya Reli ya Dar es Salaam -Dodoma ya *TRC*? Ni hasara gani inayotokea kwa kuongeza *load* ambayo vinginevyo ingepita kwa treni baina ya Dar es Salaam na Dodoma? Hiyo *TRC* nayo imekithiri uchafu na huduma mbaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu kwa maswali haya ya juu, naomba niambiwe ni lazima waje wataalamu kutoka India kutuonyesha namna ya kufanya usafi ndani ya matreni na kufanya ukarabati wa mara kwa mara wa mataruma? Naomba maelezo ya kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika reli zetu utaongeza *traffic* ya mizigo itakayopitia Bandari ya Dar es Salaam, hali ambayo pia itaongeza mapato kwa njia hiyo ya Bandari.

Mheshimiwa Spika, Mungu ametupa hazina ya rasilimali, mojawapo ikiwa ni kuwa na *geographical advantage* ya kuwahudumia nchi jirani. Hivi hili, wenzetu wa Miundombinu hawalioni? Tusiogope kukopa kwa Mashirika ya Fedha ili tufanye uwekezaji wa kijamii *(Social instruments)* ambazo zinakwenda sanjari na malengo na mwongozo wa dhana za uwezeshaji wa kiuchumi, kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Naomba Wizara inipe maelezo ya kutambua umuhimu wa uwekezaji wa miradi hii ya kijamii na nihakikishiwe kwamba Serikali itaanza kufanya tathmini ya mahitaji ya uwekezaji *required physical investment* ili tumkabidhi Mheshimiwa Meghji jukumu ya kututafutia pesa hizo na Taifa zima tukubali jukumu la kubeba dhamana hiyo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia masuala ya Wilaya ya Mkuranga. *Rehabilitation* ya Mkuranga – Kisiju *Road* yenye kilometa 48, imetengewa Shilingi milioni 40. Barabara hii ndio mlango wa watu wa Wilaya ya Mafia ambao wamepitia Bandari ya Kisiju. Naomba Serikali itambue kwamba ujenzi wa Gati wilaya ya Mafia unakwenda sambasamba na ujenzi wa Bandari ya Kisiju. Shilingi milioni 40 zifanye nini?

Mheshimiwa Spika, naomba nihakikishiwe kuwa Wizara ya Miundombinu inatambua kwamba utekelezaji wa ujenzi wa Gati la Mafia ni sanjari na Bandari ya Kisiju.

Mheshimiwa Spika, mimi nina imani kubwa na Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu - Edward Lowassa kama Viongozi wangu Wakuu wa Serikali ya CCM ya Ari mpya, Nguvu Mpya na Kasi mpya. Wakati nachangia kwenye hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilionyesha wasiwasi wangu kwamba tuna wenzetu katika nafasi za utekelezaji ambao ama hawaelewi tafsiri ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, ama hawana uwezo au nia ya kwenda na mdundo wetu. Naomba sana Wizara ya Miundombinu na wahusika wote watambue kwamba Serikali wanayoitumikia ni ya CCM na inaongozwa na Ilani. Hatuwezi kukubali kama Wabunge wengi walivyochangia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, natarajia kupata maelezo ya kujitosheleza kwa maelezo haya niliyoyawasikisha. Kwa kuzingatia hayo, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja ya Waziri wa Miundombinu.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, mimi sina hoja tofauti na wengine, bali naunga mkono Bajeti hii. Naomba kuzungumzia kuhusu wananchi wa Liwale na Kilwa, ambao wanalazimika kusafiri umbali mrefu kuifikia Liwale, yaani Dar es Salaam – Liwale.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi niliowataja hapo juu waweze kufika Liwale, inabidi wavuke Wilaya kadhaa toka Dar es Salaam hadi Liwale zikiwemo Mkoa wa Pwani - Kilwa - Lindi - Ruangwa au Masasi - Nachingwea na hatimaye Liwale.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Miundombinu itutengenezee barabara ya Nangurukuru – Liwale ambayo ni fupi yenye kilometa chache ukilinganisha na mzunguko nilioutaja, ambao ni kero kubwa kwa wananchi wa Liwale na Kilwa. Barabara hii ni kiungo kikubwa cha Wilaya ya Kilwa na Liwale pia ni njia au barabara kuu ya kuupokelea Mwenye wa Uhuru.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Njianne – Kipatimu huko Kilwa, barabara hii kihistoria imepita katikati ya makazi ya wananchi, kwa kuwa hapo awali Wamisionari ndio waliopitisha njia ya mkato bada ya kuona wasingeweza kuzunguka njia ya Utete, wananchi hawaelewi ni lini ilibadilishwa ikawa ya Halmashauri ya Wilaya. Vile vile hawaelewi ni lini ilibadilishwa ikawa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, vile vile wananchi wana hamu sana na barabara hii, lakini kitendo cha kutowalipa mali zao ambazo zipo pale, nyumba zao ambazo zimejengwa na zimechorwa *X*, wakidaiwa kwamba wameifuata barabara, ni kero kubwa na ni dhuluma kubwa kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Miundombinu atembelee eneo hili ambalo bomoabomoa ilitakiwa kuanza mwishoni mwa mwezi uliopita, mwezi June, 2006 ili apate hali halisi kusiwepo tena migogoro.

Mheshimiwa Spika, eneo la barabara ni lile lile, wananchi ni wale wale, nyumba na mazao ni yale yale. Hivyo basi, naiomba Wizara iwaeleze wananchi wa Kilwa, ni lini hati ya kuwa barabara ya Wilaya au ya Mkoa ilitolewa ili wananchi wasiendelee kudai malipo ya eneo hilo la Njianne Kipatimu kwa mali zao zitakazobomolewa na kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa pongezi kwa hotuba nzuri ambayo imezingatia utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010.

Katika kuleta mafanikio ya kiuchumi, ukombozi ni kufungua barabara za lami kati ya Mkoa na Mkoa na barabara za ndani ya Mkoa ili kusaidia kuendeleza kilimo hasa kuwawezesha wakulima kusafirisha mazao yao.

Mheshimwia Spika, kwa upande wangu ningependa kuwasilisha yafuatayo:-
Kwanza, tunashukuru CCM na Serikali yake kwa kuipa kipaumbele barabara ya Tunduma - Sumbawanga kwamba itaanza kuwekwa lami mwaka wa fedha 2006/2007. Tunaomba ijengwe barabara ya lami na siyo barabara kwa kiwango cha lami. Natumaini nimeeleweka.

Pili, umuhimu wa kuunganisha Mpanda na Makao Makuu ya Mkoa unaeleweka na pia kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma na Tabora itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa maendeleo ya Ukanda wa Mikoa ya Magharibi.

Tatu, ujenzi wa Bandari ya Kasanga na barabara ya lami kuunganisha Sumbawanga na Bandari ya Kasanga ni muhimu sana katika kuendeleza biashara kati ya Tanzania na Zambia, Kongo na Burundi kupitia Ziwa Tanganyika.

Nne, ni wakati muafaka sasa kuhamasisha mpango wa kutengeneza barabara ya lami kati ya Rukwa na Zambia, kupitia Kasesya na Mbala (Zambia).

Tano, kilio cha kutokuwa na barabara katika eneo la Bonde la Rukwa ni cha miaka mingi sana. Nashukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kutenga Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuanza matengenezo ya barabara ya Myangalua mpaka Kilyamatundu.

Sita, naomba mpango wa kutengeneza barabara na Munze – Kilyamatundu uanze mwaka huu chini ya msaada wa *DANIDA*. Fedha iliyotengwa awamu hii Shilingi milioni 290 ni kidogo, zinatosha kilomita 25 tu wakati barabara ina urefu wa kilometa 146. Nashauri zitengwe Shilingi milioni 500 kwa mwaka huu ili madaraja na *drift* zote za barabara hiyo zijengwe mwaka huu wa fedha. Mwaka kesho ndipo kazi ya kulima barabara ifanyike yote, kwa vile mpango wa kujenga barabara hii ni wa miaka miwili.

Saba, naomba Wizara itekeleze ahadi yake ya mwaka 2005 ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Muze - Kasesya kupitia Mfinga – kilometa 21. Kiasi cha Shilingi milioni 55 zilizotengwa zinatosha kilometa tano tu. Naomba Shilingi milioni 210 ambazo ndizo Bodi ya Mkoa ilipitisha.

Eneo hili, wananchi wanasafirisha mazao yao kwa shida hasa kwa kutumia punda na Wizara mnafahamu yote hayo. Naomba wananchi wa Jimbo langu waishio katika Kata ya Mfinga na Muze watendewe haki.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:**Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Nampongeza Mheshimiwa Makongoro Mahanga kwa kuwa Waziri wa kwanza kutembelea Wilaya yetu . Ninaomba Serikali/Wizara iangalie yafuatayo:-

Kwanza, barabara ya Songea - *Mbamba Bay.* Ukurasa wa 27 ibara ya 34 inaonyesha kwamba upo uwezekano wa kupata fedha mwaka 2006/2007 kwa kipande cha Matemanga – Songea. Hii ni kazi nzuri. Lakini kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais ni barabara ninayoitaja itengenezwe kwa kiwango cha lami, ni wazi kwa kasi hii, lengo hili linaweza lisifikiwe.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, Serikali kwa fedha yake ianze kwa kuendeleza ile lami toka pacha ya kwenda Peramiho au kwa kuanzia Mbinga kuja Songea.

Pia, nashauri kwamba, kasi ya kutafuta fedha kwa kuhusisha Wahisani wengine kama *EU,* zifanyike sasa.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbinga – Litembo – Kitura ni barabara inayoelekea pia Hospitali kubwa ya Litembo. Hali ya barabara ni mbaya sana. Kwa sasa mkandarasi amepewa kilometa 10 tu kutoka Mbinga Mjini. Barabara hii haijatengenezwa kwa kipindi cha miaka mitano. Naomba sana barabara hii sasa itengenezwe. Ni gharama hata kwa Serikali kwa sababu kwenda Litembo au Kitura inabidi kupita Ndengo ambako ni mbali sana.

Mheshimiwa Spika, katika suala la mawasiliano, napenda kusema kwamba Kata zifuatazo hazina mawasilisno ya simu (mkononi). Kata hizo ni Miji midogo, nayo ni Magu, Matiri, Ruanda na Litembo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iyahimize Makampuni husika ili yaharakishe mipango ya huduma kuja katika Miji hiyo, lakini kwa Kata zote katika Jimbo la Mbinga Mashariki kwa mfano Mpapa, Langiro, Mbuyi, Mikalanga, Kitura, Litumbandyozi na Namswea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa masharti.

Kwanza, napenda nishukuru sana juhudi zilizofanywa na Serikali katika harakati zake za kuinua uchumi wa nchi yetu. Katika hotuba ya Waziri Mkuu nilizungumzia Barabara la Usagara - Geita kwamba haikuwemo katika ujenzi. Pamoja na kutokuwekwa kwenye Bajeti hii, barabara hii hadi sasa ni mbovu, sasa haipitiki kiurahisi. Nimeangalia sana, sikuona imetengewa kiasi gani cha fedha kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa kuwa ndio kiungo kikubwa katika Kanda ya Ziwa. Kipande kilichobaki cha kilometa 92 kinatia aibu Taifa letu hasa ukizingatia yafuatayo:-

1. Kutoka Geita - Buzilayombo - Kyamunyorwa -Muleba hadi Mtukula, barabara zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

2. Kutoka Mtukula - Kampala - Kisumo - Sirari - barabara hii yote ni lami tupu.

3. Kutoka Sirari - Musoma - Magu hadi Mwanza ni lami tu.

Mzunguko huu ni wa Afrika Mashariki, lakini unatiwa dosari na kipande hiki cha Usagara hadi Geita cha kilometa 92. Kama nilivyoanza kusema, hata matengenezo ya kawaida ya barabara hii hayatiliwi maanani. Ukitoka Usagara kwenda Geita, unachukua muda mrefu sana shauri ya mashimo. Ninafanya mpango wa kujenga barabara hii kwa lami, basi matengenezo ya kawaida yafanyike haraka iwezekanavyo. Kama ikibidi toeni fedha sehemu yoyote ile ili kuwanusuru wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimwa John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake mzuri wa kuanza kujenga barabara hii *point C* kuja *B*. Kumbe barabara hii ingeanza kujengwa Usagara Geita, kipande hiki kingebaki bila kutengenezwa milele na milele.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati wa majumuisho, kama kweli wanatutakia mema, basi waonyeshe uzalendo wao wa kutupatia na kuendelea kuitengeneza barabara hii mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Geita ina barabara nyingi sana na ningependa pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Tatu, imefanya kazi kubwa sana kufungua njia nyingi zilizokuwa zimejifunga kama njia ya Geita, Kagu, Nzera hadi Nkome Mchangani imefunguliwa, lakini naomba awamu hii, barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Nzera kwenda Nyahunga, miaka iliyopita tulikuwa tunapewa fedha. Kipindi hiki barabara hii imenyimwa fedha kabisa! Naomba Waziri anieleze ni kigezo kipi kimesababisha barabara hii isipatiwe fedha wakati ujenzi wake haujaisha? Barabara hii imejengwa kuanzia Nzera hadi Rwezera tu, kama kilometa tisa. Eneo lingine halijatengenezwa na fedha hakuna. Wananchi wa maeneo haya tunawatakia mema?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya kina.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Miundombinu.

Mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Kilwa, naomba kuandika yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu mpango wa kuwezeshwa kila Halmashauri, kuwa magreda, nadhani mpango huu utasaidia. Kama Halmashauri zikiwa na vyombo itasaidia sana kutengeneza barabara zetu.

Pili, kuhusu barabara ya kutoka Mkocho kwenda Kivinje, barabaa hii ni muhimu kwa kuwa inakwenda kwenye Hospitali Kuu ya Wilaya. Barabara hii ni kero kubwa, ni mbovu kweli mpaka inafanya wagonjwa kushindwa kupelekwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ni ahadi ya Rais wakati wa Kampeni. Naiomba Wizara kufikiria barabara hii.

Kuhusu Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko, kiwanja kinahitaji matengenezo ya hali ya juu. Uwanja una umuhimu mkubwa sababu Kilwa ni Mji wa Kitale.

Mheshimiwa Spika, naomba Kilwa tufikiriwe kuboreshewa Uwanja wetu.

Kuhusu barabara ya Pande - Limario. Barabara hii ina umuhimu mkubwa kwa sababu Pande na Limario ni Kata zinazozalisha korosho kwa wingi. Naomba barabara hii itengenezwe ili wakulima wetu waweze kuongeza uzalishaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba matatizo ya wakandarasi Nangurukuru kwenda Mbwemkuru *(SICCO)* yashughulikiwe. Hawa itawasaidia jamii inayoishi kandokando kupata huduma yeyote. Kibaya zaidi sehemu ya Mavuji wamevunja kisima cha maji ambacho kiliwasaidia wana-kijiji wa Mavuji. Naomba Wizara ifuatilie hilo.

Kuhusu ajira, hawa *SICCO,* Wachina wanaendesha magari wenyewe. Hii inawafanya vijana wetu madereva kukosa ajira.

Kuhusu mawasiliano ya simu za mkononi, kuna tatizo la mawasiliano hayo huko Nanjirinje na Likawange. Naomba Wizara itusaidie kwa hilo huko Kilwa kwa kupata huduma hii.

Kuhusu Barabara ya Tingi - Kipatimu ya kilometa 50, nashukuru sana Wilaya yetu imepata barabara. Lakini nataka niseme kuhusu uzembe wa Wizara kuchelewesha kwa miaka miwili. Hilo lilifanya mwaka huu kupata kilometa 30 tu na siyo kilometa 50 kama ilivyoandikwa kwenye hotuba ya Waziri.

Kuhusu fidia kutokana na Barabara ya Nanguruku – Mbwemkuru, bado hilo ni tatizo kubwa sana.

Pia, naomba Wizara itilie mkazo wa kulipwa wote walioathirika na bomoa bomoa hii. Naona kuna uonevu kiasi fulani. Kibaya zaidi wengine wamelipwa wengine hawajalipwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii. Nashukuru sana.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba - Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari - Naibu Waziri wa Miundombinu na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga -Naibu Waziri Miundombinu, Katibu Mkuu na timu yake ya wataalamu kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, mawasiliano ya simu za mkononi katika Kata ya Madibira. Kata hii imekosa mawasiliano yote ya simu na barabara iko mbali na Makao Makuu ya Wilaya Rujewa kilometa 83. Kwa hiyo, naomba Wizara iongeze nguvu katika kusisitiza Makampuni ya Simu za Mkononi hasa *CELTEL* ambayo tayari ilianza kufanya utafiti ili kuwaondolea adha wananchi hawa wa Kata hii.

Pili, Mradi wa Kilimo wenye thamani ya Shilingi bilioni 24.00 Sekondari ya Bweni ambayo imefadhiliwa na *TANAPA* na kuungwa mkono na Mheshimiwa Maua Daftari kwa njia ya harambee, lakini Kata hii haina mawasiliano ya simu, ni mpaka uende Mafinga kilometa 70 au Rujewa kilometa 83 kitu ambacho ni hatari sana kwa wanafunzi na Walimu. Vile vile, hawawezi kutoa taarifa yoyote matatizo yanapotokea.

Tatu, barabara ya kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya na barabara kuu ya Iringa kwenda Mbeya imekuwa ikipewa kiasi kidogo sana Shilingi milioni 6.0 – 13.0 tu. Je, lini itatengenezwa kwa kiwango cha lami kama zilivyo Wilaya nyingine? Barabara hii Igawa – Rujewa ina kama kilometa nne tu.

Nne, Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga imetengewa Shilingi milioni 70.0 tu. Pesa hizi ni kwa ajili ya nini? Kwa barabara ambayo tayari imekwishawekwa kwenye mpango wa kutengenezwa kwa kiwango cha lami, upembuzi yakinifu tayari na usanifu tayari, kwa nini Serikali isishirikiane na *ADB* ambayo tayari wameamua kufadhili barabara hii chini ya Mpango wa *AMSDP* kwa kiasi cha Sh. 1,146,361,100/= ulioko chini ya Waziri Mkuu? Mkandarasi alianza kazi na kulipwa Sh.194,334,367/=, ameshindwa kuendelea na barabara imetelekezwa na ameanza kuondoa vifaa vyake. Sasa kwa nini Wizara ya Miundombinu isianze kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami ikiungana na mfadhili huyo? Naomba kupewa maelezo ili wananchi wajue nini kinaendelea baada ya kutoa Shilingi milioni 70 ambazo hazitotengeneza urefu mkubwa.

Mwisho, naomba kushauri Serikali kuhusu pesa zinazopelekwa Mikoani. Utaratibu uangaliwe upya pesa zipelekwe zote kwa muda muafaka badala ya utaratibu wa sasa, Meneja wa *TANROADS* (Mkoa) hukaa sana kusubiri pesa mpaka mkandarasi anashindwa kuendelea na matengenezo na hatimaye kufanya pesa zisitumike baada ya mwaka wa fedha kuisha.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu ni kusikitika na kushangaa sana. Tabora ina matatizo gani katika nchi hii? Nadhani tukubali kuwa Uwanja wa Ndege ni mbovu, barabara mbovu, treni ndio kama hivyo. Wananchi wanasemaje? Kuhusu

kuwajali suala lao la usafiri matokeo yake mnasema mkoa usioendelea mnategemea utaendeleaje bila hata njia? Tabora kuna Kampuni moja tu ya Ndege inayokuja hapo na hata hizo ndege zenyewe sio nzima. Inatokea hata siku tatu ndege haijafika Tabora. Bado tujiulize: Je, wananchi wetu wanaweza kupanda ndege wote?

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Manyoni - Itigi -Tabora nadhani sio ndefu sana ila kuna ukiritimba, uchoyo na njia mojawapo ya kurudisha nyuma maendeleo ya Mkoa wetu. Je, haya mambo yote yanayoandaliwa kama MKUKUTA, sisi Tabora yanatufikia kweli! Au MKUKUTA utakuwa wa maneno ya msamiati na maneno magumu katika makaratasi!

Mheshimiwa Spika, sidhani kama tuko pamoja na haya yanayopangwa na Serikali ili kuleta maendeleo kwa kila mtu na maisha bora. Ubora wa miundombinu uko wapi Tabora?Tunalima tumbaku na asilimia 5.2 imeongezeka na kodi inapanda kwenye sigara ina maana hayo yote hamuyaoni kama nao wanachangia mapato ya nchi hii.

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara. Kwanza, niipongeze Wizara, kwenye ukarasa 53 wa hotuba inayoelekeza kuomba simu za kukoroga na kuweka mtambo wa kisasa kwenye Wilaya ambazo hazina simu za kisasa na kuweka simu za kisasa ikiwemo ile ya Sikonge.

Mheshimiwa Spika, bado naiomba Wizara iangalie uboreshaji wa Posta Wilayani Sikonge, Kituo kilichopo ni kidogo na hakikidhi haja ya watumiaji kama Wilaya.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limetaka kunielekeza kutounga mkono hoja hii ni juu ya kutelekezwa kwa Barabara yaTabora, Ipole – Rungwa. Barabara hii ni barabara kuu, lakini ina hali mbaya, hasa eneo la Ipole – Rungwa. Kipindi chote cha masika iliangalie sana suala la barabara hii iliyoachwa na inayopewa ahadi zisizotekelezwa.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri unapojibu hoja za Waheshimiwa Wabunge utoe maelezo ya kurudisha matumaini ya wananchi wa Tarafa ya Kiwere, Sikonge na Mikoa ya Mbeya na Tabora.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwamba kuanzia kipindi cha Awamu ya Kwanza hadi ya Nne imejitahidi kuboresha barabara Mikoani na Wilayani.

Pili, naishauri Serikali sasa ielekeze nguvu kubwa katika usafiri wa majini hasa wa maziwa. Ziwa Nyasa linahitaji mtazamo wa kipekee. Hali ni mbaya sana. Wananchi wa maeneo hayo wako hatarini sana kwa kutumia usafiri wa maboti yasiyo na usalama kabisa, ikiwa ni pamoja na kushindwa kusafirisha mazao yao kama muhogo, samaki na hata vyungu kuelekea kwenye masoko.

Tunashukuru kwa kutenga fedha kwa uendelezaji wa *berths* mbili lakini napenda kuishauri Serikali kufikiria kujenga *berths* mbili nyingine katika Bandari ndogo za Makonde na Matema. Maendeleo hayo ni hatari sana hasa ziwa linapochafuka sana kwa mawimbi.

Tatu, nashauri Serikali ihamasishe wawekezaji *serious* kufanya biashara ya kupeleke meli kubwa katika ziwa lile. Kimawasiliano, nashauri Serikail ihamasishe Makampuni ya simu, angalau wananchi wa Mwambao wa Ziwa lile kuwasiliana na watu wa Wilayani na Mikoani.

Nne, bado kuna haja kushughulikia uboreshaji wa barabara ziendazo katika maeneo yenye uwekezaji hasa viwanda vya Sukari *TPC*, Mtibwa na kadhalika. Mchango wao kwa njia ya kodi ni mzuri na hivyo kuboresha uchumi wa nchi.

Tano, naishauri Serikali kujizatiti katika kuboresha usafiri wa anga. *Air Tanzania* inahitaji kufanyiwa marekebisho ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya dhati na ya kizalendo katika kuhimiza uwajibikaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu yetu katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, maana yake ni kuzaliwa upya katika utendaji wa kazi na uwajibikaji. Hii kwa Watanzania wote zikiwemo Wizara zote na Taasisi zake, sekta binafsi na kadhalika. Lakini tujiulize: Je, Watendaji wa Serikali, kwa mfano, Wakurugenzi wa Wizara, Maofisa na Taasisi za Serikali wameipokeaje kauli mbiu hii ya Ari Mpya? Safari za nje haziishi! Mbona hawafuatilii mipango yao? Mbona maghorofa yanaua watu ndipo watokee?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali labda Watendaji wangekula kiapo cha uaminifu na utekelezaji kazi, labda wangemwogopa Mungu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa uchungu mkubwa sana. Mheshimiwa Rais ametembelea Wizara kwa lengo la kuhimiza utendaji kazi. Inafika mahali tuwe na ruhusa na pia tuone aibu kwa maana ya kumuunga mkono Rais wa nchi na Waziri Mkuu kwa jitihada zao wanazozifanya. Mhandisi wa barabara, mifereji, majengo, kila mmoja na fani yake atimize wajibu wake na aheshimu taaluma yake kwa kuitumia ipasavyo. Kama mradi ni wa muda wa miezi miwili, basi iwe kama ilivyopangwa na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya barabara za Mkoa wa Dar es Salaam kwa kweli zinatia uchungu sana. Dar es Salaam ni kitovu cha uchumi cha nchi na kuwa wakazi wapatao milioni 3.5. Vilevile, asilimia 80 ya mapato ya nchi yatatoka Mkoa wa Dar es Salaam. Dar es Salaam ni Mji wenye sura ya kitalii ambao wanauangalia Mkoa huu kwa maana ya miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, ingawa barabara ya uhuru iko chini ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na uwezo wa Halmashauri ni mdogo, naiomba Serikali iipe hadhi ishughulikiwe na *TANROAD*. Barabara hii ndiyo njia kuu wanapopitia wageni mashuhuri toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa barabara ya Tabata Dampo kupitia Kigogo hadi barabara ya Kawawa. Barabara hii ni kiungo muhimu sana kinachounganisha kati ya barabara ya Mandela na barabara ya Kawawa ambayo itasaidia watu wa Tabata, Segerea, Kinyerezi na Mabibo kufika katikati ya Jiji kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia *TANROAD* zipatie hadhi barabara zifuatazo ziwe chini ya uangalizi wa Serikali Kuu. Hii inatokana na uwezo mdogo wa fedha wa Halmashauri zetu nchini.

1. Barabara ya Uhuru;
2. Barabara ya Tabata (Mandela Dampo) kupitia Kigogo hadi Kawawa;
3. Mombasa - *Moshi Bar* - Chanika - Msongola;
4. *Segerea Seminary* kupitia Majumba sita hadi *Nyerere Road;*
5. *External* - Mabibo - Kisukuru - Chang'ombe - Vingunguti;
6. Banana - Kitunda - Msongola;
7. Maziwa - *Ubungo, Morogoro Road* - *Mama Land* - *Mabibo* - *External (Mandela Road)*
8. Kagera - Mburahati hadi Kigogo Darajani (Ilala)
9. Kitunda Mwanagati hadi Tandika Azimio (Temeke)

Mheshimiwa Spika, naomba zipatiwe kipaumbele maana ni msaada mkubwa kwa hali ya kidharura.

Mheshimiwa Spika, naomba mawasiliano ya simu za mkononi katika eneo la Chanika - Videte na Msongola na hasa *TIGO* na *VODACOM*. Eneo hili liko Wilaya ya Ilala Mkoa wa Dar es – Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuiunga mkono hoja ya Wizara ya Miundombinu kwa asilimia zote mia.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa ushauri wangu juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mbeya kwenda Makongorosi Chunya. Barabara hii inapitia katika barabara za Isanga, Iganzo na Mwansenkwa ndani ya Jiji la Mbeya. Mali ya watu hawa ilitathminiwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara hiyo na Serikali iliahidi kulipa fidia kwa watu hao Aprili, 2006. Mpaka sasa hili limekuwa kero ndani ya Jimbo langu.

Naomba nielezwe kwa uhakika, ni lini hasa fidia hii italipwa kwa wananchi wa Kata hizi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia maeneo machache katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Miundombinu ambayo kwa kweli ni muhimu sana katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote yenye lengo la kuleta maendeleo lazima ihakikishe nchi imefunguliwa kwa kuboresha barabara, viwanja vya ndege, vivuko, reli na njia zote za usafirishaji ikiwemo bandari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza na barabara, naishauri Serikali iache mtindo wa kufanya upembuzi yakinifu kwa muda mrefu, bali ihakikishe upembuzi huo unakwenda pamoja na *designing* ili kupunguza muda au ni vyema *designing* iende sambamba na ujenzi wa barabara kwani kwa kweli barabara kwa nchi yetu ni muhimu sana, inabidi zijengwe kwa mtindo wa dharura.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma umetengwa kwa muda mrefu sana. Barabara ni tatizo kwa miaka mingi, Wabunge waliopo na waliopita wamekuwa wakiuliza maswali mbalimbali na kupewa majibu yanayowapooza tu, bila mafanikio. Naiomba Serikali iangalie upya suala hilo. Tumechoka na ahadi zisizoeleweka.

Mheshimiwa Spika, mbali na barabara ya Kigoma – Nyakanazi na Tabora – Kigoma, nchi hii imekuwa na tatizo la barabara zinazounganisha Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa. Vilevile, Vijiji havijaunganishwa kabisa na huko ndiko uzalishaji wa malighafi na chakula unapofanyika. Je, Serikali haioni kama tunachelewesha maendeleo ya wananchi na kuboresha maisha yao? Imekuwa ngumu kwa wao kusafirisha mazao yao, matokeo yake yanaoza tu shambani.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vilivyo katika Mkoa wa Kigoma wenye kila aina ya neema vina wazalishaji wengi na wanazalisha chakula cha kulisha Mikoa mingine Tanzania. Hivyo, naomba Mkoa wetu ufunguliwe, wananchi wapate tija ya kazi ya mikono yao kwani watajipatia soko.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ilijengwa tangu enzi za ukoloni. Ni dhahiri kuwa reli ni muhimu sana. Lakini ufanisi wake umekuwa hafifu sana. Reli ya Kati inahitaji ukarabati au ujenzi mpya wa reli hiyo. Mabehewa ya mizigo na abiria yamechakaa sana. Naiomba Serikali ilitazame suala hilo.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli unaanzia Dodoma hali ambayo imeleta usumbufu sana kwa wananchi. Kwa kuwa Serikali inaonyesha imeshindwa kuiendeleza iwe makini sana katika kuibinafsisha, Mkataba uzingatie maslahi ya nchi na sio mwekezaji pekee.

Mheshimiwa Spika, bandari ni muhimu sana, lakini inasikitisha kuona Bandari ya Mkoa wa Kigoma siku hadi siku inazidi kudidimia wakati inafanya kazi nzuri ya usafirishaji wa mizigo kwenda na kutoka Zambia, Kongo, Burundi na Rwanda. Je, Serikali haioni hili? Kudorora kwa Reli ya ya Kati kunazidi kuua Bandari muhimu ya Kigoma! Tunakosa mapato mengi sana katika Taifa letu!

Mheshimiwa Spika, meli inayotumika katika Ziwa Tanganyika ni moja tu, tena imechakaa, inaitwa Mwongozo, Lihemba imekufa siku nyingi sana! Ziwa lile litabaki kuwa pambo katika nchi hii kama hatutaona umuhimu wake.

Nikiangalia upande wa Vivuko, Ziwa Tanganyika halina vivuko. Wananchi wanatumia maboti ya mbao ambayo ndiyo vyombo vya usafiri vinavyounganisha Vijiji vilivyopo kandokando ya Ziwa, lakini vyombo hivi ni duni mno na huhatarisha maisha ya wananchi kila yanapopasuka yakiwa safarini. Naomba Serikali iupatie Mkoa ya Kigoma vivuko hata viwili kimoja kiende Vijiji vilivyopo Kaskazini na kingine kiende Vijiji vilivyopo Kusini mwa Mkoa, ambavyo viko pembezoni mwa Ziwa. Lengo ni lile lile la kusafirisha mazao kama samaki, dagaa na wananchi wenyewe kwani wanategemea Hospitali Kuu ya Mkoa iliyopo Mjini.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege ni duni mno. Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kimetumiwa sana katika operesheni mbalimbali za wakimbizi, hebu Serikali iongee na wafadhili hao wa wakimbizi wakiboreshe na kama haiwezekani, basi Serikali ifanya ukarabati huo.

Mheshimiwa Spika, kiwanja hicho cha Kigoma ni muhimu, kwani reli sasa ni kama inaelekea kufa kabisa, barabara nayo inazidi kubaki ni ndogo, kwani ahadi zimetuchosha. Je, wananchi wa Kigoma hawastahili kuunganishwa na Mikoa mingine ya nchi hii?

Mheshimiwa Spika, mbali na Uwanja huo, kuna Kiwanja cha Tabora, kinatia aibu! Serikali haioni?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma ambao ni Makao Makuu ya nchi, kiwanja chake ni kidogo. Nadhani hakipanuliwi kwa sababu hakuna biashara ya usafiri wa anga. Nadhani Serikali ingewaomba *Precision Air* waanzishe *route* ya Dodoma – Dar es Salaam angalau kiwanja hiki kitakuwa hai zaidi kuliko sasa kutumiwa na Ndege za Serikali na za Mashirika binafsi pekee. Tuanze sasa, yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kila kukicha njia kuu za usafirishaji zinazidi kudidimia. Umefika wakati sasa tuwahimize Watendaji wa Mashirika ya Reli, Bandari, Ndege kuwa wazalendo na wawe na nidhamu ili watimize maadili ya kazi zao katika kuendeleza mashirika hayo.

Hebu tuangalie Bandari ya Dar es Salaam, wizi umekithiri, mapato mengi hayafiki Serikalini. Uzalendo uko wapi? Tutaendelea kweli! *ATC* inaendelea kufa, reli vivyo hivyo. Je, ni kweli vyombo hivi havikuwa vikitoa faida na kama viliendeshwa kwa

hasara, sababu ni zipi? Bado naona uzalendo kukosekana. Ni sababu mojawapo! Ubinafsi umekithiri katika nchi hii, nidhamu binafsi haipo, hayo sio rahisi maadili ya kazi yatatekelezwa ipasavyo. Tusipochukua hatua Serikali itaboresha, wachache wataharibu tena.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: -** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika Wizara ya Miundombinu.

Itakumbukwa kura Rais katika ahadi zake alizotoa wakati wa kampeni na akarudia tena kauli ya ahadi hiyo aliporudi Kibaha kuwashukuru wananchi. Moja ya ahadi inayohusisha Wizara hii ni kuhakikisha kuwa Wilaya ya Kibaha Mjini ataipendelea katika miundombinu ya barabara na ataufanya kuwa mji wa kisasa unaofanana na Makao Makuu ya Mkoa. Je, Wizara imeandaa mikakati gani ili ahadi hii itimilike.

Hivi sasa Mitaa iliyoko kandokando ya barabara kuu ya Dar es Salaam kuelekea Chalinze, *accident* hutokea mara nyingi hasa Mitaa ya Visiga, Madafu na kwa Kipofu, Kongowe kwa Matias na Maili moja, haipiti wiki mbili bila *accident* kutokea na kusababisha vifo au majeruhi. Kinachosikitisha sana, mara nyingi ajali huwapata watoto, hasa wanafunzi wa *Primary School* wanapokwenda au kutoka Shule. Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi hawa kwa kuweka matuta ya barabara katika meneo niliyoyataja?

Tatizo kubwa ni madereva kutokufuata sheria ya kupunguza *speed* wakifika katika maeneo ya Vijiji (Mitaa) iliyopo kandokando ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wanafunzi wanapta shida sana ya kupata usafiri wa kwenda na kurudi Shuleni na sababu kubwa kwa wenye magari kuwakataa wanafunzi ni kuwa nauli ya wanafunzi ni ndogo na mafuta yamepanda bei. Je, Serikali kwa nini isiagize Halmashauri kutenga Bajeti ya kununua magari ya wanafunzi, yaani *school buses*?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa magari mengi yanayotoka Dar es Salaam yanakuja Kibaha Mjini kuchota mchanga. Mengi ya magari hayo yanafanya Mkataba na wenye maeneo bila kibali cha Halmashauri wala Serikali Kuu. Ili wasiweze kuonekana, wengi wanachimba mchanga usiku wa manane. Barabara zilizojengwa kwa pesa nyingi za Serikali zinaharibiwa. Je, Wizara inatushauri nini katika suala hili?

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kabisa kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Pia, niwapongeze wote wale waliochagiwa (kuteuliwa na yeye Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa katika Chama Cha Mapinduzi).

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na timu yake kwa kueleza maelezo mazuri yenye matumaini mazuri katika kitabu chake.

Mheshimiwa Spika, kwanza jambo la kuangalia ni kwamba nchi yetu iko nyuma kimaendeleo. Je, ili tufikie mafanikio mazuri tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, bila shaka kuna mambo ambayo ni ya msingi kabisa na kama tutayatekeleza, basi nchi yetu hii itakuwa ni ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo ni barabara, elimu, maji na umeme. Mimi ningeshauri kwamba kama Bajeti ya nchi yetu ni ndogo kwa kuyamudu yote kwa pamoja, basi Serikali yetu ifanye moja moja ikianza na kujenga barabara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu katika kitabu chake hiki ukurasa wa 10 kuanzia paragraph ya pili hadi 15, ameelezea mpango mzuri wenye kuonyesha mafanikio.

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo yanataka ukweli na utekelezaji tu kama yalivyoelezwa kitabuni. Haya wanayoyaeleza Mawaziri wetu ni ya mafanikio, lakini kinachohitajika ni utendaji wa kweli na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, Bandari zetu zikitengenezwa vizuri na kuwekewa wasimamizi wazuri, wenye nidhamu na waadilifu, nchi yetu itakuwa inapata mapato mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani zimeumbwa na utajiri na sio umaskini. Lakini zinakuwa na hali ya umaskini kutokana na Watendaji wa nchi husika. Wakiwa Watendaji ni waadilifu, basi nchi hiyo itakuwa ya kimaendeleo tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Miundombinu iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Miundominu pamoja na wataalam wake wote kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri haijaonyesha kipaumbele chochote katika suala zima la kuboresha Miundombinu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya nchi hii barabara ni mbovu sana, haipitiki kabisa na wananchi wetu wameendelea kuwa maskini kwa kukosa mawasiliano ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue sasa kuwa, bila kutoa kipaumbele kwenye masuala muhimu, tutaendelea kuwa maskini na kuomba misaada nje kila leo wakati Taifa hili lina raslimali nyingi, maliasili nzuri ila hazifikiki wala kutumiwa vizuri katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, barabara zinazokwenda kwenye mbuga zetu na vivutio vingine vingi katika maeneo ya kusini hazipitiki, ni mbovu sana. Hali hii inasababisha watalii kushindwa kutembelea vivutio hivyo na hivyo kukosesha Taifa fedha nyingi za kitalii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa kutambua umuhimu wa vivutio vyetu na mchango wake katika uchumi wa Taifa. Pia, kwa kutambua umuhimu wa wananchi wanaoishi kuzunguka hifadhi hizo kunufaika na maliasili zilizopo na hivyo kusaidia kupunguza umaskini na kutoa ajira, Serikali sasa ichukue juhudi za dhati kuboresha barabara hizo angalau kwa kiwango cha changarawe wakati wanavuta nguvu ya kuweka lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapata mapato mazuri sana kutokana na kilimo cha tumbaku inayosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, barabara inayotoa Urambo – Ulyankhuru yenye kilometa 60, kwa kweli ni mbovu sana na haipitiki katika vipindi vyote vya mwaka. Wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ni wakulima wazuri sana wa zao la tumbaku na karanga. Pamoja na juhudi zao za kulima, wameendelea kuwa maskini kwa kushindwa kusafirisha mazao yao kwenda Mjini kutafuta soko zuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali isaidie wananchi hawa kujikomboa kutoka kwenye hali duni kwa kuwapatia barabara nzuri waweze kuuza mazao yao kwa bei nzuri na kusafirisha pembejeo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aende kutembelea barabara hii ili aweze kujionea mwenyewe yale yanayosemwa.

Mheshimiwa Spika, sualalingine ni kukosekana kwa mawasiliano ya simu katika maeneo mengi ya Tabora Vijijini. Tabora Vijijini ni mojawapo ya maeneo yanayolima kwa wingi mazao ya Biashara na hata yale ya chakula. Ili wananchi hawa waweze kuendelea, wanaomba wapatiwe mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri kupeleka mawasiliano ya simu katika Kata ya Usinge – Urambo Magharibi ambayo ni *center* kwa wafanyabiashara wa samamki kutoka Kigoma; nguo, kutoka Malawi na mazao yanayolimwa Vijiji vyote vya Kata hiyo. Wananchi wa Usinge hawachagui aina ya mtandao wowote, wanachotaka ni kupata mnara wowote wa simu.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kuwa, nchi za nje zinazoendelea na zinazidi kusonga mbele kwa sababu wana mipango mizuri na mikakati madhubuti ya

kutatua matatizo ya wananchi wao. Hapa kwetu hilo bado halijakuwepo, ndiyo maana kila Mbunge hapa analia na ubovu wa barabara katika eneo lake. Ifike mahali sasa kuwepo na mipango mizuri ili angalau tuseme eneo fulani limekamilika, bado eneo fulani.

Mheshimiwa Spika, nashkuru tena kwa kupata nafasi hii. Ahsante.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Waziri, lakini ninaomba nichangie machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba suala la ujenzi wa barabara ya Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa lipewe kipaumbele kujengwa kwa kiwango cha lami kama Rais alivyoahidi katika nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Dodoma – Zamahelo – Kwamtoro – Singida ni muhimu. Hivyo ninaiomba Serikali itenge fedha za kutosha ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana Makampuni ya Simu za Mkononi kwa jitihada kubwa zinazofanywa kusambaza huduma ya simu za mkononi katika Wilaya ya Kondoa. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo hayajafikiwa hadi sasa. Pamoja na minara michache kujengwa kati ya Dodoma na Kondoa, sehemu kubwa ya njia toka Dodoma hadi Kondoa hazipati huduma ya simu za mkononi. Aidha, katika barabara ya Dodoma – Zamahelo – Kwamtoro – Singida, pamoja na mnara mmoja kuanza kujengwa katika Kijiji cha Farkwa, tunaomba ijengwe minara ya kutosha ili mawasiliano yapatikane njia yote toka Dodoma – Zamahelo – Kwamtoro – Singida.

Baada ya mchango huu mdogo, ninaomba kuunga mkono Bajeti ya Wizara ya Miundombinu.

**MHE. ERNEST G. MABINA, MHE. KABUZI F. RWILOMBA, MHE. WILLIAM M. NGELEJA NA MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu – Mhe. Dr. Milton Mahanga, ahsante. Tumepokea maelezo yako mazuri, nasi tunayatunza moyoni, rohoni na akilini mpaka hapo utekelezaji utakapofanyika japokuwa ni mlolongo mrefu wa kukatisha tamaa. Wakati tunasubiri barabara ya lami, hivi sasa barabara ya Usagara - Geita ni mbaya kuliko barabara zote duniani. Tunadhani uliona wakati ulipokwenda Chato.

Kuna mpango gani wa kutusaidia angalau kwa vumbi tu, siyo tu hadi maumivu ya viungo. Sisi ni ndugu zako, tusaidie.

**MHE. MWINCHUOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, pole kwa kazi. Niliahidiwa kupatiwa orodha ya watakaofidiwa barabara ya Kilwa na Mheshimiwa Waziri. Naomba kupatiwa orodha hiyo kwa umuhimu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kujenga gati la Kyamkwikwi mwaka 2005/2006 haikuwa. Sikuona ilipoandikwa. Pengine imo, naomba nisaidiwe kuiona. Kama halimo, pia naomba nisaidiwe maana wananchi wanalijua hilo. Ahsante.

**MHE. GEORGE B.SIMBACHWENE:** Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, shikamoo *Brother*. *Budget* yenu sio nzuri sana. Iko dosari katika mgawanyo wa pesa za barabara. Ilani ya Uchaguzi imeeleza barabara mbalimbali, lakini sio haki barabara ya Marangu -Tarakea - Rongai -Kamwanga Shilingi bilioni 17 wakati barabara ya Dodoma - Iringa Shilingi milioni 900. Hapa ndipo tatizo linapokuja.

Mheshimiwa Spika, nitachangia na siridhishwi na hili. *I need your advise.*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA, MHE. ERNEST G. MABINA, MHE. WILLIAM M. NGELEJA NA MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, pole na kazi. Tumeletewa kipande cha karatasi kinachoonyesha tangazo la *The Guardian* ya tarehe 01 Julai, 2006. Tangazo hilo limetusikitisha, kwani halionyeshi kuwa barabara ya Usagara - Geita ina mwelekeo wa kutengenezwa. Tangazo linaonyesha kuwa ni kwa ajili ya *Consultancy Service,* wakati kazi hiyo ilishafanyika tangu mwaka 2004 ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu. Kwa nini kazi hiyo inarudiwa wakati ilikwishafanywa na kampuni ya Afrika ya Kusini?

Mheshimiwa Spika, tulitegemea ingekuwa *design* na *build* au *contractor* angekuwa amepatikana ili kuwepo na *Consultancy Services.*

Mheshimiwa Spika, tunaona tangazo hilo ni kurudia iliyokwishafanyika na kuzidi kupoteza muda. Hatuielewi Wizara ina maana gani. Inatusikitisha. Tafadhali tushauri**.**

**MHE. BALOZI KHAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Spika, msingi wa maendeleo ya nchi yetu ni Sekta hii ya Miundombinu, usafiri, usafirishaji na mawasiliano ya aina yote vina umuhimu wa pekee katika kuipeleka nchi au watu wake mbele.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera umebaki sana nyuma katika Sekta hii ya Miundombinu. Lipo *Ziwa Victoria* ambalo kwa usafiri, usafirishaji, biashara na kadhalika, linasaidia sana. Lakini Serikali haikufanya jitihada za kutosha. Ipo meli ya *MV Victoria* ambayo inazaidi ya miaka arobaini tangu imekuwa ikitoa huduma katika *Ziwa Victoria*. Lakini kutokana na ongezeko la watu na biashara imekuwa ni muhimu kuongeza vyombo vya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kulitazama hili. Watu wa Kagera, *MV Bukoba* ilipozama moja kwa moja walitegemea Serikali ingejitahidi kuweka meli nyingine. Bahati mbaya hii haikufanyika. Sasa Serikali kwa kutoweka meli nyingine

imesababisha hali ya usafirishaji na usafiri kuwa ngumu sana kati ya Mkoa wa Kagera na sehemu nyinginezo za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke meli nyingine. Kutofanya hivyo kumesababisha vifo vingi zaidi vya watu na kupotea kwa mali. Watu wamekuwa wanatumia mitumbwi mikubwa na hata meli ndogo za watu binafsi ambazo zimechoka na kuchakaa.

Mheshimiwa Spika, *Speed boats* kati ya Bukoba na Mwanza hazifanyi kazi tena kwa sababu ya kuchoka na kuchakaa, hivyo kusababisha hatari kubwa ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Kagera inahitaji Uwanja wa Ndege. Bukoba Mkuni kumekuwepo na kiwanja kidogo cha zamani na wakati wa mvua kali, kina hatari sana. Hatuelewi kwanini Serikali haikubali kutoa kipaumbele kutengeneza Uwanja wa Bukoba. Mwezi Aprili, Waziri Mkuu - Mheshimiwa Lowassa alifanya ziara ya kikazi. Wakati anamaliza ziara yake, ndege yake ilibidi kupunguza kwa idadi kubwa Wasaidizi wake maana ndege isingeweza kuvuka kutokana na hali mbaya ya Uwanja huo.

Hali kadhalika alipokuja Rais, Mheshimiwa Kikwete, ndege yake ilibidi ipunguze sana msafara wa Mheshimiwa Rais wetu, kwa sababu ya hali mbaya na ya hatari ya Uwanja huu. Naomba Serikali ifanye kila liwezekanalo kutengeneza Uwanja huu ili kusaidia katika usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipunguza Serikali kwa kutengeneza barabara kuu kati ya Bukoba na Masaka, Kampala (Uganda) ambayo imesaidia sana katika biashara, lakini pia usalama mpakani. Hapa natoa hongera, lakini naomba barabara kuu ya Bukoba, Biharamulo, Mwanza nayo ikamilishwe ili kuwapa Wana-Kagera fursa ya kusafiri kufanya biashara kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, barabara ni kiungo muhimu sana Vijijini na nchi mzima. Tunaishukuru *TANROAD* na Mifuko ya Barabara kwa kutengeneza barabara zetu. Ila sasa kuna tatizo moja, mfuko wa barabara hujali kutengeneza barabara zilezile zilizo katika mpango wake, hawajaweza kuweka fursa ya mipango mingine ya utengenezaji wa barabara mpya. Hii ni kero kubwa sana.

Barabara zinazoachwa kutengenezwa ni za kupitisha mazao ya wakulima Vijijini. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iruhusu *Council* kuweka mipango mipya ya utengenezaji wa barabara mpya. Sisi Wilaya ya Ruangwa tuna kero kubwa kwa wananchi kwa kutotengenezwa barabara zaidi ya zile zilizopo katika mpango wao wa Mfuko wa Barabara za Mandawa - Mputwa kilomita 27, Luchegelegwa - Nandanga kilomita nane, Manokwe - Chienjele kilomita tisa, Namichiga - Matambarare, Miheweni na vilevileMilola - Mandawa kilomita 30. Karibu shilingi 225,950 zinahitajika.

Vilevile barabara za Ruangwa – Nanjilinji – Kilwa, wananchi wamejitolea kujenga daraja la Shilingi milioni 200 ili barabara ipite hapo. Tumeomba tusaidiwe barabara hizo. Pia, suala la ukaguzi wa madaraja ufanyike mara kwa mara ili kuondoa idadi za ajali zinazotokea barabarani.

Lingine ni barabara za *OPAKI/HIPIC*. Msaada wa nchi maskini, Barabara ya Nanganga - Ruangwa na Nanganga - Nachingwea zitengenezwe.

Sisi Kusini tuna matatizo mengi ya miundombinu na ninadhani matatizo haya yote yanatokea kwa sababu zile barabara ambazo zilikuwa zitengenezwe na mradi wa *Mtwara Corridor*, hadi leo bado. Ninataka nitaje barabara zote zilizomo katika *Mtwara Corridor* na miradi yote kama ifuatavyo:-

Madhumuni ya Mtwara *Corridor* nchini ni kuondoa umaskini katika maeneo ya pembezoni mwa Tanzania ambao bado wapo nyuma, kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Kuwa na mawasiliano na nchi za Kusini mwa Afrika (Malawi, *Mozambique*, Zambia na Tanzania; kuendeleza ujirani mwema kwa mawasiliano mazuri; kuendeleza Sekta ya Kilimo, Utalii, Miundombinu na Uchimbaji Madini nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Miradi kadhaa ilipangwa ili itekelezwe katika *Mtwara Corridor.* Miradi hiyo ni uchimbaji wa mkaa wa mawe, mchuchuma na Katewaka; Uchimbaji wa Chuma/Liganga ambayo ndani yake kuna *TITANIUM* na *VANDANIUM;* kutekeleza miundombinu/barabara toka Manda hadi *Mchuchuma Project* kwa ajili ya kusafirisha umeme kutoka *Mchuchuma Village* na kwenda kuunganisha na umeme wa *grid* ili utumike katika machimbo ya *Lake Victoria* na Mikoa ya *Mtwara Corridor;* kuendeleza Bandari za Mtwara, Manda, *Mbamba Bay*; Lindi, Kilwa na Bandari kadhaa muhimu na kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Mtwara, Songea na Njombe.

Miradi mingine ni Barabara ya Mchuchuma hadi Mlimba; Daraja la Umoja wa Tanzania na *Mozambique*; Barabara ya Dar es Salaam, Mtwara Kibiti, Lindi Mtwara hadi *Mbamba Bay*; Barabara ya *Mbambabay* hadi Mtwara ya Reli; Barabara ya Mtwara – Songea – Manda ya Reli; Reli ya Manda – Mchuchuma –Mlimba; Kupatikana kwa maji safi na ya uhakika ya salama kwa Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro, na Mkoa wa Pwani; *Telecommunication* – Mawasiliano ya mikoa yote ndani ya *Mtwara Corridor*; Reli ya Tunduma – Sumbawanga – Kassanga na barabara ya gari kuboreshwa.

Mradi wa umeme wa *Stieglers Gorge Hydro Power Project*. Miradi ya Gesi ya *Mnazi Bay* na Songosongo.

Kwa vile miradi ya *Mtwara Corridor* haikutekelezwa kwa muda muafaka, sasa Mikoa hiyo bado ipo nyuma na imepata jina la Mikoa ya Pembezoni, iliyo nyuma. Tunamshukuru Rais wetu Mheshimiwa Kikwete kwa kugundua kuwa Mikoa hiyo ni maskini na iko nyuma na sasa ameamrisha kuendelezwa kwa Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mikoa ya Kusini ipo nyuma hasa Mtwara na Lindi? Mtwara na Lindi ni mikoa ambayo ipo pembezoni mwa Tanzania na ipo nyuma kwa maendeleo. Tatizo kubwa ya Mikoa kuwa nyuma ni kama ifuatavyo:-

(1) Sera za Kikoloani, Wakoloni ambao walikuwa wanatawala kabla ya uhuru, waliifanya Mikoa hiyo ni *Reserve* kwa ajili ya kupata manamba, kupata watu wa kufanya kazi ,vilevile sehemu ya kupata mazao (wakulima wengi) kwa hiyo, wakoloni hawakutaka kuendeleza Mikoa hiyo na walifanya watu wengine wasiende kuwekeza. Kwa hiyo, wakaweka vipingamizi ili watu wasiende huko kwa kuacha kutengeneza barabara zote ili wananchi wa Mikoa hiyo wasiende na wasifikiwe na wawekezaji kwa maslahi ya Wakoloni.

(2) Mawasiliano Duni ambayo yalizuiwa na mito, ukiwemo Rufiji na milima, ukiwepo likumburu, ilizuia watu wasije Kusini kufanya maendeleo kwa kuogopa kupita.

(3) Baadaye Mikoa ya Lindi na Mtwara ilitumiwa kama sehemu ya mafunzo ya vita vya ukombozi. Kwa hiyo, ili watu wengine wasione shughuli, basi walizuia shughuli za miundombinu isiwepo. Nchi kama Zimbambwe, Afrika ya Kusini na Msumbiji zilikuwa Tanzania ya Lindi na Mtwara.

(4) Njia ya Reli kufika *Mbamba Bay:* Barabara ya Mtwara hadi *Mbamba Bay* hadi barabara ya Kibiti - Lindi - Manda, zingekuwepo, tungeweza kuunganisha na Mikoa mingine.

(5) Shule za Sekondari kutaifishwa na kuingia wanafunzi kutoka nchi nzima, Sera mpya ya Elimu – Sekondari kutaifishwa ilifanya Shule za secondari kubwa kutaifishwa na hivyo kuingiza watoto toka Mikoa mingine na kuwaacha watoto wa Kusini. Mikoa imekaa miaka mingi bila kuendelezwa kwa sababu hizo.

Kwa hiyo ikawa tumetengwa kwa miaka mingi na wananchi wa Kusini, waliendelea kuchukuliwa na kwenda manamba Tanga, Zanzibar, katika mashamba ya mikonge kitendo ambacho sio kizuri. Kutengwa kwetu watu wa Kusini tukapata jina la Senderera, Senderera ni mtu au mtoto au nchi iliyotengwa au isiyofadhiliwa au kusaidiwa. Ni neno la kiingereza na kifaransa.

Maoni, kwa vile Kusini ipo nyuma kwa sababu za kimsingi na wala sio uvivu au vinginevyo, basi upendeleo maalum ufanyike ili kuendeleza Mikoa hiyo na sio kutuacha nyuma.

Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kugundua kuwa Mikoa hiyo ipo nyuma na akaagiza kuwa Mikoa hiyo iendelezwe. Tunatarajia katika Bajeti hii Serikali ituangalie kwa macho mawili ili nasi tukombolewe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi ahsante sana na hasa kwa kuzingatia muda. Sasa ni zamu ya majibu kutoka kwa Wizara husika. Nitamwita Naibu Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga. Mheshimiwa Naibu Waziri unazo dakika 13.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Lakini nikupongeze pamoja na Wasaidizi wako kwa kazi nzuri mnazofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza vilevile Mheshimiwa Rais kwa kupata Urais kwa kishindo na Uenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Vilevile natoa pongezi kwa wote ambao tumepata nyadhifa mbalimbali katika Serikali, katika Chama cha Mapinduzi na ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, lakini nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii na mimi naahidi kwamba nitafanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, niwashukuru sana Wapiga kura wa Jimbo la Ukonga kwa kuniweza kunirudisha katika Bunge hili kwa mara ya pili mfululizo na kwa kunipa kura za kishindo na kuniwezesha kuvunja rekodi yangu mwenyewe ya mwaka 2000. Mwaka 2000 walinipa kura 83,000 lakini mwaka jana wakanipa kura 127,000 na wakaweza kumpa Mheshimiwa Rais kura nyingi kuliko Jimbo lolote, kiasi cha kura 144,000. Haijapata kutokea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nichangie hoja hii kwa kuiunga mkono kwanza kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema muda mfupi, kwa hiyo nitajibu baadhi ya maswali na nina hakika mengine Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mwenzangu watayajibu. Lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, wote watapata majibu yao kwa maandishi hata kama tutakuwa tumeshindwa kupata muda wa kuyajibu hapa kwenye *podium*.

Mheshimiwa Spika, nianzie kwenye hoja za Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Alizungumzia barabara zinazotengenezwa katika kiwango cha chini kwamba zinaharibika mapema. Ukweli ni kwamba, kwa sababu tu ya ukosefu wa hela, hatuwezi kujenga barabara zote kwa lami. Tunazijenga kwa viwango mbalimbali na zile barabara za udongo kwa vyovyote zinaharibika mapema. Lakini pale uwezo utakapokuwepo tutazijenga kwa kiwango cha juu.

Vilevile Msemaji wa Upinzani alizungumzia kuporomoka kwa majengo kama ilivyotokea Dar es Salaam. Sasa tunasema, kweli wadau ni wengi, kuna wabunifu wa majengo, Wahandisi, Halmashauri na waendelezaji wenyewe. Tunaendelea kusisitiza kwamba kila mmoja atekeleze wajibu wake. Lakini vilevile Serikali imeshaona

mapungufu hayo na hivi karibuni imeteua Tume Maalum ya kuangalia matatizo hayo, nadhani watatoka na njia ambazo zitatuwezesha kupata ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaandaa rasimu ya Sheria ya Majengo ambayo mwishoni mwa mwaka huu labda tunaweza tukaileta Bungeni. Hii vilevile itaweza kusaidia katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, pia Kambi ya Upinzani ilizungumzia miradi isiyokamilika kutokana na kuibiwa mafuta na kadhalika. Nadhani hili ni suala la usimamzi tu kati Wizara yetu na Makandarasi wahusika. Tutazingatia. Alizungumzia mpango wa *network* ya barabara zote nchini na sisi tunasema kwamba mpango huo tunao tuna *Ten Years Transport Sector Programme* ambao kesho utajadiliwa na wadau mbalimbali wakiwemo na wafadhili kutoka nje na hii itatupa dira kuona sasa tunafanyaje katika kuunganisha barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani vilevile alizungumzia suala la msongamano wa magari Dar es Salaam na kwamba tuwe na boti za majini. Hili limeshachukuliwa hatua. Kuna Wakandarasi wawili ambao baada ya miezi sita wataanza kazi hizo kati ya Magogoni na Kigamboni na vilevile Magogoni kwenda mpaka Bagamoyo. Lakini katika kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, kuna Kamati ambayo imeshapendekeza barabara za kukarabati na za kutengeneza katika Jiji lile. Zinatakiwa kama Shilingi bilioni 8.3 na katika barabara hizo zilizoainishwa, tutakwenda kwa awamu. Vilevile masuala ya taa za barabarani na mpango wa mabasi yaendayo kwa kasi, yote hayo ni katika kuangalia kwamba tunakabili hilo tatizo.

Mheshimiwa Spika, Vivuko vya Alina Kigamboni, Kigogo - Busisi na kwa kweli na vingine vyote kwamba vimekuwa vikiharibika, hii ni kweli. Lakini tumekuwa tukijaribu kutengeneza vivuko hivi mara kwa mara na tuna mpango ambao umeelezwa na baadaye naweza nikatawanya *copy* mwone jinsi ambavyo vivuko vyetu tunafanyia matengenezo. Lakini kivuko cha Alina, tutanunua *engine* mbili. Lakini vilevile tutafanyia ukarabati vivuko vya Kigamboni na Sengerema. Kwa sasa hivi tulitangaza zabuni lakini hawakujitokeza wazabuni na tutangaza tena mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Usiwe Kupe hatunacho tena kilishauzwa toka mwaka 2001. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu kutochanganya bidhaa za petroli, chakula na abiria katika vivuko. Ushauri huo tumeuchukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa ni sera ya kuuza nyumba. Labda Mheshimiwa Waziri atalielezea zaidi. Lakini nieleze tu kwa kifupi kwamba tulikuwa na sera ya kuuza nyumba chakavu zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali na nyumba hizo zilishauzwa zote. Kwa hiyo, hilo nalo wala hakuna sababu ya kuendelea kulizungumzia. Kwa hiyo, tunachozungumzia sasa ni kwamba baada ya kuuza zile nyumba tunafanya nini? Kwa sababu kuna watumishi wanaostahili kupewa nyumba kwa mujibu wa mikataba yao ya ajira kama Wakuu wa Wilaya na wengine lazima tuwajengee

nyumba na hizo nyumba hazitauzwa sasa. Hizi nyumba ambazo tutawajengea hawa ambao wanastahili na kuuziwa nyumba zitakuwa *type quarters.*

Mheshimiwa Spika, lakini sera nyingine ni hii ya kujenga nyumba kwa ajili ya kuwauzia Watanzania. Nasi kama Wizara ya Miundombinu, *TBA* kazi yetu itakuwa ni kuwajengea wale watumishi wa Umma na *National Housing* watajenga nyumba kwa ajili ya Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya Mheshimiwa George Lubeleje, alizungumzia Mfuko wa Barabara kutotosha. Hii inaangaliwa. Lakini itabidi tutathmini ubovu wa barabara za Wilayani na hata zile ambazo zinamilikiwa na Wizara yetu kabla ya kufikia kwamba Serikali iongeze kiwango gani kutoka asilimia 30 kwenda asilimia 40 au asilimia 50 au vipi itakavyoamuliwa. Kuna barabara alizozitaja, nyingine ni za Wilaya, aendelee kusisitiza Halmashauri ya Wilaya iweze kuzitengeneza. Kuhusu Daraja la Kitala, sisi tulisaidia ile *lift.* Lakini kwa kweli lile ni daraja la Wilaya, nadhani angeweza kufuatilia. Hata barabara ya Ngulwe mpaka Fufu vilevile ni barabara ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hizi barabara za Dodoma - Singida, Nangurukuru - Lindi na Mingoyo zinaendeleaje, nadhani kinachotakiwa hapa ni *time frame*. Niseme tu kwamba, barabara ya Dodoma - Manyoni, tunadhani itakamilika mwishoni mwa mwaka kesho pamoja na ile barabara ya Nangurukuru kwenda Mbwemkuru. Ile barabara ya Manyoni - Singida na ile Mbwemkuru mpaka Mingonyo mwisho mwa mwaka kesho kutwa. Ndiyo makisio yetu ambayo tunayo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakandarasi wasio na uwezo wasiteuliwe, kwa kweli tunatumia Sheria ya Manunuzi. Nadhani tutaendelea kusisitiza na kuangalia kwamba ile sheria tunaifuatilia vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii alizungumzia barabara ya Manyoni - Itigi na ni kweli ilizungumziwa na wengi. Tabora -Nzega tunasema tumetenga Shilingi milioni 535 kwa ajili ya usanifu wa kina. Lakini barabara hiyo inayoendelea mpaka Mbeya itaanza kutengenezwa mwaka huu wa fedha kuanzia Mbeya mpaka Makorongosi na fedha zipo Shilingi bilioni 11 kwa ajili ya hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi hazikutendewa haki, nadhani hii sio kweli. Ukipiga hesabu Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi na nime-*list* hapa barabara nyingi zinazoendelea kutengenezwa katika hatua mbalimbali za usanifu, za ujenzi zinafika karibu Shilingi bilioni 76 kwa ujumla kwa Kanda zote mbili. Ni hela nyingi labda, kuliko Kanda nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwamba miradi itekelezwe kikanda ili kutenda haki, hiyo ni kweli kwa sababu tuna Kanda tisa ambazo tunazingatia katika kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Eustace Katagira alizungumzia barabara za Bugene Kaisho, Mrongo kwamba Mkandarasi azingatie ubora, tumezingatia hilo. Zile

barabara za kupandishwa daraja, nadhani nimeshalisema, tutaliangalia katika Sheria mpya ya Barabara. Kuhusu barabara ya Kyaka-Kayanga kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami, tatizo ni fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah alizungumzia daraja la Mpiji kwamba haliunganishi Dar es Salaam na Tanga. Linaunganisha Dar es Salaam –Tanga kama utapitia Bagamoyo. Lakini ni ukweli kwamba huko mbele kuna daraja la Makurunge na Kisauke ambalo kwa kweli litafanyiwa matengenezo. Kwa kweli ile barabara ya Bagamoyo kwenda Sadani tayari *feasibility study* imetengewa Shilingi milioni 400 na daraja la Makurunge vilevile linafanyiwa *design* na bilioni moja imetengwa. Daraja la Chomba linakwenda polepole, tutazingatia hilo. Lakini wizi wa vifaa nadhani mkandarasi tu awe makini.

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Pangani tayari kimesimamishwa na kinatengenezwa kwa sasa. Ila tunasema tu habari nzuri, ni kwamba jana tayari Benki ya Dunia imetoa *no objection* kwa ajili ya kununua kivuko kipya cha Pangani. Kwa hiyo, hili suala nadhani sasa tutakuwa tumelimaliza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanne Mchemba nadhani tumeshazungumza suala la Itigi, nimelijibu. Mheshimiwa Bujiku Sakila barabara zake alizungumzia kwamba hela ni kidogo kuliko urefu wa barabara, ni kwamba tunakwenda kwa awamu, siyo kwa barabara nzima, tunakwenda kilomita chache kutokana na hela.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi alizungumzia barabara zake na kwa kweli tumezingatia barabara ya Mbuzi - Kasambala na tutafanya usanifu wa daraja la Momba na zile barabara nyingine vilevile zitaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto tumezingatia ushauri wake kuhusu kutumia Shilingi milioni 800 kutoka Mwandinga kwenda Manyovu. Mheshimiwa Said Arfi alizungumzia barabara ya Sumbawanga - Mpanda. Fedha zipo katika Mpango wa *PMMR,* zitaendelea kutengenezwa. Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, tumepata suala la matatizo ya barabara kule Kigamboni, tutajaribu kuangalia kwamba umwagiliaji wa maji hautaathiri barabara ile.

Mheshimiwa Ruth Msafiri tumepata vilevile mawazo yake, lakini hawa Wahandisi tunajaribu kuwapa elimu, kuna mipango ambayo inafanywa na *Engineering Registration Board* ya kuwafundisha karibu Wahandisi 712. Tayari tunasisitiza wale wa Wilayani na wenyewe wahakikishe kwamba wanakwenda kwenye mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga aliuliza kwa nini barabara ya Itigi - Manyoni tena? Nadhani hili limeshazungumziwa. Mheshimiwa Juma Njwayo, tumeweka fedha nyingi kule Tarakea, nadhani litajibiwa vizuri. Lakini kuna maeneo ambayo tumeweka fedha nyingi zaidi kuliko hata kule kama kule Kanda ya Ziwa na vilevile hata barabara ya Dodoma - Singida tumetenga Shilingi bilioni 21 na barabara ya Nangurukuru - Mingoyo tumetenga Shilingi bilioni 22.2.

Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, tumepokea mawazo yako ya *connectivity* ya barabara, tutazingatia. Mheshimiwa Iddi Azzan, nadhani tumeona, lakini kwa kweli kwenda Soko la Tandale kwa sasa uwezo wa fedha haupo. Aidha, upo, onana na Manispaa ya Kinondoni. *(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, naomba tena kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kabisa hii ni moja ya zile Kanuni ambazo zinatupa shida. Kwa sababu ni vizuri Serikali ipewe nafasi ya kutosha kuweza kujibu. Lakini sasa hivi tunafungwa, lazima wote wawe ndani ya saa moja. Mnasemaje? Tuitengue sasa hivi! Hapana. Tumechelewa kidogo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ukiitengeua tutashukuru sana. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima wa Afya njema na kuweza kukutana leo hii Bungeni kujadiliana juu ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni mara yangu kwa kwanza, niruhusu nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunipa nafasi nimsaidie katika Wizara hii mpya ya Miundombinu. Kwa niaba ya familia yangu, naomba azipokee shukrani zangu za dhati na ninaahidi kutenda kazi yangu kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Amani Karume kwa ushindi alioupata. Nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa kwa dhati kabisa kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu. Nimwombe tu, asisite kunionya pale atakaponiona sifanyi kazi zangu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Spika wa Bunge letu la Tanzania. Nakiri wewe ni mtu wa viwango na uadilifu na uchapa kazi wako unanifanya mimi binafsi siku zote nikisimama hapa nijipime iwapo ninakidhi kweli viwango vilivyowekwa. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wenzangu kwa kufanikiwa kuchaguliwa na Wapigakura wao katika Majimbo yao. Mategemeo ya Wapigakura wetu ni kukidhi matatizo yao ambayo naamini kwa ushirikiano wa karibu, Wizara ya Miundombinu itaendelea kuwaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wenzangu wote waliopata nafasi mbalimbali katika Chama cha Mapinduzi na Serikali na ninaahidi ushirikiano wangu kwao na kweli mimi ni mmoja ambaye ninahitaji sana busara zenu. Muda ulionipa ni dakika 12 na Sekta ninayoisimamia ina *sub-sector* 12, labda nitakuwa na dakika moja. Kama sitakidhi mahitaji ya Wabunge kama wenzangu, nitajaribu na mimi kuandika na kuwapa Waheshimiwa Wabunge yale yote waliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu ni chachu ya ukuaji na uendelezaji wa uchumi wa nchi hii na inachangia kwa kiasi kikubwa kumwondolea mwananchi umaskini iwapo tu itawezeshwa kutimiza malengo na matarajio yake. Mwananchi mnyonge wa Kijijini anategemea nguvu zake kwa kutumia jembe la mkono, anaweza kusaidia kuboresha shughuli zake za uzalishaji wa mazao kwa kutumia Wizara hii, pindi atakapowezeshwa kupata mbolea na pembejeo kwa wakati ambazo zitamfikia kwa njia ya reli, barabara, meli au kwa namna nyingine ya usafirishaji na pia kupata taarifa za hali ya hewa kwa wakati muafaka ili aweze kutayarisha mashamba yake na kubwa zaidi ni kumwezesha kusafirisha mazao yake mpaka sokoni kwa wakati ili nguvu zake na jasho lake zisipotee bure na apate tija na aweze kubadilisha hali ya maisha yake na ya jamii.

Mheshimiwa Spika, ulimwengu sasa umebadilika, dunia imekuwa kama Kijiji. Teknolojia ya mawasiliano na habari ni nguvu nyingine ya kumsaidia mwananchi popote alipo. Kuendelea kwa nchi kunapimwa kwa kuona ni namna gani wananchi wake ana uelewa na mwamko wa mambo ya kiulimwengu kwa kutumia taarifa mbalimbali za bure zinazopatikana katika mitandao mbalimbali. Ujenzi wa miundombinu wa Viwanja vya Ndege utakuwa na manufaa kwa wananchi katika maeneo husika pale tu watakapokitumia Kiwanja hicho cha Ndege kikamilifu kwa kuzalisha mazao na kuyasafirisha nje ya nchi. Hivyo basi, wakati umefika wa kutazama mbele na kupanga ipasavyo kwa vile Viwanja vya Ndege ambavyo vimeboreshwa vinasaidiaje jamii katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumejenga viwanja vya ndege na tutaendelea kujenga Kiwanja kikubwa cha Ndege cha Songwe Mbeya. Je, wananchi wa Mbeya na Vitongoji vyake na Mikoa ya jirani wameelimishwa kiasi gani kupokea ujio wa Uwanja huo wa Ndege kikamilifu utakapomalizika? Je, Sekta mbalimbali zinazohusika kwa mfano Kilimo na nyinginezo zimewaandaa vipi wananchi kujiandaa na uzalishaji wa mazao gani kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi? Je, wenzetu wa Masoko wamefanya utafiti na kuona mazao gani sasa yenye tija na ambayo yanaweza kulimwa na kupata soko zuri nje ya nchi? Haya yote ni maandalizi na yanahitaji ushirikiano wa pamoja. naamini Waheshimiwa Wabunge wenzangu watapata changamoto tosha ya kuwaandaa wananchi na Wapigakura wao umuhimu wa kujishughulisha na kujiweka tayari kwa matumizi ya Uwanja huo mkubwa wa Ndege wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, sasa niruhusu nijibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, nitakuja kwenye Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia wamefurahishwa na huduma za mawasiliano ya simu za mikononi Mijini na Vijijini. Wamepongeza sana *Celtel* na Kampuni nyingine ambazo zinatoa huduma. Tunawashukuru na pongezi tunazipokea na ninaahidi kwa yale maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwamba hazijafika huduma za simu za mikononi, tutawahimiza wenzetu wafikishe huduma hizo huko. Nia ni mawasiliano yafike Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Uchukuzi, tutakuja kwenye Viwanja vya Ndege. Naomba nizungumzie tu Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka huu wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, tuna viwanja vingi vya ndege, lakini nitasema vichache. Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tutaendelea na ukarabati wa maegesho ya ndege na barabara, viungio vyake na pia hapa tutapeleka gari moja la Zimamoto. Kiwanja cha Songwe tunaendelea na ujenzi wa maegesho, vifaa na mitambo pamoja na mfumo wa maji kiwanjani na tutakamilisha ujenzi wa majengo ya kiwanja hicho. Kiwanja cha Kigoma, tutafanya ukarabati wa jengo la Ofisi pamoja na mfumo wa umeme, ujenzi wa uzio wa usalama wenye urefu wa kilomita tatu na ukarabati wa njia ya kutua na kuruka ndege na tutapeleka gari moja la Zimamoto. Kiwanja cha Manyara, tutajenga vilevile uzio wa kilomita moja na tutakarabati njia ya kurukia ndege.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Tabora, tutakarabati barabara ya kurukia ndege na tutafanya upembuzi yakinifu na usanifu. Hii ni kwa ajili ya kutafuta *Funding Bank* ambao wameonyesha nia ya kukisaidia hiki Kiwanja cha Ndege na tutapeleka na gari la Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, tutajenga uzio wa kilomita moja na ununuzi wa *generator* na ujenzi wa barabara ya kuingilia ndege. Kiwanja cha Ndege Arusha, tutapeleka gari la Zimamoto, tutajenga Ukumbi wa kufikia abiria, Kituo cha Polisi, *runway,* usanifu wa michoro ya *apron* mpya na barabara ya kuingia kiwanjani. Ukarabati wa njia ya kutua ndege iliyobaki tuna nia pia ya kuimalizia na ujenzi wa uzio wenye urefu wa kilomita mbili.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ambacho kimezungumziwa sana kwa uchungu kabisa na Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza, tutanunua darubini maalum, tutafanya ujenzi wa barabara ya kuzunguka kiwanja cha ndege, ujenzi wa uzio wa usalama wenye urefu wa kilomita mbili na matengenezo ya maegesho na viungio. Mazungumzo haya Mheshimiwa Waziri amefikia mahali pazuri na tunategemea ufadhili wa wenzetu wa *BADEA*. Tunawategemea hao watafika hapa kwa ajili ya kufanya shughuli zao tarehe 7 Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, *BADEA* watatengeneza *terminal building*, *Tax ways* na *apron* na wata-*extend* kidogo Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza, sisi nia yetu ni kufanya biashara na hii ndiyo kazi ambayo mimi nimepewa. Tutapeleka na gari la Zimamoto kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, tutakarabati tanki la maji na *fire hydrants* na ununuzi wa *generator*, tutajenga uzio kwa ajili ya usalama wenye urefu wa kilomita mbili na tutapeleka na gari la Zimamoto ambalo limeshafika Dar es Salaam hivi sasa kwa ajili ya *fire tender*. Haya yote tunafanya, lengo ni kuboresha Viwanja vya Ndege viweze kuchangia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, *World Bank* wamekubali kusaidia kufanya *consultant,* kufanya *design* na *tender documents* kwa Viwanja vya Ndege vifuatavyo: Tabora, Kigoma, Arusha, Mafia na Bukoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, tutakarabati jengo la abiria, tutafanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa msaada huo wa *World Bank* na uzio na kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi.

Mheshimiwa Spika, katika Kiwanja cha Ndege cha Musoma, tutafanya upanuzi na ukarabati wa jengo la watu mashuhuri yaani *V.I.P*, ujenzi wa uzio na hii kazi itafanywa. Lakini katika Mpango wa *Transport Sector Investment Programme,* Viwanja vya Ndege vifuatavyo viwekwa katika mpango huo. Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Lake Manyara, Mafia, Mtwara, Tabora, Bukoba, Dodoma, Kigoma, Moshi, Shinyanga, Musoma, Tanga, Singida, Zanzibar, Songwe na *KIA*. Namwomba Mheshimiwa Mbunge wa Mafia asifunge, kwa sababu tunayo nia ya kutengeneza Kiwanja cha Ndege cha Mafia.

Katika Kiwanja cha Ndege cha Singida, pia tutajenga njia ya kurukia na kutua ndege na maegesho na viungio vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga tunafanya upimaji na usanifu wa barabara ya kurukia ndege. Hiki ni kitu ambacho kinaendelea na tunategemea kuingiza kwenye hiyo *Transport Sector Investment Programme* ambapo kesho tunategemea kuzungumza na Wafadhili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba uniruhusu niseme machache juu ya *TRC*. Maswali mengi tu yameulizwa kuhusu ubinafsishaji wa *TRC* kwamba maslahi ya Taifa yazingatiwe, malipo ya wafanyakazi wa *TRC* watakaopunguzwa yawekwe kwenye mkakati mzuri ili kuepuka usumbufu; sisi tunasema haya yote tunayachukua na tutayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na swali la ujenzi wa *optical fibre* kati ya Dodoma na Dar es Salaam au Dodoma na Tabora kwamba umefikia wapi? Je, mkonga huu unasaidia vipi Shirika na umeingiza kiasi gani mpaka sasa na sehemu zipi zitafaidika na mkonga huu? Mradi huu kwa kweli ulitakiwa umalizike mwezi Machi, 2007. Lakini umeshamaliza mwezi Juni, mwaka huu wa 2006, miezi minane kabla ya muda uliopangwa. Mkonga huu umesaidia sana kuboresha mawasiliano ya treni kati ya Dar es Salaam na Tabora pamoja na shughuli za kiutawala. Vilevile, mipango inafanywa ili *access capacity* iweze kuwa *utilized* ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kubinafsisha *TRC* kati ya Serikali na Mkodishwaji wamekubaliana nini? Tunasema mkodishwaji ana *rights* na baada ya Serikali kwenda kuangalia shughuli za uendeshaji walizozifanya huko Colombia na Msumbiji, tumejiridhisha kwamba wanao uwezo wa kuendesha shughuli za reli hapa nchini.

Mkataba umeainisha maeneo ambayo yataboreshwa katika upande wa huduma na upande wa miundombinu na majadiliano na Serikali na mkodishwaji bado yanaendelea ili tuafikiane kuhusu viwango vya hisa ambavyo Serikali itamiliki kwa muda kwa niaba ya wawekezaji wa ndani. Ni kwamba Serikali inao mpango wa kuwafikiria wawekezaji wa ndani katika hili. Serikali inatambua uchakavu wa njia ya reli na tuna nia hatua kwa hatua kuiboresha kutoka kilogramu 56 kwenda *pound* 120.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa moja kwa moja kwa treni kutoka Dar es Salaam, tunasema usafiri huu utarudi mara tu ukarabati wa *engine* na mabehewa utakapofanyika na kukamilika. Njia ya reli kati ya Dar es Salaam na Dodoma hivi sasa inapitika, hakuna sababu isipokuwa tunayo matatizo ya *engine* na mabehewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Reli ya Kati ya Isaka - Kigali na Arusha - Musoma kwamba upewe kipaumbele, tunakubaliana na Mheshimiwa Mohamed Missanga. Lakini Mheshimiwa Shamsa Mwangunga yeye anasema hakuna haja. Isipokuwa Reli ya Isaka na Kigali sio kipaumbele wakati tunashindwa kuimarisha na kuboresha njia za reli tulizonazo. Lakini sisi tunasema lazima tu-*tape* mizigo ya wenzetu wa *DRC* Kongo kabla wenzetu wa nchi jirani hawajachukua. Kwa hiyo, ujenzi wa reli hii ni muhimu, kwani ni mkakati kabambe wa kudaka mizigo iliyopo sasa na ijayo ya Rwanda, Burundi na *DRC* Kongo kukabiliana na ushindani na *Northern Corridor*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa kukarabati na uboreshaji wa reli yetu umepangwa na utafanywa na *TRC, RACO,* mkodishwaji na Serikali tunao mpango kabambe. Suala la Serikali kuangalia uwezakano wa kutumia usafiri wa treni Mijini kwa kuanzia Jiji la Dar es Salaam, haya yote tutamwambia mwendeshaji atakapochukua.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuondokana na matatizo yasiyokuwa ya lazima ya wafanyakazi watakaopuguzwa, hili tunalishughulikia. Kuna swali liliulizwa kwamba ni nani alibadili Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza badala ya Dar es Salaam kwenda Kigoma? Hakuna aliyebadili, bado ipo. Isipokuwa ukipakiza mizigo tunasema tu Dar es Salaam - Tabora - Isaka kwa mizigo ya Uganda na Rwanda, Dar es Salaam –Tabora, hakuna aliyebadili reli hii. Naomba tu muwe na amani wenzangu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Reli ya Mpanda kwamba hatuikumbuki, ni kwa ajili ya njaa, Mheshimiwa Arfi, tunairekebisha kila leo na kama utakubaliana na mimi, hata inapokuwa wakati wa mvua tuta lote lile huwa linafunikwa na maji na huwa tunalirudisha tena tuta upya. Kwa hiyo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tunajali sana Reli ya Mpanda na inatumika na itaendelea kutumika kama ilivyopangwa katika mpango huu wa ukodishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TAZARA*, amesema ni kwa sababu gani Serikali inazungumzia kubinafsisha *TAZARA* kwa mwekezaji mwingine badala ya kumshirikisha Mchina?

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwanne Mchemba kwamba Wachina ndiyo tuliowapa nafasi ya mwanzo kwamba wao ndiyo waliojenga na ndiyo wanaojua uchungu wa ile reli. Tumewaambia wao wakodishe hii reli. *(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana na nilisema nina Sekta 12 nisingeweza kuzijibu zote. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, SIASA NA UHUSIANO WA JAMII (MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nishiriki kwenye mjadala huu. Kwanza, niseme kabisa kwamba ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwanza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Pili, ninampongeza kwa hivi juzi tarehe 25 Juni, 2006 kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kasoro kura moja kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii vilevile nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kwa hiyo, kuniteua kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi yake. Nami nitajitahidi kumsaidia ili kazi kubwa aliyopewa iweze kuwa ya mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Mohamed Shein, ambaye alikuwa Mgombea mwenza wa Chama cha Mapinduzi kwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kura Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Hili kweli ni Bunge la viwango na kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wabunge wenzangu wote, Wabunge wa Majimbo, wa Viti Maalum na wa Kuteuliwa kwa kuingia katika Bunge hili la kisasa. Lakini nitumie nafasi hii maalum nimpongeze Ndugu Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi baada ya kupendekezwa na Rais kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangu achaguliwe ameongoza Bunge letu, ameongoza Serikali kwa uwezo mkubwa, lakini haishangazi kwa sababu wale wanaomjua na sisi tunaomjua Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, ni Kada wa Chama cha Mapinduzi, ni Kada aliyeandaliwa, kwa hiyo, si mambo ya ajabu, lakini nataka nikuhakikishie kwamba sote tutajitahidi kukusaidia ili kazi zako ziwe nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile niwapongeze wajumbe wapya wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. Sekretarieti ambayo imesukwa na Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi na kuidhinishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa. Nampongeza Ndugu Yusuf Makamba, Katibu Mkuu mpya wa Chama chetu, nakuhakikishia utapata ushirikiano wetu sote makada wa Chama cha Mapinduzi. Ndugu Jaka Mwambi, Naibu Katibu Mkuu, *Comrade* Aggrey Mwanri endelea kupiga nondo, watu waelewe misimamo sawa sawa, Katibu wa Itikadi na Uenezi Ndugu Asha-Rose Migiro, Katibu wa *NEC* wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Ndugu Rostam Azizi, Katibu wa *NEC* wa Uchumi na Fedha na Ndugu Kidawa Hamid Salehe, Katibu wa *NEC* wa *Organization. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliomba nishiriki sio kwa sababu ya kujibu maswali hasa, lakini kwa sababu nimesisimka kidogo na mazungumzo mazuri sana ambayo tumekuwa nayo tangu jana hapa. Michango mizuri sana, mimi naamini kwamba upande wetu wa Serikali tutayatafakari yaliyosemwa na Wabunge mbalimbali na mengi yake tutayafanyia kazi. Ningependa nisisitize moja ama mawili katika yale yaliyosemwa.

Moja ni lile walilosisitiza wasemaji wenzangu kwamba ili ilani yetu itekelezwe vizuri, ni vizuri tuzingatie vipaumbele katika kupanga mipango yetu. Mimi nadhani hilo ni jambo kubwa na ni muhimu, tuzingatie vipaumbele vya kiuchumi lakini vile vile kuna vipaumbele vya kero na kadhalika. Mimi nadhani hili ni jambo ambalo itabidi tulifanyie kazi.

Pili, tumepewa wazo zuri hapa ya kwamba ni muhimu tukusanye nguvu zetu za ndani za fedha ili tuweze kutekeleza mipango yetu. Tunajua bajeti yetu bado ni tegemezi, lakini tunao uzoefu ambao ametuachia Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Serikali yake ya Awamu ya Tatu, walikuwa wanatenga fedha kiasi cha shilingi 1.8 bilioni kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu kwa makusudi kabisa. Sasa mimi naamini utaratibu huo ukiboreshwa suala hili la barabara linaweza likapata nguvu zaidi likawa bora zaidi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kutoa wazo kuna dhana ya Kanda ambayo imejitokeza hapa katika mazungumzo. Nashauri ni vizuri nayo hii tukaichambua kwa sababu kuna upande mmoja ambao ni mzuri dhana ya Kanda inatumika vizuri, inasaidia sana katika kuendesha mambo ya nchi. Lakini dhana hiyo hiyo ya Kanda nayo inaweza vile vile ikakuleteeni matatizo. Dhana ya Kanda inatumika hapa kwetu kwa mfano unapotaka kuzungumzia masuala ya kijiografia, kwa hiyo, unazungumzia Kanda ya Nyanda za Juu, Kanda ya Pwani, Kanda ya Maziwa, mimi nadhani matumizi kama hayo hayana matatizo yanasaidia tu watu kuelewa zaidi unachojaribu kuelezea.

Mheshimiwa Spika, vile vile dhana ya Kanda inatumika katika kurahisisha utoaji wa huduma katika nchi. Kwa mfano, watu wa Mahakama Kuu wamekuwa na Kanda kwa sababu Majaji ni wachache, huwezi kuwa na Majaji katika kila Mkoa kwa hiyo, wanapanga Kanda ili kurahisisha utoaji wa huduma zao. Nilipokuwa *RC* Mbeya nakumbuka Wakaguzi wa Sekondari walikuwa na Kanda. Wakati ule nadhani alikuwa

Mkuu wa Kanda *Southern Highland* alikuwa anakaa Iringa lakini alikuwa anakuja kote Mbeya, Ruvuma, Rukwa na kadhalika.

Kwa hiyo, nasema huo ni utaratibu mzuri. Lakini kuna matumizi ya Kanda ambayo yana hatari ni Kanda ya kugawa watu kisiasa. Katika nchi ambapo kazi yenu kubwa ni ya kuwaleta watu pamoja mkianza kufanya kazi ya kuanza utaratibu wa kugawa watu kwa Kanda mnaanza kuleta kasoro katika jamii. Mtapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, wakati fulani hapa tulikuwa na uchaguzi nadhani ulikuwa wa *East African Community,* kuna watu walianza habari za Kanda. Ohoo, wa Kanda hii, Kanda hii, wanaanza ku-*negotiate* kwa Kikanda. Sisi wa CCM ilibidi tukutane na tukamwomba Makamu Mwenyekiti wetu Mheshimiwa John Malecela aelezee kidogo kwamba katika CCM sisi hatuna habari ya Kanda. Kwa hiyo, tusiingie huko, sio sera yetu sisi. Sasa nilidhani ni vizuri kwamba tutumie dhana ya Kanda pale ambapo inatusaidia. Lakini tukianza kuitumia Kanda katika maana ya kisiasa tukaanza kugawana gawana, tutaweza kupata matatizo.

Mheshimiwa Spika, kengele imelia na si vizuri mimi nikagongewa tena. Kwa hiyo, namaliza kwa kusema nashukuru sana kupata nafasi na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kujaribu kufafanua baadhi ya mambo. Kwanza niseme binafsi kwamba nimefurahi sana kwamba mjadala kwa hapa ulikuwa wa kuchangamsha. Hakuna mtu ambaye angeweza akasinzia, hata mimi sikuchoka, nilichangamka. Kwa hiyo, nawashukuru sana wale wote waliochangia na ningependa wabaki wakiamini kwamba nimepokea hoja zote, nimezielewa na nitazizingatia kwa moyo safi, bila ya kutazama nyuma, mimi siku zote natazama mbele. *(Makofi)*

Naomba niwashukuru waliochangia kwa kuanza na Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Wengine waliochangia nitakwenda haraka haraka na naomba muelewe tu kwamba *protocol* siizingatii sana Mheshimiwa fulani nitataja tu majina. Nianze kwa wale waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Capt. John Chiligati na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi.

Wengine ni Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Hassan Kigwalillo, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Clemence Lyamba na Mheshimiwa Ponsiano Nyami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza ana kwa ana ni Mheshimiwa Mohamed Missanga kama nilivyosema na Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Abdukarim Shah, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Dr. Maua

Abeid Daftari na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Wote hao na wengine ambao pengine sikuwataja hapa nawashukuru sana na naomba wale ambao sikuweza kuwataja bila kukusudia wanisamehe kwa sababu haikuwa kusudio langu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya siwezi kuwajibu wote hawa kwa sababu alizoeleza Mheshimiwa Spika, kwamba muda ni mfupi. Lakini kama walivyoeleza Manaibu wangu tutajaribu kuwaandikia na kujibu hoja zenu ili muweze kuwa na rekodi inayoeleweka. Niseme kwamba nakubaliana kabisa na naelewa kabisa uchungu uliowakumba wale ambao kwa kweli barabara kwao ni kama bidhaa adimu. Barabara yoyote ni bidhaa adimu barabara ya lami ni bidhaa adimu zaidi. Hao ndio wengi tulio hapa na walichokuwa wanasema kwa aina yoyote ile na kwa lugha yoyote ile walistahili. Kwa sababu gani, kwa sababu tatizo kubwa la miundombinu katika nchi hii ni barabara. Tatizo namba moja ni barabara na tutakuwa nalo kwa muda mrefu na linachukua muda mrefu sana katika Wizara yangu. Lakini tuna matumaini kwa sababu wale tuliokuwepo wakati wa Uhuru tunajua kwamba hata kuja Dar es Salaam tu kutoka mji wowote wa Tanzania ilikuwa taabu. Awamu ya kwanza tumejaribu kufanya kazi kubwa ya kuunganisha nchi kwa barabara na reli na hasa *TAZARA* na kadhalika lakini bado.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili, nafikiri historia itakuja kuandika kwamba Rais Ali Hassan Mwinyi, alifanya kazi kubwa sana kwenye eneo hili la barabara. Kati ya mambo makubwa tutakayokuja kumkumbuka ni hilo. Lakini maskini wa Mungu hakuwa na fedha. Kwa hiyo, alifanya lile aliloweza. Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa alikuwa na fedha zaidi kidogo kwa sababu kodi ilianza kulipwa vizuri. Akaendeleza aliporithi kwenye barabara tukapata hata uwezo chini ya Waziri Mheshimiwa John Magufuli wa kuwa na mradi maalum wa barabara kwa kutumia fedha zetu sisi wenyewe. Rais Ali Hassan Mwinyi na Rais Benjamin Mkapa tutawakumbuka sana katika historia yetu ya barabara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Nne ameonyesha njia, hajakaa pale kiasi cha kuweza kusema lolote zaidi ya kusema kwamba ametuachia Ilani ya Uchaguzi. Anayo Ilani na kwenye Ilani hii barabara zimeandikwa. Juzi kwenye Mkutano Mkuu wa Chama, samahani wale ambao hamkupata namna ya kuhudhuria alituachia kitabu kingine cha ukumbusho kwamba barabara ni hizi jamani. Kwa hiyo, alipokuwa anauliza Mheshimiwa Jackson Makwetta juzi tunaelekea wapi. Mimi nasema tunaelekea hapa ukurasa wa 49 wa Ilani ya Uchaguzi, tunaelekea hapa maagizo maalum ya Mkutano Mkuu Maalum wa Chama cha Mapinduzi, huko ndiko tunakoelekea. Hii ndiyo misahafu yetu na misahafu inasema nini. Kwanza kamilisha barabara zilizokuwepo zile ambazo awamu ya tatu imetuachia. Kwanza kamilisha, kuna za kukamilisha kwa lami na kuna za kukamilisha kwa changarawe, hiyo ndiyo kazi ambayo tumekwishaianza. Barabara hizo ni zipi? Dodoma - Manyoni, Manyoni - Singida, Singida - Shelui, Shelui-Igunga, Igunga - Nzega - Ilulla, Muhutwe - Kagoma, Nangurukuru-Mbwemkuru - Mingoyo, Mkuranga - Kibiti, Pugu - Kisarawe, Chalinze-Morogoro - Merela, Tunduma - Songwe, Kyabakari - Butiama, Dodoma - Morogoro, Kigoma - Biharamulo - Lusahunga,Tabora - Kaliua, Malagarasi-Uvinza - Kigoma, Usagara - Chato - Biharamulo na Ndundu - Somanga. Hizi ndizo barabara tulizozikuta, lazima tuendelee nazo. Kwa sababu hatuwezi kuziacha katikati. *(Makofi)*

La pili, Ilani ya Uchaguzi ikatuambia unganisha Mikoa yote Mkoa kwa Mkoa, Mkoa kwa Wilaya na nchi kwa nchi jirani. Unganisha kazi hiyo, tunaifanya. Nne, tukaambiwa anza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara mpya za Tunduma - Sumbawanga, Marangu - Tarakei - Longai, Minjingu - Babati - Singida, Rujewa - Madibira - Mafinga, Mbeya - Chunya - Makongolosi, Msimba - Ikokoto, Mafinga, Arusha - Namanga, Tanga - Horohoro na ukarabati wa barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, Mandela, Dar es Salaam, Sam Nujoma, Dar es Salaam. Kisha tukaambiwa sukuma ujenzi wa daraja la Kigamboni, iko hapa.

Mheshimiwa Spik,a kisha tukaambiwa mambo mengine unganisha endelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya Arusha - Musoma, Isaka - Kigali na kwa ukanda wa Mtwara, ambaye itaunganisha bandari ya Mtwara, Songea, *Mbambabay.* Mchuchuma na Liganga na mengine tuliambiwa hapa, haya ndiyo ninayofanya. Nimeshaanza hata mengine ambayo ni ya kufanyiwa tu usanifu kwa bahati kazi imetangulia, tumeshaanza. Mfano ni daraja la Ruvu tunalijenga, ilikuwa sasa hivi liwe linasanifiwa tu, tunajenga. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndugu zangu mimi kamwe siwezi kwenda nje ya Ilani ya Uchaguzi, ndiko ninakoelekea katika miaka yote hii mitano. Kwa hiyo, kuna miradi hii ambayo imeingia sasa, kuna miradi itakayoingia mwakani, kuna miradi itakayoingia mwaka keshokutwa ili mradi tukifika mwaka wa tano wa Awamu ya Nne tuwe tumekamilisha majukumu yote tuliyopewa katika kitabu hiki. Hii ndiyo kazi ninayofanya. Hapa miradi hii tuliyopewa kwenye kitabu kule Chimwaga ni ahadi za Rais ambazo nilianza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zifuatazo Tunduma - Sumbawanga mwaka huu nafanya, Marangu -Tarakei - Longai mwaka huu nafanya, Minjingu - Babati - Singida mwaka huu nafanya, Rujewa - Madibira - Mafinga nafanya, Mbeya -Chunya - Makongolosi nafanya, Msimba - Ikokoto - Mafinga nafanya, Arusha - Namanga nafanya, Tanga - Horohoro nafanya, barabara ya Kilwa - Mandela - Sam Nujoma nafanya na msongamano wa magari ya Dar es Salaam nafanya. *(Makofi)*

Mimi nilidhani ni mtu wa kuombewa maisha marefu niendelee kufanya, Manaibu wangu tuendelee kufanya. Ilani ikasema lingine kuna madaraja ya kushughulikia. Daraja la Malagarasi, daraja la Kilombero, yako madaraja yametajwa hapa ya kushughulikiwa. Viko na viwanja vya ndege. Kwa hiyo, kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi wa daraja la Mto Kilombero, Mto Mwatisi katika Mkoa wa Morogoro, Daraja la Ruvu leo nimeshaanza, Malagarasi, daraja la Umoja kati yetu na Msumbiji, hili nafanya tayari. Nimeshaanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, halafu kitabu kikaendelea kusema kwamba kuna suala la fedha, *item* ya kwanza kabisa endelea kuimarisha Mfuko wa Barabara yaani *Tanzania Road Fund* limezungumzwa sana hapa. Mheshimiaw Zakia Meghji, Waziri wa Fedha, ameshafanya, maana juzi kwenye bajeti ameongeza shilingi 10 kwa lita hazitoshelezi lakini ameshaanza mwaka wa kwanza, mwakani ataongeza, mwaka wa kesho kutwa ataongeza mwaka 2010 atakuwa ameshafanya mara tano. Sasa!!! Kwa sababu….

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe na utulivu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, bila mitaji hakuna namna tutafanya haya yote tunayotaka kuyafanya, hakuna. Tunaanza kwenye bajeti lakini haitoshi. Waziri Mkuu ni shahidi, miezi sita hii mimi nimekwenda ng'ambo mara mbili kutafuta fedha za ziada. Mara mbili nimekwenda na wiki ijayo nataka kwenda lakini sijazungumza na Waziri Mkuu. Wananiita na wanasema njoo hapa tuzungumze habari za fedha. Shahidi wangu hapa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika nilipokwenda juzi mimi nafuata miundombinu nikakuta miundombinu ambayo sio kwenye *portfolio* yangu umwagiliaji, nimemkabidhi Mheshimiwa Christopher Chiza, muulizeni, muulizeni Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, nimemkabidhi mtu. Mwekezaji *Stigler's Gorge* umeme sio kwamba nakwenda tu kuokoteza okoteza vya kwangu nikipata vya Taifa naleta. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili la fedha ndiyo kikwazo kikubwa. Kesho sisi tumeshaandaa mpango wa namna ya kushughulikia sekta hii ya miundombinu, namna ya kupata fedha. Kesho Jumatano maana ilikuwa tumaini hapa mtanipa usingizi mzuri, niamke kesho baada ya kupitisha nishughulikie fedha kesho wanakuja hapa watu tunawaleta kwa ndege watashukia hapa tunazungumza nao kila mmoja namna ya kutoa fedha kwa miundombinu. Wafadhili na wale wote ambao ni washirika wetu katika maendeleo, tunawaita hapa.

Baadhi ya Wabunge tunawaita Mwenyekiti wangu wa Miundombinu atahudhuria na Mameneja wangu wote wale waliojaza kule juu leo Spika amekosa nafasi ni Mameneja wangu waangalieni pale wanahudhuria kesho. Kila mmoja aeleze ya kwake na kila mmoja atoke hapo na kitu. Hatuwezi kutegemea bajeti kwa sababu hamna fedha za kutosha, ndiyo maana tunazungumza habari za *Build Operate and Transfer (BOT)* ni utaratibu mzuri na ndio wanaotaka kutumia watu wa *NSSF*. Mimi kimsingi naunga mkono umekuwa kwenye bajeti na Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha peleka kuzungumza kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini bahati mbaya kwenye Wizara yangu hatuna uzoefu wa kumiliki miradi ya miundombinu ya *BOT*. Kwa hiyo, tumekuwa tukizungumza na Benki ya Dunia watusaidie utaalamu wa namna ya kumiliki miradi ya miundombinu. Nadhani ndiyo hilo watu waliona sisi tukienda kule wakasema ooh, Mramba amekwenda kuomba fedha za *NSSF* kwani umesikia *NSSF* wameshindwa? Mimi nimekwenda kuomba utaalamu wa namna ya kumiliki miradi ya *BOT*. Wiki hii mimi nimesaidia sana kuuza magazeti, kila gazeti linasema kila jambo ili mradi Mramba aonekane yupo, kila mtu atanunua, lakini hawanipi hata *bonus*. Hawa wangepaswa kunipa *incentive* ya kuuza magazeti yao. Mradi Mramba ameonekana *frontline* kila mtu ananunua, kumbe mambo yote haya hayapo wanayosema haya. Wengine wanasema mimi nashirikiana na wezi. Nianze wapi umri wangu huu nianze nikakimbia polisi.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mambo ambayo tunayafanya na haya ndiyo mambo yatakayotutoa. Mheshimiwa Aggrey Mwanri alisema vizuri sana jana kwamba bila kuwa na mtaji hatuwezi kuendelea na ndivyo ilivyo na sisi tumetambua na ndivyo tunavyoendelea. Ndugu yangu Mheshimiwa Lucas Selelii ningependa kutoa ziada juu ya hoja ya barabara ile. Barabara hii ya Manyoni - Itigi - Tabora mpaka Kigoma ni barabara

ambayo ninaweza nikasema kwenye bajeti hii imekuwa na bahati mbaya tu lakini sio sana kwa sababu kuna shilingi milioni mia tano. Tulipata matumaini ya mfadhili wiki mbili zilizopita mfadhili katuambia kusema hapana. Kwa bahati nzuri Rais alipokwenda safari hii ya mwisho nje, alipita Uarabuni. Mfuko wa *Abudhabi Fund,* alikwenda na akazungumzia barabara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu samahani, nalazimika nikuongeze dakika tano zaidi kwa sababu ulitumia muda mwingi sana kutaja majina tu ambayo ilikua si kujibu hoja. Kwa hiyo, nakuongeza tena badala ya dakika tano utakuwa nazo dakika kumi sasa. *(Kicheko/ Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Mheshimiwa Rais akaambiwa lipa fedha kidogo nikupe fedha nyingi. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji ameshalipa dola za Marekani 500,000. Mimi wiki ijayo naanza safari ya kwenda kupiga hodi kwenye huo mfuko ili nipate fedha za barabara hii ya Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma kwa sababu ndivyo Rais alivyoniagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nikishafika pale hapo Malagarasi tumeshapata Wakorea tumeshazungumza nao, mazungumzo ya kitaalam yanaendelea kati yetu sisi, Hazina na Korea ili daraja la Malagarasi liweze kutengenezwa na Wakorea. Kwa hiyo, shilingi milioni 500 tutafanya nazo kazi sasa hivi lakini mwakani *Inshallah,* mimi nafikiri tutafanikiwa.

Naomba wale wa Ukanda ule tusaidiane kusali jambo hili tena lisipate *mushkeri.* Ndugu yangu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na wale wa Mikoa ya Kusini, nilichukua muda jana nilihofu mambo haya kwa kusoma vizuri kanuni, niliona hakuna muda mpaka Spika akuhurumie, hatakiwi akuhurumie, mtu inatakiwa afuate sheria na taratibu.

Mheshimiwa Spika, nakuheshimu sana umenihurumia. Nilijua itatokea, nikawaomba Wabunge wale njooni jamani niwaelezeni mengi zaidi kuliko yale ambayo nitaweza kueleza pale Bungeni na niliwaeleza. Lakini nataka kuwahakikishia ndugu zangu, ukweli kabisa nilivyoeleza kule Lindi wakati tukiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sisi kama Serikali hatuwezi kukubali mtu atutengenezee madaraja kwa kutumia saruji mbovu au vifaa vilivyo vibovu. Kwa sababu baada ya mwaka madaraja yale yatavunjika, tutarudi pale tulipokuwa bila barabara, mgogoro pale unajulikana ni juu ya kokoto na *quality* ya madaraja.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiandikiana na Waziri Mkuu anajua, tunajibizana, lakini keshokutwa tunakutana tena na hawa wakandarasi wameomba ruhusa ya kuja kuniona tuweze kuona kama tunaweza tukaelewana namna ya kumaliza kazi hii na mimi niko tayari, ila ukweli ni kwamba barabara hii hiki kipande hiki cha Nanguruku - Mbwemkuru na hiki kipande cha Dodoma - Manyoni kwa eneo hili. Vipande hivi viko kwenye usuluhishi. Kwa sababu huyu anasema hiki na sisi tunasema hiki, tutafute mtu wa tatu atusaidie na ndivyo nilivyo mweleza hata Waziri Mkuu juzi. Kwa hiyo, mimi nina matumaini kwamba haitafika mahali tuachane iwe talaka kwa sababu ni gharama sana kwa Serikali na vile vile ni gharama na jina baya kwa mkandarasi.

Kwa hiyo, tutafika mahali tutaelewena, ningependa kukuhakikishia kwamba kwa kipindi hiki ambacho sisi tumeingia kwa awamu ya nne, tumejitahidi kuhakikisha kwamba hawa wanarudi kazini na kazi zinaendelea wakati huku tunaendelea na mazungumzo ya kutatua matatizo ya pale ambapo tulikuwa tumefarakana.

Mheshimiwa Spika, *Air Tanzania,* tuna mgogoro mkubwa sasa hivi kati ya Serikali ya Tanzania kwenye Shirika la ndege la *Air Tanzania Limited* na shirika la ndege la Afrika ya Kusini. Tumefika mahali tumekubaliana kwamba tuachane salama, kwa sababu migogoro hii ikienda mahakamani ni gharama kubwa na itachukua muda mrefu. Lakini sasa tunadaiana, tukiachana nani atamlipa nani, nani atamfidia nani. Haya ndiyo mambo yanaoendelea. Lakini Serikali imeamua kwamba hakuna mjadala juu ya kuwa na shirika lenye rangi za bendera yetu ya Tanzania.

Kwa hiyo, tutakuwa na jambo hilo lakini kwanza tumalize huu mwiba huku ndiyo tuje jinsi ya kwenda kwenye amani huku upande wa pili au tufanye yote mawili. *Actually* tunafanya yote mawili. Tunachoanza kuchunguza ni iweje na huku tunasema tuharakishe mazungumzo. Kuna kamati inayoongozwa na Katibu Mkuu Hazina na Mwanasheria Mkuu natumaini kwamba jambo hili tutalipeleka kwa kasi kama walivyokuwa wameshauri Waheshimiwa Wabunge ambao mimi nakubaliana nao kabisa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo niseme tu lile la reli kwamba siku tatu zilizopita tumekuwa na kikao kingine mazungumzo yanaendelea vizuri wafanyakazi watapata mafao yao kabla hawajaondoka wala si baada ya kuondoka wakati wowote kuanzia sasa na sisi kwa upande wa Serikali kwenye kikao juzi tumeona kwamba waendelee muda si muda wataelewana na wakishasaini utaratibu mpya wa kuendesha reli utaanza na kwa taarifa yenu Serikali itakuwa humo ndani. Siyo kwamba tunawakabidhi halafu twende *no*, tunakua huko ndani hata kwenye bodi zao tutakaa na tuna masharti fulani fulani tumewapa ya kuhakikisha kwamba tukiona wanalegalega tunaweza hata tukainyakua reli yetu kama Mheshimiwa Edward Lowassa, alivyonyakua yale maji kule Dar es Salaam. Tutafanya hivyo, tumejiwekea utaratibu wa kisheria wa kunyakua chetu kabla ya hakijaribika.

Mheshimiwa Spika, pia tumejiwekea utaratibu wa kisheria wa siku ile anapoondoka huyu na sisi tuweze kuchukua chetu katika hali njema zaidi na tutaendelea kufanya mengine ya kupanua reli ya kuimarisha reli, ya kuongeza uzito wa reli kama wengi wenu mlivyokuwa mkishauri.

Mheshimiwa Spika, narudia, naomba mnielewe kwamba mimi niko nanyi, mimi ni Mbunge huu Uwaziri unafikiri nimezaliwa nao au unafikiri nitazeeka nao? Haya ni mazungumzo tu baada ya habari ya maana ni Ubunge. Kwa hiyo, hayo mliyosema mmenisemea na mimi, maana Tanzania hii ni moja nyie mna Majimbo na mimi nina Jimbo siku nikija huko nitazungumza hivyo hivyo kama nyie.

Kwa hiyo, lakini kwa kuwa sasa tumefikia uelewa mmoja wazungu wanasema *the same wavelength* tuko kwenye masafa yale yale. Kwa kuwa sasa tuko kwenye masafa

yale yale, basi naomba kutoa hoja kwamba Waheshimiwa Wabunge waidhinishe bajeti hii mimi nitoke hapa na elimu kubwa ambayo nimepata niinge kazini kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo iko mbele yetu na inahitaji niwahoji ili kuikubali kabla hatujaingia kwenye Kamati. Wanaoafiki hoja hiyo waseme ndiyo, wasio afiki waseme sio. Naona walioafiki wameshinda, kwa hiyo sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kukiri jambo moja, katika Kamati ya Matumizi iliyopita Ofisi ya Waziri Mkuu sikumtendea haki hata kidogo Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi nilimkatiza kabla ya dakika tano. Napenda kuwaarifu kwamba nilimwomba radhi kwa maandishi kwa sababu tunafanya kazi kwa uadilifu. *(Makofi)*

Sasa naomba nieleze utaratibu kwa sasa unatafsiri Kanuni ili Kamati hii iende vizuri. Kwanza kabisa tusifuate ule mtindo wa zamani wa kukurupuka kusimama kabla hata tarakimu hazijatajwa. Naomba mtulie ikishatajwa tarakimu katika kifungu kinachohusika basi nitatoa nafasi kama dakika moja, nitaangaza macho yangu ukumbi mzima wale wote watakao kuwa wamesimama kutafuta ufafanuzi Katibu ataorodhesha. Nitawaruhusu wote watoe hoja zao na ziwe zinajibiwa. Kwa hiyo, nafasi ipo wote mtaonekana wale mnaotaka kuhoji. Halafu tutakuwa tunaendelea kifungu kwa kifungu hadi mwisho. Nitawashukuru sana kwa ushirikiano huo ahsante sana.

**Fungu 98 - Wizara ya Miundombinu**

Kifungu 1001 - *Administration and General...* sh. 3,822,430,000/=

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimwa Mwenyekiti, Kanuni ya 81, kifungu cha pili (b). *Vote* 98, *sub vote* 1001, mshahara wa Waziri.

Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwasilisha hoja yake alizungumzia barabara ya kutoka Nzega kuja Tabora kupitia Sikonge - Ipole kuelekea Rungwa mpaka Mbeya na katika maelezo yangu wakati nachangia kwa maandishi nimeelezea barabara hiyo lakini vile vile mimi mwenyewe nilishamuona Mheshimiwa Waziri na nikazungumza na Naibu Waziri, lakini kwenye majibu ya Mawaziri wote waliochangia hakuna maelezo ambayo kwa kweli yameniridhisha na mbaya sana barabara hii kipande hiki hakikutengewa fedha

kiasi chochote. Kutokana na hali ambayo barabara hii inayo ni chakavu katika kipindi cha masika haipitiki kabisa. Kiangazi tunaacha barabara tunapita mbugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, barabara hii tena barabara kuu naomba nipate maelezo yatakayo niridhisha mimi na yawaridhishe vilevile wapiga kura wangu wa Sikonge.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Said Nkumba ni kati ya barabara ambayo tunaendelea kuitafutia fedha na kama ambavyo tumeeleza kuanzia Mbeya kuja Makongorosi tumeanza kujenga na hii barabara ya kuanzia huku kwa sasa tutakachoweza kufanya kwa mwaka huu kuendelea kufanya matengenezo ambayo yatafanya barabara hii iendelee kupitika wakati tunatafuta fedha za kuijenga kwa kiwango kikubwa zaidi.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba ni kiasi tu kama nilivyosema unaanzia wapi lakini barabara hii na yenyewe itawekwa kwenye kipaumbele katika bajeti zinazofuata.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naridhika na maelezo. Lakini maelezo yake yananionyesha kwamba kuna fungu sijui anakolitafuta lakini ninachokizungumza hapa barabara iko kwenye hali mbaya, huko alikoanzia sijui ataishia wapi. Lakini tunakopita sisi ni kutoka Ipole kwenda mpaka Rungwa. Maeneo aliyoanzia Mheshimiwa Naibu Waziri anapozungumzia ni maeneo ambayo barabara inaishia Chunya. Sasa hiki kipande ambacho hakipitiki kabisa kikiendelea kubaki hivyo bila kifungu chochote napata wasiwasi naomba maelezo ambayo yataniridhisha kwamba fungu lipo. Naomba Waziri aji-*commit*.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatenga fedha kwenye fungu la *maintenance* ambalo linakuwepo kwa pamoja katika mfuko wa *TANROADS* wa kufanya matengenezo ya *routine*. Kwa hiyo, zitakuwepo fedha.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika.

**MHE. JOHN M.CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema kwamba tatizo la kutokuwa na barabara ni kwa sababu ya maamuzi ya Wizara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, lazima uende kwenye kifungu, huanzi hotuba mpya.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho namba 1001 kwenye 250100 *basic salaries*, ambapo Mheshimiwa Waziri yumo humo. Nilisema kwamba uamuzi *either* zijengwe barabara inaonekana unakaa kwa maamuzi ya Wizara na zaidi Waziri. Sasa Waziri amepanga barabara zitengenezwe kwa kutumia

*TANROADS* peke yake na wafadhili. Hakuna isipokuwa shilingi milioni 800 fedha za kodi ambayo sisi walipa kodi tunalipa zaidi karibu sasa bilioni 200 kwa mwezi. Sasa nataka maelezo yeye amepewa shilingi bilioni 280 kwa Wizara nzima. Ni kwa nini Waziri hakutenga zaidi ya fedha ambazo ametenga ili kuhakikisha kwamba baadhi ya barabara kwa mfano Mkoa wa Shinyanga zilizopewa shilingi bilioni moja tu zinaongezewa fedha kutokana na hela ambayo wamepewa ya shilingi bilioni 280?

Kwa hiyo, nataka maelezo. Pia mambo haya ya *TANROADS* ambayo ndiyo tunategemea Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba mfuko wa *TANROADS* umeongezewa na hii imefanywa na Mheshimiwa Zakia Meghji. Lakini takwimu hazionyeshi hivyo. Mwaka jana mfuko kwa hotuba yake anasema ulikusanya shilingi bilioni 80.413, matumizi shilingi bilioni 58.9, shilingi bilioni 22 hatuna maelezo zilitumika kwa kitu gani?

Pili mwaka huu zimepungua. Mategemeo yake ni shilingi bilioni 77.123, matumizi ni shilingi bilioni 53.322. hatujui pia shilingi bilioni 23.8 zitakwenda wapi. Kwa hiyo, inaoneka kuwa kwamba shida tunazopata kwa upande wa barabara ni maamuzi ya Wizara. Nataka maelezo atafanya nini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa John Cheyo kwamba Mikoa imetengewa fedha kidogo na kwa hiyo, imebidi igawe kidogo kidogo. Labda niieleze Kamati yako kwamba wakati awamu ya nne ilipoingia madarakani, bajeti ilikuwa imeshakwenda mbali sana katika maandalizi na haikuwezekana kuifumua ili kufanya mambo sawasawa na tuliyotaka sisi. Lakini kuna uamuzi ndani ya Serikali kwamba bajeti ijayo itaendana na hali halisi ya mahitaji ya Ilani ya Uchaguzi. Hilo la kwanza.

La pili, sekta mbili zitapewa kipaumbele cha hali ya juu zaidi kuliko mwaka huu nazo ni kilimo na miundombinu. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba badala ya vihela vya hapa na pale tutaweza baadaye kupata fedha nyingi zaidi hasa kama zitasaidiwa na njia kama nyingine ambazo nilikuwa nikieleza hapo. Kwa hiyo, kwa sasa hivi hali ndivyo ilivyo lakini siyo hali ya kudumu ni hali ya mwaka huu wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri utofauti wa zile fedha za *TANROADS* ambazo zinarudi shilingi bilioni 22 mwaka jana na kadhalika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa maswali aliyouliza Mheshimiwa John Cheyo kwamba kwa nini zilizokuwa zinakadiriwa ni nyingi kuliko zile zilizopangwa katika kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Sheria ya *Amendment Act* namba 2 ya mwaka 1998 ilianzisha mfuko wa barabara na katika mfuko ule asilimia 70 ya fedha zinazotengwa ndizo zinakwenda *TANROAD* chini ya Wizara ya Miundombinu. Asilimia 30, zinaenda Tawala za Mikoa. Kwa hiyo, zile shilingi bilioni 53 zilizopangwa hapa ni katika ile asilimia 70 iliyoenda kwenye Wizara ya Miundombinu. Asilimia 30 ilipitishwa

na Mheshimiwa John Cheyo kwenye bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kipengele cha Tawala za Mikoa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia jedwali la ukurasa 79 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri utaona kwamba ugawaji ule ni pamoja na *TANROAD,* TAMISEMI, Miundombinu, Bodi ya Mfuko na bado kuna salio kama ukichukua fedha yote iliyokusanywa. Kwa hiyo, anayoeleza Mheshimiwa Waziri wa zamani wa Ujenzi tayari imeshajumuishwa katika jedwali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sijaridhika, hizo fedha ziko wapi na kama mfuko huu unatumika kwa kazi nyingine dhidi ya kazi ambazo sheria imesema na kwa mgawanyo uliotajwa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, lakini mimi nikitizama hapo, cha kutazama ni mapato halisi, sio kutazama makadirio halafu ukalinganisha na matumizi, lazima uangalie mapato halisi ambayo ni shilingi bilioni 58 na *column* ya mwisho matumizi ni shilingi bilioni 58 au sijakuelewa?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imezungumzia juu ya halisi zilizokusanywa. Ukurasa wa 59 anasema hivi: “Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Bodi ilikusanya shilingi bilioni 80.413. Kwa hiyo, haikuwa kwamba imekadiliwa ilikusanya... Halafu juu ya makasio ambayo ndiyo ya mwaka huu inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 77.123.” Kiswahili naona wote tunaelewa haya ni maneno ya bajeti na ni maneno ya Waziri, ndiyo maana nasema mfuko huu haujaboreshwa kama vile alivyokuwa anajibu, *actually* mfuko umepelea.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichoandikwa kwenye bajeti ukurasa wa 59 ni makisio ya makusanyo hadi tarehe 30 Juni, lakini ukiangalia pale katika jedwali analolizungumzia kuna nyota inayoonyesha kwamba ile shilingi bilioni 58 karibu shilingi bilioni 59 ni mpaka Mei. Kwa hiyo, mwezi Juni ndiyo ingefikisha ile shilingi bilioni 80 ili kufikia kiasi kile ambacho kimetajwa kwenye kitabu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hizi fedha zinategemewa kwamba zingekusanywa basi hii ingeonekana katika matumizi ya *TANROAD* kama vile ilivyoainishwa katika ukurasa wa 110 wa kitabu cha Waziri ambayo inasema wazi kabisa *TANROAD* itapokea shilingi bilioni 53 ambayo ukiongeza pale bado haijafanana na hela ambazo zimekusanywa. Labda tu tungeleezwa kwamba huu mfuko ni kweli hela zote zinakusanywa au tunayopewa hapa ni makisio na ndiyo maana miradi ya barabara inapelea, hakuna fedha kwa sababu hakuna uangalizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, kwa mujibu wa Kanuni imefikia wakati sasa utoe hoja yako unachotaka ni nini ili tukipigie kura. Kwa sababu huwezi kuongea zaidi ya mara tatu ukatufunga tu hivyo hivyo tukawa tunasikiliza tu basi. Sasa kama una hoja mahsusi iseme hiyo ili wanakamati hapa waone ina mantiki waipigie kura.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka ni maelezo ambayo yanakidhi. Kwa hiyo, kama Serikali itasema hawana maelezo, watatupa baadae, naweza nikaridhika.

Mheshimiwa Spika, lakini, maelezo yaliyotolewa hayaridhishi na kwa kuwa hayaridhishi, basi tupige kura kwamba mshahara wa Mheshimiwa Waziri ufutwe kwenye Kasma hiyo.

**MWENYEKITI:** Hiyo ni kinyume cha utaratibu. Hakuna hoja ya namna hiyo. Ulitakiwa utoe hoja inayohusu makadirio yenyewe na majibu yapo yametolewa. Tumechanganya Makadirio na Makusanyo. Inawezekana lugha katika *paragraph* hapa ikawa ina matatizo. Lakini ukitazama kwenye haya majedwali, inawiana. Tuendelee.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru sana kunipa hii nafasi. *Vote Number 98*, *Subvote 1001*, *Item Number 250100*, yahusu mshahara wa Waziri.

Naomba ufafanuzi kuhusu bomoa bomoa ya Tingi - Kipatimo, Nangurukuru - Mbwemkuru na Nanganga - Lwangwa, kuhusu fidia za wananchi wakati barabara hii inataka kujengwa sasa hivi. Nimefuatilia kwa Naibu Waziri wa Miundombinu, lakini sijapata jibu la kueleweka mpaka sasa hivi na wananchi wako tayari kuondoka, lakini wajue tu kama fidia yao itakuwaje. Napenda kuwasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bomoa bomoa alilouliza Mheshimiwa Riziki Lulida, kuna wengine ambao wako mahakamani lakini kuna wengine ambao tumewaeleza kwamba wale ambao hawako kwenye hifadhi ya barabara lakini barabara itapinda ikawaingilia, watafidiwa. Lakini wale ambao kwa mujibu wa sheria ya hifadhi ya barabara wako kwenye hifadhi, kwa mujibu wa sheria hawastahili kufidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ambavyo tumekuwa tukizungumza hapa, Serikali inajaribu kuangalia sheria hii ya hifadhi ya barabara na kuona kwamba ni mazingira gani yaliyowapeleka wananchi katika maeneo hayo ya hifadhi ya barabara ili na ubinadamu utumike. Kama walikwenda pale, kwa mfano wale wa Nangurukuru ambao walikwenda maeneo yale kwa kupelekwa kutokana na vijiji vya ujamaa na si kwamba wao walipenda, bali walipelekwa kwa ajili hiyo. Basi tuweze kuwafikiria. Kwa hiyo, suala hili tutalifikiria na kama kunakuwa na haja hawa walioko mahakamani tutawaomba waondoe kesi mahakamani ili tuweze kuzungumza na tuyamalize.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nahitaji ufafanuzi juu ya jambo moja tu. *Programme 10, Sub vote 1001, 250100*. Mshahara wa Waziri. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Lindi, alimwita na Waziri wa Miundombinu. Sisi Wabunge wa Mkoa wa Lindi tulimwomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwamba tuna taarifa vifaa vyote, mitambo ile ya matengenezo ya barabara vinataka kuhamishiwa Mtwara kwa sababu Meneja aliyekuwepo Mtwara hataki kuhamia

Lindi. Tukamwomba Waziri azuie hiyo kwa msingi ule ule aliowekea pale kwamba ukiweka pale Lindi ndio inakuwa katikati kati ya Kilwa, Liwale, Mtwara, Masasi na Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alitoa maagizo pale alituambia kwamba vitu hivyo havitohama. Lakini kwa bahati mbaya miezi miwili iliyopita, mara tu mlipotoka Lindi, vitu hivi vimehamishwa, mitambo yote imepelekwa Mtwara.

Je, kwa ajili ya utendaji kazi mzuri, Waziri sasa atatuhakikishia hapa kwamba atatoa amri vifaa vile virudi pale pale Lindi ili kuwapunguzia matatizo watu labda wanaotengeneza barabara ya kwenda Kipatimo, watu wanaokwenda Liwale kwa umbali ule? Mheshimiwa Waziri atatubadilishia jambo hilo hivi sasa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikijibu, nitaomba nizungumze pia kwa kimombo ili wahusika wanielewe vizuri, kuna wasioelewa Kiswahili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba vifaa vile vitabaki Lindi! Vifaa vitabaki Lindi na nilitoa maagizo hayo mara niliporudi kwa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* mwenyewe kwamba vifaa vinabaki Lindi. *The road construction equipments shall remain in Lindi and I so instructed the Chief Executive of TANROADS and he is hearing me, only that he cannot participate in this debate*. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo aliyotoa Waziri, aliyatoa nikiwepo Lindi. Kwa hiyo, nitataka pia kujua hatua zitakazochukuliwa dhidi ya mtu huyo ambaye hakutekeleza maelekezo ya Waziri wa Miundombinu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo! Ndiyo! Hatua zitachukuliwa kwa sababu huyo mtu hana nidhamu na hatua naitamka sasa hivi hapa kama vifaa vilikwenda Mtwara kwa kukodishwa na watu wa Mtwara, ili virudi ni suala lingine. Kama havikwenda hivyo, anasimamishwa kazi kuanzia kesho asubuhi na nataka hilo litekelezwe! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Loh! Natumaini huyu Mhusika haangalii kipindi cha Bunge hivi sasa. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge! *(Makofi)*

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 98, Sub vote 1001*, Kifungu kidogo 250100, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hotuba hii, nilizungumzia suala la Wizara kuangalia uwezekano wa kuisaidia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kutengeneza barabara inayokwenda sokoni Tandale kwa sababu barabara ile ni muhimu na nilisema kwamba ama bajeti hii ama bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayakuniridhisha. Naomba nipate majibu ambayo yataniridhisha, lakini pia yataridhisha wapiga kura wangu. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilizungumzia suala la tatizo la usafiri kwa wanafunzi Dar es Salaam, lakini katika maelezo ya Waziri na Naibu Waziri hawakuligusia. Naomba nipate maelezo ya kina na bahati nzuri wenyewe wapo hapa. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la barabara ya Tandale kama nilivyosema, ile barabara haiko chini ya Wizara hii. Hilo lilikuwa ni ombi ili tuone kama tunaweza tukasaidia. Sasa unapoomba sidhani kama unaweza ukashika shilingi ya Waziri wa Miundombinu, labda Waziri wa TAMISEMI kwa sababu barabara ile iko chini ya TAMISEMI. Haya ni maombi yaliyoletwa kwetu na nadhani kwa sababu tumesema kwa sasa hatuna pesa ya kusaidia barabara ambazo haziko chini ya Miundombinu, basi tuendelee kujadiliana tuone kama huko mbele ya safari tunaweza tukapata hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tatizo la usafiri la wanafunzi, kwa kweli hili ni tatizo kubwa na mimi najua kwamba wadau mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni Wizara mbalimbali pamoja na Jiji la Dar es Salaam tunatakiwa tukae kwa pamoja tuone ni namna gani tunaweza tuka-*solve* tatizo hili. Moja ya mapendekezo ni ku-*designate* UDA ifanye kazi ya kusafirisha wanafunzi kwa kuongezewa mabasi na kupata ruzuku toka Serikalini. Haya mambo ni ya kuendelea kuyazungumza. Lakini tunakiri kwamba tatizo la wananfunzi Dar es salaam ni kubwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, nashangaa maana yake kivuko kinatengenezwa cha Pangani, kipya kinanunuliwa, lakini labda unalo lingine. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nia njema tu kwa sababu nimezungumzia Kivuko pamoja na barabara. Suala la Kivuko nimeridhika na suala la barabara siyo kwamba sikuridhika, isipokuwa nataka kuhoji tu kidogo ili tupate ufafanuzi. *Subvote* 1001, mshahara wa Waziri 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi imezungumzia utengenezaji wa barabara kutoka Bagamoyo hadi Saadan. Lakini vile vile ahadi ya Mheshimiwa Rais, amezungumzia barabara kuiendeleza hadi Tanga kupitia Pangani. Nafahamu kwamba hii barabara inataka kujengwa kwa utaratibu wa *Build, Operate and Transfer(BOT)* na nafahamu kwamba kuna mwekezaji ambaye amekwishaonyesha nia ya kutaka kuwekeza katika barabara hiyo, lakini muda umekuwa ni mrefu.

Mheshimiwa Spika, nataka Mheshimiwa Waziri anipe maelekezo au ufafanuzi, je, endapo tutapata mwingine ambaye yuko tayari kufadhili barabara hiyo. Je, Wizara yake iko tayari kumpokea na ili azungumze naye kwa kufuata taratibu zote kupitia ngazi ya Mkoa hadi Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimemjibu toka mwanzoni. barabara hii tayari tumeanza kufanya *feasibility study* na shilingi milioni 400 zimetengwa kwa mwaka huu. Lakini si kweli kwamba tumeshafikia maamuzi ni namna gani au ni nani atajenga barabara hii. Lakini kama Mheshimiwa Mbunge atakuwa na mtu ambaye anataka tuzungumze naye baada ya kumaliza hizi hatua za awali, sisi tuko tayari kuzungumza na mfadhili yeyote au mjenzi yeyote anayeweza kuja mradi masharti yake yawe kwa manufaa ya taifa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Natumia *Programme Number10, Subvote 1001*, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Mimi nasikitika kwamba majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri hapa, yalikuwa kwa kweli ni ya kusafisha tu ili bajeti hii ipite. Ni kama ile hadithi ya funika kombe, mwanaharamu apite. Lakini kwa kweli mimi sijaridhika kabisa kama ndiyo majibu ya Serikali ya namna hii. Sisi wote ni wana CCM, tunajua Ilani ya Uchaguzi. Tumeimba kwenye majukwaa, tumeeleza ndiyo maana tuko hapa tena kwa kura nyingi sana na hasa za Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nilizozisema, nilitamka wazi kutoridhika kabisa na mpangilio uliokuwa, umewekwa wa pesa kuzirundika katika eneo moja. Mheshimiwa Waziri amekuja hapa anaimba anasema nitafanya, nitafanya, nitafanya, bila kuonyesha vifungu kwenye Makadirio ya vitabu vya hesabu! Atafanya, atafanya kutoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi sijaridhika. Kwa sasa natumia Kanuni ya Bunge ya mwaka 2004, Kifungu cha 81(b). Kabla hajanishawishi kutumia Kifungu cha (c). Natumia cha (b) ili nipate maelezo ya kutosha. Kielelezo kizuri cha kueleza kwamba maelezo haya ilikuwa ni bla bla, ni juu ya barabara hii ya Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma na mimi nilisema kabisa barabara nilizitaja nyingi. Nilitaja Mwandiga - Manyovu, nilitaja Ipole - Koga - Mpanda, nilitaja Nzega - Tabora, nilitaja Sumbawanga - Nyakanazi, nilitaja Usagara - Mwanza. Lakini amejibu moja tu hii ya Itigi - Tabora - Kigoma na katika majibu umemsikia mwenyewe amejichanganya, mara shilingi milioni 500, mara dola 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna hii bado mimi narudia, bado mimi na wapigakura wangu wa Jimbo la Nzega sijaridhika na maelezo ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri. Aniambie kwanza, hii aliyosema anafanya *design*, anafanya usanifu au anajenga! Maana yake kasema tu nitafanya, nitafanya, unafanya nini? Kwenye kitabu cha bajeti hajasema chochote, kwenye kitabu chake cha hotuba hajasema chochote. Ilani ndiyo imesema hivyo na yeye anarudia Ilani. Hatuko kwenye uchaguzi sasa hivi. Tuko kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa na taadhima, naheshimu sana kiti chako. Naogopa kwenda kwenye kifungu cha (c). Naomba tafadhali, hapa wote tumetumwa na wananchi kwamba yeye ametumwa na wananchi na bahati nzuri ametumwa na Serikali, asimame hapa ajibu kama Serikali. Bunge lako ni Bunge Tukufu, linahitaji lipewe maelezo ya kina ili na sisi tunaporudi kule tunasema kitu ambacho kinaeleweka. Siyo kutuimbisha tu sana, tutafanya. Dakika zinakwenda, unakwenda, basi imetoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani. Bado nahitaji maelezo ya kina, vinginevyo nitaenda kwenye kifungu (c).

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Mbunge, hata kiti hakijakuelewa. Unazungumzia barabara zote ulizozitaja?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na kwamba asiseme zote, basi hata hii ambayo inanihusu mimi ya kutokea Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma, aiseme vizuri. Amebabaika katika kutaja, ametaja *figures* ambazo siwezi kuelewa! Ameanza amesema shilingi 500 milioni, amesema *five billion US dollars,* amesema sijui ngapi, haieleweki. Lakini unaposema hizo pesa, kwanza ziko wapi lakini pili unafanya nini? unafanya *design?* Je, unafanya usanifu au unajenga? Hajasema, kasema tu nitafanya. Atafanya nini sasa? Wanijibu basi, hiyo kwanza. Acha zingine ajibu hii na ya Nzega. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo ni hizo barabara mbili. Manyoni - Kigoma na Nzega - Tabora - Ipole.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudie nilichosema. Kwenye bajeti hii, barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora mpaka Kigoma, ziko shilingi 535 milioni na shilingi 535 milioni ambazo zimetengwa kwa ajili ya usanifu wa kina *(detailed design)* na hizo ziko kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema hapa, wakati tukitumia hizi shilingi 535 milioni, tunatafuta fedha za *Abudhabi Fund* na mimi nikasema nina matumaini kwa sababu Waziri wa Fedha ameshaanza kulipa madeni ya *Abudhabi Fund*. Kwa hiyo, nikasema kwa sababu amelipa na yeye mwenyewe ameniambia sasa ameshatimiza masharti, wiki ijayo sasa *whatever time*, *as soon as possible* baada ya leo, tutakwenda kupeleka maombi yetu rasmi sasa kama ilivyo kwenye taratibu. Sisi tuna matumaini kwamba kwa namna majadiliano yalivyokwenda kati ya Mheshimiwa Rais na viongozi wa *Abudhabi Fund* na viongozi wengine wa Serikali kule, fedha hizi zitapatikana na Rais mwenyewe alitaka fedha hizi zitumike kwa barabara hii tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunajua kiasi cha fedha zitakazotakiwa kulingana na utaalam, tutaziomba hizo. Tutakwenda nazo taratibu mpaka tufike Kigoma. Nikasema la pili, kwamba Daraja la Malagarasi halitohusishwa na fedha hizi kwa sababu kuna mkopo tayari ambao tumeishaahidiwa na Serikali ya Korea Kusini. Kwa hiyo,

majadiliano yanaendelea. Daraja hili litajengwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea Kusini ambayo itatumia Benki yake inaitwa *Exim Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri ndivyo ninavyojaribu kueleza. Sasa barabara ya Tabora - Nzega, barabara ya Ipole - Tabora - Ipole - Mbeya, hii ndiyo aliyoulizia Mheshimiwa Said Nkumba. Hii haiko kwenye bajeti, lakini ndiyo hiyo ambayo tumesema kwamba itahitaji matengenezo ya *spot improvement* kama alivyoeleza Naibu Waziri na kwamba fedha hizo ingawa hazipo hapa lakini kuna mfuko wa namna hiyo kule *TANROADS* ambao unaweza ukatumika kwa kazi hiyo. Mimi nina hakika tunaweza tukasimamia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama kwenye hilo nimeeleweka!

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado narudia tena kueleza vizuri. Anasema hizi shilingi milioni 500 za barabara kutoka Manyoni - Itigi - Tabora, zipo. Zipo wapi? Mimi nilizoziona ni shilingi milioni 500 kwa barabara kutoka Nzega kwenda Tabora. Lakini hizi milioni 500 anazozisema hazipo kwenye vitabu! Sasa bado ninasisitiza majibu yawe sahihi, kwa sababu Serikali haiendi kwa maneno. Inaenda kwa taratibu, kanuni na sheria na Bunge lako haliendi hivi hivi pamoja na kwamba tuna *Hansard*, aeleze kwenye kifungu gani ziko hizi shilingi milioni 500 za kufanya *design* kwa barabara hii ya Manyoni - Itigi - Tabora. Baada ya hapo kutoka Tabora kwenda Kigoma! Ametamka hapa hapa. Sasa, hivi anarudi shilingi milioni 500, wakati ametamka pale ilikuwa bilioni 5. Tungekubali pale tungeondoka na mawazo kwamba Serikali imetutengea shilingi bilioni 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado anionyeshe ziko wapi? Nakuambia hizi pesa hazipo! Na mimi nasikitika, sijui kanuni zetu zikoje lakini nasikitika, sisi wa Kanda ya Magharibi tukishaanza kutetea maslahi ya maeneo yetu, Serikali inainuka na kuanza kutusema mambo ya Ukanda. Mambo ya Ukanda, Serikali ndiyo mnaazisha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, acheni upendeleo kwenye Kanda zingine muweke kule, sisi tusiseme, kwanza hatuna reli, hatuna barabara, hatuna ndege, tukasemee wapi na wananchi wametuamini wametuweka hapa ili tuseme. Tusiposema tumwambie nani! Tuwashitakie kwa Mungu! Tutawashitakia kwa wapiga kura. Lakini, lazima tuwaambie. Hakuna Ukanda, tunatetea maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili bado sijaridhika hizi pesa, hazimo. Aeleze ziko kifungu gani, ndiyo nitakubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sijui, au hazipo! *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora - Nzega, ziko shilingi 535 milioni. Ndiyo! Zipo, Zipo!

**MWENYEKITI:** Hiyo ni Tabora - Nzega, ni tofauti kabisa na Manyoni - Tabora kuendelea huko na hapa inabidi Mwenyekiti, mimi kama Spika inabidi ni-*declare interest,* maana yake nisiwe mnafiki hapa. Inanihusu pia hiyo. Lazima niseme, kanuni zinanihitaji kusema hivyo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko! Tabora - Nzega, sasa, Kigoma - Uvinza - Tabora. Kuanzia Itigi hakuna fedha. Itigi - Manyoni - Tabora, hakuna fedha. Hakuna fedha. Ndiyo, hakuna fedha. Hizo ndizo tulizosema tunatafuta. Manyoni - Itigi - Tabora hakuna fedha.

**MWENYEKITI:** Kuendelea mbele? Haishii hapo, inakwenda Kigoma.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, Kigoma - Uvinza - Tabora, kuna shilingi 853 milioni na milioni 3.279. Samahani, niko tayari kumwonyesha Mheshimiwa Mbunge, siwezi kuisoma hii sawa sawa, *I can't read this, I can't read.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maandiko hapa lakini siwezi kuyasoma. Siwezi kuyasoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezisikiliza kwa makini sana na kwa usikivu sana hoja za Waheshimiwa Wabunge juu ya barabara hiyo. Nimesikiliza pia majibu ya Serikali juu ya barabara hiyo. Naomba kutoa ahadi hapa kwamba barabara hiyo itapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba inajengwa kabla ya mwisho wa kipindi chetu cha miaka mitano. Kwa hiyo, tunaomba Wabunge tuwaahidi hivyo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kuhusu utaratibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 50. Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni. Kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni na ya kubahatisha tu na Spika au Mbunge mwingine yeyote aweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake. Mbunge anayetakiwa kufanya hivyo atawajibika kutoa uthibitisho huo katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, amesema hapa katika Kamati hii kwamba Waziri wa Fedha amempatia fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma na kwamba anafuatilia fedha hizo kutoka *Abudhabi Fund*. Kwa maana hiyo ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu amelidanganya Bunge, ameidanganya Kamati ya Bunge. Naomba ama afute kauli hiyo au athibitishe kwamba fedha kwa ajili ya Barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora kweli amepewa na Waziri wa Fedha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naikataa kabisa hoja hiyo kwa sababu uongo unaozungumzwa kwenye kanuni hiyo, ni uongo unaoelekea kwenye udanganyifu wa dhahiri kabisa. Mheshimiwa Waziri hapa, naona katika zile *column* za tarakimu alikuwa anababaika kuhusu tarakimu. Kwa tafsiri hiyo, haiwezi kuitwa ni uongo. Kwa hiyo, haiwezi kukubalika hata kidogo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi! Ni kwamba Tanzania imekuwa inadaiwa fedha na *Abudhabi Fund* na baada ya Mheshimiwa Rais kukutana na uongozi wa *Abudhabi Fund,* ilionekana kwamba ili kwa kweli kuanza mazungumzo na wao kuwa na uwezo wa kuweza kutupa mikopo, basi angalau tuonyeshe ule ubinadamu wa kulipa angalau fedha. Kwa hiyo, fedha zilizopelekwa ni kweli ni shilingi milioni 500 zilishapelekwa tarehe 05 Juni, 2006. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucas Selelii, naona ulikuwa bado unataka kuongea. Lakini sasa mimi, kwanza ni Mwenyekiti hapa, pili kikubwa zaidi mimi ni kaka yako na kule nyumbani kwetu mimi ni *Chief.* Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa tabasamu hilo linaonekana. Mimi nachukua dhamana, tutasaidiana na Serikali barabara hizo ziweze kujengwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, yangu ni machache sana kwa sababu muda umekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 98, Programme Number 10*, *SubVote 1001*, Kifungu kidogo zaidi 250100, mshahara wa Waziri. Katika kuchangia nilijaribu kuwasilisha hofu yangu kwa niaba ya wananchi wa Muleba kuhusu barabara ya Kagoma - Muleba - Bihalamuro - Lusaunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 22 katika *bullet* ya pili kutoka juu, ameeleza barabara ambazo zinasubiri kukamilishwa ukarabati wake kwa sababu zimeanza kwa kiwango cha lami. Lakini, katika barabara zilizoorodheshwa, imeandikwa Kigoma - Bihalamuro - Lusaunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaomba nifahamishwe ni makosa ya uchapishaji kwamba walikusudia kuandika Kagoma, wakaandika Kigoma, au la! Sikupata ufafanuzi. Lakini kwenye vitabu kuna mkanganyiko humo, mara Kagoma kwenye fedha, kwenye hotuba ambayo ni ya msingi zaidi pia. Nikaomba ufafanuzi huo. Mimi nadhani hili ni la kulieleza tu. Walikusudia hiyo Kigoma - Bihalamuro - Lusaunga au Kagoma - Muleba - Bihalamuro - Lusaunga. Hilo la kwanza. Ili wajibu lote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, barabara hiyo kwa sababu ujenzi wake uko kwenye hatua za juu zaidi, jambo ambalo tunaishukuru Serikali sana. Wananchi wamelalamika kwamba Serikali katika kutoa fidia, inakamilisha fidia kwa baadhi ya watu ambao nyumba zao zitabomolewa katika mji wa Muleba.

Lakini, wengine hawakushirikishwa hata katika kutathmini au kuthamanisha *(Evaluation)* nyumba zao. Kwa hiyo, wamepewa amri nyumba hizo zibomolewe haraka

sana. Waliopewa fidia ya kutosha, wanabomoa kwa *speed*. Lakini ambao walipewa pesa, wakiambiwa hiki ni kianzio bomoa robo mtakuwa mnaishi nyuma, tutakuwa tunaleta nyingine, sasa wametiwa hofu na amri ambayo imetoka sasa kwamba wanapaswa katika siku 28 wawe wameondoka kwenye nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo tunaishukuru sana wananchi wamelalamika kwamba Serikali katika kutoa fidia imekuwa inakamilisha fidia kwa baadhi ya watu ambao nyumba zao zitabomolewa katika Mji wa Muleba. Lakini wengine hawakushirikishwa hata katika kutathimini au kuthaminisha *(valuation)* nyumba zao kwa hiyo, wamepewa amri nyumba hizo zibomolewe haraka sana. Waliopewa fidia ya kutosha wanabomoa kwa *speed* lakini ambao walipewa fedha wakiambiwa hiki ni kianzio bomoa robo mtakuwa mnaishi nyuma tutakuwa tunaleta nyingine. Sasa wametiwa hofu na amri ambayo imetoka sasa kwamba wanapaswa katika siku 28 wawe wameondoka katika nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, Serikali inachukua hatua gani suala hili? Je, inakubali ushauri niliowapa kwamba waende watalaam watatu na hata Waheshimiwa Mawaziri, wakipenda wakae na wananchi wale waondoe ile hofu ya kwamba ama kuna upendeleo au kuna rushwa katika kuamua nani afidiwe kiasi gani na nani afidiwe. Jambo ambalo nadhani linatekelezeka kwa kushirikisha wananchi na kwenda kukaa na wananchi na kwenda kukaa na wananchi ili kuwaondoa hofu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu nadhani ya muda mfupi sikupata maelekezo. Lakini wananchi ambao wanapaswa kupata majibu wananisikiliza sasa hivi. Wabomoe, waondoke na fidia isiyoridhisha au Mheshimiwa Waziri anakubali ushauri wangu watalichukua Serikali wakubali yaishe twende waongee na wananchi wapate fidia kamilifu. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kukumbusha tu kwamba baada ya dakika tano kwa maana ya kwamba zitakuwa zimesalia dakika 10 kufikia muda wa kuahirisha kwa mujibu wa Kanuni 81(6) itabidi niwahoji kwa mafungu yote bila mjadala wowote. Kwa hiyo, tuna dakika tano. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza haikuwa makusudi, ilikuwa ni makosa ya uchapishaji jina lililotakiwa ni Kagoma siyo Kigoma. Kuhusu fidia, *valuation* imefanyika upya kama ambavyo wananchi wamekuwa wakitulalamikia pamoja na Mheshimiwa Mbunge na kwa sasa *valuation* ile imetoka na wale ambao wanastahili kuongezewa fidia wataongezewa ili suala hili liishe.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, hayaeleweki upesi, anasema *valuation* imefanyika upya lini maana yake malalamiko ninayoyazungumza ni ya mchana huu. Kama anaahidi kwamba watakwenda wazungumze na wananchi ikibidi wafanye *valuation* upya hiyo ndiyo inaweza ikaeleweka. Lakini wakisema imefanyika upya na

wananchi watalipwa hiyo ndiyo wanayolalamikia pengine. Maana yake zimefanyika kama mara tano na mpya ni kama nne. Naomba ufafanuzi zaidi ni mpya itafanyika kuanzia leo.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu *valuation* mpya hiyo ni kwamba bado inalalamikiwa tutapeleka watalaam ili tuone kama tunaweza kufanya upya. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi hii. *Vote* 98 *subvote 1001* kifungu kidogo 250100 mshahara wa Waziri.

Mimi nilitaka kufahamu jambo moja, japokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, upande wa mawasiliano amenipa tamaa ya kusema kwamba Uwanja wa Ndege unashughulikiwa na huenda akapata mfadhiri kutoka *BADEA* au kutoka *World Bank* nilikuwa nataka nifahamu kwamba uwanja huu kwanza hizi shilingi bilioni 2 zilizotengwa Serikali itakuwa tayari kuipa Mafia zote ili utakapokuja huo msaada kutoka *BADEA* au kutoka *World Bank* au hiyo *MCC* basi mamlaka ya viwanja vya ndege iwe ilishaanza kazi ama ya usanifu kwa sababu usanifu naamini wanao na tayari walishautayarisha haiwezekani miaka 20 kiwanja kile kiwe kinajengwa wao wasijue au wasiwe na *documents* ya kuweza kusema kwamba hiki kinahitaji kijengwe namna gani. Sasa je, nataka nifahamu Serikali itakuwa tayari kuzitoa hizi bilioni 2 kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Mafia?

La pili katika *gate* kuna fedha shilingi milioni 500 zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa ajili ya wale watakaohamishwa pale. Serikali itakuwa tayari mamlaka ya Bandari kwenda sasa hivi kuzilipa ili tuanze kusafisha na hao wajenzi wa bandari ambao atutamkie Waziri kwamba nani atafadhili na ujenzi utaanza lini wa *gate* rasmi. Lakini la mwisho nataka nijue vifaa vya barabara kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mafia halikuzungumzwa kabisa wala sikupata majibu. Serikali ina mpango gani wa kutupatia vifaa hivi haraka iwezekanavyo ili kumnusuru Waziri aliyekuwa wa ujenzi kwamba baada ya kuliambia Bunge kwamba tutapata na akaielekeza kwamba *Road Fund Board* itoe na ikawa haikutekeleza maelezo ya Waziri wakati fedha wanazo na ninafahamu kwamba hata katika uwanja wa Arusha bado kuna shilingi 1.8 bilioni ambazo ziko *standby* kwa ajili ya uwanja ule kumalizia kazi ndogo ndogo. Maswali yangu haya matatu nikiridhishwa na mimi nitaridhia na hata hicho chakula nitaendelea kula kesho. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Kama nilivyomwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajenga uwanja wa ndege wa Mafia na kweli kwa kupitia huu mradi wa *MCC* tayari *principle* imekubalika Mafia kufadhiliwa. Sasa wanasubiri kupata *approve value* ya bodi kufadhiliwa. Kwa hiyo, hivi sasa wakati tunasubiri hayo ni kwamba shilingi bilioni 2 ambazo mlitengewa ninyi na Arusha zinakwenda Mafia kufanya shughuli hizo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

Kwa mujibu wa Kanuni 21 (4) nisingependa niisome kwa sababu ya muda, Bunge lako Tukufu linaruhusiwa kuongezewa muda kwa kipindi cha dakika 30 ili kuweza kumaliza shughuli ambayo inayoendelea. Kwa hiyo, nilikuwa naomba muda uongezeke kwa muda wa dakika 30.

**MWENYEKITI:** Hakuna aliyetoa hoja kwanza na haiwezi kutolewa bila taarifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kuongeza muda wa Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Sikupata taarifa kwa hiyo haiwezekani. Tunaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *gate* tumemhakikishia kwamba Mheshimiwa Mbunge kwamba mamlaka ya bandari italipa fidia na fidia ni shilingi milioni 600 zimetengwa na mamlaka ya bandari. Kuhusu greda tumemhakikishia Mheshimiwa Mbunge, litanunuliwa na vifaa vitafikishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Waheshimiwa Wabunge, kwa hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, ambayo imeanguka. Spika, inabidi apewe taarifa ili amuagize Waziri wa Nchi, atoe hoja ya kuongeza muda haitolewi na mtu, kila Mbunge tu anatoa hoja ya kuongeza muda hatuna utaratibu huo.

Kwa hiyo, taarifa ilitakiwa ije kwangu kwanza ili mimi nimwelekeze Waziri wa Nchi, atoa hoja ya kuongeza muda na niwahoji mkubali ndiyo tunaendelea. Kwa muda huu tuliofika Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni niliyoitaja ya 81(6) sasa nitamuomba Katibu na nitawahoji kwa mafungu bila mjadala wowote.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya rekodi ya kikao chako naarifiwa kwamba pale mwanzo kabisa ile iliyoandikwa *(e) estimate of the amount required)* ukurasa wa 274 pale yako mabadiliko ambayo yameletwa baada ya vitabu hivi kuchapishwa kutoka hazina ambayo ningependa kwa rekodi yako sijui niyasome ama nikupe baadaye uyaangalie kama itakuwaje. Maneno ya kuchukua nafasi ya yale yaliyokuwepo au niwape *addendum*.

**MWENYEKITI:** Basi utatawanyie *addendum* inatosha kabisa. Waheshimiwa Wabunge, tutatawanyiwa hii *addendum* ambayo itaonyeshwa kabisa mabadiliko yaliyomo katika Kasma hiyo.

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**FUNGU 98 - WIZARA YA MIUNDOMBINU**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... Shs. 1,152,200,000/=

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... .. ... ... ... ... ... Shs. 2,053,115,000/=
Kifungu 2001 - *Electrical and Mechanical* ... ... ... ... ..Shs. 2,157,790,000/=
Kifungu 2003 -*Transport and Communication* ... ... Shs. 100,210,084,00/=
Kifungu 3001 - *Supplies and Services* ... ... ... ... ... ... Shs. 1,894,073,000/=
Kifungu 5001 - *Buildings Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Shs. 3,481,907,000/=
Kifungu 6001 - *Trunk Roads* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Shs. 60,465,038,000/=
Kifungu 7001- *Rural Roads* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 1,899,018,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ...Shs. 300,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* . ... ... ... ... ... ... Shs. 2,150,000,000/=
Kifungu 2001 - *Electrical and Mechanical* ... ... ... ...Shs. 7,300,000,000/=
Kifungu 2003 - *Transport and Communication* ... ...Shs. 16,620,590,000/=
Kifungu 6001 - *Trunk Roads* .. ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 233,764,780,000/=
Kifungu 7001 – *Rural Roads* .. ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 20,612,620,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, narudia, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hawakusikii.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 kwa Wizara ya Miundombinu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote pamoja *addendum*. Naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, natoa taarifa kwamba shughuli zilizokuwa zimepangwa katika orodha ya shughuli za leo sasa zimekwisha na kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, tarehe 5 Julai, 2006 saa tatu asubuhi)*